

2 NOVEMBA, 2022
BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Pili – Tarehe 2 Novemba, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2022)*.

2 NOVEMBA, 2022

MHE. YAHAYA O. MASSARE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2022*).

MHE. AIDA J. KHENANI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa na Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

MHE. GEORGE N. MALIMA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):

2 NOVEMBA, 2022

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwezeshaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali. Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, na Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala sasa aulize swali lake.

Na. 21

Fidia kwa Wananchi Walioathirika na Mabomu – Mbagala

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya mapunjo ya fidia kwa wananchi walioathirika na mlipuko wa mabomu Mbagala?

SPIKA: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera na Uratibu, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU) alijibu:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa mkono wa pole na siyo fidia, kwa wananchi 12,647 waliothirika na milipuko ya mabomu iliyotokea tarehe 29 Aprili, 2009 katika Kambi ya JWTZ Mbagala. Malipo hayo, yalitolewa kwa awamu sita kuanzia mwaka 2009 hadi 2020. Vile vile, Serikali ilitoa kifuta machozi pamoja na kugharamia huduma za mazishi kwa familia 29 zilizopoteza wapendwa wao kutokana na milipuko hiyo ya mabomu ya Mbagala.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kutoa mkono wa pole kwa waathirika lilisitishwa rasmi na Serikali mnamo mwezi Machi, 2020 baada ya walengwa wote waliokusudiwa kujitokeza na kulipwa.

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu hayo ya Serikali: Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kutoa ufafanuzi kwa wananchi hao ya tofauti kati ya fidia na kifuta machozi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Je, kutokana na malalamiko ya wananchi hao kuwa mengi, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana nami jimboni ili kwenda kuwasikiliza wananchi hao na hatimaye kutatua matatizo hayo? *(Makofi)*

2 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ulirejea kukaa, ulipaswa kuwa umesimama hapa hapa mpaka maswali yako yaishe. Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chaurembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze na swali la pili kwamba niko tayari wakati wowote kufuatana na Mheshimiwa Mbunge ili kwenda kuwasikiliza wananchi. Bahati nzuri nilipata fursa ya kukutana na baadhi yao na kwa niaba yangu alikutana nao Mheshimiwa Jafo Dar es Salaam, na tulipokea barua yao na baadhi yao tunaendelea kuwasiliana nao. Tutafanya hivyo ili tukawasilikilize kule kule kwa sababu ndiyo kazi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni ufafanuzi wa tofauti ya maafa au fidia na kifuta machozi. Maafa yanasababisha na majanga, majanga na huwa si jambo lililopangwa au kutarajiwa, majanga yanaweza kutokana na nguvu za asili, inaweza ikawa na mafuriko, au Tsunami, pia majanga yanaweza yakatokana na matokeo mbalimbali ya nguvu ambazo siyo za kawaida. Inaweza ikawa ni mlipuko wa magonjwa, na yenyewe hayo pia ni majanga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yanapotokea maafa, huwezi ukayawekea utaratibu wa kulipa fidia. Kwa hiyo, hakuna utaratibu wa fidia kwa majanga, bali ambacho hutokea, jamii au Serikali huweza kutoa kifuta machozi au

2 NOVEMBA, 2022

mkono wa pole kwa walioathirika. Kwa hiyo, Serikali ilifanya hivyo na iliwalipa kifuta machozi. Pia Serikali ililipa kifuta machozi kiasi cha Shilingi 17,464,944,954/=, fedha hizi ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ilishughulikia mazishi ya wale ambao walifariki katika tukio lile. Naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaelekea ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge Rorya sasa aulize swali lake.

Na. 22

Mamlaka ya Mji Mdogo Shirati Kuwa Mamlaka Kamili

MHE. JAFARI W. CHEGE aliuliza:-

Je, ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo Shirati katika Wilaya ya Rorya itaanza kufanya kazi kama Mamlaka kamili?

SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Shirati itaanza mara baada ya Halmashauri mama ya Rorya kukamilisha mchakato wake wa kukusanya na kuimarisha mapato ya ndani ili iweze kuzihudumia Halmashauri mama na Mamlaka ya Mji mdogo wa Shirati.

SPIKA: Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nitakuwa na swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo, mamlaka ambayo imeahidiwa kwa muda mrefu kwa zaidi ya miaka kumi sasa. Mwaka 2009 Waziri Mkuu aliyemaliza muda wake Mheshimiwa Mizengo Pinda, aliahidi; pia imetajwa kwenye awamu karibu tatu za Ilani ya Uchaguzi ya Chama changu cha Mapinduzi. Mwaka 2020 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepo naye aliahidi kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mji Mdogo. Nilitaka nijue tu Mheshimiwa Waziri kama yuko tayari sasa kuongozana nami kwenda kujiridhisha sababu hizi zinazosema kwamba uanzishwaji wake unacheleweshwa kwa sababu ya mapato ya ndani. Tuongozane ili twende kujiridhisha kwa kukaa na wataalam na Halmashauri ili tuweze kupata jibu la pamoja la uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Shirati.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niko tayari na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge ndani ya wiki mbili tutakaa na Baraza la Madiwani pamoja na Wakurugenzi katika Halmashauri yake, kuainisha na kutangua vyanzo vyote vya mapato ili tuone kama vinaweza kuhudumia ili mamlaka hii ndogo iweze kuanza.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke, sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Kumaliza Mgogoro wa Ardhi Katika Kata ya
Yombo Vituka - Temeke**

MHE. DOROTHY G. KILAVE aliuliza:-

Je ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa Ardhi kati ya Wananchi na Serikali katika Kata ya Yombo Vituka?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa

2 NOVEMBA, 2022

Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na Serikali ili kupisha ujenzi na upanuzi wa Shule ya Msingi Uwanja wa Ndege, ulihitimishwa tarehe 26 Septemba, 2022 baada Mahakama ya Rufaa kutupilia mbali Shauri la Rufaa Na. 116/2019 lililofunguliwa na walalamikaji 56 ambao walishindwa kuthibitisha madai yao.

SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Ili kuepusha hii migogoro: Je, ni lini sasa Serikali itaweza kwenda kuweka mipaka halisi ya ile sehemu ili tuendeleo na shule kwa sababu mgogoro huu umekuwa ukijirudia mara kwa mara? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nawaagiza Halmashauri ya Temeke kwamba baada ya rufaa hii kwisha, mara moja waanze mchakato wa kuweka mipaka halisi ili watu wasiende

2 NOVEMBA, 2022

kuvamia hilo eneo. Kwa hiyo, mchakato uanze mara moja kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaelekea Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 24

Fidia kwa Wananchi wa Cheketu Kupisha Mradi wa Umeme

MHE. FRANCIS K. NDULANE aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Kitongoji cha Cheketu Somanga Kusini watalipwa fidia kupisha ujenzi wa miundombinu ya umeme?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TANESCO inatarajia kujenga njia ya kusafirisha umeme yenye urefu wa kilomita

2 NOVEMBA, 2022

190 ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi hadi Somanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imelipa jumla ya Shilingi milioni 37.5 kwa wahanga 11 kati ya 13 wanaoathiriwa na mradi huu. Wahanga wawili waliobaki walitathminiwa kuwa maeneo ya Serikali ya Kijiji cha Cheketu, lakini kumekuwepo na mgogoro baina yake na wananchi. Serikali italipa malipo hayo baada ya utatuzi wa mgogoro huo.

SPIKA: Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika mgogoro huu wa madai ya fidia, hivi sasa umechukua miaka mitano na jumla ya watu 63 wamehusishwa katika jambo hili: Je, Serikali ipo tayari kulipa fidia ya nyongeza kutokana na ucheleweshaji wa malipo haya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, napenda kutaka kujua: Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuwa na nafasi ya kuweza kuambatana nami twende kwa pamoja tukasuluhishe huu mgogoro? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nianze na la pili, tukimaliza kipindi hiki cha Bunge, tutapanga ratiba vizuri na Mheshimiwa ili tuweze kuona namna ya kumaliza jambo hili kwa pamoja kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza, Serikali ipo tayari kumlipa mtu fidia kwa kadri anavyostahili kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, kama nilivyosema, tutaenda pamoja na kusaidiana kutatua jambo hili, na lipatakapokwisha wale wanaostahili kulipwa fidia na kwa mazingira tuliyokuwa nayo, aidha ya ucheleweshaji au nyongeza, itafanyika kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake.

Na. 25

Kukatika Umeme Mara kwa Mara Mikoa ya Kusini

MHE. CECIL D. MWAMBE aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kumaliza kero ya kukatikakatika kwa umeme Mikoa ya Kusini hasa Wilaya ya Masasi na Vijiji vyake?

SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Mtwara imeendelea kuimarika na kuwa ya kuridhisha ukilinganishwa na kipindi cha nyuma. Serikali inao mkakati wa dhati wa kumaliza changamoto hii kwa mikoa ya Kusini na maeneo mengine ya Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa changamoto hii, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya kurekebisha miundombinu katika *line* za Newala, Nyangao, Masasi na Mahuta. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 2.2 zimetengwa kwa ajili ya kujenga njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Nanganga hadi Masasi. Pia, jumla ya shilingi bilioni mbili zimetengwa kuweka transfoma kubwa kati ya Tunduru na Namtumbo ili kupata umeme mkubwa kutoka Ruvuma bila kuathiri watumiaji wengine.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kudumu wa kuimarisha Gridi ya Taifa, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 250 kujenga Gridi ya Taifa kutoka Songea – Tunduru – hadi Masasi. Kwa mwaka 2022/2023 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 66.7 kuanza ujenzi wa njia hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kumekuwa na uendelezaji mdogo sana wa miradi ya REA iliyopo kwenye Majimbo yote ya Mkoa wa Mtwara.

2 NOVEMBA, 2022

Swali la kwanza; pamoja na mikakati hii ya Serikali ya kutaka kuimarisha upatikanaji wa umeme kwenye wilaya zetu, ni lini sasa tutahakikisha Miradi ya REA iliyopo kwenye Majimbo yote ya Mkoa wa Mtwara inakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tunataka kufahamu kwa uhakika kwa sababu mpaka sasa kuna vijiji zaidi ya 300 havijapatiwa umeme, wanaleta umeme wa *grid* kutoka Mtwara na hii wanayosema kutoka Mombika ili kuimarisha upatikanaji wa umeme kwenye Wilaya ya Masasi, nayo tunaomba kufahamu miradi hii itaanza kutekelezwa lini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Cecil Mwambe kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikataba mingi ya REA III, round two ilikuwa inatakiwa kuisha Desemba, lakini kwa changamoto ambazo zilijitokeza ambazo tayari tulishazisema, muda wake wa kukamilika utaongezeka kidogo kulingana tofauti tofauti ya maeneo. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kwamba Serikali kupitia Wizara ya Nishati inahakikisha kwamba mikataba hii inakamilika na wananchi wanapata umeme katika vijiji vyao, kwa sababu pesa ipo na usimamizi unaendelea kufanyika wa karibu. Kwa hiyo, tutaendelea kulisimamia hili ili umeme uweze kupatikana katika maeneo yetu.

2 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. JUMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni miezi mitatu sasa katika Wilaya ya Kyela, umeme haupatikani mchana. Je, ni lini wananchi wa Kyela watajisikia kwamba nao wana haki ya kupata umeme asubuhi na mchana?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Jumbe, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya hapa nikafuatilie ili kufahamu kwa nini Mheshimiwa Mbunge katika jimbo lake kwa miezi mitatu hakupatikani umeme mchana. Ninachofahamu ni kwamba kwa sababu ya upungufu wa umeme kumekuwa na kupungua kwa umeme kwenye baadhi ya maeneo, lakini jambo la kwamba miezi mitatu mchana wote hakuna, hilo ni jambo la kufuatilia, halafu tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kutatua changamoto hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani hilo ungewajibu Wabunge wote kabla sijampa Mbunge anayefuata, kwa sababu kuna malalamiko ya ukatikaji wa umeme kila maeneo. Yaani hapa kila Mbunge angepewa nafasi ya kusimama angesimama. Maeneo ambayo yote ambayo umeme umeshafika kwa juhudi za Serikali kuna changamoto, umeme unakatikakatika sana. Kwa hiyo, toa

2 NOVEMBA, 2022

maelezo ya jumla kwa watu wote na siyo Kyela peke yake ambako umeme unakatikakatika. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kuongeza kidogo maelezo kwamba tunayo changamoto kidogo ya upungufu wa vyanzo vya uzalishaji wa umeme hasa kwenye maji, takribani *megawatt* kama 190 hazipatikani kama tulivyotaraji kwa sababu ya upungufu wa maji. Hilo pengine limesababisha baadhi ya maeneo kukatika umeme au kupewa umeme kwa vipindi tofauti.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeji-*commit* kuhakikisha kwamba kabla ya mwezi unaokuja kuisha Mradi wetu wa Kinyerezi *One Extension* utakaotupatia *megawatt* 185 umekamilika ili kuondoa matatizo ya kukatikakatika kwa umeme kwa sababu upungufu wa umeme. Hata hivyo, kama tulivyokwishaeleza tayari Serikali imetenga bilioni 500 kwa ajili ya kuimarisha *grid* lakini na bilioni 300 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu mingine isiyokuwa ya *grid* kuhakikisha kwamba umeme haukatikikatiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunao uhakika kwamba tunakoelekea kumaliza mwaka huu majibu ya haraka yatapatikana, lakini tunapomaliza mwaka huu wa fedha majibu makubwa ya muda mrefu yatapatikana kuhakikisha tatizo la kukatikakatika kwa umeme linakwisha katika maeneo yetu.

SPIKA: Ahsante sana. Wakati mkilifanya hilo, mtazame maeneo ya kipaumbele, nafahamu huwa mna vipaumbele maeneo ya afya, huduma lakini maeneo pia ya biashara sehemu ambazo huwa mchana kunafanyika biashara

2 NOVEMBA, 2022

umeme uwepo ili watu wasiingie gharama kubwa sana ya kutumia mafuta ama kutumia majenereta kwa sababu wanaingia gharama kubwa sana. Kwa hiyo, hiyo changamoto inaeleweka lakini wale mameneja wa mikoa waangalia namna ambayo wanaweza kutoa vipaumbele mbele muda ambao maeneo fulani matumizi ya umeme yanakuwa ni makubwa basi wapeleke huko hasa maeneo ya biashara.

Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Naomba Serikali ituambie hususani Wizara ya Nishati, kuna kigugumizi gani hasa katika suala la REA? Maana yake kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa hawa Wakandarasi hawatoi ushirikiano, lakini hawashughuliki kabisa na miradi ile inayotakiwa ifanyike kule. Mfano kwenye jimbo langu ule mkataba uliopita haujatekelezwa hata katika kijiji kimoja. Sasa Serikali ina kigugumizi gani katika jambo hili, ituambie ukweli?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niombe kupata ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni case by case kwamba Mkandarasi hana ushirikiano mzuri na Mbunge. Wako Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wanatoa sifa nzuri na *recommendation* nzuri kwa wakandarasi waliokuwa nao kwamba wanatoa ushirikiano. Kwa hiyo,

2 NOVEMBA, 2022

naomba kwa wale ambao wanapata changamoto ya ushirikiano, basi tuwasiliane ili tuweze kutatua changamoto hizo katika maeneo yao ili tuweze kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo lingine, tuwasiliane pia na kupeana taarifa na *updates* sahihi za ni lini umeme umewaka wapi na utawashwa wapi na pale ambapo tunaona kuna changamoto za ucheleweshaji usiokuwa na sababu kwa pamoja tuweze kushirikiana na kuchukua hatua ili tufikie azma ya kuwasha umeme katika vijiji vyetu vyote kwa kadri ya mikataba, lakini na lengo la Serikali Awamu ya Sita inaongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

SPIKA: Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza kuhusu suala la Mkandarasi wa REA katika Mkoa wetu wa Songwe. Nafikiri hili tatizo Waziri analifahamu na binafsi nimekwenda ofisini kwake mara kadhaa kuhusu huyo Mkandarasi. Kwa kifupi huyu mkandarasi ana kiburi, mpaka sasa hivi amewasha vijiji vitano tu mkoa mzima na ana majibu ya jeuri, Waziri mwenyewe ameshuhudia. Sasa nini mkakati wa Wizara au Waziri yuko tayari kwenda Songwe kuonana na huyu mkandarasi kuhusu tatizo la REA, Mkoa wa Songwe? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, naona umeuliza maswali mawili, wakati ni swali la nyongeza. Kwa hiyo, Mheshimiwa

2 NOVEMBA, 2022

Naibu Waziri, chagua jepesi kati ya hayo umpe majibu Mheshimiwa Mbunge katika swali mojawapo. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkandarasi anayeteteleza mradi wa *REA III, Round Two* katika Mkoa wa Songwe, ni mkandarasi anayeitwa *Derm Electric* ambaye pia anafanya kazi hiyo katika Mkoa wa Dodoma. Mkandarasi huyu siyo hohehahe, siyo legelege, ni mojawapo ya wakandarasi ambao tunawatarajia wafanye kazi nzuri. Changamoto ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema tumeshaanza kuifanyia kazi na tutaendelea kusukumana na kusimamiana ili kazi hizo zote za maeneo husika ziweke kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshapanga kikao na wakandarasi hawa, mwishoni mwa mwezi huu ili tuweze kwa pamoja changamoto ambazo zinatokea kwa upande wao ili tuweze kuzitatua na kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati.

SPIKA: Mheshimiwa Dennis Londo, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, naungana na Wabunge wenzangu, mkandarasi ambaye amepewa Miradi ya REA katika Wilaya za Mvomero, Ulanga, Malinyi, Kilosa mpaka sasa hajawasha umeme katika kijiji hata

2 NOVEMBA, 2022

kimoja. Sasa na hilo nalo wananchi wa Jimbo la Mikumi wanataka kujua nini kauli ya Serikali kwenye hili?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya hapa niwasiliane naye ili nijue changamoto hasa kwenye eneo lake ni sehemu gani anasema hakujawasha hata kijiji kimoja. Baada ya hapo tutafuatilia kujua changamoto iko wapi, pengine ni kwa sababu mkandarasi anakuwa na maeneo manne, matano, sita pengine kaanzia kwingine kwake hajafika. Zile hatua za awali za kuhakiki mipaka, kuhakiki maeneo ya kuweka miundombinu na kuhakiki urefu, tayari zimeshafanyika kwenye maeneo yote inafuata kuweka nguzo, kuvuta wires na sasa kuwasha umeme. Kwa hiyo, tukishafuatilia tutajua hatua gani imefikiwa katika eneo lake, lakini kazi hiyo lazima ifanyike na kukamilika.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mbunge wa Mtoni, sasa aulize swali lake.

Na. 26

2 NOVEMBA, 2022

**Uhitaji wa Kupambana na Visababishi vya Maradhi
Yasiyoambukiza**

MHE. IDRISSA JUMA ABDUL-HAFAR aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupambana na visababishi vya maradhi yasiyoambukiza?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dr. Godwin Mollel, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Idrissa Juma Abdul-Hafar, Mbunge wa Jimbo la Mtoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga shilingi milioni 725 kwa ajili ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Kitaifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza (2021 – 2026) ambao umeainisha mikakati mahsusi ya udhibiti wa visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo:-

- (1) Kuimarisha uratibu na ushirikishwaji wa sekta mtambuka;
- (2) Kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma;

2 NOVEMBA, 2022

- (3) Kuwajengea uwezo watumishi katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza;
- (4) Kuimarisha na kusimamia shughuli za utafiti; na
- (5) Kuhamasisha wananchi kuhusu njia za kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

Njia hizi ni pamoja na kufanya mazoezi, pamoja na kuzingatia kanuni bora za lishe.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Idrissa Juma Abdul-Hafar, swali la nyongeza.

MHE. IDRISSA JUMA ABDUL-HAFAR: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu haya ya Mheshimiwa Waziri, lakini kumekuwa na ongezeko la malazi ya kisukari, malazi ya moyo pamoja na kansa kwa watoto walio chini ya miaka mitano na hata watoto kwa mujibu sheria za nchi zetu walio chini ya umri wa miaka kumi na nane. Je, Serikali haioni sasa iwe na utaratibu maalum wa kuhudumia kwa asilimia mia moja matibabu ya malazi yasiyoambukiza kwa watoto wote walio chini ya miaka 18? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ni kweli suala la kuhudumia watoto chini ya miaka mitano ni suala ambalo kiutaratibu wanatakiwa kupata huduma bure, bila malipo yoyote. Ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya kwamba wanahitaji huduma lakini baadhi ya dawa zinakosekana. Pia, tuna mzigo mkubwa kweli wa magonjwa hayo yasiyoambukiza, ndiyo maana tunaleta Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote wenye lengo la kusababisha sasa matatizo anayoyataja Mheshimiwa Mbunge yaweze kusuluhishwa.

Mheshimiwa Spika, ukiona uwekezaji mkubwa ambavyo umewekezwa kwenye miundombinu, vifaa tiba na tunaona mwaka huu kuna bilioni 10.7 zinaenda kutumika ni kwa ajili ya kuhakikisha wale wasiojiweza pia wanapata huduma bila malipo.

SPIKA: Mheshimiwa Mariam Mwinyi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza ni gharama sana. Je, Serikali wanasaidia vipi wananchi kwenye gharama hizi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba arudie amesema sijui wananchi wenye nini, sikumsikia vizuri.

2 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Anataka kujua kwenye hayo magonjwa gharama zake Serikali inasaidia vipi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwa mwaka mmoja, Serikali inatumia bilioni 670 kwa *exemption* yaani kwa maana na hasa asilimia kubwa ya fedha hizo zinaelekea kwenye kuwasaidia hawa wenzetu ambao wana matatizo ya magonjwa yasiyoambukiza, zinatumika hizo fedha kwa ajili ya *exemption*.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Muswada wa Bima ya Afya, unakuja hapa ndani, hilo ndiyo litakuwa suluhisho na mnajua pamoja na kwamba tuna Muswada wa Bima ya Afya, Rais wetu ametenga bilioni 149.77 kwa ajili ya kuwapatia bima wale wasiojiweza. Kwa hiyo, mikakati ndiyo hiyo ya kwenda kuboresha na kuhakikisha watu wanapata huduma.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Na. 27

Kujenga Bwawa Kata ya Nyanzwa – Kilolo

MHE. JUSTINE L. NYAMOGA aliuliza:-

2 NOVEMBA, 2022

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga bwawa la maji katika Kata ya Nyanzwa kwa ajili ya skimu ya umwagiliaji?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, majibu.

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na Skimu ya Umwagiliaji Nyanzwa. Aidha, mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bwawa na Skimu ya Umwagiliaji Nyanzwa.

SPIKA: Mheshimiwa Justine Nyamoga, swali la nyongeza.

MHE. JUSTINE L. NYAMOGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza; katika Kijiji cha Mgowelo ambacho kiko katika Kata hiyo hiyo ya Nyanzwa, kumetengwa zaidi ya hekta 3000 kwa ajili ya *block farming*. Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti kwenye eneo hilo na

2 NOVEMBA, 2022

kuona umuhimu wa kuweka skimu pia kwenye hilo eneo kwa sababu ni hekta nyingi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwenye Bunge lililopita, niliomba Naibu Waziri au Waziri kutembelea eneo hili na kuangalia changamoto tunazopata za skimu mbalimbali, lakini mpaka sasa ziara hiyo haijafanyika. Je, Waziri ananiahidi lini atafika Jimboni Kilolo kwa ajili ya kutembelea na kuona tunaweza tukashauriana vipi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, maswali yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufika jimboni kwake naomba nimuahidi yeye na wananchi, nitakwenda mwenyewe baada ya Bunge hili kwa ajili ya kwenda kufanya kazi hiyo pamoja na kuangalia mwendelezo wa mradi wetu wa pamoja wa chai ambao yeye mwenyewe alikuwa muasisi wa kuanzisha huo mradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hii *block farm*, naomba nimwombe baada ya kikao cha Bunge tukutane ofisini ili nimkabidhi timu ya watu ambao wataenda kufanya *soil analysis* na kuchukua mipaka ili tuiweke kwenye mipango ya Wizara.

SPIKA: Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

2 NOVEMBA, 2022

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali ilituahidi kwamba mwezi wa Saba tungepata *consultant* kwa ajili ya Bwawa kubwa la Mkomazi, lakini mpaka leo kuna ukimya. Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mnzava, kuhusu Bwawa la Mkomazi yeye mwenyewe anafahamu hivi karibuni timu ya Wizara ya Kilimo ilikuwepo kule na tatizo lililokuwepo katika suala la Mkomazi, *design* iliyokuwa imefanyika toka awali na zile skimu zilizoko maeneo yale ilikuwa ina makosa. Kwa hiyo, wataalam wa Wizara wamefanya kazi ya kwanza kwa ajili ya kwenda kutembelea na kuangalia na nimuahidi tu yeye na wananchi wa jimbo lake, kwamba *next financial year* ya 2023, Bwawa la Mkomazi litakuwa kwenye miradi itakayojengwa na Wizara ya Kilimo kwa ajili ya eneo hilo na skimu zote zilizoko katika ukanda ule ambazo ziko saba.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakarabati Bwawa la Nyangokorwa lililoko Wilaya ya Bariadi ili liweze kutumika katika kilimo cha umwagiliaji?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

2 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Midimu na Wabunge wote wa Mkoa wa Simiyu, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Wizara sasa hivi inachokifanya ni kuangalia namna gani tunaweza kutumia *resource* ya maji inayotoka katika Ziwa Victoria na kwa kuwa kuna Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria, unayoyatoa maji Ziwa Victoria kuyaleta Mkoa wa Simiyu, sasa hivi tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Maji, ili tuweze ku-*tap* yale maji yanayotoka Ziwa Victoria ili kuweza ku-develop skimu katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo Simiyu, ni maeneo yenye ukame na Wilaya zote za Simiyu zina ukame na zinapata mvua za muda mfupi. Kwa hiyo, njia ya kudumu ni ya kuyatumia maji ya Ziwa Victoria kwa ajili ya kutengeneza miradi ya umwagiliaji katika Mkoa wa Simiyu.

SPIKA: Mheshimiwa Robert Maboto, swali la nyongeza.

MHE. ROBERT C. MABOTO: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Wizara ya Kilimo itasambaza lini mbegu za alizeti katika Halmashauri ya Mji wa Bunda?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Robert, Mbunge wa Bunda na Wabunge wote, kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulisambaza jumla ya tani 2,000 za zao la alizeti za *standard seed* ambazo zilikumbana na changamoto na mwaka huu tutasambaza *certified seed* tani 2,500. Nitumie nafasi hii, kusema kwamba, halmashauri ambazo ziko tayari kushirikiana na Wizara ya Kilimo, zilete maombi na tukubaliane, mbegu hizo tunazozigawa kwa ruzuku ni namna gani fedha ile itarudi kwa sababu tutazigawa kwa ruzuku ya asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine ambao watakuwa tayari, tumeshafanya hivyo Mkoa wa Singida na maeneo mengine ambao watakuwa tayari hasa Ukanda wa Kati na Ukanda wa Kanda ya Ziwa ambako uzalishaji wa alizeti unafanya vizuri zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 28

Matokeo ya Tafiti za Kilimo

MHE. MICHAEL M. KEMBAKI aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha matokeo ya tafiti za kilimo yanawafikia wakulima?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha matokeo ya tafiti za kilimo yanawafikia wakulima, Taasisi za Utafiti na Idara ya Ugani hutumia njia mbalimbali kufikisha taarifa za utafiti na matumizi ya teknolojia ambazo ni pamoja na kufungua mashamba darasa na mashamba mfano katika maeneo ya kilimo, kutengeneza na kusambaza majarida ya tafiti za kilimo, uwezeshaji wa shughuli za ugani, kuwepo kwa siku ya mkulima, warsha kwa wadau, ushirikishwaji wa wakulima kwenye tafiti na kukusanya takwimu za kiutafiti.

Mheshimiwa Spika, vilevile, safari za mafunzo, vituo mahiri na atamizi vya uhaulishi teknolojia katika viwanja vya Nanenane, maonesho ya kilimo na biashara, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii. Vilevile simu za kiganjani, maandiko ya kisayansi na machapisho.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Taasisi za Utafiti zimeshiriki katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Kitaifa Jijini Mbeya katika Kiwanja cha John Mwakangale na Viwanja vingine vya Kikanda.

SPIKA: Mheshimiwa Michael Kembaki, swali la nyongeza.

MHE. MICHAEL M. KEMBAKI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninaipongeza Serikali kwa hatua hizi zinazofanya za kuwafikia wakulima, lakini hatua hizi ambazo

2 NOVEMBA, 2022

wamezichukuwa zinalenga hasa wakulima wakubwa. Kama mnavyojua, wakulima wa Tanzania wengi wao wana uchumi mdogo, ni wakulima wadogowadogo ambao wanalima heka moja, nusu heka. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, wengi wa wakulima hawana uwezo...

SPIKA: Swali Mheshimiwa.

MHE. MICHAEL M. KEMBAKI: Mheshimiwa Spika, ni mkakati gani hasa Serikali inao wa kuwafikia wakulima wadogo ambao hawana uwezo wa kununua simu, hawana uwezo wa kununua TV au kuweza kufika kwenye warsha na maonesho ya Nanenane. Je, Serikali ina mkakati gani hasa wa kuwafikia? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu niliyoyatoa kwenye swali la msingi, Serikali inachukuwa hatua mbalimbali: Moja, sasa hivi tumeanza kusajili wakulima, kwa muda mrefu tumekuwa tukihudumia watu tusiowatambua. Kwa hiyo, sasa hivi tumeanza process ya kuwasajili wakulima kuwatambua walipo, kuchukua hadi *fingerprints*, vilevile tunaenda kuchukua *GPS coordinate* za mashamba yao, zoezi hili linaendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunalolifanya ni kumwezesha Afisa Ugani ili awe na uwezo wa kuwafika wakulima. Tunao upungufu wa Maafisa Ugani katika nchi yetu wasiozidi Elfu Saba, kwa hiyo ili kuhudumia kaya Milioni

2 NOVEMBA, 2022

Saba inakuwa tatizo. Kwa hiyo, Serikali imewekeza kuwapatia pikipiki na sasa tunawapatia nyezo na hivi karibuni tutawapatia vishikwambi ambavyo vitakuwa vinachukua taarifa za kila mkulima aliyemtembelea katika eneo lake. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge hii *extension program* itatuchukua kwa kipindi cha miaka mitatu ili kuweza kufika kule ambapo tunapotaka na kutambua mkulima ni nani na kila Afisa Kilimo kukabidhiwa idadi ya wakulima atakaokuwa anawahudumia kwa siku. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Madini, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 29

Upatikanaji wa Madini Nanyumbu

MHE. YAHYA A. MHATA aliuliza: -

Je, Serikali ina taarifa juu ya upatikanaji wa madini Nanyumbu na Je, wananchi wananufaikaje?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu: -

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kwa Niaba ya Waziri wa Madini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi yake ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), ilifanya utafiti wa awali katika Wilaya ya Nanyumbu iliyopo kwenye *Quarter Degree Sheet (QDS) 316* na kubaini uwepo wa madini mbalimbali. Utafiti huo ulionesha kuwepo kwa madini ya dhahabu katika vijiji vya Lukwika, Chungu, Chipuputa na Masuguru. Katika kijiji cha Masuguru utafiti huo ulibaini pia uwepo wa madini ya *sapphire*, *Acquamarine* na *rhodolite*. Aidha, Wilaya ya Nanyumbu imebainika kuwa na madini mengine yakiwemo madini ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini katika Wilaya ya Nanyumbu imetoa leseni za uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu 73, madini ya chuma nane, madini ujenzi mbili, madini ya vito 10 na leseni mbili za utafutaji wa madini ambapo moja ni kwa ajili ya utafutaji madini ya nikeli na nyingine ni kwa ajili ya madini ya dhahabu. Aidha, katika maeneo hayo shughuli za utafiti na uzalishaji zinaendelea. Kufuatia shughuli hizo wananchi wamekuwa wakijipatia kipato, ajira na mzunguko wa biashara kuwepo katika vijiji hivyo.

Mheshimwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, swali la nyongeza.

2 NOVEMBA, 2022

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Wizara kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Wilaya yangu kuna vikundi vya vijana ambao wamejiunga pamoja katika shughuli mbalimbali za utafutaji na uchimbaji wa madini. Kuna vikundi kama Chugu, Chiswala na wanaapolo *group*, changamoto walionayo ni ukosefu wa vitendeakazi sahihi vya uchimbaji. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia vijana hawa vitendea kazi ili nao waweze kupata mapato halali ya kuwezesha kujikimu kimaisha? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi yake au Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*), limeingia makubaliano na Taasisi za Kifedha hapa nchini, ikiwepo benki ya *NMB*, *CRDB*, *KCB* na Benki hizi zimeanza kutoa mikopo ya kuwawezesha wachimbaji wadogo. Hadi sasa zimeshatoa jumla ya Shilingi Bilioni 36 ambazo zimepopeshwa na inaendelea na jitihada ya kuzungumza na taasisi hizi ili waweze pia kutoa msaada wa vifaa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara inaendelea kuhakikisha uchimbaji mdogo unaendelea kurasimishwa nchini na katika mwaka wa fedha 2021/2022 tumeweza

2 NOVEMBA, 2022

kutoa leseni za uchimbaji mdogo 6,000. Niendeleo kumuomba Mheshimiwa Mbunge, kwamba ahamasishe vikundi katika Jimbo lake, wajipange na waweze kufuatila uwezekano wa kupata mikopo hiyo kupitia mabenki ambayo tumeingia makubaliano nao kupitia STAMICO. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, sasa aulize swali lake.

Na. 30

Kutoa Kipaumbele cha Ajira kwa Vijana Waliopitia JKT

MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kutoa kipaumbele cha ajira kwa Majeshi yote nchini kwa Vijana waliohitimu JKT?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo: -

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2013 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa maelekezo kwa Wizara zote pamoja na Vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana waliohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Utaratibu huo umekuwa ukitekelezwa na Vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kuanzia mwaka 2013 yalipotolewa maelekezo hayo. Aidha, inakumbushwa kuwa lengo la mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwapatia vijana wa Tanzania elimu ya uzalendo, ujasiriamali na kujifunza stadi za kazi ili waweze kujijajiri mara wamalizapo mkataba. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, swali la nyongeza.

MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini na maswali mawili la nyongeza.

Swali la kwanza; agizo la Serikali kwa Wizara nyingine kutoa kipaumbele cha ajira kwa Vijana wa JKT limetekelezeka kwa kiwango gani tangu 2013?

Swali la pili; inafahamika kuwa malengo ya mafunzo ya JKT siyo ajira, bali ni kufundisha ujasiriamali na uzalendo. Je, Serikali haioni haja sasa kuaajiri kutoka JKT kwa kufuata mtiririko ule wa *first in first out*? Kwa maana operesheni ya mwanzo wawahi kuajiriwa kuliko wale wanaofuata ili kutovunja moyo vijana wetu wazalendo. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

2 NOVEMBA, 2022

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Antipas Mgungusi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la *first in first out*, huu ndiyo utaratibu ambao unatumika, lakini wakati mwingine kunakuwa kuna uhitaji wa utaalum maalum au sifa maalum, kwa hiyo pamoja na kwamba mfumo wa *first in first out* unatumika, unaweza ukatumia mfumo huu lakini kundi la kwanza usipate watu wenye zile sifa maalum ambavyo Vyombo Vyetu vya Ulinzi na Usalama wanatafuta, kwa hiyo unalazimika kwenda kwenye kundi la pili.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Mbunge nimeielewa na ndiyo maana hata Waheshimiwa Wabunge wengine wamepiga makofi wakiashiria kwamba ni swali la msingi. Kwa hiyo, tunachokifanya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa hivi nimeunda Kamati ambayo tunashirikisha Wizara mbalimbali hasa Wizara ambazo ni *productive sectors*. Wizara ya Kilimo, tayari tunashirikiana nao ninamshukuru Mheshimiwa Bashe, upande wa Kilimo cha kimkakati, tunashirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, tunataka tupanue mawanda au scope ya JKT kwa kushirikisha sekta nyingine. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Viwanda na Biashara na taasisi ambazo zipo chini ya Wizara hizi. Kwa mfano, *SIDO, VETA, TIRDO, TEMDO* lakini benki yetu ya *TADB*. Asilimia 10 za vikundi kwenye Halmashauri tukae pamoja kama Serikali tuwe na mkakati wa pamoja ambao

2 NOVEMBA, 2022

utashirikisha Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara hizi na Taasisi hizi ili kusaidia kutengeneza *commitment* ya ajira Milioni Nane ambazo tumeahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kupitia Jeshi la Kujenga Taifa kwa sababu tunaandaa vijana kwenye kujifunza stadi za kazi, basi kwa mawanda hayo tunaweza tuka-*absorb* vijana wengi zaidi ambao wanamaliza mafunzo ya kujitolea wanarudi nyumbani.(Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litauliza kwa niaba yake na Mheshimiwa Grace Tendega.

Na. 31

Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mkalama

MHE. GRACE V. TENDEGA K.n.y. MHE. JESCA D. KISHOA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Mkalama?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkalama ni Kituo cha Daraja A. Ujenzi wake ulianza mwezi Juni, 2015 na ulisimama kutokana na kukosekana kwa fedha. Katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi 467,148,000 ili kukamilisha ujenzi wa kituo hiko. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Wilaya ya Mkalama ina gari mmoja ambalo pia ni bovu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, wanapomaliza ujenzi wa kituo hicho wanawapa na nyenzo kama magari na pikipiki maalum?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Jimbo la Kalenga pia kuna kituo cha Polisi cha Kata ya Ifunda lakini hawana nyumba Askari hao na pia hawana magari, je, ni mkakati gani wa Serikali unao ili kuhakikisha kwamba kituo hiko kinapata nyumba za watumishi pamoja na magari?
(Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

2 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, kuhusu Kituo cha Mkalama baada ya kukamilika kupewa nyenzo za kutendea kazi ikiwemo magari, hilo ni wazi, gari lililopo kama ni bovu, kituo kitakapokamilika tutawapa gari ili waweze kutimiza majukumu yao vizuri. Kwa bahati nzuri tumeanza kupokea magari hayo na yameanza kugawiwa kule ambako kuna mahitaji makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kalenga, hii Kata ya Ifunda, kuwa na kituo ambacho hakina nyumba wala magari; tutawasiliana na uongozi wa Polisi wa Mkoa, nadhani ni Iringa hii, ili kuona kama wanalo eneo la kutosha basi waingize kwenye mpango wa ujenzi waweze kufikiriwa kujengewa. Nashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimwa Francis Mtinga, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Mkalama pamoja na kuwa Kituo hicho kimekuwa gofu muda mrefu lakini pia Askari ni wachache sana, katika Kata zote 17 ambazo zinamtawanyiko mkubwa, sehemu kubwa tunatumia mgambo. Serikali inatuambia nini kuhusu kutupatia Askari wapya katika mgao unaokuja. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

2 NOVEMBA, 2022

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Mtinga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wilaya nyingi hasa ambazo hazikuwa na Vituo vya Polisi, wamekuwa na Askari kulingana na uwezo wa vituo vilivyopo kuwabeba. Tunashukuru baada ya kupata ajira ya zaidi ya Askari 4,200 waliotoka kwenye mafunzo mwanzoni mwa mwaka huu, wameweza kugawiwa kwenye vituo hivi, vikiwemo mpaka ngazi za Kata. Naamini Mheshimiwa Francis anafahamu kwamba sasa hivi tunao Askari Kata ngazi ya Cheo cha Mkaguzi Msaidizi wa Polisi kwa ajili ya kusimamia usalama katika ngazi hizo. Kwa hiyo, naamini atakuwa amepata Askari hao kwenye Jimbo lake la Mkalama. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itamalizia Kituo cha Polisi cha Galapo ambacho iliahidi kwamba itatekeleza katika mwaka huu wa fedha 2022/2023?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Sillo, kama ifuatavyo: -

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tumeshazungumza juu ya jambo hili na Mheshimiwa Sillo, nimeahidi baada ya Bunge hili kutembelea eneo lile la Galapo kwa sababu ni eneo ambalo ni kubwa sana kibiashara linahitaji Kituo cha Polisi. Tumeingiza kwenye mpango wa kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ili wananchi wa eneo hilo waweze kupata huduma za usalama wa raia na mali zao.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Kata ya Nanjilini katika Jimbo la Kilwa Kusini, wamekamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi wakishirikiana nami Mbunge wao. Je, Serikali iko tayari kutoa maelekezo kupitia Bunge hili kwa Uongozi wa Polisi Mkoa wa Lindi ili wakakague kituo hicho na hatimae kupeleka Askari Polisi pale Nanjilini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassinge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze kwa kukamilisha ujenzi wa kituo hicho, hivyo ni wajibu wetu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hususan Jeshi la Polisi, kupeleka Askari. Kupitia Bunge lako naomba kuelekeza Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Lindi wafanye ukaguzi

2 NOVEMBA, 2022

kama kinakidhi wa wapangie Askari ili waweze kutoa huduma za usalama wa raia kwenye eneo hili la Nanjilini. Nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, Mbunge wa Vitu Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 32

Mauaji ya Vijana wa Kike – Zanzibar

MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru maisha ya vijana wa kike kwa kudhibiti wimbi la mauaji Visiwani Zanzibar?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saada Mansour Hussein, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kufuatilia kwa karibu matukio ya mauaji yanayotokea maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Zanzibar. Matukio haya tumebaini yanasababishwa na migogoro ya ardhi, wivu wa kimapenzi na migogoro ya ndoa, imani za kishirikiana, wananchi kujichukulia sheria mikononi, ulevi, na matukio ya uhalifu.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Oktoba 2022 jumla ya matukio manne (4) ya mauaji ya wanawake yametokea Zanzibar. Matukio haya yamehusishwa na wivu wa mapenzi na migogoro katika ndoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kutoa elimu kwa jamii kufuata sheria za nchi na njia sahihi za kutatua migogoro ya aina hiyo. Tunawashauri wahusika kuzishirikisha familia zao, viongozi wa dini, viongozi wa jamii, viongozi wa siasa, wazee wa mila, watu maarufu na wenye ushawishi katika jamii pamoja na Ofisi za Serikali za Mitaa ili kupunguza athari za migogoro hiyo. Aidha, kwa migogoro inayoshindikana ifikishwe katika vyombo vya dola hususan Polisi na Mahakama ili kupata suluhisho la kisheria.

SPIKA: Mheshimiwa Saada Mansour Hussein, swali la nyongeza.

MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni hatua gani zilizochukuliwa na Serikali hadi sasa kwa wote waliohusika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YANCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saada Mansour Hussein kama ifuatavyo: -

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, watuhumiwa wa mauaji haya yaliyotokea Zanzibar, wote walikamatwa na kesi zao zinaendelea mahakamani. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Wizara ya maliasili na utalii, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, sasa aulize swali lake.

Na. 33

Kupunguza Msitu wa Mbiwe kwa Matumizi ya Kiuchumi

MHE. MASACHE N. KASAKA aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kupunguza eneo la Hifadhi ya Msitu wa Mbiwe ili litumike kwa matumizi ya wananchi na shughuli za kiuchumi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masache N. Kasaka, Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzishwa hifadhi hiyo ni kulinda bayoanuai zilizomo ndani ya hifadhi ikiwemo vyanzo

2 NOVEMBA, 2022

vya maji vinavyotumika kwa matumizi ya binadamu na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Serikali haioni haja ya kupunguza eneo la hifadhi ya Msitu wa Mbiwe. Aidha, Sheria ya Misisitu inaruhusu uchimbaji wa madini ndani ya hifadhi kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizopo kwa njia endelevu.

SPIKA: Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, swali la nyongeza.

MHE. MASACHE N. KASAKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana; nimeyapokea majibu ya Serikali. Kwa kuwa kwenye jibu la msingi amesema Serikali inaruhusu shughuli za kiuchumi kuweza kufanyika kwenye eneo la misitu zikifuata sheria, lakini sheria hizi zimekuwa ngumu sana kwa wachimbaji wadogo hawa kuweza kuzi-meet ili waweze kupata hivi vibali. Je, serikali haioni haja sasa kuweza kupunguza masharti ya kutoa vibali vya kuingia ndani ya misitu ili wananchi wetu hawa waweze kupata vibali hivyo waweze kufanya shughuli zao za uchumi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali imekuwa inaendesha zoezi la kuweka *beacon* katika mipaka kati ya vijiji pamoja na hifadhi. Zoezi hili limeweza kufanyika katika Kata za Mafyeko, Kambikatoto pamoja na Matwiga. Zoezi hili limeweza kufanyika bila kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika.

Je Serikali haioni haja sasa kuweza kuweka bikon zile upya katika maeneo yale ya mipaka ya asili ili wananchi

2 NOVEMBA, 2022

hawa waweze kufanya shughuli zao vizuri bila kuleta taharuki?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masache N. Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza aliloliongelea Mheshimiwa Mbunge, kuhusu kupunguza masharti ili kuruhusu wachimbaji wadogowadogo waweze kuingia katika maeneo yaliyohifadhiwa. Nimtaarifu tu Mbunge kwamba, masharti haya tuliyoyaweka, yanazingatia pia kuhifadhi maeneo ya misitu na masharti haya kwa wachimbaji wadogowadogo tumeyaweka ni machache sana.

Mheshimiwa spika, kwa mfano, kwa ridhaa yako napenda tu nielezee kuhusu suala la masharti ya wachimbaji wadogowadogo ambao wanapaswa kupata leseni. Pia wanatakiwa kufanya *Environmental Protection Plan (EPP)*, ambayo huwa haifanani na *EIA*, ni masharti madogo ambayo yanamfanya mchimbaji aweze kufuzu ili aweze kupata kibali cha kuingia kuchimba. Kwa hiyo sisi tunaona masharti haya ni nafuu sana na tunaendelea kuhamasisha wananchi kwamba tunapohifadhi ni kwa ajili ya uhifadi endelevu na wakati huo huo tunaruhusu shughuli za uchimbaji ndani ya hifadhi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwenye hili zoezi la *beacon*, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapokuwa tunaweka mipaka, tunashirikisha pia Wizara ya Ardhi, ambapo wanakuwepo wapima ardhi ambao wanazisoma na kutafasiri ramani ambazo zinaonyesha ramani kamili ya hifadhi husika. Endapo kama kuna mgogoro uliojitokeza, basi nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutawashirikisha tena Wizara ya Ardhi ili tujiridhishe na wananchi kwamba mipaka hii ni sahihi ama siyo sahihi. Kama itaonekana bikon zimewekwa nje ya mipaka hiyo, basi tutafanya marekebisho. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 34

Ongezeko la Watoto wa Mitaani

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia watoto wa mitaani ambapo kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: alijibu:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika; kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na ongezeko la watoto wa mitaani hivi karibuni. Hii inatokana na sababu mbalimbali za kifamilia.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza watoto wa mitaani Serikali inafanya mikakati ifuatayo;

Kuimarisha Kamati za Ulinzi na Usalama wa Wanawake na Watoto katika ngazi za jamii ambapo hadi sasa kuna jumla ya Kamati 18,186 katika ngazi za taifa, vile vile kutoa elimu kwa wazazi au walezi kuhusu malezi chanya ya watoto kupitia Ajenda ya Taifa ya uwajibikaji wa Wazazi katika malezi ya watoto kwenye familia. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikifanya zoezi la kuwatambua na kuwaondoa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani kwa kuwarudisha katika familia zao.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watoto ambao familia zao hazipatikani Serikali imekuwa ikiwapeleka katika makao ya watoto yanayomilikiwa na Serikali na yale yanayomilikiwa na taasisi binafsi, ambako wanapata huduma zote za msingi ikiwa ni pamoja na kuwaandalia mazingira ya kujitegemea kutokana na uwezeshaji wa elimu ya ufundi na mitaji ya kuanzia maisha.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa viongozi na jamii kwa jumla kutimiza wajibu wao katika kuimarisha malezi chanya ya watoto katika familia.

SPIKA: Mheshimiwa Taska Mbogo, swali la nyongeza.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, watoto hawa wa mitaani ndio watoto ambao wanazalisha makundi kama panya *road*, damu chafu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inazo nyumba za kulelea hawa Watoto. Ningeomba kujua Serikali ina vituo vingapi vya kulelea watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Nchi yetu ya Tanzania imesaini mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu Watoto. Kwa mfano *The UN Convention on the Right of the Child* na mkataba wa Afrika wa *The African Charter on the Right of the Child*. Swali langu; je, Serikali inamkakati gani wa kuhakikisha kwamba watoto wa Tanzania ambao wako mitaani wanapata elimu ambayo ni haki yao pamoja na kujua haki zao za msingi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa

2 NOVEMBA, 2022

Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Taska kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inavituo viwili vya kulea Watoto ambavyo inavimiliki. Vituo hivyo ni Kurasini ambacho kipo Dar es Salaam na Kikombo ambacho kipo Dodoma. Vituo hivyo vina idadi ya Watoto 142 ambapo 88 wakiwa ni wakiume na 54 ni wa kike.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, watoto wote ambao wanalelewa katika vituo vya watoto ambavyo vinamilikiwa na Serikali wanapata haki zote za msingi ikiwemo elimu ya msingi, sekondari, vyuo vikuu na elimu ya ufundi (VETA). Wanapomaliza wanapewa vifaa maalum vya kujiendeleza ili waweze kujijiri wenyewe. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Julilana Masaburi, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. MASABURI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kumekuwa na wimbi kubwa la wazazi kuwafanyia vitendo vya kikatili watoto. Je, Serikali inampango gani wa kuwajengea watoto uwezo au uelewa mashuleni wa kujitetea pindi wanapopitia ukatili wa kijinsia?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika kukubaliana na hili, Serikali inatekeleza afua mbalimbali za kutoa elimu za malezi na makuzi, pamoja na elimu ambayo inakabiliana na ukatili dhidi ya watoto. Aidha, kuimarisha Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wanawake na watoto zilizopo ngazi zote nchini kwa ajili ya kuwa elimu wananchi wa jamii yetu.

SPIKA: Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Watoto wa mitaani hususani watoto wa kiume wamekuwa wakipitia unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia hususan suala la kulawitiwa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuchukua hatua za haraka ikiwemo mabadiliko ya sheria ili kuweka sheria kali na za mfano kwa watu wanaotenda vitendo vya ulawiti kwa watoto?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na ukatili kwa watoto ambao wanalawitiwa. Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, pamoja na maafisa wetu wa maendeleo na ustawi wa jamii, tunahakikisha kwamba, watuhumiwa wote ambao wanafanya vitendo vya ukatili kwa watoto wetu wanachukuliwa hatua kali pale inapostahiki. Ahsante.

2 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi!)*

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, swalli lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Esther E. Malleko.

Na. 35

Serikali Kuweka Fedha Katika Benki za Kibiashara

MHE. ESTHER E. MALLEKO K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. DAVID aliuliza: -

Je, ni lini Benki Kuu itaweka utaratibu mzuri kwa Serikali na taasisi zake kuweka fedha katika Benki za biashara ili kuwa na mzunguko mzuri wa fedha?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa wa Serikali na taasisi zake kutunza fedha za Benki Kuu ni mzuri na wa uwazi zaidi kwa kuwa unachochea ukuaji wa huduma jumuishi za

2 NOVEMBA, 2022

kifedha. Aidha, mfumo wa sasa unaiwezesha Serikali kusimamia kwa ufanisi utulivu wa uchumi jumla, hususan sarafu yetu na mfumuko wa bei nchini ambao ni msingi wa ukuaji endelevu wa uchumi jumuishi. Vilevile, utaratibu wa sasa unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwanini Serikali isipunguze riba inapokopesha benki za biashara ili gharama hizo ziweze kushuka na Watanzania wengi waweze kukopa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwanini Serikali isipunguze riba inapouza hati fungani ili Watanzania wengi waweze kupeleka fedha zao katika benki hizo kama *fix deposit*.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majiibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Malleko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, viwango vya riba vimepungua kwa asilimia 16.60 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 16.41, mwaka 2022 ili kuwezesha benki kukopesha wananchi kwa riba nafuu na kupunguza mikopo chechefu.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, riba za hatifungani haziwekwi au kupangwa na Benki Kuu ya Tanzania bali ni matokeo ya mchakato wa mauzo na ununuzi wa hatifungani kutoka soko la fedha linaloendeshwa kwa mfumo wa soko huria. Hata hivyo, takwimu za karibuni zinaonesha kuwa riba za hatifungani zimepungua.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Ahmed Salum, Mbunge wa Solwa sasa aulize swali lake.

Na. 36

**Ujenzi wa Barabara ya Mwanangwa – Mwakitolyo
Hadi Bulige**

MHE. AHMED A. SALIM aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mwanangwa – Mwakitolyo hadi Bulige Wilayani Kahama kama ilivyodainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salim, Mbunge wa Solwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mwanangwa – Mwakitolyo hadi Bulige yenye urefu wa kilomita 118.8 ni sehemu ya barabara itokayo Mwanangwa – Misasi - Salawe – Solwa - Kahama yenye urefu wa kilomita 148.8. Serikali tayari imeanza ujenzi kwa awamu ambapo kilomita 5.65 kuanzia Kahama kuelekea Solwa na sehemu ya mita 450 katika mji wa Bulige zimekamilika kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, kiasi cha Shilingi milioni 750.62 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kilometa 1.2. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ahmed Ally Salim, swali la nyongeza.

MHE. AHMED A. SALIM: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana, inaunganisha wilaya tatu, kwa maana ya Kahama, Shinyanga pamoja na Misungwi, na kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni mazuri lakini kwa namna ambavyo wameanza, ni jambo jema sana na namshukuru sana kwa sababu hatua za awali zinaonesha kwamba barabara hii tayari imeanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kilometa 5.6, ukienda kwa utaratibu huu...

SPIKA: Swali Mheshimiwa.

2 NOVEMBA, 2022

MHE. AHMED A. SALIM: Mheshimiwa Spika, kama Serikali itaendelea kujenga kilometa 5.6, maana yake tutachukua zaidi ya miaka 20 kwenye ukamilishaji wake. Swali la kwanza; je, mwaka huu wa fedha kwanini Mheshimiwa Naibu Waziri, au Wizara hii isiongeze fedha angalau kilometa zaidi ya 20 au 30 ili barabara hii iweze kuonyesha mwelekeo wa kukamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara hii, ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi wa 2015-2020 na 2020-2025, ilani ya chaguzi mbili na kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana. Je, kwanini Serikali isiweke na kuonesha *commitment* kabisa ya moja kwa moja, ikatenga fedha kwenye ukamilishaji wa barabara hii, ikajengwa mpaka kukamilika kwake kabisa kabla ya mwaka 2025?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ahmed Ally Salim, Mbunge wa Solwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Solwa, kwa jinsi anavyofuatilia ujenzi wa barabara hii; na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunachokifanya ni kile ambacho tumekipata na fedha inayopatikana kwa kiasi chochote sisi tutaendelea kujenga, tunapunguza.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuijenga barabara hii mihimu ambayo ni njia ya mkato kutoka Mwanza kwenda Kahama. Kama alivyoainisha, imeainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi. Tunaamini ndani ya mwaka huu, katika miaka inayokuja, barabara hii itatengewa fedha ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kadri fedha itakavyopatikana. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Festo R. Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali langu dogo la nyongeza, barabara ya Makete-Mbeya-Isionji, ni barabara ambayo tayari upembuzi yakinifu, hatua za manunuzi, na hata upekuzi wa kampuni iliyoshinda umeshafanyika. Mheshimiwa Waziri mbele ya Mheshimiwa Rais alituahidi mwezi wa tisa mkandarasi atafika *site*.

Je, ni lini mkandarasi atasaini mkataba ili aanze kujenga barabara hii ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Wilaya ya Makete?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara anayoitaja Mheshimiwa Festo ilitangazwa, lakini ilikosa Mkandarasi kwa sababu ya

2 NOVEMBA, 2022

udogo, Mheshimiwa Rais akaongeza kilomita. Barabara hii ilishatangazwa na tayari mikataba imeshaandaliwa. Tunapoongea sasa hivi iko kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kuifanyia *vetting* na tunategemea mara itakapotoka mwezi huu, basi mikataba hiyo itasainiwa ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 37

Ujenzi wa Bandari Kavu – Kigoma

MHE. SYLVIA F. SIGULA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Bandari Kavu katika Mkoa wa Kigoma?

SPIKA: Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Bandari Kavu umepewa kipaumbele katika Mpango Kabambe wa Mamlaka ya Bandari Tanzania ulioanza 2009 na utaisha 2028. Mpango

2 NOVEMBA, 2022

huo umeziainisha Bandari Kavu za King'ori iliyoko mkoani Arusha, Ihumwa (Dodoma), Inyala (Mbeya), Shinyanga (Isaka), Fela (Mwanza), Katosho (Kigoma), Kwala (Pwani) na Songea kuwa bandari za kipaumbele kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa shehena katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia TPA imetenga fedha kwa ajili kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa bandari hizo ikiwemo ya Katosho ilioko mkoani Kigoma. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu inatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2023. Kukamilika kwa kazi hiyo kutapelekea manunuzi ya Mkandarasi wa ujenzi wa bandari hiyo ambayo ni muhimu kwa kuhudumia shehena za nchi jirani za ukanda wa Ziwa Tanganyika. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali la nyongeza.

MHE. SYLVIA F. SIGULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwanza kwa majibu mazuri ya Wizara, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Katosho wamepisha eneo la ujenzi wa bandari ya nchi kavu kwa zaidi ya miaka sita sasa na majibu haya ya usanifu yamekuwa yakitolewa kwa zaidi ya miaka sita na kuwaumiza sana wananchi: Je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kuharakisha huu upembuzi yakinifu ili eneo hilo lifanyiwe kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ili bandari ya nchi kavu iweze kuwa na tija kwa Taifa lazima kuwe kuna

2 NOVEMBA, 2022

miundombinu wezeshi ikiwemo uwepo wa reli, uwepo wa meli, uwepo wa mabehewa ya kutosha na barabara za uhakika. Ukizingatia Mkoa wa Kigoma bado tuko nyuma sana kimiundombinu:-

Mheshimiwa Spika, nini mpango wa Serikali kuhakikisha miundombinu wezeshi inatekelezeka ili bandari hii iwe na tija? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bandari hii imechukua muda mrefu, lakini tangu mwaka 2019 tulijenga uzio ama ukuta wa eneo hili. Nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Kigoma kwamba ifikapo Aprili mwakani 2023 upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unakwenda kukamilika na tayari tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari hii.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili angependa kufahamu miundombinu wezeshi katika kufanikisha bandari yetu kavu na miundombinu hiyo wezeshi ni pamoja na reli, barabara na kupata mzigo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, bandari hii kavu tayari ipo karibu kabisa na bandari nyingine ya Kigoma, pia ipo karibu kabisa na barabara kuu inayokwenda Kigoma Mjini. Pia

2 NOVEMBA, 2022

tumewaelekeza mamlaka ya bandari nchini pamoja na TRC, wapo kwenye majadiliano kwa ajili ya kupeleka reli ili iwe rahisi kupeleka mzigo utakaokuwa unahudumiwa na nchi rafiki na nchi jirani kati ya Congo, Rwanda, Burundi pamoja na Zambia. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, Mbunge wa Tandahimba sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Na. 38

Mradi wa Maji wa Mkwita – Tandahimba

MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MHE. KATANI A. KATANI
aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa maji wa Mkwita utakamilika ili kupunguza tatizo la maji katika Kata ya Mangombya, Mkwiti na Litehu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwa niaba ya Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Katani Ahmed Katani Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa maji wa Mkwiti utakaohudumia Kata za Mangombya, Mkwiti na Litehu zenye jumla ya vijiji 16. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu nne ambapo awamu ya kwanza na ya pili zimekamilika na ilihusisha ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa kilometa 13 na ufungaji wa pampu kwenye chanzo. Utekelezaji wa awamu ya tatu na ya nne unaendelea na umefikia asilimia 50 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022. Kazi zinazofanyika ni pamoja na ujenzi wa matanki sita yenye jumla ya ujazo wa lita 300,000, ulazaji wa bomba lenye urefu wa kilometa 89 na ujenzi wa vioski 48 vya kuchotea maji. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kimsingi ninachotaka kufahamu ni kwamba mradi huu utakamilika lini? Kwa sababu kumekuwa na tatizo kubwa sana la maji kwenye Wilaya ya Newala, Tandahimba pamoja na Nanyamba hasa zaidi wakati wa kiangazi ambacho ndiyo tunakwenda sasa hivi. Sasa nataka kufahamu ili kuwapa *comfort* wananchi, mradi huu utakamilika lini ili waweze kupata maji safi, salama na ya kutosha?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi, nimeeleza kuwa awamu ya tatu na ya nne itakamilika mnamo mwezi Desemba, mwaka huu wa 2022.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kavejuru Eliadori Felix, Mbunge Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 39

**Mazingira Bora ya Uwekezaji Kwenye Kilimo
cha Michikichi – Kigoma**

MHE. KAVEJURU E. FELIX aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kuweka Mazingira bora ya uwekezaji kilimo cha Michikichi pamoja na kiwanda cha kuchakata mafuta – Kigoma?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Felix, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuongeza uzalishaji wa mbegu za michikichi, Serikali imeanzisha Kituo Maalum cha Utafiti wa Zao la Michikichi cha TARI Kihinga, mkoani Kigoma ili kuendeleza zao hili kwa ufanisi. Vile vile, Serikali kupitia Wizara yangu, imepanga kujenga viwanda viwili vidogo vya kuzalisha mafuta ya mawese katika Kijiji cha Nyamuhoza kilichopo Wilaya ya Kigoma (DC) na Kijiji cha Sunuka kilichopo Wilaya ya Uvinza.

Mheshimiwa Spika, juhudi zote hizo zimeleza kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwenye zao la michikichi mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix swali la nyongeza.

MHE. KAVEJURU E. FELIX: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa michikichi mkoani Kigoma, viwanda vidogo vidogo havitoshelezi kuchakata mafuta na bidhaa zinazotokana na zao la chikichi: Je, Serikali ina mikakati gani ya kuleta viwanda vya kati na vikubwa mkoanii Kigoma (*secondary and tertiary industry*)? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Serikali ina mipango gani ya kutenga maeneo ya viwanda vya kati na vikubwa katika wilaya zote za Mkoa wa Kigoma? (Makofi)

2 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kavejuru Felix, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Kavejuru kwa ufuatiliaji mkubwa kuhusiana na zao la chikichi na mnyororo mzima wa thamani katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ni kweli jitihada zilizopo ilikuwa ni kuanza na viwanda hivi vidogo ambavyo vilikuwa vinakidhi mahitaji wakati ule uzalishaji wa michikichi ulipokuwa katika hali ya chini kwa maana ya malighafi. Sasa juhudi kubwa zimefanywa na Serikali, tunaamini tuna malighafi ya kutosha, kwa hiyo, mipango ya Serikali sasa ni kuanza kuvutia wawekezaji wakubwa ili waweze kuwekeza katika viwanda vitakavyochakata mnyororo mzima wa thamani wa mchikichi katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, hii ni pamoja na kuboresha miundombinu. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba sasa tumeshapata umeme wa *grid* ya Taifa katika Mkoa wa Kigoma ambayo ilikuwa ni moja ya kikwazo, pia barabara zinaboreshwa ambavyo ni vitu muhimu sana kwa ajili ya kuvutia wawekezaji. Kwa hiyo, tunaendelea kuweka mazingira wezeshi na bora kwa ajili ya uwekezaji katika mikoa ya pembezoni ikiwemo Mkoa wa Kigoma.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutenga maeneo ya uwekezaji kwenye kilimo pia na maeneo ya kujenga viwanda, kwanza nimshukuru sana kwa ushauri wake. Sisi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tunaendelea kutenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya mashamba makubwa. Pia niwaombe Serikali za Mkoa na Halmashauri ili waendeleo kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji, kwa sababu hii ni endelevu, tunatakiwa tuwe na maeneo sahihi na yenye miundombinu wezeshi ili wawekezaji wakubwa wanapokuja kuwekeza viwanda hivi wasihangaikie tena kupata ardhi ambayo wakati mwingine inakuwa mgogoro mkubwa kwa ajili ya kuweka viwanda hivi vikubwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Serikali ina mkakati gani wa kujenga kiwanda cha kukamua mchuzi wa zabibu ili kuweza kuondoa adha ya wakulima wa zabibu wa Mkoa wa Dodoma wanaotembea na mabeseni barabarani wakitembeza zabibu na kuiuza bila faida yoyote? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti Majala, kuhusiana na sekta ya kilimo hasa kwenye zao la zabibu.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshaanza juhudi mbalimbali za kusaidia kuchakata zabibu ili ziweze kuwa katika hali ya mchuzi wa zabibu anaosema, ambapo tayari kuna wadau mbalimbali wameshaanza kuchukua, wakiwemo kiwanda cha Jambo ambao wapo Shinyanga. Vilevile wengine wameshaanza kuchukua zabibu hizo ambazo naamini wadau hawa ambao tumewahamasisha watapunguza adha ya kutembea kuuza zabibu ambazo hazijachakatwa ambazo wakulima wenzetu wa Mkoa wa Dodoma wanahangaika nazo. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na Serikali kuweza kutoa majibu. Sasa nilete matangazo kwenu yaliyoko hapa mbele. Wabunge wanaotembea naomba mketi, ahsante sana.

Tutaanza na tangazo la wageni walioko Bungeni siku ya leo. Kwanza ni wageni 17 ambao wako Jukwaa la Spika kutoka *Living Together Autistic Foundation (Li-TAFO)* taasisi kutoka Jijini Mwanza inayojihusisha na watu wenye usonji wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Mhandisi Shangwe Mgaya. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali; kwanza ni wageni watano wa Mheshimiwa Dennis Londo ambao ni wananchi kutoka Kata ya Uleling'ombe Jimbo la Mikumi Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

2 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni Wakurugenzi wa *Extramind Tanzania Company Limited* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga ambaye ni mfanyabiashara kutoka Makete Mkoa wa Njombe, Ndugu Fransisco Sangai Kamikaze, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mengine, moja ni tangazo linatoka kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa kuwa ,Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)...

Mheshimiwa Waziri naona umesimama, una jambo?

Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge, kwamba Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), watatoa huduma ya upimaji wa afya kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi katika Kituo chetu cha Afya kilichopo hapa Bungeni, Jengo la Utawala Annex. Zoezi hili litaanza leo tarehe 2 Novemba, 2022. Upimaji huo utahusu magonjwa yafuatayo; magonjwa ya moyo, magonjwa ya ndani (kisukari, figo na ini), uchunguzi wa magonjwa ya mifupa na mgongo, uchunguzi wa magonjwa ya kinywa na meno, uzazi na magonjwa ya wanawake. Zoezi hili linashirikisha Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Magonjwa ya Moyo ya JKCI na Taasisi ya Mifupa (MOI).

2 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine pia linatoka kwa Katibu wa Bunge, mnatangaziwa wale ambao bendera za magari yao zimechakaa na wanahitaji kubadilisha bendera hizo, basi wafike chumba namba 209 ghorofa ya pili jengo la Utawala ili waweze kupewa bendera mpya.

Waheshimiwa Wabunge, nimesimama hapa mbele, nasikia minongono mingi kabisa, mnaongea. Sikilizeni yanayosemwa hapa mbele, mengi yanawahusu.

Sasa nitoe mwongozo ambao aliombwa jana na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava kuhusu maswali yake aliyokuwa ameuliza jana.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 1 Novemba, 2022 katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Tisa wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava aliomba Mwongozo wa Spika kwa maelezo kwamba swali lake la pili la nyongeza halikujibiwa kikamilifu na Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava aliuliza swali la msingi namba 15 kwa Wizara ya Afya kwamba; je, nini chanzo cha vifo kwa akinamama wanaojifungua kwa njia ya upasuaji siku chache baada ya upasuaji? Swali hilo lilijibiwa na Naibu Waziri kama ifutavyo, nanukuu; “Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa vifo vinavyotokana na uzazi uliofanywa na Wizara ya Afya kuanzia mwaka 2018 hadi 2021 umeonesha kuwa vifo ambavyo vilisababishwa na matatizo ya dawa za ganzi/nusu kaputi na upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni ni

2 NOVEMBA, 2022

58 (3.3%) mwaka 2018, vifo 80 (4.8%) mwaka 2019, vifo 65 (4.0%) mwaka 2020, na vifo 65 (4.1%) mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, sababu kuu za vifo hivi ni nne ambazo ni ajali ya dawa za ganzi/ nusu kaputi, kupoteza damu wakati au baada ya upasuaji, tatizo la damu kuganda na maambukizi ya bakteria baada ya upasuaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma inatekeleza mkakati wa kuwajengea uwezo watumishi wa Vituo vya Huduma za Afya kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali za Taifa katika eneo la utoaji ganzi/nusu kaputi na upasuaji kwa usalama kwa kuzingatia miongozo ya Wizara.” Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Christina Mnzava aliruhusiwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambapo aliuliza nanukuu; “Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umesema kwamba Wizara imeshafanya ufuatiliaji wa hivyo vifo na sababu zake, na moja ya sababu ni kutokana na matatizo ya dawa za ganzi/nusu kaputi; je, kuna watumishi wa kutosha wa kutoa dawa za nusu kaputi katika vituo vyetu vya afya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa mwaka 2021 ni 4.1% ya akinamama waliopoteza maisha baada tu ya kujifungua kwa *operation*.

Je, kuna utafiti wowote ambao Wizara imeufanya ili kubaini sasa ni dawa gani ambazo zinasababisha akinamama wanapoteza maisha?

2 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimwa Naibu Waziri alijibu maswali hayo pamoja na mambo mengine alisema, nanukuu; “Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

“Moja, anasema kama tuna uhakika wa kuwa na watalam wa kutoa dawa ya nusu kaputi kwenye nchi. Juzi mlisikia Mheshimiwa Waziri wa Afya akieleza kuhusu mkakati wa Rais wetu Samia Suluhu Hassan ametoa bilioni nane kwa ajili ya kusomesha wataalam 524 kwa mwaka huu. Mojawapo ya eneo linaloangaliwa ni eneo hilo. Kwa kweli kuanzia kwenye hospitali zetu za Wilaya kushuka chini kumekuwepo na wachache, lakini kwa wanaofaulu kumaliza mwaka huu wataenda kumaliza kupunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa sana.

Swali lake la pili, baada ya uchunguzi wetu kwamba imegundulika nini na tunatakiwa kufanya nini katika eneo hilo la kupunguza vifo vya akinamama; moja ndio maana unaona kuna eneo hili la kusomesha, imefanyika kazi kubwa sana, lakini baada ya Serikali yetu kutoa zile fedha za tozo, vituo vya afya 238 vimejengwa kwa mwaka huu tu peke yake. Pia mwaka huu ambulance 663 zinaenda kununuliwa, nazo mnajua zinavyokwenda kuweza kupunguza kwenye eneo hilo la vifo vya akina mama na watoto.” Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na majibu hayo, Mheshimiwa Dkt. Christina Mzava aliomba Mwongozo wa Spika, akizungumzia Kanuni ya 53(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2020, akieleza pamoja na mambo

2 NOVEMBA, 2022

mengine kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya hayaendani na swali lake la pili la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maombi hayo ya mwongozo huo, nilitoa majibu kuwa nitapitia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) ili niweze kufahamu kama swali la pili la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge Dkt. Mnzava iwapo lilijibiwa kikamilifu na kama sivyo basi apatiwe fursa ya kujibiwa upya wakati mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, nimepitia Taarifa Rasmi za Bunge na nimeona maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Dkt. Christina Mnzava. Aidha, nimepitia majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel kwa swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava. *Hansard* inaonyesha kuwa swali la pili la nyongeza lilitokana na maelezo ya Serikali kuwa Mwaka 2021 ni asilimia 4.1 ya akina mama walipoteza maisha baada tu ya kujifungua kwa *operation*, hivyo Mheshimiwa Mnzava alipenda kujua iwapo kuna utafiti wowote ambao Wizara imeufanya ili kubaini dawa zinazosababisha akinamama kupoteza maisha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, swali hilo lilijibiwa na Mheshimiwa naibu Waziri wa Afya ambapo alieleza kuwa Serikali inafanyia kazi tatizo la vifo vya akinamama na watoto. Aidha, alifafanua kwamba zaidi ya mafunzo yanayotolewa juu ya matumizi sahihi ya dawa Serikali imejenga Vituo vya Afya 238 na vile vile *ambulance* 663 zitanunuliwa ili kupunguza tatizo hilo.

2 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutafakari maombi ya Mwongozo huu na baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 51 na 53 ya Kanuni za kudumu za Bunge za Mwaka 2020, kuhusu maswali ya nyongeza, nimeridhika kuwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya hayakukidhi kiu ya Mheshimiwa Mnzava kupata majibu ya swali lake kikamilifu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoieleza swali lililenga kujua iwapo utafiti umefanyika ili kubaini aina ya dawa za usingizi zinazosababisha akinamama kupoteza maisha. Majibu ya Mheshimwa Waziri kwenye swali hilo yalitoa ufafanuzi wa namna Serikali ilivyoweka jitihada za kupunguza vifo kwa kujenga vituo vya afya na kununua *ambulance*, majibu ambayo si ya kuridhisha kwa swali liloulizwa.

Kutokana na upungufu huo, naelekeza kwamba swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava lipatiwe majibu kikamilifu hapo litakapopangwa wakati mwingine. Huo ndio muongozo wa Spika kuhusu jambo hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo na kutoa mwongozo huu, sasa tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

NDG RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

2 NOVEMBA, 2022

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali
(Na.3) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous
Amendments) (No. 03) Bill, 2022*)**

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada kusomwa kwa mara ya pili na hivyo nimwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Feleshi Mbuki.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwakuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 03) Bill, 2022*).

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba uniruhusu nitoe shukurani zangu kwako pamoja na Bunge lako Tukufu. Serikali yote chini ya uongozi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Mawaziri wote na viongozi wote kwa ujumla katika nyanja mbalimbali, kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote hiki kwa utumishi wangu kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kufikisha kwako salamu za rambirambi kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Mkoa wa Mjini Magharibi, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, kilichotokea Zanzibar tarehe 13 Oktoba, 2022. Naomba utufikishie salamu

2 NOVEMBA, 2022

hizi kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa na watu wote waliofikwa na msiba huu. Mungu ailaze roho ya Marehemu mahala pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu vyema na kwa umahiri mkubwa. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayofanya katika kusimamia shughuli mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Sita kwa weledi na umahiri mkubwa. Hongereni sana na Mwenyezi Mungu aendeele kuwabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao vya mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Naishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nanelwa Joyce Mwihambi *(ndc)* na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa uteuzi wako, kuwa Mwenyekiti wa Kundi la Kijiografia Kanda ya Afrika la Umoja wa Mabunge Duniani, (*Chairperson of the African Geopolitical Group Inter-Parliamentary Union - IPU*). Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Dkt. Boniface Nalija Luhende kuwa Wakili Mkuu wa Serikali na Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Nawaahidi ushirikiano wangu na wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa, kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bwana Onorious John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunatambua na tutaendelea kuhakikisha tunaendeleza majukumu yetu kwa weredi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya Nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti,

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kuupitia Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioalikwa na Kamati na kisha kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu. Moja ya mashauriano baina ya Serikali na Kamati hii ni kuondoa katika Muswada mapendekezo ya kurekebisha Sheria Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226 ili yaweze kufanyiwa kazi zaidi kwa kuzingatia maoni ya Kamati na wadau kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 03) Bill, 2022)* unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Saba. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha ni kuboresha utekelezaji wa masharti ya Sheria husika pamoja na kuondoa upungufu uliobainika katika utekelezaji wa masharti mbalimbali ya sheria hizo. Baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika Muswada huu, ni kubadilisha vifungu vya sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu na kuviandika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebisha kupitia Muswada huu kama ulivyowasilishwa

2 NOVEMBA, 2022

Bungeni kwa mara ya kwanza mnamo 23 Septemba, 2022, ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria ya Malikale, Sura ya 333 (*The Antiquities Act, Cap. 333*);
- (ii) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342 (*The Banking and Financial Institutions Act, Cap. 342*);
- (iii) Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 (*The Capital Markets and Securities Act, Cap. 79*);
- (iv) Sheria ya Madini, Sura ya 123 (*The Mining Act, Cap. 123*);
- (v) Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281 (*The National Museum of Tanzania Act, Cap. 281*);
- (vi) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 (*The Public Finance Act, Cap. 348*); na
- (vii) Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226 (*The Tanzania Commission for Science and Technology Act, Cap. 226*).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nane. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali ya sheria yanavyopendekezwa kurekebishwa katika Muswada.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Malikale, Sura ya 333 ambapo inapendekezwa kufanya marekebisho ya jumla kuhusu muundo wa kitaasisi ulioainishwa katika sheria hiyo ili kuendana na mabadiliko ya muundo wa sasa wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Mabadiliko ya muundo wa kitaasisi yanayopendekezwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Malikale badala ya Baraza la Kitaifa la Malikale kama ilivyo sasa katika sheria. Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambazo sheria hii inazisimamia.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 4, 11, 12, 13, 17 na 23 vinapendekezwa kurekebishwa kwa kumwondolea Mkurugenzi wa Malikale majukumu mbalimbali ya kiutendaji yaliyoainishwa katika vifungu hivyo ambapo inapendekezwa kuhamishia majukumu hayo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kutenganisha majukumu ya kiutendaji ambayo yanapaswa kutekelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa na majukumu ya kisera ambayo kimsingi yanapaswa kutekelezwa na Wizara kupitia kwa Mkurugenzi wa Malikale. Hatua hii itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Mkurugenzi Mkuu kama yalivyoainishwa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5 kinachohusu makatazo ya vitendo ambavyo havipaswi kufanywa kwenye malikale, kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa madhumuni ya kuweka kinga kwa Mkurugenzi Mkuu

2 NOVEMBA, 2022

wa Makumbusho ya Taifa dhidi ya masharti yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 5(1). Msingi wa kumpa Mkurugenzi Mkuu kinga hiyo unatokana na utekelezaji wa majukumu mapya yenye kinga hiyo ambapo awali Mkurugenzi Mkuu hakuwa anayatekeleza.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Vifungu vya 8, 10(3) na 17(6) vinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka rejea sahihi ya Bodi ya Makumbusho ya Taifa tofauti na ilivyo sasa ambapo Sheria bado inatambua Baraza la Wadhamini wa Makumbusho ya Taifa lililofutwa mwaka 1980 kupitia Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuongeza kifungu kipyua cha 17A ili kuweka masharti kuhusu usajili wa makumbusho yanayoanzishwa na taasisi, asasi au watu binafsi. Lengo la marekebisho haya ni kuyatambua na kuyarasimisha makumbusho yanayomilikiwa na taasisi, asasi au watu binafsi. Hatua hii inalenga kukuza ushiriki na kuboresha huduma zitolewazo na sekta binafsi katika kuhifadhi na kutunza malikale na hivyo kukuza utalii wa nchi na kuimarisha usimamizi na utunzaji wa malikale.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kuweka adhabu zinazozingatia ukubwa wa kosa lililotendwa kwani adhabu zilizopo kwa sasa imepitwa na wakati. Marekebisho haya yanakusudia kuongeza utii wa sheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali, inapendekezwa kurekebisha Jedwali lililopo katika sheria ili kufuta muundo

2 NOVEMBA, 2022

wa wajumbe wa Baraza la Kitaifa la Malikale na badala yake kuweka muundo wa Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Malikale.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342. Vifungu vya 3, 17, 21, 25 na 28 vinavyohusu mitaji ya mabanki na taasisi za fedha vinapendekezwa kurekebishwa ili kuiwezesha Benki Kuu kuweka viwango vya ukokotoaji wa utoshelevu wa mitaji ya benki na taasisi za fedha. Hatua hii itaiwezesha Benki Kuu kuhakikisha kuwa kila wakati viwango hivyo vinaendana na viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa sheria inadainisha viwango vinavyozingatia utoshelevu wa mitaji kwa kuzingatia vihatarishi kwenye mikopo na masoko na kuacha vihatarishi vingine. Kutokana na upungufu huo, sheria iliyopo haiwezeshi kutathmini kiwango sahihi cha mtaji wa benki au taasisi ya fedha husika. Aidha, sheria ilivyo sasa imeainisha kigezo kimoja tu cha upimaji wa ukwasi. Hivyo, marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kuwezesha utelekezaji wa viwango vipya vya upimaji wa utoshelevu wa mitaji ya benki na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka ulinganifu katika viwango vya upimaji wa utoshelevu wa mitaji ya benki na taasisi za fedha kulingana na viwango vya kimataifa. Aidha, maboresho yanayopendekezwa yanalenga pia kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ya fedha hususani sekta ndogo ya benki na masoko ya mitaji, kulinda amana za wateja, kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa watu wengi,

2 NOVEMBA, 2022

kuongeza uwezo wa taasisi za fedha na kuhamasisha utunzaji wa akiba, kukuza sekta ya benki yenye ufanisi na inayokidhi mahitaji ya watumiaji na yenye ushindani pamoja na kuboresha upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya biashara, miundombinu na makazi

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 kwa kuongeza kifungu kipya cha 134A kinachohusu wajibu wa watoa dhamana pamoja na hatua zinazoweza kuchukuliwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana dhidi ya mtoa dhamana atakayekiuka wajibu huo. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwapa watoa dhamana wajibu utakaohakikisha maslahi ya wawekezaji wenye hisa chache yanalindwa. Marekebisho haya yanalenga pia kuimarisha uwezo wa mamlaka kusimamia haki za wawekezaji wenye hisa chache na ushiriki wao katika kufanya maamuzi

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123, ambapo kifungu cha 7 kinarekebishwa ili kuongeza leseni ndogo ya uchenjuaji wa madini katika orodha ya leseni zinazotolewa chini ya sheria hii. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwatambua wachenjuaji wadogo wa madini ili kuweza kuwasimamia na kuwawekea utaratibu utakaosimamia shughuli zao. Hatua hii itasaidia kudhibiti mapato yatokanayo na shughuli za uchenjuaji na kuzuia utoroshaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza Vifungu Vidogo vya (3), (4), (5)

2 NOVEMBA, 2022

na (6) kwa lengo la kumpa Waziri mamlaka ya kurejeshwa Serikalini maeneo ya uchimbaji au utafiti wa madini ambayo leseni zake zimeisha muda kwa mujibu wa sheria. Dhumuni la marekebisho ni kuiwezesha Serikali kuyatunza na kuyaendeleza maeneo hayo ili yawe na tija kijiolojia na uchumi. Baada ya kurejeshwa Serikalini maeneo haya yatakuwa chini ya Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi wa hisa za Serikali kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Spika, utunzaji na uendelezaji wa maeneo hayo kijiolojia na kiuchumi kutaiweka Serikali katika nafasi nzuri wakati wa majadiliano na wawekezaji wanaokuja kwa ajili ya kuwekeza katika maeneo hayo. Aidha, mamlaka hayo hayataathiri utaratibu wa Waziri wa kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kifungu hiki kimefanyiwa maboresho zaidi kwa kuzingatia maoni ya kamati, kama inavyooneka kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kurekebisha Kifungu cha 27A kwa kuipa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania uwezo wa kufanya tafiti za kimkakati katika maeneo ya uchimbaji wa madini yaliyorejeshwa kwa mujibu wa Kifungu cha 15. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuongeza tija ya kijiolojia katika maeneo yaliyorejeshwa kupitia tafiti za Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania. Kifungu hiki kimefanyiwa maboresho zaidi kwa kuzingatia maoni ya Kamati kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Kifungu cha 32(1) kwa lengo la

2 NOVEMBA, 2022

kuongeza uhuishaji wa leseni kwa awamu ya pili kwa kipindi kisichozi miaka miwili. Madhumuni ya marekebisho ni kuainisha muda wa leseni iliyotolewa kwa awamu ya pili. Aidha, Kifungu hicho kinarekebishwa kwa lengo la kumpa Waziri mamlaka ya kutenga maeneo ambayo leseni ya uchimbaji wa madini imeisha muda wake na kurejeshwa Serikalini kwa mujibu wa Kifungu cha 15.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 55 kinarekebishwa kwa kuweka sharti kuhusu muda wa kuanza shughuli za madini baada ya leseni ya uchimbaji mdogo wa madini kutolewa. Aidha, Kifungu Kipya cha 60A kinaongezwa ili kuainisha utaratibu wa kuomba leseni, muda wa leseni na muda wa kuanza shughuli za uchenjuaji mdogo wa madini. Madhumuni ya marekebisho katika Kifungu cha 55 na Kifungu Kipya cha 60A ni kutambua muda wa leseni ya uchenjuaji mdogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, cha 129 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuihuisha adhabu kwa madhumuni ya kuzuia uvunjifu wa masharti ya sheria. Aidha, kwa kuzingatia maoni ya Kamati, Jedwali la Marekebisho linapendekeza kuboresha zaidi Kifungu hicho cha 129 kwa lengo la kuweka adhabu mbadala kutokana na ukiukwaji wa hitaji la kushirikisha wazawa watakaozidi kiasi cha adhabu ya *fine* inayopendekezwa. Vilevile inapendekezwa kurekebisha Kifungu cha 159 kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuweka Kanuni za utaratibu za uwekaji wa adhabu mbadala chini ya Kifungu cha 129(6).

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya

2 NOVEMBA, 2022

Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281. Kifungu cha 2 kinarekebisha kwa kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati na kuongeza tafsiri za misamiati mingine kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo, kama ilivyotumika katika masharti ya sheria hii kuondoa mkanganyiko wa kitafsiri unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuongeza Kifungu Kipya cha 3A ili kuainisha majukumu ya Makumbusho ya Taifa na kutofautisha kazi za makumbusho ya Taifa na majukumu ya Bodi ya Makumbusho ya Taifa. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuweka usimamizi bora wa sheria. Kifungu Kipya cha 4A kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutangaza makumbusho yoyote kuwa makumbusho ya Taifa. Utekelezaji wa Mamlaka haya utasaidia utambuzi, ukuzaji na uendelezaji wa makumbusho nchini.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 6 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) kwa lengo la kuiwezesha bodi kuwekeza sehemu ya fedha za Makumbusho ya Taifa baada ya kupata idhini ya Waziri. Kifungu cha 11A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu usimamizi na uendeshaji wa maeneo yenye kumbukumbu za urithi wa utamaduni kuwa chini ya Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa. Marekebisho haya ya sheria yanaendana na marekebisho katika Sheria ya Malikale, Sura ya 333 ya Uhamisho wa Majukumu ya Kiutendaji kutoka kwa Mkurugenzi wa Malikale. Jedwali la Kwanza linarekebisha kwa kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Makumbusho ya Taifa kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na kuimarisha utendaji.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 ambapo Kifungu Kipya cha 6A kinaongezwa ili kuainisha wajibu wa Mlipaji Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa mali za umma. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuweka bayana majukumu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, ambapo miongoni mwa majukumu hayo ni kuandaa miongozo kuhusu upatikanaji na utumiaji wa mali za umma, kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mali za umma na kusimamia mali zilizotaifishwa. Vilevile Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebisha ili kumuondolea Mhasibu Mkuu jukumu la usimamizi wa mali za umma tofauti na fedha ili jukumu hilo litekelezwe na Mlipaji Mkuu wa Serikali na hivyo kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mali hizo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada iliyokuwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226 inapendekezwa kuondolewa kupitia Jedwali la Marekebisho, kama ilivyoelezwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2022*) na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimae marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**MUSWADA WA SHERIA WA MAREKEBISHO YA SHERIA
MBALIMBALI (NA. 3) WA MWAKA 2022 (THE WRITTEN LAWS
(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) BILL, 2022) - KAMA
ULIVYOWASILISHWA BUNGENI**

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)

ISSN 0856 - 01001X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

No. 10

31st August, 2022

SPECIAL BILL SUPPLEMENT

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.34. Vol. 103 dated 31st August ,
2022*

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

(NO. 3) ACT, 2022

2 NOVEMBA, 2022

ARRANGEMENT OF SECTIONS

Section *Title*

PART I PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of certain written laws.

PART II AMENDMENT OF THE ANTIQUITIES ACT, (CAP. 333)

3. Construction.
4. General amendment.
5. Amendment of section 2.
6. Amendment of section 4.
7. Amendment of section 5.
8. Amendment of section 8.
9. Amendment of section 10.
10. Amendment of section 11.
11. Amendment of section 12.
12. Amendment of section 13.
13. Amendment of section 17.
14. Addition of section 17A.
15. Amendment of section 18.
16. Amendment of section 20.
17. Amendment of section 23.
18. Repeal and replacement of section 27.

PART III AMENDMENT OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS ACT, (CAP. 342)

19. Construction.
20. Amendment of section 3.
21. Amendment of section 17.
22. Repeal and replacement of section 21.
23. Amendment of section 25.
24. Amendment of section 28.

PART IV AMENDMENT OF THE CAPITAL MARKETS AND SECURITIES ACT,

2 NOVEMBA, 2022

(CAP. 79)

- 25. Construction.
- 26. Addition of section 134A.

PART V AMENDMENT OF THE MINING ACT, (CAP. 123)

- 27. Construction.
- 28. Amendment of section 7.
- 29. Amendment of section 15.
- 30. Amendment of section 27A.
- 31. Amendment of section 32.
- 32. Amendment of section 55.
- 33. Addition of section 60A.
- 34. Amendment of section 129.

PART VI AMENDMENT OF THE NATIONAL MUSEUM OF TANZANIA ACT, (CAP. 281)

- 35. Construction.
- 36. General amendment.
- 37. Amendment of section 2.
- 38. Addition of section 3A.
- 39. Amendment of section 4.
- 40. Addition of section 4A.
- 41. Amendment of section 6.
- 42. Addition of section 11A.
- 43. Amendment of First Schedule.

PART VII AMENDMENT OF THE PUBLIC FINANCE ACT, (CAP. 348)

- 44. Construction.
- 45. Addition of section 6A.
- 46. Amendment of section 8.

PART VIII AMENDMENT OF THE TANZANIA COMMISSION FOR SCIENCE AND TECHNOLOGY ACT, (CAP. 226)

2 NOVEMBA, 2022

- 47. Construction.
- 48. Amendment of section 3.
- 49. Amendment of section 12.
- 50. Addition of Part IIIA.
- 51. Addition of sections 37A and 37B.

NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dodoma,
30th August, 2022

HUSSEIN A. KATTANGA
Secretary to the Cabinet

A Bill
for

An Act to amend certain written laws.

ENACTED by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I PRELIMINARY PROVISIONS

- | | |
|-----------------------------------|---|
| Short title | 1. This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2022. |
| Amendment of certain written laws | 2. The written laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts. |

PART II AMENDMENT OF THE ANTIQUITIES ACT, (CAP. 333)

- | | |
|-----------------------|--|
| Construction Cap. 333 | 3. This Part shall be read as one with the Antiquities Act hereinafter referred to as the “principal Act”. |
|-----------------------|--|

2 NOVEMBA, 2022

- General amendment 4. The principal Act is amended generally by deleting the word “Council” wherever it appears and substituting for it the word “Committee”.
- Amendment of section 2 by- 5. The principal Act is amended in section 2, (a) deleting the word “Tanzania” wherever it appears in the definition of the term “monument” and substituting for it the word “Tanganyika”; and (b) adding in the appropriate alphabetical order the following definition:
““Board of the National Museum” means the Board of the National Museum of Tanzania established under the National Museum of Tanzania Act;”.
- Cap. 281
- Amendment of section 4 6. The principal Act is amended in section 4 by deleting subsection (1) and substituting for it the following:
“(1) The Director or any other person authorised by him may, at all reasonable times, enter and inspect any monument.”.
- Amendment of section 5 by adding the words “or Director General of the National Museum of Tanzania” immediately after the word “Director” appearing in paragraphs (a) and (b).
- Amendment of section 8 8. The principal Act is amended in section 8(2) by deleting the words “Trustees of the Museum” and substituting for them the words “Board of the National Museum”.
- Amendment of section 10 by- 9. The principal Act is amended in section 10, (a) adding the words “or Director General of the National Museum of Tanzania” immediately after the word “Director” appearing in subsection (2); and (b) deleting the words “Trustees of the Museum” appearing in subsection (3) and substituting for them the words “Board of the National Museum”.

2 NOVEMBA, 2022

- Amendment of section 11
10. The principal Act is amended in section 11(1), by-
- (a) deleting the words “or a person acting on his behalf” appearing in the opening phrase and substituting for them the words “, Director General of the National Museum of Tanzania or persons acting on their behalf,”; and
 - (b) deleting the word “Director” appearing in paragraph (c) and substituting for it the words “Director General of the National Museum of Tanzania”.
- Amendment of section 12
11. The principal Act is amended in section 12 by deleting the word “Director” wherever it appears in that section and substituting for it the words “Director General of the National Museum of Tanzania”.
- Amendment of section 13
12. The principal Act is amended in section 13 by deleting the word “Director” wherever it appears in that section and substituting for it the words “Director General of National Museum of Tanzania”.
- Amendment of section 17
13. The principal Act is amended in section 17, by-
- (a) deleting the word “Director” wherever it appears in subsections (4) and (5) and substituting for it the words “Director General of the National Museum of Tanzania”; and
 - (b) deleting the words “Trustees of the Museum” appearing in subsection (6) and substituting for them the words “Board of the National Museum”.
- Addition of section 17A
14. The principal Act is amended by adding immediately after section 17 the following:
- “Operation of private museum
- 17A.-(1) A person who intends to operate, control or manage a museum under this Act shall apply for registration to the Director in a prescribed form.
- (2) The procedures and requirements for registration of a museum shall be prescribed in

2 NOVEMBA, 2022

the rules made under this Act.

(3) A person who operates or undertakes any activity relating to operation, control and management of a museum without registration commits an offence and shall, upon conviction, be liable -

(a) in the case of an individual, to a fine of not less than five million shillings but not exceeding twenty million shillings or to imprisonment for a term of not less than two years but not exceeding five years or to both;

(b) in the case of a body corporate, to a fine of not less than twenty million shillings but not exceeding forty million shillings.”.

Amendment of section 18 15. The principal Act is amended in section 18 by deleting the word “Conservator” appearing in paragraph (b) and substituting for it the word “Director”.

Amendment of section 20 16. The principal Act is amended in section 20 by deleting subsection (1) and substituting for it the following:

“(1) There is hereby established a Committee to be known as the National Antiquities Advisory Committee.”.

Amendment of section 23 17. The principal Act is amended in section 23 by deleting the word “Director” appearing in subsections (1) and (2) and substituting for it the words “Director General of the National Museum of Tanzania”.

Repeal and replacement 18. The principal Act is amended by repealing section 27 and replacing for it the following:

2 NOVEMBA, 2022

- of section 27 “Penalty 27. A person who commits an offence under this Act shall, upon conviction, be liable-
- (a) in case of an offence under section 4(2), 11(2), 14(2), 15(4), 17(3) or 23(2), to a fine of not less than five million shillings but not exceeding twenty million shillings or to imprisonment for a term of not less than one year but not exceeding five years or to both; and
 - (b) in case of an offence under section 10(5), to a fine of not less than one million shillings but not exceeding three million shillings or to imprisonment for a term of not less than six months but not exceeding one year or to both.”.

PART III AMENDMENT OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS ACT, (CAP. 342)

Constructions 19. This Part shall be read as one with the
Cap. 342 Banking and Financial Institutions Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment 20. The principal Act is amended in section 3
of section 3 by deleting the definition of the terms “core capital” or “Tier 1 capital”, “supplementary capital” or “Tier 2 capital” and “total capital”.

Amendment 21. The principal Act is amended in section 17,
of section 17 by-

- (a) deleting subsection (1) and substituting for it the following:

2 NOVEMBA, 2022

“(1) Every bank or financial institution shall commence operations with and maintain at all times a minimum capital as the Bank may prescribe.

(2) Every bank or financial institution shall at all times maintain capital as a percentage of risk weighted assets and off-balance sheet exposures at levels and in the manner as the Bank may prescribe.

(3) Without prejudice to subsection (2), the Bank may prescribe additional capital buffers.

(4) Every bank or financial institution shall maintain a leverage ratio as the Bank may prescribe.”; and

(b) renumbering subsections (2) and (3) as subsections (5) and (6), respectively.

Repeal and replacement of section 21

22. The principal Act is amended by repealing section 21 and replacing it with the following:

“Liquidity ratios

21.-(1) Every bank or financial institution shall maintain minimum liquidity ratios at levels prescribed by the Bank.

(2) The Bank may impose on any bank or financial institution which fails to maintain the minimum liquidity ratio prescribed pursuant to this section, a penalty charge of not less than two percentage points at an annual rate above the interest rate prevailing in the most recent ninety-one day Treasury Bill auction on the amount of the deficiency, and the penalty charge may be recovered by deduction from any balance of, or moneys owing to the bank or financial institution concerned, or by way of summary suit under Order

2 NOVEMBA, 2022

Cap. 33

XXXV of the Civil Procedure Code.”.

Amendment
of section 25

23. The principal Act is amended in section 25 by deleting the words “twenty five percent of the core capital of the bank or financial institution, or three percent of core capital for a financial institution that is a micro-finance company” appearing in subsection (1) and substituting for them the words “a percentage of the capital of the bank or financial institution at the level prescribed by the Bank”.

Amendment
of section 28

24. The principal Act is amended in section 28 by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

“(2) The limitation under subsection (1) may include-

- (a) limiting an investment in an entity to a specified percentage of that entity’s share capital;
- (b) limiting an investment in an entity to a percentage of the capital of the bank or financial institution making the investment at the level prescribed by the Bank; and
- (c) limiting the aggregate amount of such investments that a bank or financial institution may hold.”.

PART IV AMENDMENT OF THE CAPITAL MARKETS AND SECURITIES ACT, (CAP. 79)

Construction
Cap. 79

25. This Part shall be read as one with the Capital Markets and Securities Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Addition of
section 134A

26. The principal Act is amended by adding immediately after section 134 the following:

“Responsibilities of issuer of securities
134A. An issuer of securities shall-
(a) submit for the Authority’s approval any announcement concerning meetings

2 NOVEMBA, 2022

of shareholders, any announcement on corporate actions or timetable for corporate actions affecting the rights of existing shareholders or price of share of the issuer;

Cap. 212

- (b) when conducting statutory meetings as required under the Companies Act, invite the Authority to attend the meeting as an observer to enable it to monitor the participation of shareholders in the decision making process;
- (c) ensure minority shareholders are represented in the Board of Directors of the issuer; and
- (d) comply with corporate governance principles as may be prescribed by the Authority.”.

PART V AMENDMENT OF THE MINING ACT, (CAP. 123)

Construction
Cap. 123

27. This Part shall be read as one with the Mining Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment
of section 7

28. The principal Act is amended in section 7(1), by-

2 NOVEMBA, 2022

(a) adding immediately after the opening phrase of paragraph (d) the following:

“(i) a primary processing licence;” and

(b) renaming subparagraphs (i) to (iii) as subparagraphs (ii) to (iv) respectively.

Amendment of section 15 by adding immediately after subsection (2) the following:

29. The principal Act is amended in section 15

“(3) Notwithstanding subsection (1), the Minister may, subject to the prescribed regulations, cause any vacant area other than a reserved area to be reverted to the Government.

(4) An area reverted to the Government pursuant to subsection (3) shall be held by the holder of shares of the Government issued in accordance with section 10 who shall be issued with a certificate of revisionary mineral rights.

(5) The procedure and other matters relating to issuance of the certificate of revisionary mineral rights shall be prescribed in the regulations by the Minister.”.

Amendment of section 27A by-

30. The principal Act is amended in section 27A, by-

(a) adding immediately after subsection (2) the following:

“(3) Notwithstanding subsection (2), the Geological Survey of Tanzania may, for the purposes of facilitating reversion of an area to the Government pursuant to section 15(2), conduct strategic prospecting and exploration.”; and

(b) renumbering subsections (3) and (4) as subsections (4) and (5) respectively.

Amendment of section 32 by-

31. The principal Act is amended in section 32(1), by-

(a) adding immediately after paragraph (b) the following:

“(c) where an application for renewal has been made by the holder in the

2 NOVEMBA, 2022

prescribed form, for the second period of renewal for which the applicant has applied, a period not exceeding two years;”;

(b) deleting paragraph (d) and substituting for it the following:

“(d) where a prospecting licence is no longer renewable, the prospecting area shall revert to the Government and be dealt with in accordance with section 15”;

(c) renaming paragraphs (c) to (e) as paragraphs (d) to (f) respectively.

Amendment
of section 55

32. The principal Act is amended in section 55 by adding immediately after subsection (4) the following:

“(5) A holder of a primary mining licence shall commence mining operations within a period of six months or such other period as the licensing authority may permit from the date of the grant of the licence.”.

Addition of
section 60A

33. The principal Act is amended by adding immediately after section 60 the following:

“Application for primary processing licence 60A.-(1) A person who intends to conduct ball mill operations or sluicing shall apply to the Commission for a primary processing licence.

(2) A licence issued under this section shall be valid for a period of one year and may be renewable.

(3) Conditions and procedures for grant of primary processing licence shall be as prescribed in the regulations.”.

Amendment
of section
129

34. The principal Act is amended in section 129 by deleting subsection (6) and substituting for it the following:

2 NOVEMBA, 2022

“(6) Any regulations made under this Act may prescribe for any breach thereof for matters relating to local content a fine not exceeding ten billion shillings and in any other case a fine not exceeding one hundred fifty million shillings.”.

PART VI AMENDMENT OF THE NATIONAL MUSEUM OF TANZANIA ACT, (CAP. 281)

- Construction
Cap. 281 35. This Part shall be read as one with the National Museum of Tanzania Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.
- General
amendment 36. The principal Act is amended generally by deleting the word “Director” wherever it appears and substituting for it the words “Director General”.
- Amendment
of section 2 37. The principal Act is amended in section 2,
by-
- (a) deleting the words “National Culture” appearing in the definition of the term “Minister” and substituting for them the word “museum”;
 - (b) deleting the definition of the term “National Museum of Tanzania” and substituting for it the following:
 - ““National Museum of Tanzania” means the National Museum of Tanzania established under section 3;”;
 - (c) inserting in the appropriate alphabetical order the following new definitions:
 - ““monument” includes-
 - (a) any building, fortification, interment, midden, dam or any structure erected, built or formed by human agency in Tanganyika before the year 1863;

2 NOVEMBA, 2022

- (b) any rock painting or any immovable object painted, sculptured, carved, incised or modified by human agency in Tanganyika before the year 1863;
- (c) any earthwork, trench, admit, well, cave, tunnel or other modification of the soil or rock dug, excavated or otherwise engineered by human agency in Tanganyika before the year 1863, whether or not the monuments have been modified, added to or restored at a later date and whether or not it is included in a list published by the Director of Antiquities;
- (d) any site or immovable structure declared to be a monument under section 3; and
- (e) such adjoining land as may be required for the purposes of fencing, covering or otherwise preserving the monument;

“National Museum” means the museum declared by the Minister under section 4A;”.

Addition of section 3A

38. The principal Act is amended by adding immediately after section 3 the following:

“Functions of National Museum of Tanzania

3A. The functions of the National Museum of Tanzania shall be to-

- (a) identify, protect, preserve and transmit cultural and natural heritage of Tanzania;
- (b) conduct research and disseminate knowledge in the fields of scientific, cultural,

2 NOVEMBA, 2022

- technological and human evolution;
- (c) promote Tanzania cultural heritage resources in academic, social and economic development;
- (d) engage formal and informal education and lifelong learning, through development and transmission of knowledge, programmes and exhibitions;
- (e) interpret and disseminate knowledge on collections, monuments, conservation areas and sites within its specific areas of expertise and to organise exhibition as appropriate; and
- (f) perform any other functions necessary for the promotion, control and management of museums.”.

Amendment of section 4 by-

39. The principal Act is amended in section 4,
- (a) deleting subsection (4); and
 - (b) renumbering subsection (5) as subsection (4).

Addition of section 4A

40. The principal Act is amended by adding immediately after section 4 the following:
- “Declaration of national museum 4A.-(1) The Minister may, upon recommendation of the Board and by notice published in the *Gazette*, declared any museum

2 NOVEMBA, 2022

to be a national museum.

(2) The procedure for declaration of a national museum under this section shall be prescribed in the regulations.

(3) A museum declared under subsection (1) shall be under the National Museum of Tanzania.”.

Amendment
of section 6

41. The principal Act is amended in section 6, by-

(a) designating the contents of section 6 as subsection (1); and

(b) adding immediately after subsection (1) as designated the following:

“(2) The Board may, with prior approval of the Minister, invest any part of money available in the funds of the National Museum of Tanzania in such manner as the Board may deem fit.”.

Addition of
section 11A

42. The principal Act is amended by adding immediately after section 11 the following:

“Management and operations of monuments, conservation areas and sites
Cap. 333
11A.- (1) For the purposes of better preservation, protection and promotion of monuments, conservation areas or sites, the National Museum of Tanzania shall undertake the day to day management and operations of monuments vested to it in terms of the Antiquities Act.

(2) In implementing the responsibilities under subsection (1), the Director General may-

(a) enter and inspect any monument, conservation area or site;

(b) fence, repair, protect or preserve any monument, conservation area or site;

2 NOVEMBA, 2022

Cap. 333

- (c) search and excavate for relics in any monument, conservation area or site and remove any relics undiscovered; or
- (d) implement anything or undertake any other responsibility as provided under the Antiquities Act.

(3) Where a monument is a place of ordinary habitation or occupation, the Director General shall give the occupier not less than forty-eight hours' notice in writing of his intention to search and excavate for relics.

(4) Nothing in this section shall be construed to authorise-

- (a) the exclusion of the owner or any person beneficially interested in a monument, conservation area or site or any person authorised by him, from any part of the monument, conservation area or site;
- (b) the excavation of any monument or any search for relics in a monument, conservation area or site which is a place of ordinary habitation or occupation without the consent of the owner.

(5) Any person who willfully obstructs the Director

2 NOVEMBA, 2022

General or any other person authorised by him in that behalf in the exercise of his powers under subsection (2) commits an offence.”.

Amendment
of First
Schedule

43. The principal Act is amended in the First Schedule, by-

(a) deleting paragraph 1 and substituting for it the following:

“Composition of Board consist of-

1. The Board shall

(a) the Chairperson who shall be appointed by the President;

(b) the Director of Antiquities;

(c) five other members appointed by the Minister as follows:

(i) a representative of higher learning institutions;

(ii) a representative from the Tanzania Commission for Science and Technology;

(iii) three other members appointed by the Minister.

(2) In appointing members under subparagraph 1(c), the Minister shall have regard to persons who have experience and proven knowledge in sciences or cultural heritage, tourism marketing, economics, financial matters, administration or

2 NOVEMBA, 2022

education.

(3) The Director General shall be the Secretary to the Board.”.

PART VII AMENDMENT OF THE PUBLIC FINANCE ACT, (CAP. 348)

Construction
Cap. 348 44. This Part shall be read as one with the Public Finance Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Addition of
section 6A 45. The principal Act is amended by adding immediately after section 6 the following:

“Oversight of 6A-(1) The Paymaster
public General shall be responsible for
property the oversight of public property
in public sector entities.

(2) In overseeing public property, the Paymaster General shall-

- (a) develop, monitor, evaluate and review implementation of guidelines relating to acquisition, maintenance, utilisation and disposal of public property;
- (b) establish and maintain systems for oversight of public property;
- (c) analyse reports on accidents and losses of public property and process compensation claims;
- (d) manage public property disposal;

2 NOVEMBA, 2022

- (e) conduct verification and inspection of public property; and
- (f) be responsible for management of confiscated or forfeited property.”.

Amendment of section 8 46. The principal Act is amended in section 8 by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

“(2) The Accountant-General shall be responsible to the Permanent Secretary for the compilation and management of the accounts and the custody and safety of the public moneys and for that purpose the Accountant-General may, in the manner prescribed by the Minister, and with prior consent of the Permanent Secretary, give such instructions of a general or specific character to accounting officers as may be necessary for the effective implementation of the purposes and provisions of this Act.”.

PART VIII AMENDMENT OF THE TANZANIA COMMISSION FOR SCIENCE AND TECHNOLOGY ACT, (CAP. 226)

Construction of section 3 47. This Part shall be read as one with the Tanzania Commission for Science and Technology Act, hereinafter referred to as the “principal Act”.

Amendment of section 3 48. The principal Act is amended in section 3 by inserting in their appropriate alphabetical order the following new definitions:

““research” means any type of systematic investigation, testing or evaluation designed to develop or contribute to a body of knowledge;

“researcher” means a person trained to design and implement research protocols, collect, analyse and interpret data and report results in

2 NOVEMBA, 2022

a scientific format;”.

Amendment of section 12 49. The principal Act is amended in section 12 by adding immediately after subsection (2) the following:

“(3) The Minister may, by order published in the *Gazette*, amend or vary the list of institutions provided for in the Second Schedule.”.

Addition of Part IIIA 50. The principal Act is amended by adding immediately after Part III the following new Part:

“PART IIIA RESEARCH SUPERVISION

Functions of National Research Clearance Committee 14A. Notwithstanding the generality of the functions of the committees established under section 14, the National Research Clearance Committee shall, in particular, have the functions to-

- (a) register persons intending to conduct research;
- (b) ensure researchers comply with the procedures, standards, code of ethics and guidelines;
- (c) monitor and evaluate researches;
- (d) uphold standards of professional conduct of research; and
- (e) issue permits to accredited researchers, research projects and programmes.

Registration of researchers 14B.-(1) A person shall not conduct research unless such person is registered under this Act.

2 NOVEMBA, 2022

(2) A person who intends to conduct research shall, on payment of the prescribed fees, apply for registration to the Commission in the manner prescribed in the regulations.

(3) The provisions of this section shall not apply to institutions affiliated to the Commission pursuant to section 12.

Issuance of research permit 14C. The Commission shall, where an applicant has met the criteria set by this Act or regulations made thereunder, register and issue a research permit to such an applicant.

Register 14D. The Commission shall keep and maintain a register into which shall be entered-

- (a) the names of researchers and research institutions; and
- (b) any other information as the Commission may determine.

Suspension, cancellation and deregistration 14E. Where a person has failed to comply with the provisions of this Act, the Commission may, subject to the procedure specified in the regulations, cancel or suspend a permit issued to such person provided that, in case of a serious contravention or habitual offender, the Commission may deregister such person from the register of researchers.”

Addition of 51. The principal Act is amended by adding

2 NOVEMBA, 2022

sections 37A immediately after section 37 the following:
and 37B

“Procedures,
standards,
ethics and
guidelines

37A. A person permitted to conduct research under this Act shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under this Act.

Monitoring
and evaluation

37B.-(1) The Commission shall conduct monitoring and evaluation in respect of each research permitted under this Act for purposes of assessing and evaluating the process of research being conducted in the manner prescribed in the regulations.

(2) In undertaking monitoring and evaluation under subsection (1), the Commission shall have the power to inquire into the programmes, management or any other relevant matter concerning a person and may interview any employee, call for or impound, examine and review any documents, reports or information held or kept by the person and access any facilities affiliated to the person or utilise such methods or modalities of monitoring and evaluation as the Commission deems fit.

(3) A researcher or research institution which is the subject to the process of monitoring and evaluation under this section shall supply such documents, reports or information as the Commission or its agent may request.”.

2 NOVEMBA, 2022

OBJECTS AND REASONS

This Bill proposes amendment to seven laws, namely the Antiquities Act, Cap. 333, the Banking and Financial Institutions Act, Cap. 342, the Capital Markets and Securities Act, Cap. 79, the Mining Act, Cap. 123, the National Museum of Tanzania Act, Cap. 281, the Public Finance Act, Cap. 348 and the Tanzania Commission for Science and Technology Act, Cap. 226.

The proposed amendments intend to keep updated the respective laws with changes so far observed in their implementation.

The Bill is divided into Eight Parts. Part I deals with preliminary provisions which include the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended are amended in their respective Parts.

Part II of the Bill proposes to amend the Antiquities Act, Cap. 333. The Act is amended generally by replacing the term “Council” with the term Committee throughout the Act so as to align the Act with the organisational structure of the Ministry of Natural Resources and Tourism.

Section 4 is proposed to be amended for the purposes of relieving the Director of Antiquities operational functions which are proposed to be imposed on the National Museum of Tanzania. Section 5 is proposed to be amended in order to extend protection to the Director General of the National Museum from the requirements under section 5(1). Section 10 is proposed to be amended for the purpose of extending administrative responsibilities concerning declaration of relics to the Director General of the National Museum.

Sections 11, 12 and 13 are proposed to be amended with a view to transfer to the Director General of the National Museum mandate relating to assessment and grant of excavation licence, including powers to deal in excavation of relics without requiring a licence to do so.

Section 17A is proposed to be added for the purposes of providing regulatory control of private operated museums. Sections 17 and 23 are proposed to be amended for the purposes of transferring from the Director of Antiquities to the Director General of the National Museum the responsibilities relating to identification of relics discovered prior to 1964 and protection and notices around relics.

Part III of the Bill proposes to amend the Banking and Financial Institutions Act, Cap. 342. The Act is amended generally in order to align the provisions of the Act with the global applicable standards in determining capital requirements in the banking industry. Further, the proposed amendments intend to create a sound legal environment aimed at facilitating private sector participation in the financial sector, especially the banking and capital markets sub-sectors, facilitating access to loans, increasing the capacity of banks and financial institutions to encourage savings, promoting an efficient banking sub-sector, which is competitive and meets consumer needs as well as improving access to long - term loans for business, infrastructure and housing.

2 NOVEMBA, 2022

Sections 3, 17, 21, 25 and 28 are amended in order to improve standards enshrined in the Act in determining capital requirements for banks and financial institutions. The standards currently provided for in the Act prescribe minimum capital requirements for banks and financial institutions based on their risk-weighted assets, leaving out other risks. Following the observed loop-holes, the standards currently provided for in the Act cannot be relied on to correctly assess the minimum capital requirement and liquidity of banks and financial institutions. Hence, the proposed amendments intend to facilitate implementation of the new standards for determination of capital requirement for banks and financial institutions. This will enhance the safety and stability of the banking industry and ensure that banks and financial institutions hold an adequate amount of capital to meet their obligations. Further, this measure will lead to a safer financial system and reduce the possibility of affecting the country's economic growth.

Part IV of the Bill proposes to amend the Capital Markets and Securities Act, Cap. 79 by introducing a new section 134A which deals with responsibilities of the issuer of securities. The aim of the amendment is to impose on the issuer of securities obligations which intend to safeguard the rights of minority shareholders. The amendment further aims at enhancing the Authority's oversight on the rights of minority shareholders and their full participation in the decision making process.

Part V proposes to amend the Mining Act, Cap. 123. Section 7 is proposed to be amended by including primary processing licence as one of licences issued under the Act. The purpose of this amendment is to formalize the activities of primary mining processers and to supervise their activities accordingly. This step will help to collect revenue generated from the mining sector as well as to prevent smuggling of minerals.

Section 15 is proposed to be amended by adding subsection (2) in order to enable the Minister responsible for mining to grant revisionary mineral rights over vacant areas to the Government upon expiration of the mining licences. The objective is to preserve the geological and economic potentials of such areas. Upon reversion to the Government, such areas will be held by the Treasury Registrar as the holder of Government shares issued pursuant to section 10 of the Mining Act. Geological and economic preservation of such areas will be advantageous to the Government in negotiations with investors intending to invest in the mining sector.

Section 27A is proposed to be amended by giving the Geological Survey of Tanzania mandate to conduct strategic prospecting and exploration studies on areas granted reversionary mineral rights in terms of section 15. The objective of the amendment is the realization of geological potential of reverted areas through survey undertakings by the Geological Survey of Tanzania.

Section 32(1) is proposed to be amended by putting a requirement that specifies the lifespan of renewed prospecting licence to be for a period not exceeding two years. The objective of the amendment is to specify longevity of licences issued for the second term. Further, the amendment aims at empowering the Minister to set aside areas in respect of which licenses have expired and areas reverted to Government in terms of section 15.

2 NOVEMBA, 2022

Section 55 is amended to provide for operational period of a primary mining licence. Section 60A is added to provide for application procedure, duration of primary processing licences, and other related matters. The objective of amendment in section 55 and 60A is to ascertain the operational period of primary mining licence. Furthermore, section 129 is amended by enhancing the penalty with a view to deter contravention of the provisions of the Act.

Part VI proposes amendment in the National Museum of Tanzania Act, Cap. 281. Section 2 is proposed to be amended by adding new definitions and amending definitions of certain terms with the aim of ensuring that the terms used are correctly defined in order to avoid any ambiguity. Section 3A is proposed to be added in order to provide for functions of the National Museum of Tanzania so as to distinguish its functions from those of the Board. Section 4A is proposed to be added in order to give to the Minister powers to declare any museum to be a national museum.

Section 6 is proposed to be amended by adding subsection (2) in order to enable the Board to invest part of the monies of the National Museum of Tanzania after the approval of the Minister. Section 11A is proposed to be added in order to transfer the functions of the Director of Antiquities of managing and operating monuments to the Director General of the National Museum of Tanzania in compliance with the directives of the Government. The First Schedule is proposed to be amended by reducing the number of members of the Board in order to ensure better management of the National Museum of Tanzania and reducing operational costs.

Part VII of the Bill proposes to amend the Public Finance Act, Cap. 348, whereby it is proposed to add a new section 6A so as to provide for the Paymaster General's power to oversee public properties. The amendment aims at clearly specifying and explaining the responsibility of the Paymaster General in the oversight of public properties. The role proposed to be clearly stated includes the responsibility to develop guidelines relating to acquisition, maintenance, utilisation and disposal of public property, to conduct verification and inspection of public property and to manage confiscated or forfeited property. Further, section 8 is proposed to be amended in order to eliminate the responsibility of managing property other than public money from among responsibilities vested in the Accountant-General.

Part VIII proposes amendment in the Tanzania Commission for Science and Technology Act, Cap. 226 whereby section 3 of the Act is amended by adding the definition of the terms "research" and "researcher" for the purpose of clarifying the terms in order to increase clarity during implementation of various provisions of the Act. Section 12 is proposed to be amended so as to enable the Minister to amend the list of affiliated institutions provided for in the Second Schedule. The aim of the amendment is to ensure that at all times the list correctly reflects the institutions which are affiliated with the Commission.

Further, the Act is amended by adding a new Part IIIA which provides for the functions of National Research Clearance Committee, registration of researchers, issuance of research permits, establishment of register and matters that can lead to suspension, cancellation of research permits as well as events that can disqualify a person from carrying out research under the Act. The purpose of these amendments is to give the Commission powers to oversee research matters in the country by putting in place specific provisions catering for research matters.

2 NOVEMBA, 2022

The Act is amended by adding new sections 37A and 37B which introduce provisions regarding procedures, standards, ethics and guidelines on research as well as monitoring and evaluation of research. The aim of this amendment is to enable the Commission to monitor research projects from the start to finality.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria Saba zifuatazo; Sheria ya Mali Kale, Sura ya 333, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342, Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79, Sheria ya Madini, Sura ya 123, Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281, Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 na Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226.

Mapendekezo ya marekebisho yanalenga kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria husika.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nane. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali ya Sheria yanavyopendekezwa kurekebishwa.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mali Kale, Sura ya 333. Inapendekezwa kurekebisha neno “Baraza” sehemu yoyote linapojitokeza katika Sheria na badala yake kuweka neno “Kamati” ili kuendana na mabadiliko ya miundo katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa madhumuni ya kumuondolea Mkurugenzi wa Mali Kale majukumu ya kiutendaji ambapo inapendekezwa kuhamishia majukumu hayo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa. Kifungu cha 5 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa madhumuni ya kuweka kinga kwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa dhidi ya masharti yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 5(1). Kifungu cha 10 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa madhumuni ya kumpa Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa majukumu kuhusiana na kutangazwa kwa tunu za Taifa.

Vifungu vya 11, 12 na 13 vinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kuhamishia kwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa mamlaka ya kutathmini na kutoa vibali vya uchimbaji wa malikale, na inajumuisha mamlaka yake kufanya shughuli za uchimbaji pasipo kuhitaji leseni.

Kifungu kipya cha 17A kinapendekezwa kuongezwa kwa madhumuni ya kusajili makumbusho zinazoanzishwa na taasisi, asasi na watu binafsi. Vifungu vya 17 na 23 vinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kuhamisha kutoka kwa Mkurugenzi wa Mali Kale kwenda

2 NOVEMBA, 2022

kwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa majukumu kuhusiana na utambuzi wa tunu za Taifa za kabla ya 1964 pamoja na kinga na uwekaji matangazo kwenye tunu.

Sehemu ya Tatu inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342. Kwa ujumla lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka ulinganifu katika viwango vya upimaji wa utoshelevu wa mitaji ya benki na taasisi za fedha kulingana na viwango vya kimataifa. Aidha, maboresho yanayopendekezwa yanalenga kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ya fedha hususani sekta ndogo za benki na masoko ya mitaji, kulinda amana za wateja, kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa watu wengi, kuongeza uwezo wa taasisi za fedha kuhamasisha utunzaji wa akiba, kukuza sekta ya benki yenye ufanisi, inayokidhi mahitaji ya watumiaji na yenye ushindani, pamoja na kuboresha upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya biashara, miundombinu na makazi.

Vifungu vya 3, 17, 21, 25 na 28 vinapendekezwa kurekebisha kwa lengo la kuboresha viwango vya upimaji wa utoshelevu wa mitaji ya benki na taasisi za fedha. Kwa sasa Sheria inaainisha viwango vinavyozingatia utoshelevu wa mitaji kwa kuangalia vihatarishi kwenye mikopo na masoko na kuacha vihatarishi vingine. Kutokana na upungufu huo, Sheria iliyopo haiwezeshi kutathmini kiwango sahihi cha mitaji wa benki au taasisi ya fedha husika. Aidha, Sheria hii imeainisha kigezo kimoja tu cha upimaji wa ukwasi. Hivyo, marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kuwezesha utelekezaji wa viwango vipya vya upimaji wa utoshelevu wa mitaji ya benki na taasisi za fedha. Hatua hii itaimarisha mitaji na ukwasi na hivyo kuiwezesha sekta ndogo ya kibenki kuhimili misukosuko mbalimbali na kupunguza uwezekano wa kuathiri uchumi wa nchi.

Sehemu ya Nne inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 kwa kuongeza kifungu kipya cha 134A kinachohusu wajibu wa watoa dhamana. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwapa watoa dhamana wajibu utakaohakikisha maslahi ya wawekezaji wenye hisa chache yanalindwa. Marekebisho haya yanalenga pia kuimarisha uwezo wa Mamlaka kusimamia haki za wawekezaji wenye hisa chache na ushiriki wao katika kufanya maamuzi.

Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123, ambapo kifungu cha 7 kinarekebisha ili kuongeza leseni ndogo ya uchenjuaji wa madini katika orodha ya leseni zinazotolewa chini ya Sheria hii. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuwatambua wachenjuaji wadogo wa madini ili kuweza kuwasimamia na kuwawekea utaratibu utakaosimamia shughuli zao. Hatua hii itasaidia kudhibiti mapato yatokanayo na shughuli za uchenjuaji na kuzuia utorohaji wa madini.

Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebisha ili kuongeza kifungu kidogo cha (2) kwa lengo la kumpa Waziri mamlaka ya kurejesha Serikalini maeneo ya uchimbaji wa madini ambayo leseni zake za uchimbaji zimeisha muda. Dhumuni la marekebisho ni kuwezesha Serikali kuyatunza na kuendeleza maeneo hayo yawe na tija kijiolojia na kiuchumi. Baada ya kurejeshwa Serikalini, maeneo haya yatakuwa chini ya Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi wa hisa za Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini. Utunzaji na uendelezaji wa maeneo hayo kijiolojia na kiuchumi kutaiweka Serikali katika nafasi nzuri wakati wa majadiliano na wawekezaji watakaokuja kwa ajili ya kuwekeza katika maeneo hayo.

2 NOVEMBA, 2022

Kifungu cha 27A kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuipa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania uwezo wa kufanya tafiti za kimkakati katika maeneo ya uchimbaji wa madini yaliyorejeshwa kwa mujibu wa kifungu cha 15. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuongeza tija ya kijiolojia katika maeneo yaliyorejeshwa kupitia tafiti za Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania.

Kifungu cha 32(1) kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuongeza uhuishaji wa leseni kwa awamu ya pili kwa kipindi kisichozidi miaka miwili. Madhumuni ya marekebisho ni kuanisha muda wa leseni iliyotolewa kwa awamu ya pili. Aidha, kifungu hicho kinarekebishwa pia kwa lengo la kumpa Waziri mamlaka ya kutenga maeneo ambayo leseni ya uchimbaji madini imeisha muda wake na kurejeshwa Serikalini kwa mujibu wa kifungu cha 15.

Kifungu cha 55 kinarekebishwa kwa kuweka sharti kuhusu muda wa kuanza shughuli za madini baada ya leseni ya uchimbaji mdogo wa madini kutolewa. Aidha, kifungu cha 60A kinaongezwa ili kuanisha utaratibu wa kuomba leseni, muda wa leseni na muda wa kuanza shughuli za uchenjuaji mdogo wa madini. Madhumuni ya marekebisho katika kifungu cha 55 na 60A ni kutambua muda wa uchenjuaji mdogo wa madini. Vilevile kifungu cha 129 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuhuisha adhabu katika kifungu hicho kwa madhumuni ya kuzuia uvunjifu wa masharti ya Sheria.

Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281. Kifungu cha 2 kinarekebishwa kwa kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati na kuongeza tafsiri za misamiati mingine kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa misamiati hiyo kama ilivyotumika katika Sheria hiyo ili kuepuka utata wowote unaoweza kujitokeza. Kifungu cha 3A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuainisha majukumu ya Makumbusho ya Taifa ili kutofautisha majukumu ya Makumbusho ya Taifa na majukumu ya Bodi. Kifungu cha 4A kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutangaza makumbusho yoyote kuwa Makumbusho ya Taifa.

Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) kwa lengo la kuiwezesha Bodi kuwekeza sehemu ya fedha za Makumbusho ya Taifa baada ya kupata idhini ya Waziri. Kifungu cha 11A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuhamisha majukumu ya Mkurugenzi wa Mali Kale ya kusimamia na kuendesha maeneo yenye kumbukumbu za urithi wa utamaduni kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali. Jedwali la Kwanza linarekebishwa kwa kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi ya Makumbusho ya Taifa kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji.

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, ambapo kifungu kipya cha 6A kinaongezwa ili kuainisha wajibu wa Mlipaji Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa mali za umma. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuweka bayana majukumu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali ambapo miongoni mwa majukumu hayo ni kuandaa miongozo kuhusu upatikanaji na utumiaji wa mali za umma, kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mali za umma na kusimamia mali zilizotaifishwa kwa Serikali. Aidha, kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumuondolea Mhasibu Mkuu jukumu la usimamizi wa mali za

2 NOVEMBA, 2022

umma tofauti na fedha ili jukumu hilo litekelezwe na Mlipaji Mkuu wa Serikali na hivyo kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mali hizo.

Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226 ambapo kifungu cha 3 cha Sheria kinarekebishwa ili kuweka tafsiri ya maneno "utafiti" na "mtafiti" kwa madhumuni ya kuongeza ufafanuzi na uelewa katika utekelezaji wa masharti mbalimbali ya Sheria hii. Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kurekebisha orodha ya taasisi zenye ushirika na Tume iliyopo katika Jedwali la Pili. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa wakati wote orodha hiyo inaakisi kwa uhalisia taasisi ambazo Tume inashirikiana nazo.

Sheria inapendekeza kurekebishwa kwa kuongeza Sehemu mpya ya IIIA ambayo inaainisha majukumu ya Kamati ya Taifa ya Utoaji wa Vibali vya Utafiti, usajili wa watafiti, utoaji wa vibali vya watafiti, kuanzisha rejesta na masuala yanayoweza kusababisha kusitishwa au kufuta kwa vibali vya tafiti na pia sababu zinazomuondolea mtu sifa za kufanya utafiti chini ya Sheria hii.

Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 37A na 37B ambavyo vinaainisha taratibu za ufuatiliaji na tathimini wakati wa kufanya tafiti. Vifungu hivi vinaainisha taratibu, viwango, maadili na miongozo ya kufuata wakati wa kufanya tafiti. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuiwezesha Tume kufuatilia miradi ya utafiti kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Dodoma,
29 Agosti, 2022

ELIEZER MBUKI FELESHI
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, awasilishe Maoni ya Kamati. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge, kama ilivyowasilishwa Mezani.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Kikao cha Tisa cha Mkutano wa Nane, Tarehe 23 Septemba, 2022 kwa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni ya 96(1). Baada ya hatua hiyo na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14), ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kuteleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mbunge, siku ya Jumatatu Tarehe 17 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika mkutano wa kupokea maoni ya wadau uliofanyika siku ya Jumatano Tarehe 19 Oktoba, 2022 ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika Mkutano huo, Kamati ilipokea maoni ya wadau wafuatao:-

2 NOVEMBA, 2022

- (1) TWaweza
- (2) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)
- (3) JamiiForums
- (4) *Tanzania Chamber of Mines*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote waliowasilisha maoni ambayo kwa sehemu kubwa yameongeza mawanda ya uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua maoni ya wadau na baadae kufanya majumuisho na Mwanasheria Mkuu wa Serikali siku ya Jumanne tarehe 25 Oktoba, 2022 ili kujadili mapendekezo ya marekebisho ya Ibara mbalimbali za Muswada. Katika kikao hicho, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliambatana na Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko Mbunge, Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa Mbunge na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Omari Juma Kipanga Mbunge, kwa lengo la kutoa ufafanuzi katika marekebisho mahsusni yanayofanyika katika Sheria zilizowasilishwa na Wizara zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Muswada. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 umegawanyika katika Sehemu Kuu Nane. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi wakati Sehemu ya Pili hadi ya Sehemu ya Nane ya Muswada zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho katika Sheria Kuu Saba kama ifuatavyo:-

2 NOVEMBA, 2022

- (1) Sheria ya Mali Kale, Sura ya 333
- (2) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342
- (3) Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79
- (4) Sheria ya Madini, Sura ya 123
- (5) Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281
- (6) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348
- (7) Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba, marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa masharti mbalimbali ya Sheria hizo. Hivyo basi, Kamati ilichambua mapendekezo hayo kwa kufanya tathmini ya kina kuhusu kiwango cha marekebisho yanayofanyika pamoja na kufanya upembuzi wa maudhui ya masharti yanayopendekezwa kama ambavyo imefafanuliwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Moja ni Marekebisho ya Sheria ya Mali Kale, Sura ya 333. Marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 18 ya Muswada. Pamoja na masuala mengine, Serikali inapendekeza katika Ibara ya 4 kufanya mabadiliko ya kimuundo kwa kuanzisha Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Mali Kale na kulifuta Baraza la Kitaifa la Mali Kale lililokuwa linaundwa kwa Kifungu cha 20 cha Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu Kipya cha 17A katika Sheria hii, kuweka masharti ya ulazima wa kusajili

2 NOVEMBA, 2022

makumbusho zinazoanzishwa na taasisi, asasi, kampuni na watu binafsi. Aidha, Kifungu Kipya cha 17A(3)(a) kinaweka adhabu ya faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano na isiyozidi Shilingi Milioni Ishirini au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano kwa kwa mtu binafsi ambaye atakiuka masharti ya Kifungu Kipya hicho.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati, adhabu inayopendekezwa ni kubwa kwa kuwa mawanda ya uendeshaji wa makumbusho hizo kwa mtu binafsi ina tafsiri pana. Aidha, Kamati imezingatia ukweli kwamba, watu wa makabila tofauti nchini wamekuwa na desturi ya kusambaza maarifa ya kitamaduni na malikale na kushiriki elimu isiyo rasmi ya ukuzaji na usambazaji wa maarifa kupitia tamaduni zao. Hivyo basi, baada ya majadiliano, Serikali imekubaliana na Kamati kupunguza adhabu kwa mtu binafsi ili iwe kiasi kisichopungua Shilingi Milioni Moja na kisichozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, Mbili ni Marekebisho ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 442. Marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika Ibara ya 19 hadi Ibara ya 24 ya Muswada. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheria hiyo kwa kuweka hitaji kwa benki na taasisi za fedha kuweka viwango vya upimaji wa utoshelevu wa mitaji. Kwa kufanya hivyo, masharti mapya yatasaidia kuimarisha mitaji na ukwasi na hivyo kuiwezesha sekta ndogo ya kibenki kuhimili misukosuko na kupunguza uwezekano wa kuathiri uchumi wa nchi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali ambayo pamoja na faida nyingine, maboresho ya sheria hiyo ni:-

- (1) Yatawezesha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ndogo za benki na masoko ya mitaji
- (2) Yataongeza ulinzi wa amana za wateja
- (3) Yatawezesha upatikanaji wa mikopo kwa watu wengi
- (4) Yataongeza uwezo wa taasisi za kifedha kuhamasisha utunzaji wa akiba.

Mheshimiwa Spika, Tatu ni Marekebisho ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79. Katika Ibara ya 26 ya Muswada, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria hiyo kwa kuongeza Kifungu Kipya cha 134A. Masharti mapya yanayopendekezwa yana lengo la kuwapa watoa dhamana wajibu utakaohakikisha kwamba, maslahi ya wawekezaji wenye hisa chache yanalindwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo itaimarisha uwezo wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kusimamia haki za wawekezaji wenye hisa chache na ushiriki wao katika kufanya maamuzi. Hata hivyo, baada ya uchambuzi wa Kamati, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuongeza masharti ya ziada katika Muswada kwa lengo la kuainisha makosa na adhabu kwa watoa dhamana watakaoshindwa kuzingatia masharti ya Kifungu Kipya cha 134A.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Nne ni Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123. Marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika Ibara ya 27 hadi Ibara ya 34 ya Muswada, ambapo kwa sehemu kubwa Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali pia imeishauri Serikali kufanya marekebisho ya msingi katika baadhi ya Ibara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika ya Ibara ya 8 mathalani, Serikali inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 7 cha Sheria hii ili kuongeza leseni ndogo ya uchenjuaji wa madini katika orodha ya leseni zinazotolewa chini ya Sheria hii. Kamati inaipongeza hatua hiyo ambayo itaiwezesha Serikali kutambua wachenjuaji wadogo wa madini kwa utaratibu wa kisheria ambao utasimamia shughuli zao na hivyo kudhibiti mapato yatokanayo na shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa yatapatikana katika Ibara ya 29 ya Muswada inayorekebisha Kifungu cha 15 cha Sheria. Serikali inapendekeza kuongeza masharti yanayompa Waziri wa Madini mamlaka ya kurejesha Serikalini maeneo ya uchimbaji wa madini ambayo leseni zake za uchimbaji zimeisha muda. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini nia njema ya Serikali ya kuyatunza na kuendeleza maeneo hayo ili yawe na tija ya kijiolojia na kiuchumi kwa uwekezaji wa baadae.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia hiyo njema, kwa uchambuzi wa Kamati, uandishi wa Kifungu Kidogo Kipya cha 15(3) kinachopendekezwa unaweza kutafsiriwa kwamba, utaratibu wa zabuni unaoainishwa katika Kifungu

2 NOVEMBA, 2022

cha 15 (1) hautazingatiwa. Kwa muktadha huo, Kamati imeishauri Serikali kuboresha uandishi wa masharti yanayopendekezwa ili kubainisha kwamba, maudhui ya Kifungu cha 15(1) yatazingatiwa kikamilifu kwa lengo la kuweka uwazi katika mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, Tano ni Marekebisho ya Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281. Marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika Ibara ya 35 hadi Ibara ya 43 ya Muswada. Baada ya uchambuzi wake, Kamati imekubaliana na Serikali kuhusu marekebisho mengi yaliyofanyika isipokuwa katika maeneo machache yanayohusu uandishi na uchapaji pamoja na maudhui. Moja kati ya mapendekezo ya Serikali ni kuongeza masharti katika Sheria hiyo ambayo yanaainisha majukumu ya Makumbusho ya Taifa ili kutofautisha kazi zake na majukumu ya Bodi ya Makumbusho ya Taifa.

Moja kati ya mapendekezo ya Serikali ni kuongeza masharti katika sheria hiyo ambayo yanaainisha majukumu ya Makumbusho ya Taifa ili kutofautisha kazi zake na majukumu ya Bodi ya Makumbusho ya Taifa. Kamati inaunga mkono mapendekezo hayo kwa kuwa yataweka usimamizi bora wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 43 ya Muswada Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika jedwali la kwanza la Sheria kwa lengo la kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Makumbusho ya Taifa. Kamati inapongeza hatua hii kwa sababu inaweza kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuokoa fedha za umma. Hata hivyo, baada ya uchambuzi kuhusu masharti ya

2 NOVEMBA, 2022

kuundwa kwa bodi hiyo, Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati kuboresha masharti hayo ili kujumuisha takwa la kuzingatia jinsi (*gender*) katika muundo wa bodi husika.

Mheshimiwa Spika, sit ani kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria hiyo kwa kuongeza masharti mapya yanayoainisha wajibu wa Mlipaji Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa mali za umma ili kuweka bayana majukumu yake. Marekebisho hayo yako katika Ibara ya 44 hadi Ibara ya 46 ya Muswada. Majukumu yanayoainishwa yanajumuisha mamlaka ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mali za umma na kusimamia mali zilizotaifishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati imekubaliana na mapendekezo ya marekebisho yanayofanywa katika Sheria hii, na pia imeishauri Serikali kutafsiri ili kubainisha wazi maana ya maneno “mali ya umma” yaliyotumika katika Ibara ya 45. Lengo la mapendekezo haya ni kuboresha uandishi wa Sheria hii ili kuondoa utata kuhusu maana ya maneno.

Mheshimiwa Spika, saba ni Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226. Mapendekezo ya Sheria hii yameondolewa na Serikali kama ambavyo imeainishwa katika Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa. Hatua hii inafuatia uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati kwa kuzingatia maoni ya wadau mbalimbali.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, masuala ya msingi yaliyobainika wakati wa uchambuzi wa marekebisho ya sheria hii ni pamoja na umuhimu wa Serikali kutoa tafsiri sahihi na jumuishi katika kufafanua masuala ya tafiti za kisayansi. Masuala mengine yanahusisha mapendekezo ya kuweka taratibu za vibali vya tafiti na ufuatiliaji na tathmini wakati wa kufanya utafiti. Masuala haya ni muhimu na hivyo Serikali inapaswa kufanya tathimini ya kina kuhusu faida na athari za mapendekezo hayo katika marekebisho ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na mapendekezo ya kamati; Maoni ya Jumla. Uchambuzi wa Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali unaofanywa na Kamati unahusisha tathmini ya maudhui ya mapendekezo ya Serikali katika Sheria za sekta mbalimbali. Kamati inapongeza hatua ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwaalika mawaziri wa sekta zinazoguswa na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2022 ambao walipata fursa ya kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu masuala yanayogusa sekta zao. Kamati inashauri Serikali kuendelea na utamaduni huo ambao unaboresha majadiliano kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, Serikali imeanza kuzingatia masuala ya msingi katika uandishi wa sheria ikiwemo kuhusisha suala la jinsi katika muundo wa bodi mbalimbali zinazoteuliwa na mawaziri wa kissekta. Mfano wa hatua hii ni Marekebisho ya Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281 katika Ibara ya 43 ya Muswada ambapo Serikali imeweka sharti la kuzingatia jinsi

2 NOVEMBA, 2022

katika muundo wa bodi. Kwa muktadha huo, Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho ya masharti ya sheria zote zinazofanana na hii ili kuzingatia takwa hili la msingi ambalo ni sehemu ya malengo ya maendeleo endelevu la kuhakikisha kwamba watu wa jinsi zote wanashiriki kikamilifu katika ngazi mbalimbali za maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226. Pamoja na kwamba Serikali imeondoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii, Kamati inashauri kwamba, Wizara husika kwa kushirikiana na wadau ifanye tathmini ya kina kuhusu umuhimu wa marekebisho ya Sheria hiyo. Aidha, iwapo Serikali itaona ulazima wa kurejesha tena mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hiyo, ni vyema Kamati husika za Bunge zikahusishwa kikamilifu ili kuhakikisha kwamba Sheria hiyo inaboreshwa kwa viwango vinavyostahili.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambao katika kutekeleza majukumu yao kikatiba walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi

2 NOVEMBA, 2022

wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Aidha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, nakupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kundi la Kijiografia na Kisiasa Afrika (*African Geopolitical Group of IPU*) katika Mkutano wa 145 wa Umoja wa Mabunge Duniani (*IPU*) uliofanyika jijini Kigali, nchini Rwanda mwezi uliopita.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (Mb), akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole kwa ushirikiano wao wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Aidha, nawashukuru watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na watendaji wa taasisi mbalimbali zinazotekeleza Sheria mbalimbali zinazorekebisha na Muswada huu, ambao wamehusika katika kuandaa mapendekezo ya Muswada pamoja na Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelewa J. Mwihambi, *ndc*, kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2022 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No, 3) Act, 2022*] pamoja na marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na mtoa hoja.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA. 3 WA MWAKA 2022 [THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 99 (5)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2022 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2022]**.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza katika Kikao cha Tisa cha Mkutano wa Nane, tarehe 23 Septemba, 2022 kwa utaratibu ulioainishwa katika **Kanuni ya 96 (1)**. Baada ya hatua hiyo, na kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 97 (1)** ikisomwa pamoja na **Kanuni ya 136 (14)**, ulitumia mamlaka yako kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ili ufanyiwe uchambuzi.

1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa

2 NOVEMBA, 2022

Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kuteleza jukumu hilo, Kamati ilianza uchambuzi kwa kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (Mb.), siku ya Jumatatu tarehe 17 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo Kamati ilipokea na kujadili maoni ya wadau katika Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau (*Public Hearing*) uliofanyika siku ya Jumatano tarehe 19 Oktoba, 2022 ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika Mkutano huo, Kamati ilipokea maoni ya wadau wafuatao: -

- a) TWaweza
- b) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)
- c) Jamii Forums
- d) Tanzania Chamber of Mines

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote waliowasilisha maoni ambayo kwa sehemu kubwa yameongeza mawanda ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua maoni ya wadau, na baadae kufanya majumuisho na Mwanasheria Mkuu wa Serikali siku ya Jumanne tarehe 25 Oktoba, 2022 ili kujadili mapendekezo ya marekebisho ya Ibara mbalimbali za Muswada. Katika kikao hicho, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliambatana na Waziri wa Madini, Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri wa Madini, Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.) na Naibu Waziri wa Elimu,

2 NOVEMBA, 2022

Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Juma Kipanga (Mb.) kwa lengo la kutoa ufafanuzi katika marekebisho mahsusni yanayofanyika katika Sheria zinazosimamiwa na Wizara zao.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

2.1 Maelezo ya Awali

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2022 umegawanyika katika Sehemu Kuu Nane (8). Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi wakati Sehemu ya Pili hadi ya Sehemu ya Nane ya Muswada zinaweka masharti mbalimbali kwa lengo la kufanya marekebisho katika Sheria Kuu saba (7). Sheria hizo ni: -

- a) Sheria ya Mali Kale, Sura ya 333 (*The Antiquities Act, Cap. 333*);
- b) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342 (*The Banking and Financial Institutions Act, Cap. 342*);
- c) Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 (*The Capital Markets and Securities Act, Cap. 79*);
- d) Sheria ya Madini, Sura ya 123 (*The Mining Act, Cap. 123*);
- e) Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281 (*The National Museum of Tanzania Act, Cap. 281*);

2 NOVEMBA, 2022

f) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 (*The Public Finance Act, Cap. 348*); na

g) Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226 (*The Tanzania Commission for Science and Technology Act, Cap. 226*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba, marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa masharti mbalimbali ya Sheria hizo. Hivyo basi, Kamati ilichambua mapendekezo hayo kwa kufanya tathmini ya kina kuhusu kiwango cha marekebisho yanayofanyika pamoja na kufanya upembuzi wa maudhui ya masharti yanayopendekezwa kama ambavyo inafafanuliwa katika aya zinazofuata.

2.2 **Marekebisho ya Sheria ya Mali Kale, Sura ya 333 (*The Antiquities Act, Cap. 333*)**

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 18 ya Muswada. Pamoja na masuala mengine, Serikali inapendekeza katika Ibara ya 4 kufanya mabadiliko ya kimuundo kwa kuanzisha Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Mali Kale na kulifuta Baraza la Kitaifa la Mali Kale lililokuwa linaundwa kwa Kifungu cha 20 cha Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu Kipya cha 17A katika Sheria ili kuweka masharti ya ulazima wa kusajili makumbusho zinazoanzishwa na taasisi, asasi, kampuni na watu binafsi (*private museums*). Aidha, Kifungu Kipya cha 17A (3) (a) kinaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tano

2 NOVEMBA, 2022

na isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano kwa kwa mtu binafsi (*individual person*) ambaye atakiuka masharti ya Kifungu Kipya hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi wa Kamati, adhabu **inayopendekezwa** ni kubwa kwa kuwa mawanda ya uendeshaji wa makumbusho hizo kwa mtu binafsi ina tafsiri pana. Aidha, Kamati imezingatia ukweli kwamba, watu wa makabila tofauti nchini wamekuwa na desturi ya kusambaza maarifa ya kitamaduni na malikale na kushiriki elimu isiyo rasmi ya ukuzaji na usambazaji wa maarifa kupitia tamaduni zao. Hivyo basi, baada ya majadiliano, Serikali imekubaliana na Kamati kupunguza adhabu kwa mtu binafsi ili iwe kiasi kisichopungua shilingi milioni moja na kisichozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja.

2.3 **Marekebisho ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342 (*The Banking and Financial Institutions Act, Cap. 342*)**

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika Ibara ya 19 hadi Ibara ya 24 ya Muswada. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheria hiyo kwa kuweka hitaji kwa benki na taasisi za fedha kuweka viwango vya upimaji wa utoshelevu wa mitaji. Kwa kufanya hivyo, masharti mapya yatasaidia kuimarisha mitaji na ukwasi na hivyo kuiwezesha sekta ndogo ya kibenki kuhimili misukosuko na kupunguza uwezekano wa kuathiri uchumi wa nchi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali ambayo pamoja na faida nyingine, maboresho ya sheria hiyo:-

- a) yatawezesha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ndogo za benki na masoko ya mitaji
- b) yatauongeza ulinzi wa amana za wateja
- c) yatawezesha upatikanaji wa mikopo kwa watu wengi; na
- d) yataongeza uwezo wa taasisi za fedha kuhamasisha utunzaji wa akiba.

2.4 Marekebisho ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 (*The Capital Markets and Securities Act, Cap. 79*)

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 26 ya Muswada, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria hiyo kwa kuongeza Kifungu Kipya cha 134A. Masharti mapya yanayopendekezwa yana lengo la kuwapa watoa dhamana wajibu utakaohakikisha kwamba maslahi ya wawekezaji wenye hisa chache yanalindwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo itaimarisha uwezo wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kusimamia haki za wawekezaji wenye hisa chache na ushiriki wao katika kufanya maamuzi. Hata hivyo, baada ya uchambuzi wa Kamati, Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuongeza masharti ya ziada katika Muswada kwa lengo la kuainisha makosa na adhabu

2 NOVEMBA, 2022

kwa Watoa Dhamana watakao shindwa kuzingatia masharti ya Kifungu Kipya cha 134A.

2.5 **Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 (The Mining Act, Cap. 123)**

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika Ibara ya 27 hadi Ibara ya 34 ya Muswada, ambapo kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali lakini pia imeishauri Serikali kufanya marekebisho ya msingi katika baadhi ya Ibara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika ya Ibara ya 8 mathalani, Serikali inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 7 cha Sheria ili kuongeza leseni ndogo ya uchenjuaji wa madini katika orodha ya leseni zinazotolewa chini ya Sheria hii. Kamati inapongeza hatua hiyo ambayo itaiwezesha Serikali kutambua wachenjuaji wadogo wa madini kwa utaratibu wa kisheria ambao utasimamia shughuli zao, na hivyo kudhibiti mapato yatoakanayo na shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa yanapatikana katika Ibara ya 29 ya Muswada inayorekebisha Kifungu cha 15 cha Sheria. Serikali inapendekeza kuongeza masharti yanayompa Waziri wa Madini mamlaka ya kurejesha Serikalini maeneo ya uchimbaji wa madini ambayo leseni zake za uchimbaji zimeisha muda. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini nia njema ya Serikali ya kuyatunza na kuendeleza maeneo hayo ili yawe na tija ya kijiolojia na kiuchumi kwa uwekezaji wa baadae.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia hiyo njema, kwa uchambuzi wa Kamati, uandishi wa Kifungu Kidogo Kipya cha 15 (3) kinachopendekezwa unaweza kutafsiriwa kwamba, utaratibu wa zabuni unaoainishwa katika Kifungu cha 15 (1) hautazingatiwa. Kwa muktadha huo, Kamati imeishauri Serikali kuboresha uandishi wa masharti yanayopendekezwa ili kubainisha kwamba maudhui ya Kifungu cha 15 (1) yatazingatiwa kikamilifu kwa lengo la kuweka uwazi zaidi katika mchakato huo.

2.6 Marekebisho ya Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281 (*The National Museum of Tanzania Act, Cap. 281*)

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria hii yanapatikana katika Ibara ya 35 hadi Ibara ya 43 ya Muswada. Baada ya uchambuzi wake, Kamati imekubaliana na Serikali kuhusu marekebisho mengi yaliyofanyika isipokuwa katika maeneo machache yanayohusu uandishi na uchapaji pamoja na maudhui. Moja kati ya mapendekezo ya Serikali ni kuongeza masharti katika Sheria hiyo ambayo yanaainisha majukumu ya Makumbusho ya Taifa ili kutofautisha kazi zake na majukumu ya Bodi ya Makumbusho ya Taifa. Kamati inaunga mkono mapendekezo hayo kwa kuwa yataweka usimamizi bora wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 43 ya Muswada, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Jedwali la Kwanza la Sheria kwa lengo la kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi ya Makumbusho ya Taifa. Kamati inapongeza hatua hii kwa sababu inaweza kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuokoa fedha za umma.

2 NOVEMBA, 2022

Hata hivyo, baada ya uchambuzi kuhusu masharti ya kuundwa kwa bodi hiyo, Serikali imekubaliana na mapendekezo ya Kamati kuboresha masharti hayo ili kujumuisha takwa la kuzingatia jinsi (*gender*) katika muundo wa bodi husika.

2.7 Marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 (*The Public Finance Act, Cap. 348*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria hiyo kwa kuongeza masharti mapya yanayoainisha wajibu wa Mlipaji Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa mali za umma ili kuweka bayana majukumu yake. Marekebisho hayo yako katika Ibara ya 44 hadi Ibara ya 46 ya Muswada. Majukumu yanayoinishwa yanajumuisha mamlaka ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mali za umma na kusimamia mali zilizotaifishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati imekubaliana na mapendekezo ya marekebisho yanayofanywa katika sheria hii, na pia imeishauri Serikali kutafsiri ili kubainisha wazi maana ya maneno ‘mali ya umma’ yaliyotumika katika Ibara ya 45. Lengo la mapendekezo haya ni kuboresha uandishi wa Sheria ili kuondoa utata kuhusu maana ya maneno.

2.8 Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226 (*The Tanzania Commission for Science and Technology Act, Cap. 226*)

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Sheria hii yameondolewa na Serikali kama ambavyo imeainishwa katika Jedwali la Marekebisho (*Schedule of Amendment*) lililowasilishwa. Hatua hii inafuatia uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati kwa kuzingatia maoni ya wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, masuala ya msingi yaliyobainika wakati wa uchambuzi wa marekebisho ya sheria hii ni pamoja na umuhimu wa Serikali kutoa tafsiri sahihi na jumuishi katika kufafanua masuala ya tafiti za kisayansi. Masuala mengine yanahusisha mapendekezo ya kuweka taratibu za vibali vya tafiti na ufuatiliaji na tathmini wakati wa kufanya utafiti. Masuala haya ni muhimu na hivyo Serikali inapaswa kufanya tathmini ya kina kuhusu faida na athari za mapendekezo hayo katika marekebisho ya sheria hiyo.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

3.1 Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali unaofanywa na Kamati unahusisha tathmini ya maudhui ya mapendekezo ya Serikali katika Sheria za sekta mbalimbali. Kamati inapongeza hatua ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwaalika mawaziri wa sekta zinazoguswa na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2022 ambao walipata fursa ya kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu masuala yanayogusa sekta zao. Kamati

2 NOVEMBA, 2022

inashauri Serikali, kuendelea na utamaduni huo ambao unaboresha majadiliano kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, Serikali imeanza kuzingatia masuala ya msingi katika uandishi wa sheria ikiwemo kuhusisha suala la jinsi katika muundo wa bodi mbalimbali zinazoteuliwa na mawaziri wa kisékta. Mfano wa hatua hii ni Marekebisho ya Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281 katika Ibara ya 43 ya Muswada ambapo Serikali imeweka sharti la kuzingatia jinsi katika muundo wa bodi. Kwa muktadha huo, Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho ya masharti ya sheria zote zinazofanana na hii ili kuzingatia takwa hili la msingi ambalo ni sehemu ya malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) la kuhakikisha kwamba watu wa jinsi zote wanashiriki kikamilifu katika ngazi mbalimbali za maamuzi.

3.2 **Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Sura ya 226 (*The Tanzania Commission for Science and Technology Act, Cap. 226*)**

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imeondoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii, Kamati inashauri kwamba, Wizara husika kwa kushirikiana na wadau ifanye tathmini ya kina kuhusu umuhimu wa marekebisho ya Sheria hiyo. Aidha, iwapo Serikali itaona ulazima wa kurejesha tena mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hiyo, ni vyema Kamati husika za Bunge zikahusishwa kikamilifu ili kuhakikisha kwamba Sheria hiyo inaboreshwa kwa viwango vinavyostahili.

2 NOVEMBA, 2022

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ambao katika kutekeleza majukumu yao kikatiba, walichambua, kujadili, na kutoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa kutambua mchango wao, naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. - Makamu
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. - Mjumbe
3. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb. - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb. - Mjumbe
5. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb. - Mjumbe
6. Mhe. Zainab Athman Katimba, Mb. - Mjumbe
7. Mhe. Noah Lemburis Ole Saputu Mollel, Mb.- Mjumbe
8. Mhe. Asha Abdullah Juma, Mb. - Mjumbe
9. Mhe. Omar Ali Omar, Mb. - Mjumbe
10. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb. - Mjumbe
11. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb. - Mjumbe
12. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb. - Mjumbe
13. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb. - Mjumbe
14. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb. - Mjumbe
15. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb. - Mjumbe
16. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb. - Mjumbe
17. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb. - Mjumbe
18. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb. - Mjumbe
19. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb. - Mjumbe
20. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb. - Mjumbe

2 NOVEMBA, 2022

21. Mhe. Rashid Abdalla Rashid, Mb. - Mjumbe
22. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb. - Mjumbe
23. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb. - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa dhati wewe binafsi, ukisaidiwa na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge hili na kwa namna ambavyo umeipa Kamati ushirikiano. Ushauri wako na maelekezo yako vimekuwa ni nyenzo muhimu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Aidha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, nakupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kundi la Kijiografia na Kisiasa Afrika (*African Geopolitical Group of IPU*) katika Mkutano wa 145 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika jijini Kigali, nchini Rwanda mwezi uliopita.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (Mb.), akisaidiwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) Ndg. Onorius Njohole kwa ushirikiano wao wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Aidha, nawashukuru watendaji wote chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na watendaji wa taasisi ambazo zinatekeleza Sheria mbalimbali zinazorekebisha na Muswada huu, ambao wamehusika katika kuandaa mapendekezo ya Muswada pamoja na Jedwali la Marekebisha.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Nanelwa J. Mwihambi, ndc, kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2022 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2022]** pamoja Marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb.

MWENYEKITI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria

02 Novemba, 2022

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti, tunakushukuru sana kwa kusoma maelezo ama mapendekezo ya Kamati. Waheshimiwa Wabunge kama utaratibu wetu ulivyo sasa tutaanza uchangiaji kwenye Muswada huu; na ninayo majina hapa ya Wabunge walio omba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, atafatiwa na Yahaya Omary Massare, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia

2 NOVEMBA, 2022

kwenye Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.3 ya Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kuchangia, madhumuni na nia ya kurekebisha Sheria mbalimbali au kutengeneza Sheria mpya ni kwa sababu ya maendeleo ya kijamii, kielimu, biashara, kisiasa na maendeleo ya taifa kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni hayo taifa lolote ambalo linategemea kuwa na taifa bora ni lazima liangalie sheria zake na kuzirekebisha ili ziweze kuendana na hali halisi katika jamii husika, kwa maana ya sisi Watanzania kwenye nchi yetu na kufuata misingi ya autawala bora wa sheria (*rule of law*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kutanguliza maelezo hayo, kwamba kwa nini tunarekebisha Sheria sasa niende kuchangia Muswada wenyewe ambao umewasilishwa mbele yako na mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, kamati imejadili kwa mapama na marefu katika maeneo ya Sheria mbalimbali ambayo zimetajwa na zilikuwa takribani sheria karibu sita.

Mheshimiwa Spika, tulianza na Sheria ya Mali Kale Sura Namba 333. Sheria hiyo ilikuwa inabadilishwa maeneo kadhaa ili iweze kuendana na Sheria ya Makumbusho ya Taifa, kwa maana ya Bodi ya Taifa iweze kushughulikia majukumu ambayo yalikuwa yanashughulikiwa na wadhamini.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikubaliana na marekebisho ya Serikali kwa sababu yameendana na hali halisi na yamekidhi matakwa ya Sheria ya Makumbusho ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilileta marekebisho ya Sheria ya Ibara ya 14 kuongeza kifungu kipyua cha 17A. Kifungu hiki ni kwa ajili ya kuangalia faini mbalimbali zinazoweza kutozwa kwenye taasisi mbalimbali na watu ambao wanatunza mali kale. Kwa hiyo katika misingi hiyo, kama Kamati tuliangalia Tanzania kama nchi ambayo ina makabila zaidi ya 122, kwa hiyo wananchi wetu kwa maana ya kutunza mali kale watakuwa na mambo mbalimbali wanayotunza kwa ajili ya kulinda mali zao, mila na desturi. Lakini baadaye tukaona kwamba tukiweka faine kubwa italetu shida katika kutunza mali kale kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini baadaye Serikali iliweza kutuletea sababu ambayo tumeona ni sababu muhimu kwa sababu kumekuwepo na uharibifu wa mali kale; na kama tujuavyo mali kale ikishaharibiwa kuirudisha inakuwa ni changamoto kwa sababu ni *non-renewable resources*. Haiwezekani pale ambapo mali kale imeharibiwa, kwa sababu kuna maeneo mengi ambayo majengo ya mali kale yamebomolewa na wananchi na baadhi ya watu ambao hawana nia njema ya kutunza mali kale; ambayo baadaye inakuwa ni changamoto katiaka kuirudisha.

Mheshimiwa spika, lakini pia tuliangalia kwenye Ibara ya 18 kwenye Marekebisho ya kifungu cha 27, adhabu hiyo ilikuwa iwe ni Shilingi milioni tano mpaka milioni Ishirini, kwa sababu ambazo nimeshazitaja, au kifungu cha mwaka mmoja hadi miaka mitano. Serikali ilitoa sababu mbalimbali

2 NOVEMBA, 2022

ambazo tuliona kwa kweli ni kwa sababu ya kuhakikisha kwamba mali kale zetu zinakuwa salama na zinaendelea kudumu hadi vizazi vijavyo. hivyo hatukuwa na sababu ya kuendelea kukataa pendekezo hili na moja kwa moja. Kama Kamati tulikubaliana jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine ambayo tuliingalia ilikuwa ni Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha Sura Namba 342. Katika Sheria hii, marekebisho yake ilikuwa ni kuangalia mitaji ya benki ili kuendana na matakwa ya Sheria za Kimataifa za Benki ya Dunia na kadhalika ili kuangalia ku-*regulate* masuala yetu ya kiuchumi ndani na nje ya nchi; ambayo kwa mwanzo ilikuwa bilioni tano kwa ajili ya mitaji ya benki. Sasa tulipendekeza kuwa Bilioni kumi na tano. Lakini pia kutatengenezwa Sheria ndogo (*regulation*) ambayo itaweka utaratibu wa kuona mitaji kulingana na hali halisi ya uchumi kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, suala hilo linasaidia sana benki zetu kuwa imara na kuimarika ili kuwa na uwezo wa kujiendesha na kutoa mikopo kikamilifu na kujenga imani kwa wananchi kutumia benki hizo.

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine ni Sheria ya Masoko na Mitaji Sura namba 79. Sheria hii ilikuwa inarekebishwa Ibara ya 26 kwa kuongeza kifungu kipya kidogo cha 134, ambayo inaweka adhabu ya wale ambao wanashughulika na masuala ya mitaji. Kamati hatukuwa na ubishi kwa sababu mambo yote katika kifungu hiki tumekubaliana na adhabu iliyokuwa imewekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Sheria ya Madini Sura namba 123, ililetwa kwa ajili ya marekebisho kwa

2 NOVEMBA, 2022

kurekebisha Ibara ya 29 kifungu cha 15(1) kuweka kifungu cha 15(3). Ilikuwa hoja, kwamba Waziri awe na mamlaka ya kutwaa maeneo pale ambapo yalikuwa hayatumiki kuyarudisha Serikalini. Kulikuwa na mjadala mrefu katika Kamati yetu na tukaishauri Serikali kwamba eneo hilo la madini lirudishwe tu Serikalini pale ambapo hakutakuwa na mtu aliyewasilisha maombi ya zabuni katika eneo hilo. Kama kutakuwa na maombi ya zabuni basi Waziri hawezi kuruhusiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hili nalo Serikali imelikubali, na kwakweli tunaishukuru Serikali kwa sababu imekuwa ikikubali mambo kadhaa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yalikuwa ni madogomadogo ya kusahihisha maneno katika Ibara 33 na Ibara ya 34, ambayo ilirekebisha pia kifungu cha 149 kinachohusu makosa yanayohusiana na *local content*. Ambayo Serikali ilitoa maelezo kwamba kama tutashindwa kusimamia maeneo ya *local content* italeti shida sana kwa sababu itawanyima fursa mbalimbali wananchi wetu kushiriki katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya tuliona ni muhimu sana katika kukubaliana na Serikali ili iweze kuleta tija katika uchimbaji wa madini na uchenjuaji wa madini kwenye taifa letu. Hasa ukizingatia kwamba kumekuwepo na suala la ubadhirifu na wizi katika migodi na maeneo kama hayo. Sheria hii iweze kusaidia kupunguza na kuondoa changamoto hizo za ujanja ujanja ambao unaweza ukawepo katika maeneo yetu.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine ilikuwa ni Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura Na. 281, ambayo ilikuwa inaelezea masuala mbalimbali, ikiwemo suala la muundo wa wajumbe katika Sheria hiyo. Kama tunavyofahamu, kwa upande wa muundo wa wajumbe tulikuwa tunashauri kwamba lazima uendane kama vile ilivyo kwenye zile Sheria za Mabaraza ya Ardhi. Sheria ya Mabaraza inaeleza wazi kwamba, lazima pawepo na asilimia kadhaa ya wanawake ili kuwawezesha kufanya maamuzi ambayo yanakuwa sawa wakati wa kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yahaya O. Massare atafuatiwa na Agnesta L. Kaiza, Mheshimiwa Jerry W. Silaa ajiandae.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya leo, na mimi nichangie kwenye Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, viko vipengele vingi ambavyo tunatakiwa tuvichangie na tuvisemee sisi ambao tuko kwenye Kamati ya Katiba na Sheria. Nianze na sehemu ya tano, na kama muda utakuwepo nitaangalia sehemu nyingine. Sehemu hii ina upande ambao Serikali inaenda kutoa kama kitu kipya hivi. Tulikuwa na leseni za uchenjuaji kwa kampuni kubwa, zile *smelter*; lakini sasa tunaenda kutoa leseni za uchenjuaji kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo. Ilikuwa ukitaka kuchenjua lazima uwe na leseni ya

2 NOVEMBA, 2022

uchimbaji. Fursa hii itasaidia wawekezaji wa ndani na hasa wananchi ambao mitaji yao ni midogo ambao hawana nguvu ya kununua mashine zile za kuchenjua. Ilikuwa mtu anaweza akaleta pale na akajiegemeza kwa mchimbaji mdogo na akawa anachenjua na kutoza tozo ambzo Serikali pia haipati makusanyo ya maduhuri yake au kodi kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo marekebisho haya yanakuja kutengeneza na kuongeza ajira kwa watu wetu katika sehemu hii ya uchimbaji. Wachimbaji wadogo hata kwetu Mkoa wa Singida tunao pale Sambalu na maeneo mengine ya Geita kule, wale wanaochenjua ni watu ambao hawalipi kodi kabisa. Kwahiyo, Sheria hii inakwenda kutibu na kuongeza kiwango na wigo wa maduhuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya tano, Ibara ya 29 inarekebishwa ili kumpa mamlaka Mheshimiwa Waziri kuchukua maeneo ya uchimbaji na maeneo ya utafiti ambayo yamekuwa na mtu kwa muda mrefu. Kwa kawaida sheria iliyopo inamruhusu mtu kupata *leseni*, lakini wakati akitafiti baada ya muda fulani ana-renew ya kwanza, ana-renew ya pili na renew ya mwisho ni ya tatu. Hivyo, kama *lessen* ni kubwa (PL) huwa anatumika kama miaka tisa hivi anaendelea kumiliki.

Mheshimiwa Spika, sheria iliyokuwepo ilikuwa inampa fursa mtu yule yule kujibadilisha na kuomba leseni upya kwa sura nyingine. Sasa Serikali inakwenda kuona kama uwezekano wa kuirudisha ile ardhi kwa Msajili wa Hazina, kwa maana Serikali inaweza ikaingia ubia na mtu mwenye

2 NOVEMBA, 2022

nguvu kuliko aliyekuwepo. Maana yake tunaweza kwenda kuongeza migodi mingine mipya kwa marekebisho haya. Migodi iliyopo ni ile ambayo Serikali ilikuwa na hisa kwa maana ya *STAMICO* au *MEREMETA* kwa makampuni yake ambayo yalikuwepo, lakini migodi ambayo imeanzishwa upya kabisa ni michache sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunakwenda kutengeneza kitu ambacho ni fursa kwa nchi pengine kuja na uwezeshaji wa kupata ajira kwa watu wetu, makusanyo ya mirabaha na maduhuli ya Serikali kupitia sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ambalo linampa mamlaka Waziri kuchukua ardhi hiyo ambayo ni ya utafiti au uchimbaji, tumeitaka Serikali ilete na iweke ushindani, isiwe tu kwamba ikifika mahali imekwisha, basi inabeba, inakunyakua. Lazima iweke ushindani, itangaze tenda. Kama hakuna mtu anaonesha nia, hapo ndiyo Serikali iweze kuchukua na kumpa Msajili wa Hazina. Maana yake tutaendelea kuweka ushindani ulio wazi lakini kuhakikisha kwamba wawekezaji wa mitaji ambao wanakuja kuwekeza katika sekta hii, kuwapa *security* ya fedha watakazowekeza katika utafiti.

Mheshimiwa Spika, katika sekta hii, sehemu kubwa ni Kamari, utafiti wa madini, hususan madini yenye thamani kama dhahabu. Ndiyo maana hata *GST* wanaenda kupewa mamlaka ya kutafiti kwa kina zaidi. Utafiti unatumia gharama kubwa, ndiyo maana watu wetu namna ya kuchimba unapoanza wakati mwingine inachukua mitaji mikubwa sana. Mtu anawekeza pesa, inafika mahali sasa

2 NOVEMBA, 2022

mamlaka ya Waziri yanampoka, ndiyo maana tuna tumeiambia Serikali na bahati nzuri Mwanasheria Mkuu huyu ni mtu msikivu sana, na hata Waziri aliyepo, Mheshimiwa Dotto Biteko alipokuja kwenye kamati, wameridhia kwamba lazima wataweka kwanza ushindani kabla ya kuirudisha kwa Msajili wa Hazina ili kulinda wale watakaokuja kwenye sura ya uwekezaji wenye tija na nchi hii na watu wetu.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 30 ya sehemu hii ya tano, inampa mamlaka *GST* kutafiti kwa kina zaidi. Mwanzo alikuwa anafanya *mapping* na kutambua maeneo yenye mashapo ya dhahabu, lakini hakuwa na mamlaka ya kuchimba; kufanya *drilling* na kujua kiasi ambacho anaweza akahodhi zile leseni zilizokuwa kwa Msajili wa Hazina, akawa na taarifa ambazo anaweza akaziweka sokoni. Siku moja mwekezaji mwenye dhamira na nia nzuri ya kuwekeza katika eneo hili, akaja kutokana na taarifa za *GST*, zikamshawishi sasa kuweka mtaji. Iliyoy kwa sasa, anakupa tu taarifa za juu juu, ili wewe ndio uende na mtaji wako ukafanye *drilling* na *exploration* ya kina.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mabadiliko haya, yanaenda kumpa mamlaka *GST* kufanya kazi ya kitafiti ya kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 34 inazungumzia habari ya *local content*. kizungumkuti kikubwa katika eneo la uwekezaji, na katika eneo ambalo lina kandarasi kubwa ni hiki kipande cha *local content*. Wakandarasi au wale wachimbaji wenyewe, makampuni makubwa hatuwezi kuyataja hapa kwa sababu ni watu wetu, makampuni

2 NOVEMBA, 2022

makubwa yanayochimba, huwa wanaunda vikampuni vidogo vidogo miongoni mwao na wanaagiza bidhaa na wanafanya manunuzi wakijifanya ni watu ambao ni Watanzania. Wanawekwa watu boshen, Yahaya Massare anaingizwa pale kwamba ni mbia wa kampuni, kumbe hana chochote, anapewa tu kamshahara.

Mheshimiwa Spika, adhabu kubwa inakuja katika kipande hiki ili kuifanya nchi na watu wetu, wananchi wa Tanzania waweze kunufaika na uwekezaji huu mkubwa ambao unakuja katika marekebisho haya. Kipande hiki nimeona nikisemee na ndiyo maana leo Mwanasheria Mkuu yupo, kaja na sheria hii, nami nakubali na ninaunga mkono. Naomba nishawishi Bunge lako Tukufu, likubali marekebisho haya kwa sababu ya manufaa makubwa sana kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ndogo ya tatu ambayo nitaitolea maelezo kwa kiasi kidogo ni Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha. Sheria hii ilikuwa imeweka kiwango maalum cha mtaji wa benki. Kulingana na namna uchumi uavyokwenda na mabadiliko ya dunia, unapoweka kiwango kwenye sheria, unamnyima fursa Governor wa Benki Kuu kuamua kutokana na upepo uliopo huko duniani, lakini kutokana na ukwasi na namna ambavyo Taasisi za Fedha zinavyojiendesha kulingana na dunia inavyokwenda, kwa hiyo, marekebisho haya, yanampa mamlaka Governor wa Benki Kuu kupitia kanuni, kuweka kanuni na kwa kipindi fulani, kwamba sasa tutakwenda kuweka benki katika nchi hii, uje na mtaji wa kiasi hiki.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kuna namna nyingi ambazo zina ufafanuzi, sitaki kwenda sana huko.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hii ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, na nishawishi Bunge lako likubali kupitisha Marekebisho haya kwa nia njema na dhamira njema kabisa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Agnes Lambati Kaiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ajiandae.

MHE. AGNES L. KAIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kwa uchache niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika marekebisho ya Sheria ya Benki na Taasisi za Kifedha, Sura ya 342 kifungu cha 21 ambacho kinapendekeza marekebisho ya sheria katika kipengele cha 17 ambayo ni sheria mama kwa kukifuta na kukiandika upya ambacho kinapaswa kusomeaka kama ifuatavyo, naomba kunukuu: *“Kila benki au taasisi ya fedha itatakiwa kuwa na kiwango cha chini cha mtaji na kuhakikisha kuwa nyakati zote kiwango hicho hakipungui kadiri itakavyoelekezwa na benki kuu.”* Mwisho wa kunukuu.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwanza ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na nimeshiriki kuupitia huu Muswada pamoja na wenzangu na mwisho wa siku sasa upo mbele yako kwa ajili ya kujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, mtazamo au maoni ya Kamati katika Muswada huu ilikuwa ni kwamba Muswada utaje moja kwa moja kiasi halisi ambacho Benki au taasisi za fedha zinapaswa kuwanacho wakati wanaendesha shughuli zao. Maoni haya au mtazamo wa kamati ulikuwa ni kwa nia njema ili mwisho wa siku kuondoa changamoto mbalimbali ambazo kwa njia moja ama nyingine zingeweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sana, nimepitia jedwali la marekebisho la Serikali, sijaweza kuona kifungu hiki cha 21 kikionesha marekebisho yoyote ambayo yatasababisha kifungu hiki sasa kutumika katika ustawi mzima wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika Kamati Serikali kinagaubaga na ikasema kwamba kiwango hiki kitatajwa katika kanuni mbalimbali ambazo zitaenda kutungwa ili mwisho wa siku kiweze kutekelezeka. Serikali haikuona umuhimu wowote Muswada huu kuingizwa moja kwa moja kwenye sheria kwamba hiki kiwango kitajwe sasa kwa uwazi kwamba ni Shilingi ngapi *exactly* ambayo taasisi hizi zinapaswa kuwa nayo?

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya Serikali ndani ya Kamati, Serikali ilisema kinagaubaga kwamba, kiasi cha

2 NOVEMBA, 2022

Shilingi bilioni 15 ndicho kiasi ambacho ni *minimum capital* ambayo taasisi na benki wanapaswa kuwa nacho.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu na kutambua kwamba ziko benki ambazo zina sura ya kitaifa, lakini pia zipo taasisi za kifedha na baadhi ya benki ambazo zina-*operate* shughuli zake za kiuchumi kwa maana ya kukopesha fedha kwa wananchi pasipo kutumia dhamana au amana za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, kuwawekea kiwango kimoja kwamba sasa wanapaswa kuwa na Shilingi bilioni 15 za Kitanzania. Kwa upande wangu naona kwamba hapa sio sahihi, kwa sababu tunatambua zipo taasisi za fedha na wengine tumo katika hizo taasisi, zinatuhudumia. Tunatambua kwamba hizi taasisi unakuta ni mtu binafsi kabisa, ametafuta Mtaji wake, amepambana huku na kule au ni kikundi kimeji-*organize*, kimefungua taasisi ya fedha kwa ajili ya kukopesha wananchi, lakini hakikusanyi amana yoyote kutoka kwa hao watu ambao anaenda kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, kupitia Muswada huu, ikiwa sasa tutasema na taasisi hizo zinapaswa kuwa na mtaji wa Shilingi bilioni 15, naona sasa tunapoelekea tunaenda kuondoa kabisa hizi taasisi ambazo kimsingi zimekuwa ni mkombozi kwa wananchi na hususan kwa Wabunge wenzangu ambao tunatoka vijijini. Taasisi hizi zimekuwa ni faraja na msaada mkubwa kwa wananchi wetu na wapiga kura wetu.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, taasisi hizi kwanza hazina masharti magumu. Kama tunavyofahamu, Watanzania asilimia kubwa ni wanyonge, hawana dhamana, hawana nyumba, hawana viwanja wala magari. Sasa kupitia taasisi hizi wananchi wameweza kujikomboa kwa kukopa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tunapokuwa tunakwenda kukubaliana na mapendekezo ya Serikali kwamba utaenda kuwekwa kwenye Kanuni, mwisho wa siku tukipitisha Muswada huu, moja kwa moja taasisi zote za kifedha bila kujali hali zao za kiuchumi, bila kujali kwamba taasisi hizi hazichukui chochote kile kutoka kwa wananchi, bali zina-*deliver service* tu kwamba nina mtaji wangu, sasa nakopesha wananchi Shilingi laki moja, laki mbili au laki tatu.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba taasisi hizi ndogo mdogo za kifedha zina-*operate* kwa kuangalia *nature* ya watu zinaowahudumia. Mfano, kule kijijini ninakotoka, haiwezekani ukaenda kukutana na mteja ambaye anasema anahitaji Shilingi milioni 20, Shilingi milioni 30 au Shilingi milioni 50. Kwa hiyo, unapoilazimisha ile taasisi kwamba wewe ni lazima uwe na mtaji wa Shilingi bilioni 15 ili uweze ku-*operate*, hata hao wateja huko vijijini huwezi kuwapata. Pia tutakuwa tumefunga mlango na kufungua mlango wa wawekezaji wakubwa kutoka nje, au ndani ya nchi ambao ni wachache sana watakaokwenda kushikilia uchumi, jambo ambalo siyo jema kwa mustakabali mzima wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba uchumi imara ni ule ambao unamilikiwa na wananchi wote. Sasa ili

2 NOVEMBA, 2022

uchumi huu umilikiwe na wananchi wote, hatuna budi kuangalia suala hili. Nikubaliane kwamba Benki zenye sura ya Kitaifa lazima zidhibitiwe kwa sababu zimebeba dhamana/amana za wananchi. Ila hizi taasisi ndogo ndogo na baadhi ya benki ambao zimejipambania zenyewe, zimejikwamua; mtu anakwambia sasa nina mtaji huu nakwenda kuwakopesha wananchi, sheria hii isifanye kazi kwao na badala yake uangaliwe utaratibu mwingine ambao utaweza kutumika ili kuhakikisha taasisi hizi zinaendelea siyo tu kuwa msaada, bali kuhakikisha zinasaidia wananchi wetu huko vijijini ambao uhitaji wao ni wa fedha ndogo ndogo kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nieleze madhara ambayo naona yatatukumba kama nchi ikiwa tutaruhusu huu utaratibu wa kwenda kutunga hizi kanuni pembeni. Sote tunatambua kanuni zinatungwa nje ya uwepo wa Bunge na zinapotungwa nje ya uwepo wa Bunge, *which means* sisi kama Bunge tunakuwa tumekaa pembeni ili kuweza kudhibiti watunga hizo Kanuni wasiweze kutunga Kanuni ambazo mwisho wa siku haziangalii maslahi mapana ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, niseme kwamba tukiruhusu huu utaratibu twende nao kama mapendekezo yalivyokuja, niseme kwamba, cha kwanza, taasisi zote ambazo hazina uwezo wa hizo Shilingi bilioni 15 *automatically* tutakuwa tumeziona katika uwanja wa huduma, jambo ambalo siyo jema sana kwa sababu mwisho wa siku huwezi ukakuta CRDB Bank, NMB, sijui

2 NOVEMBA, 2022

Barclays ukazikuta huko *interior* kwako Mbeya ndanindani kule kabisa. Haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine nilikuwa najaribu kutafakari jambo hili; mimi kama Mbunge au wewe mwenyewe, *the way* unavyowapenda watu wako wa Mbeya, ukaamua kwamba kuanzia sasa nataka nikafungue kitaasisi cha fedha kwa ajili tu ya kuwahudumia wapiga kura wangu wa Mbeya, halafu unaambiwa *you need fifteen billion* kwa ajili tu ya kuwakopesha wale akina mama wa mboga mboga Shilingi 50,000/=, Shilingi 100,000/= na vitu kama hivyo. Haiwezekani. Mwisho wa siku hata hizo fedha kama utakuwanazo hutaweza kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naweka angalizo kwamba tuangalie namna ya kudhibiti hizi Benki zenye sura ya Kitaifa, lakini turudi chini tuangalie hizi taasisi ambazo zimekuwa ni mkombozi wa Watanzania kwa kipindi chote, tuone namna ya kuweka moja kwa moja sheria kwenye Muswada huu ambayo itasema moja kwa moja kwamba taasisi hizi hazihitaji kubanwa ndani ya hii Sheria ya kwamba lazima wawe na shilingi bilioni 15.

Mheshimiwa Spika, vile vile tukubaliane kwamba taasisi hizi ndogo ndogo za kifedha zimesaidia kwa asilimia kubwa sana kuondoa umasikini kwa wananchi wetu hususan kule vijijini. Tukienenda na huu utaratibu, ina maana tunaenda kukaribisha umasikini zaidi kuliko umaskini tulio nao sasa kwa wananchi wetu ambao wengi wako kule vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikisikia hapa Waheshimiwa Mawaziri tukiwemo na sisi kwamba mama

2 NOVEMBA, 2022

yetu Mheshimiwa Samia anaupiga mwingi, na nikubali kwamba Mama Samia anaupiga mwingi. Sisi kama wanawake pasipo kujali vyama vyetu, tunasema jambo la mwanamke ni jambo la kwetu sote. Kwa hiyo, hatuna budi kumuunga mkono mwanamke mwenzetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa mfumo huu tunaokwendanao kwenye huu Muswada, kweli tutakuwa tunamsaidia mama yetu Mheshimiwa Samia? Tunapokwenda kudidimiza taasisi ndogo ambazo zimekuwa ni mwarobaini kwa wananchi wetu wanyonge huko chini, sidhani kama tutakuwa tunamsaidia Mheshimiwa Rais wetu. Pia kingine hii inaweza ikaenda kuwa ni bomu kubwa zaidi kuliko hata tozo. *(makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuomba kupitia Bunge lako tukufu kwamba suala la *minimum capital* liangaliwe kwa hizi Benki zenye sura ya Kitaifa na siyo vinginevyo, lakini sheria ya hizi benki na taasisi ndogo ndogo iingizwe moja kwa moja kwenye hii sheria na iseme waziwazi kabisa kwamba watu hawa hawatabanwa kabisa na hii sheria ya Shilingi bilioni 15.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, halafu mtoa hoja ajiandae.

MHE. ABDALLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kuanza kwa kukushukuru kwa dhati kwa kunipatia nafasi ili kuchangia machache kwenye

2 NOVEMBA, 2022

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika ningependa kuanza kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwanasheria Mkuu pamoja na Serikali na Wizara za Sekta ambazo kwa kipindi ambacho tupo kwenye Kamati tulikuwa tunajadiliana kwa kina. Kwa hakika wametupa ushirikiano mkubwa sana na kazi kubwa ya Muswada huu, imefanyika na ikakamilika ndani ya Kamati. Mambo mengi tuliyokuwa tumeyashauri yalipokelewa na wenzangu hawa walionitangulia leo wamezungumza kwa msingi kwa yale ambayo yalikuwa yana utata kidogo, lakini kwa ujumla wake tumekubaliana na tumepata ushirikiano mkubwa na wamepokea mapendekezo yetu. Kwa hiyo nimefilisika, sina mengi sana ya kuzungumza ndio Muswada huu ilanangependa kuzungumza kwa ujumla katika sekta hizi ambazo zimeathirika na zimeguswa na hizi sheria.

Mheshimiwa Spika, eneo kubwa la uwekezaji katika hizi sheria limegusa Sheria ya Madini na ningependa mazungumzo yangu yagusie hapo. Uwekezaji kwa ujumla wake katika nchi yoyote unapenda *stability* (utulivu), *certainty* (uhakika) hasa maeneo ambayo uwekezaji wake unagusia fedha nyingi sana. Sekta ya Madini unawekeza na ina-*contribute* katika uchumi wetu na inawekezwa fedha nyingi sana, mabilioni ya dola. Wawekezaji ambao wanawekeza fedha nyingi sana wana mambo ya msingi ambayo yanawavutia. La kwanza miongoni mwao, ni sera ambayo ina utulivu na la pili ni sheria ambazo zinadumu kwa muda. Ukiona eneo linabadilishabadilisha sera au kuna

2 NOVEMBA, 2022

marekebisho ya mara kwa mara ya sheria ina viashiria vikuu viwili:-

Mheshimiwa Spika, kiashiria cha kwanza, inaonesha ushirikishwaji haukuwa mkubwa na la pili ile dira ya awali pengine haikukaa sawa. Sasa yangu ilikuwa tu kutoa tahadhari, tuangalie sheria zetu hasa katika maeneo ambayo uwekezaji ni wa fedha nyingi. *Policy certainty and legislative stability* ni vitu vya msingi sana katika kukuza uwekezaji katika sekta hizi kubwa zinazogusia fedha nyingi, kwa mfano, Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kiashiria cha pili ni *business environment*, uwekezaji unataka *business environment* ambayo ni nzuri. Kuna suala mtambuka la *blueprint*, ni mfumo mzima wa kuboresha *business environment* ili tuwalete wawekezaji. Limewekwa bayana, limezungumzwa lakini kwa bahati mbaya utekelezaji wake ambao unatakiwa utekelezwe kissekta pamoja na Sekta hii ya Madini umekuwa hafifu, kwa hakika inabidi tujitahidi tutafute jinsi ya kuhakikisha *business environment* katika hizi aekta inakaa sawa, inatulia na inaondoa vikwazo vidogovidogo ambavyo vinaweza kuleta ukakasi katika *investment*.

Mheshimiwa Spika, la tatu kama ushauri, ikibidi mabadiliko ya sheria yafanyike au mabadiliko ya sera yafanyike basi tuwe tunazingatia mambo kama matatu makuu. La kwanza, ni usimamizi wa utawala bora, mabadiliko yaendane na mfumo wa utawala bora. La pili, kuna *extensive consultation* yaani ushirikishwaji wa sekta husika ambao wa uhakika na la tatu *clear communication*,

2 NOVEMBA, 2022

yale maamuzi na mabadiliko yanayofanyika yazungumzwe na yajadiliwe kwa uwazi ila sekta yenyewe itulie.

Mheshimiwa Spika, nazungumza hivi kwa sababu uwekezaji mkubwa katika sekta yoyote unatokana na fedha ambazo ni za kukopa katika masoko ya fedha ya kimataifa. *Perception* ndogo ya mabadiliko inaathiri sana uwekezaji na *investment environment* yetu ambayo tungependa iboreke ili tupate huo uwekezaji. Mheshimiwa Rais alitupa na aliwapa ya Madini *challenge* ya kuhakikisha Sekta ya Madini inachangia *GDP* yetu kwa 10% ya kipato chetu. Sasa kwa minajiri hiyo lazima tuwe makini sana katika ubadilishaji wa sera na hasa katika ubadilishaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo ya ujumla haya *specific* ambayo tumeyapitia, tumeyazugumza kwa kina na maboresho yetu yalikuwa katika mazingatio hayo ambayo nimeyazungumza kwa mapana yake na kwa hakika tumepata ushirikiano mkubwa wa Serikali pamoja na *Attorney General*.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuunga mkono hii hoja na kuwaasa wenzangu kuiunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana Waziri wa Maliasili na Utalii atafuatiwa na mtoa hoja.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini pia kuwashukuru wachangiaji wote. Tumepata wachangiaji takribani wanne

2 NOVEMBA, 2022

na kimsingi wote wanaungana na marekebisho haya ya Sheria hii ya Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie sehemu mbili, kwanza kuna Sheria ya Malikale, Sura ya 333. Eneo la pili, ni Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura 281. Nashukuru sana maoni ya Kamati wanaunga mkono marekebisho haya. *Reform* kubwa ambazo tunakuja nazo Wizara ya Maliasili na Utalii ni madhumuni ya kusajili makumbusho. Tunasema sasa hivi kuna madhumuni ya kusajili makumbusho ambazo zinaanzishwa na taasisi, asasi au watu binafsi. Huko nyuma makumbusho zetu nyingi zilikuwa ni za umma, ni za kitaifa, Makumbusho ya Taifa, lakini sasa tunakwenda na *reform*, tunasema tunaweza kuwa na makumbusho za taasisi na lazima zisajiliwe, lakini pia tunaweza kuwa na makumbusho za asasi mbalimbali lakini pia watu binafsi. Kwa hiyo hata mimi mwenyewe naweza nikaanzisha makumbusho ya Pindi Chana. Watu binafsi ruksa, kazi ulizofanya taasisi kwa maslahi ya kuelimisha umma, kwa maslahi ya mafunzo na tafiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo haya ni mazao mapya ya utalii na hususan baada ya uzinduzi wa ile *program* ya Tanzania, *The Royal Tour*. Huko tunakoenda lazima tuongeze watalii tumesema ifikapo takribani 2025, tupate watalii milioni tatu sasa lazima tuje na mazao mapya. Kwa hiyo sasa Watanzania milango iko wazi tunajua tuna Watanzania milioni 61 ruksa kuanzisha makumbusho za Taasisi, za Asasi na za watu binafsi lakini lazima zisajiliwe. Katika kusajili tulisema kwamba endapo mtu hajasajili itakuwa ni kosa na kama hajasajili ikiwa ni kosa atatozwa faini au kifungo. Tunashukuru maoni ya Kamati

2 NOVEMBA, 2022

wametuingia kwamba badili ya kutoza faini ni 5,000,000 hadi 20,000,000 tupunguze iwe ni 1,000,000 hadi 5,000,000 na katika Kamati tumelijadili tukiwa na Mwanasheria Mkuu na hili tumeafiki Serikali tumekuja na marekebisho.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusu kifungo kwamba eneo hili pia tuanze mtu akienda kinyume adhabu yake iwe ni kifungo cha miezi mitatu hadi mwaka mmoja na tumelichambua vizuri tunaafiki. Kwa hiyo tunakubaliana na Kamati na wadau waliochangia hapa .

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhusiana na Bodi. Kwenye Kamati tulijadiliana vizuri kwamba kutakuwa na bodi ambayo itateuliwa na Waziri mwenye dhamana. Bodi ya kuteua Wajumbe wa Bodi ya Makumbusho na tumeshauriwa vizuri kabisa kwamba ni vizuri wakati wa kuteua tuzingatia *gender*. Ukweli ni kwamba wakati wa uteuzi suala hili la kuzingatia *gender* ni moja ya kigezo muhimu, lakini Kamati ikashauri pamoja na kwamba tunatekeleza lakini kiandikwe bayana na sisi hatujaona changamoto ya kukiandika bayana. Kwa hiyo tunakubaliana na maoni ya Kamati kwamba wakati wa kuteua *gender* izingatiwe na hasa tukizingatia idadi ya watu ni milioni 61 na 51% ni wanawake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Dkt. Feleshi uje uhitimisha hoja yako. *(Makofi)*

2 NOVEMBA, 2022

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana tena kwa kunipatia fursa ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, tumepata faida ya kuwa na wachangiaji watano; Mheshimiwa Noah Lemburis Mollel, Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi na Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana. Naomba nianze kwa kuishukuru sana Kamati yenye dhamana na Muswada huu. Nikiri tu kwamba tunapokuwa mbele ya Kamati, Serikali inawajibika kuliwezesha Bunge kuelewa maudhui na makusudio ya Sheria inayokusudiwa kutungwa au kurekebishwa. Kwa maoni yote ambayo yameletwa na Kamati kupitia kwa Mwenyekiti wake Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, yenye Wajumbe mahiri 23, tumeyapokea na tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulikuwa na malengo; kusudio kubwa ilikuwa ni kuhuisha na kuongeza thamani ya sheria zilizotungwa na Bunge hili siku zilizopita kwenye vikao tofauti. Kwa hiyo, yote ambayo Wajumbe wa Kamati wamechangia ndio mambo ambayo yalijiri mbele ya Kamati. Tuliingia kwenye Kamati siyo kwa uelewano huu, lakini jedwali la Serikali linaonesha lengo la Serikali kuhakikisha inaleta Bungeni hapa Muswada unaokidhi matazamia na yale mambo yote mema ambayo Serikali yetu na Tanzania yetu inatamani yawe.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kaiza ameongelea suala la kima cha chini cha mtaji. Atakumbuka tulipokuwa mbele ya Kamati tulieleza vigezo ambavyo Benki Kuu inavitumia ili viendane na matakwa na viwango vya kimataifa kwamba ukiweka viwango bila kufuata zile *standards* leo, tunaweza tukajikuta uwekezaji wetu undingia kwenye mkinzano na matakwa mengine. vilevile Serikali inaweza ikajikuta inashindwa hata kuwanyanyua hawa wawekezaji, hizo taasisi ndogo wanazosisema.

Mheshimiwa Spika, akumbuke lile kabrasha kubwa la vigezo, lakini hoja ninayoileta katika maelezo yangu ya kuhitimisha hapa ni kwamba, kanuni zinapotungwa na Waziri lazima zifuate sheria mama iliyopitishwa na Bunge. Vilevile tusiendeleze hiyo dhana kwamba Bunge halishiriki kwenye mchakato wa kuhakikisha kwamba tuna kanuni nzuri. Kanuni zinapoanza kuchakatwa kuna uhusishwaji ambao hufanyika na nafikiri ndio mwelekeo wetu wa Serikali sasa kwamba kila tukija na sheria na kanuni ziwe tayari.

Mheshimiwa Spika, pale tunapokwenda kinyume Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo na Kanuni inatukagua na kuzikagua sheria zetu. Kwa hiyo, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba kanuni zitakazowekwa na Benki Kuu hazitakuwa kikwazo katika kuendeleza sekta na taasisi za kifedha. Kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Kaiza, nichukua dhamana ya Benki Kuu na Serikali kuwa wawazi kwa Kamati ya Bunge kuangalia kanuni zitakavyoweza kutungwa kwa sababu Serikali haina kitu cha kuficha, kwa sababu hata tukificha Kamati ya Sheria Ndogo itakuja

2 NOVEMBA, 2022

kutuumbua hapa na mmeona kwa taarifa ya Mkutano uliopita tunaendelea na kiwango chetu cha kufuata masharti ya sheria mama kinaongezeka

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nishukuru sana Bunge lako kwa jinsi lilivyoshiriki kuiongoza Serikali na maboresho makubwa ambayo tunayaona. Kwa mfano, kwenye Muswada huu yapo maeneo ambayo moja kwa moja yanaonesha nia njema na kama njia ya kuhakikisha kwamba tunaenda sambamba na kufungua fursa za uwekezaji na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa marekebisho ya Sheria ya Malikale amesema hapa Mheshimiwa Pindi Chana, kama makumbusho ya mtu binafsi yalikuwa hayatambuliki Serikali sasa inafungua waratibiwe ili wakiratibiwa anapokuja mtalii labda anakwenda kwenye *museum* iliyokwishasajiliwa aoneshwe na zile za watu binafsi ili akiweza kuzifikia itaongeza kipato cha yule mtu lakini kutambulika kwao vilevile kutaiwezesha Serikali kuwajengea uwezo na elimu ya namna ya *ku-handle*.

Mheshimiwa Spika, yameelezwa mambo ya uchenjuaji, tumeyaweka vizuri kwenye sheria hii. Tusingejali hawa wachenjuaji wadogo kuwawekea utaratibu wa kisheria licha ya kupoteza mapato ya Serikali, lakini ni kama kuwatelekeza na kuweka milango ya wao kunyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, eneo la *local content* tuliloliweka, nafikiri wote tunakubali si vizuri unakuwa na kampuni ya kigeni hapa ambayo ipo hapa kisheria na inafanya kazi zake kisheria, inunue mahitaji kama nyama, maziwa kutoka

2 NOVEMBA, 2022

nchi nyingine wakati hivi vitu vinapatikana hapa. Kwa hiyo, Waheshimiwa wataona adhabu inayowekwa pale lengo ni kulenga hawa wote ambao wamepata leseni za kufanya kazi, basi jamii inayozunguka nayo ineemeke kupitia uwepo wao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuishukuru sana Kamati, kuwashukuru Wabunge wote, lakini vilevile nikushukuru wewe mwenyewe, bila kuacha kushukuru na naendelea kusema kwamba uthubutu unaofanywa na hawa wenyeviti wa kamati waendeleo kufanya hivyo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele imegonga Mheshimiwa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa upande Serikali tutaendelea kwenda na watu wote ambao wanatakiwa kutoa ufafanuzi ili Kamati zetu zipate yote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naomba uniruhusu nitoe hoja, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Tutaendelea na utaatribu wetu.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

2 NOVEMBA, 2022

KAMATI YA BUNGE ZIMA

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2022*)

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 14

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

2 NOVEMBA, 2022

Kifungu cha 15

Kifungu cha 16

Kifungu cha 17

Kifungu cha 18

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza Kifungu Kipya cha 19.

Kifungu Kipya cha 19

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 20

Kifungu cha 21

Kifungu cha 22

Kifungu cha 23

Kifungu cha 24

Kifungu cha 25

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 26

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

2 NOVEMBA, 2022

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 29
Kifungu cha 30

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 34

*(Kifungu vilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40

2 NOVEMBA, 2022

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 41

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 42

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 43

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 44

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

NDG. BAKARI KISHOMA –KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza Kifungu Kipya cha 45.

Kifungu cha Kipya 45

(Kifungu kilivyotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Kifungu cha 45

Kifungu cha 46

2 NOVEMBA, 2022

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

NDG. BAKARI KISHOMA –KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapendekeza kufuta Sehemu yote ya Nane ya Muswada huu ambayo ni Kifungu cha 47 mpaka 51.

MWENYEKITI: Kufutwa kwa Sehemu ya Nane ya Marekebisho ya Sheria kunafikiwa.

Kifungu cha 47

Kifungu cha 48

Kifungu cha 49

Kifungu cha 50

Kifungu cha 51

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilifutwa)

NDG. BAKARI KISHOMA –KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Marekebisho hayo Serikali inapendekeza kupanga upya kifungu cha 19, 46 sasa isomeke Kifungu cha 20 mpaka 49.

MWENYEKITI: Kupangwa upya kwa Vifungu 19 mpaka 49 na kuwa vifungu vya 20 mpaka 49.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

2 NOVEMBA, 2022

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

T A A R I F A

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2020, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) Mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.3) Bill, 2022*), Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya Mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.3) Bill 2022*), kama ulivyorekebisha katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

2 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa nitawahoji kwa utaribu wetu Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 3 Bill 2022*).

Waliofiki wameshinda. (*Makofi*)

Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Zipatazo Saba kwa lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa Utekelezaji wa baadhi ya Masharti katika Sheria hizo (*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to keep the Laws Updated with some Challenges Observed in its Implementation*).

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) Mwaka 2022 (The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill 2022) Ulipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumeshasoma Muswada huu kwa mara ya tatu na kwa sehemu ya utungwaji wa Sheria kama ambavyo Katiba imetupa

2 NOVEMBA, 2022

mamlaka hayo, basi sisi kama Bunge tumemaliza kutunga sheria hii, kwa maana ya kwamba imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) Mwaka 2022 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill 2022*) umepitishwa rasmi na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu unazungumzia mambo mengi ambayo yako chini ya Wizara mbalimbali kwa hivyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali nae amefanya kwa sehemu yake, nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa sheria hizi, pale ambapo Rais atakuwa amefanya kwa sehemu yake kwa maana ya kusaini Muswada huu ili uwe sheria kamili.

Waheshimiwa Wabunge, nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawaziri wanaohusika kwa ushirikiano ambao wameutoa kwa Kamati katika mchakato mzima wa kutunga Sheria hii. Pia, niwashukuru sana Kamati yetu kwa kazi nzuri walioifanya, mabadiliko yote Waheshimiwa Wabunge ambayo yalikuwa yanasemwa hapo kwamba Vifungu fulani fulani vimefutwa, Vifungu fulani vinaongezwa, Vifungu vingine vina marekebisho ni kazi nzuri ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kwa hiyo tunawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri ya kuliongoza Bunge letu kwenye mwelekeo ambao tunatunga sheria ambazo zitawasaidia wananchi na pia kuisaidia nchi yetu kupiga hatua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii tutaendela na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

2 NOVEMBA, 2022

HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kuhusu
Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya
Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa
Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za
Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa
zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za
Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

na

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa
Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma
kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*Public Accounts Committee – PAC*) na kwa niaba yake amekuja Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Japhet Hasunga. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa hapo mbele ulipopita ndiyo mtihani, ilibidi uwe umezunguka kulee, nilishatoa maelekezo jinsi ya kupita hapa mbele ya Siwa, ndiyo maana watu walikuwa wanachekea, usije kusema watu wanacheka nini, ni kwa sababu nilishakataza kupita hapo mbele ya Siwa. Karibu

2 NOVEMBA, 2022

sana Makamu Mwenyekiti uje uwasilishe mawazo ya Kamati yetu ya PAC. Karibu sana.

MHE. JAPHET N. HASUNGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021 na kuliomba Bunge liipokee na kujadili. Madhumuni ya Taarifa hii ni kulijulisha Bunge lako Tukufu, iwapo matumizi ya Fedha za Umma yamefanyika kwa namna ilivyokusudiwa na Bunge na kwamba matumizi hayo yamezingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Kamati zilifanyika kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Muhtasari wa Shughuli za Kamati. Katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa za hesabu zilizokaguliwa za Mafungu 12 ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma 21, Wakala za Serikali mbili, Kaguzi Maalumu nne, Mabonde ya Maji mbili na kaguzi za ufanisi nne.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili; Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji. Matokeo ya uchambuzi. Uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mafungu mahususi ya Serikali kuu na Mashirika ya Umma pamoja na mahojiano ya Maafisa Masuuli, ulibainisha hoja katika maeneo 13 kuhusu

2 NOVEMBA, 2022

matumizi yenye dosari na usimamizi wa fedha za Umma. Hoja hizo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakisi ya ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kiasi cha Shilingi Trilioni 2,811.4 Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni 2021. Kwa upande wa makusanyo kwa Tanzania Bara na Zanzibar, kiasi halisi kilichokusanywa kilikuwa trilioni 17,897.8 iikilinganisha na makadirio ya kiasi cha shilingi trilioni 20,709.3 Kwa msingi huo, kulikuwa na nakisi ya makusanyo ya kiasi cha shilingi trilioni 2,811.4. ambayo ni sawa 14% ya makadirio ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, mapungufu yaliyosababisha *TRA* kutokufikia malengo ya makusanyo ni pamoja na haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mapungufu katika mfumo wa *ITAX* hususan katika kushughulikia madeni ya kodi. Mfano kwa mwaka huu tunapotoa taarifa hii kulitokea dosari za madeni ya kodi kwa Mikoa ya Morogoro na Arusha ya kiasi cha shilingi bilioni 11,512.6 ambayo yanatokana na dosari katika mfumo wa usimamizi wa kodi, kutoshughulikiwa ipasavyo kwa madeni ya kodi.

Mheshimiwa Spika, mathalani kwa mwaka 2020/2021 kulikuwa na ongezeko kubwa la asilimia karibia 95 ya madeni ya kodi. Ongezeko hilo lilitoka shilingi trilioni 3,875.9 hadi shilingi trilioni 7,542.1. Mapungufu mengine ni pamoja na kukadiria chini ya kiwango cha kodi ya mapato.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, dosari katika usimamizi wa mikataba na athari zake katika Matumizi ya Fedha za Umma. Eneo lingine ambalo uchambuzi wa Kamati ulibainisha uwepo wa upotevu mkubwa wa fedha za Serikali ni katika mapungufu katika usimamizi wa mikataba. Uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu za *TANROADS* ulibaini kuwa Wakala unadaiwa madai ya malipo ya shilingi bilioni 664.35 kutoka kwa wakandarasi na wahandisi washauri wa ujenzi, hivyo kupelekea Wakala husika kutozwa riba ya ucheleweshaji malipo ya shilingi bilioni 68.73 kuendana na vifungu vilivyopo katika mikataba ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo usimamizi wa mikataba umesababisha hasara kwa Serikali ni katika Wakala wa Taifa wa Chakula (*NFRA*). Kamati ilibaini kuwa, mnamo Tarehe 22 Desemba 2016, *NFRA* iliingia mkataba Kampuni ya *FEERUM SA*, kwa ajili ya usanifu, ugavi, ujenzi, ufungaji, upimaji na uagizaji (*Commissioning*) wa majengo ya *silos*, maghala na ukarabati wa majengo yaliyopo vituo vya Ruvuma, Njombe, Songwe, Dodoma, na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba husika, gharama za mradi ilitakiwa kuwa dola za Marekani 33,140,791.81, na mradi ungekamilika Tarehe 09 Disemba 2017. Hata hivyo, baadae muda wa utekelezaji uliongezwa hadi Tarehe 31 Disemba 2020. Hadi kipindi hicho, mkandarasi alikuwa tayari amelipwa kiasi cha Dola za Marekani Milioni 21.46, sawa na 65% ya gharama za mkataba, hadi muda wa ukaguzi, mnamo Disemba 2021.

Mheshimiwa Spika, uhakiki uliofanywa na CAG kwenye

2 NOVEMBA, 2022

maeneo ya ujenzi mnamo Disemba 2021, ulibaini kuwa mradi ulikuwa bado haujakamilika, ingawa muda wa kandarasi wa Tarehe 31 Disemba 2020 ulimalizika mwaka mmoja uliopita.

Mhehsimiwa Spika, hoja nyingine kuhusu dosari za usumamizi wa mikataba zinahusu TANESCO na Kampuni ya *Symbion*. Mnamo Tarehe 07 Julai 2001, Kampuni ya *Symbion Power* iliingia mkataba na TANESCO wa kukodisha mitambo ya uzalishaji umeme iliyopo eneo la Ubungo Dar es Salaam. Taarifa ya CAG inabainisha kuwa ilipofika Tarehe 24 Mei, 2016 kulijitokeza kutoelewana kati ya TANESCO na Kampuni ya *Symbion* hali iliyopelekea TANESCO kuitaka Kampuni ya *Symbion* kuondoa mitambo yake kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uamuzi huo kujitokeza masahuri mawili ya madai dhidi ya TANESCO yalifunguliwa, madai hayo toka kwa Kampuni ya *Symbion* na wanahisa wa *Symbion* yalifunguliwa Chemba ya Kimataifa ya Biashara (ICC) na Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi ya Migogoro ya Uwekezaji (ICSID).

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG inaendelea kufafanua kuwa ilipofika mwezi Julai, 2018 pande zote Mbili zilianza majadiliano ya kutatua mgogoro huu nje ya Mahakama. Mnamo Tarehe 21 Mei, 2021, pande hizo mbili zilifikia makubaliano (*Deed of Settlement*) ambapo makubaliano yalihusu malipo ya Dola za Marekani 153,434,206.83 bila ya kujumuisha kodi na gharama nyinginezo. Hivyo, TANESCO imelazimika kulipa fedha hizo kutokana na kuvunjwa kwa mkataba.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, hali ya ukwasi katika baadhi ya Taasisi za Kimkakati za Serikali yaani mashirika ya *TPDC*, *TANESCO* na *STAMICO*. Kamati ilijielekeza kwanza kwa kuangalia uwiano wa mtaji na madeni (*Debt to equity ratio*) kwa mashirika matatu ya Kimkakati ya Serikali ambayo ni *TPDC*, *TANESCO* na *STAMICO*. Kwa ujumla uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mashirika hayo matatu yana changamoto ya mtaji ambayo mali za muda mfupi hazina uwezo wa kugharamia madeni. Kwa msingi huo mashirika hayo yanategemea zaidi mikopo ili kuendesha shughuli zao za kila siku. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa *TANESCO*, *TPDC* na *STAMICO* wanatumia gharama kubwa za fedha za umma kulipia riba za mikopo katika uendeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa kaguzi maalum. Ukaguzi maalumu wa mradi wa *REA* awamu ya Pili Mkoa wa Mara, ambapo *REA* ilipata hasara ya shilingi milioni 329.62.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa, *REA* ilifanya malipo ya shilingi 106,771,469.28 (ikijumuisha *KOT*) kwa mkandarasi kwa kuzingatia hati za kuwasilisha vifaa (*delivery notes*) zilizokuwa na udanganyifu. Hii ilitokana na ukweli kwamba mzalishaji wa vifaa husika alikana kutoa hati hizo kwa Kampuni ya *DERM Electrical Tanzania Limited*. Aidha, malipo ya kiasi cha Shilingi 91,115,356.72 (ikijumuisha *KOT*) hayakuthibitika uhalali wake kufuatia mkandarasi wa Kampuni ya *DERM Electrical Tanzania Limited* kutumia hati zake za uwasilishaji wa vifaa badala ya mzalishaji na kutokuwepo kwa hati halisi zinazothibitisha kupokelewa kwa vifaa husika katika eneo la mradi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa Kampuni ya *DERM Electrical Tanzania Limited* ilinunua na kuvitumia vifaa vyenye thamani ya shilingi 329,620,735.80 (ikijumuisha KOT) wakati wa utekelezaji wa Mradi wa REA awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi Maalumu wa Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji Kuhusu Viza za Stika Bandia. Ukaguzi ulibaini kuwa wageni 33,558 waliwasili nchini kupitia KIA. Hata hivyo, taarifa za wageni hao ambazo ni pamoja na fomu za kuingia nchini, stakabadhi za mapokezi ya fedha, na taarifa za uwekaji fedha benki hazikupatikana kwaajili ya uhakiki. Kwa sababu hiyo, ukaguzi haukuweza kuthibitisha kiasi cha mapato ambacho Serikali ilipaswa kupata kutoka kwa wageni hao.

Mheshimiwa Spika, kufuatia dosari za kimfumo, ukaguzi ulibaini kuwa watumishi 32 wa Idara ya Uhamiaji KIA walifuta na kuziondoa kwenye kanzidata taarifa 21,208 za wageni walioingia nchini na ambao walilipa kiasi cha Shilingi 2,427,255,600. Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakikuwasilishwa benki na hivyo kusababisha Serikali kupoteza mapato ya takribani Shilingi 2,427,255,600.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukaguzi Maalumu wa Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo. Ukaguzi huu umetokana na kubainika kuwepo kwa udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani katika mapato na ubadhirifu katika ukusanyaji wa mapato wakati wa ukaguzi wa kawaida hivyo kupelekea Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuamua kufanya ukaguzi huu maalumu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu maalumu ulibaini kuwa,

2 NOVEMBA, 2022

pamoja na mambo mengine kuwa, stakabadhi za makusanyo ya maduhuli zilitolewa nje ya mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikali.

Mheshimiwa Spika, ilibainika kuwa, usajili wa wanafunzi kufanyika kabla ya uthibitisho wa malipo ya ada (Shilingi 17,742,000) na pia ubadhirifu ulitokana na matumizi ya stakabadhi zisizo halisi za kukiri mapokezi ya ada zenye thamani ya Shilingi 76,106,600. Mwisho CAG alibaini uwepo wa wanafunzi wa waliofanya mitihani bila ya kulipa ada ya shilingi 928,268,528.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ukaguzi Maalum wa Mradi wa Orio. Mradi huu ulikuwa na thamani ya Euro milioni 23 kulingana na makubaliano ya awali na baadaye thamani ya mkataba iliongezeka hadi kufikia Euro 23,819,509. Mradi huu ulikuwa umechangiwa na pande zote mbili kwa asilimia 50 kila mmoja. Mradi ulikuwa na lengo la kuboresha miundombinu ya Hospitali nchini Tanzania hasa katika huduma za uchunguzi wa mionzi na picha, huduma za akina mama na kuboresha huduma za kitabibu katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, CAG alibaini kuwa, Serikali ilichelewa kuweka mchango wake wa fedha kwenye akaunti ya Orio kiasi cha Euro 2, 900,000 hali iliyochelewesha mradi kwa kuchelewa kuanza kwa takribani kipindi cha miezi 19. Aidha, kulibainika dosari katika manunuzi ikiwa ni pamoja na baadhi ya manunuzi kufanyika bila ya kujumuishwa katika mpango wa mwaka wa manunuzi kinyume na Kifungu 75(1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, vile vile, kulikuwa na malipo yasiyokuwa na tija (*Nugatory expenditure*) ya kiasi cha shilingi 665,138,998. Malipo haya yalitokana na ucheleweshaji wa Serikali kulipa fedha kwa kugomboza mizigo toka bandarini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dosari za msingi zilizobainishwa na CAG. CAG alibainisha dosari za msingi katika matumizi ya fedha za umma katika maeneo mengine kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mapitio na uchambuzi wa kina wa Kamati pamoja na mahojiano na maafisa masuuli mbalimbali, umebaini uwepo wa matukio ya ukiukwaji wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura 348.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza katika eneo hili inahusu kutohibitishwa uwepo wa mapato ya kiasi cha shilingi 3,567,797,000 na matumizi ya kiasi cha shilingi 3,562,364,709 katika Shirika la Masoko Kariakoo kutokana na kuungua kwa Soko la Kariakoo na nyaraka zote za ushahidi kupotezwa hivyo CAG kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili katika eneo linahusu malipo ya fidia zaidi ya kiwango kilichopo kwenye taarifa ya tathmini kiasi cha shilingi 1,070,637,576 na malipo ya usumbufu shilingi 434,129,600 kulipwa na DART

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, CAG aliifahamisha Kamati kuwa hadi ukaguzi huu unakamilika hakuwa

2 NOVEMBA, 2022

amepewa nyaraka za kuthibitisha uhalali wa malipo hayo kwa wahusika 17 na hapakuwa na uthibitisho kuonesha kuwa Serikali ndiyo ilitoa idhini ya kulipa riba ya usumbufu kwa walalamikaji.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine katika eneo hili, ni kutoandaliwa hesabu na kutofanyika kwa ukaguzi wa hesabu za mfuko wa tuzo na tozo wa polisi katika Fungu 28 – Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, CAG alibaini uwepo wa kiasi cha Shilingi 35,382,216,828 ambayo ni fedha iliyowekwa kwenye akaunti Benki Kuu kutokana na mfuko wa tozo na tuzo. Hata hivyo pamoja na uwepo wa fedha hizo katika mfuko huo, CAG alibaini kuwa hapakuwa na kanuni za kusimamia uendeshaji wa mfuko huo na hesabu za mfuko hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kwa zaidi miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa umilikishwaji na uendeshaji wa makampuni ya uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (*KADCO*); baada ya uchambuzi wa hesabu za *KADCO*, Kamati ilibaini hoja inayohusu misingi ya kisheria ya uendeshaji wa *KADCO* hasa ikizingatiwa kuwa *KADCO* ni shirika la umma lakini kuna mkataba wa miaka 25 wa uendeshaji (*Concession Agreement*) wa Kampuni ya Uendelezaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro (*KADCO*). Mkataba huu ni baina ya Serikali na *KADCO* uliosainiwa tarehe 17, Julai 1998 ambapo masharti yake ulitakiwa uwe umepitiwa na kuhuishwa mwaka 2013 na unatakiwa kukamilika tarehe 16 Julai 2023.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizojitokeza za uendeshaji wa KADCO, Serikali iliamua kununua hisa zote za wanahisa wenza mwaka 2010 na hivyo kufanya Serikali kuwa mwanahisa pekee wa KADCO kwa asilimia 100. Kwa msingi huo, uhalali wa mkataba wa uendeshaji wa KADCO, (*Concession Agreement*) hauna misingi ya kisheria. Ikumbukwe kuwa Serikali ilitumia fedha za umma takribani Dola za Marekani milioni 5.3, fedha mabazo zilitokana na mkopo uliochukuliwa na mamlaka ya viwanja vya ndege TAA, kutoka Benki ya CRDB kununua hisa zote za KADCO.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Benki ya Tanzania ya Biashara (TCB) na Benki ya Maendeleo ya TIB. Katika uchambuzi wa hesabu za benki hizo za Serikali, hoja kuu mbili zilibainika kama ifuatavyo: -

(a) Ongezeko la Mikopo Chechefu (*Non Performing Loans, NPL*); na

(b) Hali ya Utoshelevu wa Mtaji

Mheshimiwa Spika, benki zote mbili hazina mtaji wa kutosha na pia zina kiwango kikubwa cha *non-performing loans* kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa za kikaguzi za ufanisi. Katika kipindi tunachokitolea taarifa, Kamati ilifanikiwa kupata na kuchambua jumla ya taarifa nne za ukaguzi wa ufanisi. Naomba kulifahamisha Bunge

2 NOVEMBA, 2022

Iako Tukufu kuwa hii ni hatua kubwa na ya mfano wa kuigwa kwa Bunge letu kuanza kujadili taarifa za ukaguzi na ufanisi. Naomba uchambuzi wa kamati kwa taarifa nne za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyiwa kazi uingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kamati ilifanya mapitio ya uchambuzi wa taarifa za fedha za mifuko ya hifadhi za jamii. Mifuko hiyo ni *NSSF* na *PSSSF*. Masuala yaliyobainika katika hesabu za mifuko hiyo hususani katika matumizi ya fedha za umma ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni hoja ya upungufu wa ukwasi katika mfuko wa *PSSSF* kulipa mafao, (*insufficient liquidity*). Uchambuzi wa kamati katika hesabu za *PSSSF* kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo ukiondoa mafao kabla ya mwaka 1999, umebaini kuwa kwa kipindi chote hicho, mfuko umekuwa ukilipa mafao kwa kiasi kikubwa cha fedha ukilinganisha na kiasi cha michango inayokusanywa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili inahusu mikopo ya muda mrefu iliyotolewa na mifuko ya hifadhi ya jamii kiasi cha takribani shilingi triloni 1.5. Deni la *NSSF* ni kiasi cha shilingi triloni 1.17 ikijumuisha deni la msingi ambalo ni shilingi bilioni 490.16 na riba ya shilingi bilioni 684.42. Kwa upande wa *PSSSF*, deni la muda mrefu hadi kufikia tarehe 30, Juni mwaka 2021, lilifika shilingi bilioni 323.98. Deni hili linahusu tasisi za Serikali na taasisi nyinginezo.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa Serikali kulipa madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii kunaathiri uwezo wa mifuko kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapungufu katika uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake. Baadhi ya maeneo ambayo yalikiuka sheria ya manunuzi ya umma na kanuni zake hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi kwa zaidi ya miaka minne kulikofanywa na TANESCO-Kihansi, hali iliyosababisha ongezeko la gharama za mradi kwa takribani shilingi 2.9. Aidha, fungu-57 Wizara ya Ulinzi ilifanya manunuzi ya magari yenye thamani ya shilingi 2,696,200,000 bila ya ushindani wa bei kinyume na kifungu cha 160 cha kanuni za manunuzi ya umma cha mwaka 2013, kama ilivyorejewa mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa ndani; kwenye hoja namba moja katika eneo la mfumo inahusu changamoto ya mfumo katika mamlaka ya usimamizi wa bandari (TPA), kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30, Juni mwaka 2021. TPA ilipata hati yenye mashaka, (*qualified opinion*). Sababu za msingi za kutolewa kwa hati hiyo zinatokana na mapungufu katika mfumo ya udhibiti wa ndani.

Mheshimiwa Spika, dosari nyingine iliyohusu mapungufu katika mfumo wa ICT ni Fungu 46- Wizara ya Elimu, Sanyansi na Teknolojia, wenye thamani ya Shilingi 429,470,000. Wizara ilitumia kiasi cha shilingi 429,470,000 kununua na kusimika

2 NOVEMBA, 2022

mifumo ya *ICT*. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa, hapakuwa na mpango wa namna bora mradi huo ulivyotekelezwa na kukamilika. Aidha katika mfumo huo wenye *module* nane, hadi ukaguzi unakamilika, *module* moja pekee ndiyo ilikuwa imefanyiwa kazi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho katika eneo hili ni kuhusu hoja ya mauzo ya matrekta yenye thamani ya Shilingi 981,400,000 yaliyofanywa na *SUMA-JKT* bila ya kuwa na mikataba. Kamati ilibaini kuwa, katika mradi wa mauziano wa vifaa vya kilimo wa *SUMA-JKT* waliuza kwa mkopo vifaa vyenye thamani ya shilingi 981,400,000 bila ya kuwa na mkataba kwa wakopaji (*contract agreement*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati. Mapendekezo ya kamati yanatolewa kwa kuangalia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika. Mapendekezo ya kamati yanasomwa sambamba katika randama ya kwanza iliyoambatanishwa na taarifa hii. Kwa sababu ya muda nitasoma hoja ya kamati na kisha pendekezo la azimio kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu nakisi ya ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), kiasi cha shilingi trilioni 2.8 Bunge linaazimia kwamba: -

- (a) *TRA* ikamilishe maboresho ya mfumo wa *e-tax* ili kuhakikisha mapungufu yaliyobainika na ukaguzi yanafanyiwa kazi na kutunza kumbukumbu sahihi;
- (b) *TRA*, iboreshe kitengo chake cha ufundi (*technical unit*);

2 NOVEMBA, 2022

- (c) *TRA* iboreshe hali ya utendaji katika mapitio na makadirio ya kodi ili kuondoa dosari za ukadiriaji wa kodi juu au chini ya kiwango;
- (d) *TRA* iongeze jitihada za kasi ya ukusanyaji wa madeni ya kodi ili kupunguza malimbikizo ya madeni ya kodi;
- (e) *TRA* iboreshe usimamizi wa mizigo ambayo inapita hapa nchini kwenda nchi za nje kwa kuhakikisha ushuru wa forodha unalipwa kwa mujibu wa sheria. Endapo kutabainika ukiukwaji wa sheria, hatua stahiki za kikodi zichukuliwe kwa wakati; na
- (f) *TRA* isimamie ipasavyo ukusanyaji wa ushuru katika bidhaa za mafuta yanayosafirishwa kwenda nchi za nje kupitia hapa nchini. Hili lifanyike sambamba na usimamizi wa maduhuri wa maghala (*warehouses*) ili kuepusha upotevu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dosari katika usimamizi wa mikataba na athari zake katika matumizi ya fedha za umma Bunge linaazimia kwamba, wakala wa barabara *TANROADS*, ifanye yafuatayo: -

- (a) *TANROADS* ihakikishe inaingia mikataba pale tu inapokuwa na uhakika wa fedha za kugharamia mikataba hiyo;

2 NOVEMBA, 2022

- (b) Utaratibu wa malipo ya Serikali ufanyike kwa ufanisi ili kupunguza ucheleweshaji wa malipo usiokuwa na sababu ya msingi ambao unachangia kuvunjwa kwa masharti ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Umeme Tanzania *TANESCO*, Kamati imetoa mapendekezo yafuatayo: -

- (a) *TANESCO* iboreshe eneo la usimamizi wa mkataba kwa kuhakikisha inapata ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutovunja mikataba bila kufanya upembuzi yakinifu wa matokeo ya hatua kama hiyo;
- (b) Kwa suala mahususi la malipo yaliyofanywa na Serikali kwenda *SYMBION*, Serikali itoe miongozo wa namna *TANESCO* itakavyotambua malipo hayo katika vitabu vyake vya hesabu kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa ya uandaaji wa hesabu (*IFRS*); na
- (c) Serikali iimarisha usimamizi katika suala zima la ununuzi na utekelezaji wa mikataba mikubwa kwa kuhakikisha upembuzi yakinifu unafanyika kabla ya ununuzi na wakati wa usimamizi wa mikataba husika. Aidha inashauriwa Serikali iangalie na kufanya tathmini ya kina kabla ya kutoa dhamana kwa taasisi za umma pale zinapoingia mkataba, kwani uzoefu umebaini kuwa eneo hili lina sababisha hasara kubwa kwa Serikali panapotokea kuvunjwa kwa masharti kwenye mikataba husika.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapendekezo kwenye mamlaka ya usimamizi wa bandari TPA ikamilishe majadiliano na wakandarasi wa ujenzi wa ghati ya kuegesha meli Mtwara kwa kuchukua na kutekeleza hatua stahiki kwa mujibu wa masharti ya mkataba na kwa manufaa mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya ukwasi katika taasisi za kimkakati za Serikali (TPDC, TANESCO na STAMICO). Bunge linaazimia kwamba: -

- (a) Ofisi ya Msajili wa Hazina iangalie namna bora ya kuyasaidia mashirika hayo kwa kuongeza mtaji wa ziada kwenye uwekezaji mpya ili kuzalisha mapato ya kutosha na kulipa madeni yao;
- (b) Mashirika husika yafanye mapitio ya muundo wa mitaji yao, (*capital structures*) ili kusimamia ipasavyo malipo ya mikopo na kuepuka ongezeko la riba linalotokana na ucheleweshwaji wa malipo ya mikopo husika;
- (c) Mashirika husika yafuatilie kwa karibu mtiririko wa fedha (*cashflow*) kwa kuongeza uzalishaji wa mapato kwa vyanzo vilivyopo; na
- (d) Kufanyike majadiliano na wakopeshaji ili kupata masharti nafuu ambayo yataendana na hali halisi

2 NOVEMBA, 2022

ya mtiririko wa fedha ili kuepusha riba na tozo za mikopo iliyoiva.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukaguzi Maalum, Bunge linaazimia kwamba:-

- (a) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa Mkandarasi wa Kampuni ya *DERM Electrical Tanzania Limited* kutokana na hasara iliyojitokeza. Aidha, hatua stahiki za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa watumishi wa *REA* waliohusika kusimamia mradi huo kwa kutotimiza majukumu yao ipasavyo;
- (b) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi 32 wa Idara ya Uhamiaji waliotajwa kuhusika katika suala la mauzo ya stika za viza bandia kwa kuzingatia uhusika wa kila mmoja na matokeo ya ukaguzi maalum;
- (c) Serikali ikamilishe hatua za kisheria kwa watumishi 12 waliobainika kujihusisha na ubadhirifu wa fedha za ada za wanafunzi katika chuo cha Hombolo; na
- (d) Serikali ifanye mapitio ya kina katika masharti ya Mkataba wa Orio ili kuondoa changamoto zilizomo katika masharti ya mkataba huo. Aidha, mkataba huo utoe somo la namna bora ya kubuni na kutekeleza miradi mikubwa ya afya kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha ya Umma Sura, 348, Bunge linaazimia kwamba:-

2 NOVEMBA, 2022

- (a) Shirika la Masoko Kariakoo: Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, afanye ukaguzi wa kiuchunguzi (*Forensic Audit*) wa Shirika la Masoko Kariakoo ili kubaini iwapo kuna ubadhirifu wa fedha za Umma uliofanyika na kufichwa baada ya soko hilo kuungua moto.
- (b) Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (*DART*): Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aombwe kufanya ukaguzi maalum (*Special Audit*) wa malipo ya fidia ya kiasi cha Shilingi bilioni 1,070.6 na malipo ya fedha za usumbufu kiasi ya shilingi milioni 434.1 yaliyofanyika *DART* ili kubaini iwapo yalifanyika kwa mujibu wa Sheria; na
- (c) Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi: Moja, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iandae kanuni zitakazosimamia uendeshaji wa Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na kubaini vyanzo vya mapato, mamlaka ya usimamizi, muundo wa mfuko, watumishi wa mfuko na utunzaji wa kumbukumbu za fedha na mali zake; na pili, CAG akague matumizi yote...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Makamu Mwenyekiti, tunashukuru sana, kengele ya pili imeshagonga.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu haya mambo yanayozungumziwa hapa ni mazito sana, lakini taarifa hii

2 NOVEMBA, 2022

mnayo kwenye vishikwambi na pia zile taarifa za CAG zote mnazo. Kwa hiyo, Kamati inachofanya ni kutupa mwelekeo wa mambo ambayo wameyaona. Kwa hiyo, Mwenyekiti malizia dakika moja.

MHE. JAPHET N. HASUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kukushukuru wewe binafasi kwa uongozi wako makini na kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba majina yao wote yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelewa Mwihambi, *ndc* kwa ushauri wake kwa Kamati. Natoa shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati kupitia kwa Mkurugenzi wa Idara, Ndugu Athuman Hussein, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto *ndc*, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Sostenes Maseke na Ndugu Amina Salum Namtema.

Mheshimiwa Spika, mwisho japo siyo kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa iliyoupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), na kwa

2 NOVEMBA, 2022

namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Charles Kichere. Aidha, naishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, Msajili wa Hazina, na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali na Maafisa wote kwa ushirikiano walioutoa katika kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU TAARIFA ZA MDHIBITI NA
MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU
ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU, MASHIRIKA YA UMMA NA
KAGUZI ZA UFANISI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA
TAREHE 30 JUNI, 2021 –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 na kuliomba Bunge liipokee na kujadili. Madhumuni ya Taarifa hii ni

2 NOVEMBA, 2022

kulijulisha Bunge lako tukufu, iwapo matumizi ya Fedha za Umma yamefanyika kwa namna iliyokusudiwa na Bunge na kwamba matumizi hayo yamezingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza madhumuni hayo, Taarifa hii inagusa Hesabu za Serikali kuu na Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Vilevile, uchambuzi wa Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni sehemu ya Taarifa hii. Jambo kuu katika Taarifa hii linahusu matumizi ya fedha za umma hususani dosari za matumizi ya fedha za umma zinazohitaji kufanyiwa kazi.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kurahisisha ufuatiliaji wa taarifa hii, naomba kubainisha sehemu kuu tatu ambazo ni za msingi pamoja na hitimisho lenye shukurani na utoaji wa hoja. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo muundo wa Taarifa, majukumu ya Kamati, msingi wa kazi za Kamati na muhtasari wa matokeo ya Uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lengo la Sehemu hii ni kubainisha muktadha wa Taarifa ili kuwezesha ufuatiliaji utakaosaidia kufanya uamuzi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi. Katika Sehemu hii, Taarifa inafafanua mambo ya msingi kuhusu uchambuzi na kubainisha

2 NOVEMBA, 2022

Matokeo ya uchambuzi huo. Lengo la sehemu hii ni kuonesha dosari zilizobainika katika matumizi ya fedha za Umma na kuweka msingi wa mtazamo wa Kamati kuhusu Matumizi ya Fedha za Umma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021. Sehemu hii inajenga msingi wa Sehemu ya Tatu inayohusu Maoni na Mapendekezo.

1.3 Majukumu ya Kamati

Mheshimwa Spika, maudhui ya Taarifa hii yanahusu Matumizi ya Fedha za Umma kwenye Serikali Kuu na Mashirika ya Umma nchini. Mambo hayo yanasimamiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kwa mujibu wa Kifungu hicho Kamati ina majukumu yafuatayo: -

- a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika wizara za Serikali na mashirika ya umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);
- b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na
- c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa wizara za serikali na mashirika ya umma ili kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

1.4 Njia Zilizotumika Katika Utekelezaji wa Kazi za Kamati

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge imeweka masharti kwamba Taarifa yoyote ya Kamati inayoingia Bungeni, inatakiwa kubainisha njia zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayotolewa Taarifa. Kwa msingi huo naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba kuzitaja njia hizo kama ifuatavyo: -

a) Mapitio ya Jumla ya Ripoti za CAG ili kubaini maeneo ya kuwekea mkazo na kukidhi masharti ya Ripoti hiyo ulikuwa msingi wa kazi za Kamati zilizopangwa kwenye Ratiba;

b) Kupokea Vidokezo ("*briefs*") vya Ripoti za CAG kwa hoja za ukaguzi za mafungu yaliyopangwa kujadiliwa na Kamati kabla ya Kukutana na Afisa Masuuli anayehusika. Mbinu hii iliwezesha Kamati kuzielewa hoja na wigo wa mahojiano na Afisa Masuuli kwa lengo la kupata undani wa tatizo la matumizi mabaya ya fedha za umma;

c) Mahojiano na maafisa masuuli kuhusu hoja za ukaguzi ili kupata undani wa matatizo ya matumizi ya fedha za umma na kubaini chimbuko la tatizo, wigo wa dosari na

2 NOVEMBA, 2022

uwezekano wa kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za Wakaguzi wa hesabu za Fungu linalohusika kwa pamoja na majibu ya Menejimenti za Taasisi, wizara au Shirika lililokaguliwa. Lengo ni kuelewa kwa kina muktadha wa hoja na matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma;

e) Tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma. Lengo la njia hii ni kuona na kuutumia uzoefu wa jumla unaopatikana kwa tafiti hizo ili kutathmini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kama yalivyoainishwa na CAG.

Mheshimiwa Spika, njia na mbinu hizo ziliwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina kwa nia ya kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua. Mbinu hizo ziliendana na matumizi na marejeo ya miongozo ifuatayo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoonesha dhamana ambayo Serikali imepewa na wajibu wa Bunge kuisimamia na kuishari serikali ikiwemo eneo la matumizi ya fedha za umma.

b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 inayofafanua masharti muhimu kwa ajili ya kuwezesha ukaguzi, uandaaji wa Ripoti za CAG, uwasilishaji wake na hatimaye kujadiliwa na Kamati;

c) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 inayoweka miongozo ya matumizi ya fedha za umma na

2 NOVEMBA, 2022

kusaidia kuamua iwapo kuna matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, inayohusika na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kwa kuweka taratibu za utekelezaji wa bajeti na usimamizi wake;

e) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 inayogusa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika mashirika ya umma;

f) Sheria ya Ununuzi ya Umma, Sura 410, inayoweka taratibu za kufuatwa wakati wa ununuzi wa bidhaa, huduma na kuingia mikataba kwa gharama ambazo zinahusisha matumizi ya fedha za umma;

g) Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286, inayosimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi ili kuwezesha kumbukumbu za kutumainiwa za fedha na usimamizi bora wa matumizi ya fedha za umma;

h) Sheria ya Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura 296 inayoliwezesha Bunge, Wabunge na Kamati za Bunge kupata stahili kutokana na madaraka yake na kupata ushahidi bila kukwama wakati wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma; na

i) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 zinazobainisha utaratibu wa Ripoti za CAG kuhusu matumizi ya fedha za umma kuwasilishwa Bungeni, kushughulikiwa na Kamati na hatimaye Kamati kutoa Taarifa hii.

1.5 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwezi Agosti 2022 hadi Novemba 2022, shughuli za Kamati, zililenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika wizara na mashirika ya umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2021. Aidha, shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa nyakati tofauti kwa kipindi chote cha mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2021 CAG alifanya ukaguzi wa jumla ya taasisi 331 za serikali kuu ikijumuisha wizara na idara zinazojitegemea, wakala, mifuko maalum, sekretarieti za mikoa, vyama vya siasa na bodi za mabonde ya maji. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hesabu jumuiifu za Taifa (Consolidated accounts), ukaguzi wa malipo tarajali ya pensheni, hospitali za rufaa na kaguzi maalumu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mashirika ya umma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikagua na kutoa taarifa za jumla ya mashirika ya umma 200 ikilinganishwa na mashirika ya umma 165 yaliyokaguliwa kwa mwaka 2019/2020. Vilevile Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikamilisha Kaguzi 12 za Ufanisi.


2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mafungu 12 ya serikali kuu, mashirika ya umma 21, wakala za serikali 2, kaguzi maalumu 4, mabonde ya maji 2 na kaguzi za ufanisi 4. Shughuli hizi zilitekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo Kamati ilijiwekea.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa Taasisi zilizofika mbele ya Kamati kwa mahojiano umefafanuliwa katika Chati Na. 1.1 hapa chini:-

Chati. Na. 1.1: Mchanganuo wa Taasisi zilizofika mbele ya Kamati kati ya Agosti – Novemba, 2022.

Mwenendo wa Uchambuzi na Kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021



2 NOVEMBA, 2022

Chati Na. 1.2: Mchanganuo wa mafungu yaliofika mbele ya Kamati kati ya Agosti – Novemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa kina wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati unapatikana katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

1.6 Ufuatiliaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa na Kamati

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 14(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri unaokuwa umetolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, jambo hili hufanyika kwa CAG kufanya uhakiki wa maoni na mapendekezo yanayokuwa yametolewa na Kamati kwa fungu husika. Aidha, kila fungu linapofika mbele ya Kamati, CAG huipitisha Kamati kwenye taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati kwa fungu husika kabla ya kuanza kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu za fungu hilo.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa Bunge katika matumizi ya fedha za umma umewekewa misingi, taratibu na vigezo vya kuzingatia. Katika kuliwezesha Bunge kufuatilia matumizi ya fedha za umma, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

2 NOVEMBA, 2022

Tanzania imempa CAG madaraka na Majukumu ambayo yanakamilika kwa Taarifa zake kuwasilishwa Bungeni. Tija ya utaratibu huo inafanikishwa na Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za Umma. Kutokana na ukweli huo, Kamati ilipitia na kuchambua Ripoti za CAG zilizowekwa mezani tarehe 12 Aprili, 2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo Kamati iliendelea na uchambuzi na baadaye kwa kutumia masharti ya Kanuni ya 109 ukaelekeza Taarifa hii ipangwe kwenye Orodha ya Shughuli za leo. Ili kutimiza lengo la Bunge kuipokea na kuijadili Taarifa hii, naomba kulijulisha Bunge kuhusu uchambuzi wa Ripoti za CAG. Uchambuzi huo ndio chanzo cha mtazamo na maoni ya Kamati ambayo ni msingi wa mapendekezo ya Kamati yanayowasilishwa kwa njia ya Hoja kama ilivyoelekezwa na Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge Toleo la Juni, 2020.

2.2 Vigezo vya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, uwekaji wa vigezo ni jambo muhimu katika uhakiki na tathmini yoyote. Suala la matumizi mabaya ya fedha za umma linaweza kubainika kutokana na vigezo vya matumizi ya fedha za umma. Aidha, uamuzi wa kuwahoji maafisa masuuli kutokana na Ripoti za CAG ni jambo lililohitaji kuwekewa vigezo. Kwa sababu hiyo, baada ya kupokea Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ilitengeneza vigezo muhimu vya kuzingatia katika kutimiza majukumu yake ya Kikanuni. Vigezo hivyo vilitoa mwongozo wa uchaguzi wa mafungu ambayo yalipewa kipaumbele katika uchambuzi na mahojiano na Maafisa Masuuli.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyozingatiwa wakati wa kuchagua vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za Kamati vilikuwa kama ifuatavyo: -

- a) Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na CAG;
- b) Maslahi ya Umma kuhusu hoja za fungu linalohusika;
- c) Hali ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa fungu linalohusika;
- d) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;
- e) Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa fungu linalohusika;
- f) Kuleta uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa fungu husika kwa siku za nyuma;
- g) Kutoa kipaumbele kwa Sekta na Mashirika Mkakati (Strategic sectors and parastatals) kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya sasa ya Serikali;
- h) Kaguzi maalum (Special audit) zilizofanyika hivi karibuni; na
- i) Uzingatiaji wa kaguzi za ufanisi kwa mwaka husika.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo viliisaidia Kamati kuendelea na mchakato wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Ripoti za CAG. Nikiri kuwa bila vigezo hivyo ingekuwa vigumu kugusa aina mbalimbali za matumizi mabaya ya fedha za umma.

2.3 Matokeo ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mafungu mahususi ya serikali kuu na mashirika ya umma ulibainisha mambo yafuatayo kuhusu matumizi na usimamizi wa fedha za umma: -

2.4 Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kiasi cha Sh. 2,811,461,204,503

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021. Lengo kubwa la uchambuzi wa taarifa hiyo ilikuwa ni kufanya tathmini ya hali ya ukusanyaji wa mapato chini ya Mamlaka hiyo. Hali kadhalika, Kamati ilijielekeza kupitia na kuchambua matumizi ya fedha yanayofanywa na TRA katika shughuli za ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) huandaa taarifa za hesabu katika mifumo miwili (2) tofauti, ambapo hesabu za makusanyo (Revenue statement) huandaliwa katika Mfumo wa Kimataifa wa Uandaaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS). Kwa upande wa hesabu za matumizi (Expenditure statements), TRA huandaa

2 NOVEMBA, 2022

hesabu zake kwa kutumia Mfumo wa Kihhasibu wa Kimataifa wa Uandaaji Taarifa za Hesabu za Serikali (IPSAS)¹.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021. Kwa upande wa makusanyo kwa Tanzania Bara na Zanzibar kiasi halisi kilichokusanywa kilikuwa **Sh.17,897,859,464,498** ukilinganisha na makadirio ya kiasi cha **Sh. 20,709,320,669,001**. Kwa msingi huo, kulikuwa na nakisi ya makusanyo ya kiasi cha **Sh. (2,811,461,204,503)** ambayo ni sawa **-(14%)** ya makadirio ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuchambua hesabu za TRA, Kamati ilifanya tathmini ya mwenendo wa makusanyo ya kodi kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo (2018/2019 hadi 2020/2021). Lengo la tathmini hiyo pamoja na mambo mengine lilikuwa ni kubainisha sababu za TRA kutofikia malengo ya ukusanyaji wa kodi yanayokuwa yamepangwa na kisha kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa makusanyo ya kodi kati ya mwaka 2018/2019 hadi 2020/2021 umefafanuliwa katika Jedwali Na. 2.1 hapa chini: -

Jedwali Na. 2.1: Mwenendo wa makusanyo ya kodi kati ya mwaka 2018/2019 hadi 2020/2021.

Mwaka	Bajeti (TZS)	Makusanyo halisi (TZS)	Tofauti (TZS)	%
-------	--------------	------------------------	---------------	---

¹ International Public Sector Accounting Standards (IPSAS).

2 NOVEMBA, 2022

2020/21	20,709,320,669,001.	17,897,859,464,498	-2,811,461,204,503	-14%
2019/20	19,451,124,906,570	17,930,876,799,979	-1,520,248,106,591	-8%
2018/19	18,332,665,353,745	15,764,661,229,215	-2,568,004,124,530	-14%

Chanzo: Taarifa ya hesabu za makusanyo za TRA (Revenue statements) kwa miaka 2018/2019 hadi 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kama jedwali Na. 2.1 hapo juu linavyofafanua, makusanyo ya kodi kwa miaka 2 mfululizo (2018/2019 na 2019/2020) yalikuwa na ongezeko kidogo. Hata hivyo kwa mwaka 2020/2021 makusanyo ya kodi yalipungua zaidi ukilinganisha na mwaka uliotangulia. Hata hivyo, kwa ujumla wake kwa miaka yote 3 makusanyo ya kodi yalikuwa chini kidogo ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijielekeza zaidi kuchambua mapendekezo ya ukaguzi ambayo CAG alikuwa ametoa kwa TRA ili kuondoa changamoto za ukusanyaji wa mapato. Uchambuzi wa mapendekezo hayo ulibaini kuwa, kuna mapendekezo 305 ambayo yanaendelea kutekelezwa na ambayo hayajatekelezwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo hayo, mapendekezo 29 (9.5%) yanahitaji maamuzi ya Serikali nje ya Mamlaka ya TRA hasa maamuzi kutoka kwenye vyombo vya Sheria kama Mahakama, Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB) na Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT). Aidha, katika kundi hilo kuna mapendekezo ambayo yanahitaji uamuzi wa Bunge kwa yale yaliyoombewa kibali cha kufutwa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina zaidi wa mapendekezo hayo kuhusu hoja za ukaguzi yalibaini kuwa

2 NOVEMBA, 2022

baadhi ya mashauri ya kesi na baadhi ya maombi ya kufuta kodi zisizoweza kukusanywa yameendelea kusubiri uamuzi tangu mwaka 2001/2002. Mwisho, mapendekezo 276 yanaendelea kufanyiwa kazi na TRA. Mapungufu hayo ambayo yapo ndani ya TRA ambayo CAG amependekeza yafanyiwe kazi kwa ukamilifu kwa muhtasari ni kama ifuatavyo: -

a) Mapungufu katika mfumo wa "ITAX"² hususan katika kushughulikia madeni ya kodi. Mfano kwa mwaka huu tunapotoa taarifa hii kulitokea dosari za madeni ya kodi kwa Mikoa ya Morogoro na Arusha ya kiasi cha **Sh.11, 512,649,634.68** ambayo yanatokana na dosari katika mfumo wa usimamizi wa kodi;

b) Kutoshughulikiwa ipasavyo kwa madeni ya kodi. Mathalani kwa mwaka 2020/2021 kulikuwa na ongezeko kubwa la 95% la madeni ya kodi. Ongezeko hilo lilitoka **Sh.3,875,993,883,000.00** hadi **Sh.7, 542,177,786,896.00**;

c) Mapungufu kwa kukadiria chini ya kiwango kodi ya mapato. Kwa mwaka 2020/2021 ukaguzi ulibaini makadirio ya chini ya kodi ya mapato ya kiasi cha **Sh.5, 266,357,280**;

d) Mapungufu kwa kukadiria chini ya kiwango kodi ya ongezeko la thamani ya kiasi cha **Sh.3, 662,349,921.51**;

e) Mapungufu kwa kukadiria kiasi cha chini kodi ya zuiio (Withholding tax) ya kiasi cha **Sh. 2,466,997,819.42**;

² Income Tax Management System.

2 NOVEMBA, 2022

f) Kuchelewa kutolewa maamuzi kwa mapingamizi ya kodi (Tax objection) yenye thamani ya **Sh.102, 595,793,905.00**;

g) Ucheleweshaji wa usajili wa mapingamizi ya kodi yenye thamani ya kiasi cha **Sh. 65,413,970,985.00**;

h) Dosari katika usimamizi wa mashine za kielektroniki za utoaji stakabadhi (EFD). Ukaguzi ulibaini uwepo wa Wafanyabiashara 1796 wenye mapato ya mwaka ya zaidi ya **Milioni 14** wasiotumia mashine za EFD;

i) Kutokukusanywa kwa mapato ya tozo, adhabu, faini na riba za kiasi cha **Sh.3, 474,774,234.29**;

j) Kutokukusanywa kwa ushuru wa mafuta yanayotumika ndani ya nchi ya kiasi cha **Sh. 8,176,580,659.00**; na

k) Usimamizi mbovu wa forodha kwa magari na bidhaa zinazoingiwa nchini kwa muda ili baadaye zisafirishwe kwenda nje ya nchi.

2.5 Dosari Katika Usimamizi wa Mikataba na Athari Zake Katika Matumizi ya Fedha za Umma

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo uchambuzi wa Kamati umebainisha uwepo wa upotevu mkubwa wa fedha za Serikali ni katika mapungufu katika usimamizi wa Mikataba. Uchambuzi wa Kamati umefafanua mafungu mahsusni yenye changamoto hiyo kama ifuatavyo: -

2.5.1 Riba ya Kuchelewesha Malipo Inayotokana na Kuchelewa Kulipa Wakandarasi Katika Wakala wa Barabara (TANROADS) Sh. Bilioni 68.7

Mheshimiwa Spika, masharti ya Kifungu cha 54 cha masharti ya jumla ya mkataba wa ujenzi (GCC)³ kinatamka kwamba, mwajiri atalipa mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na meneja wa mradi ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kila hati ya muda ya malipo (Mikataba iliyo katika mfumo wa Kimataifa, muda wa malipo ni siku 56 toka mkandarasi awasilishe hati ya madai). Kwa msingi huo, mwajiri akichelewesha malipo, mkandarasi atalipwa riba ya kuchelewesha malipo katika hati ya malipo inayofuata.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu za TANROADS ulibaini kuwa Wakala unadaiwa madai ya malipo ya **Sh. Bilioni 664.35** kutoka kwa wakandarasi na wahandisi washauri wa ujenzi, hivyo kupelekea Wakala husika kutozwa riba ya ucheleweshaji malipo ya **Sh. Bilioni 68.73** kuendana na vifungu vilivyopo katika mikataba ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, malipo haya yanatokana na kuingia mikataba mingi bila ya kuwa na fedha za kutosha hali inayopelekea kutotimizwa masharti ya mikataba na hivyo kuisababishia Serikali hasara.

³ General Conditions of Contract for Constructions Works.

2 NOVEMBA, 2022

**2.5.2 Mradi Uliosimama wa Ujenzi wa Vihenge Ambapo
Mkandarasi Ameshalipwa Dola za Marekani Milioni
33.4**

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Wakala wa Taifa wa Chakula (NFRA) umebainisha kuwa, mnamo tarehe 22 Desemba 2016, NFRA iliingia mkataba Na: AE/054/2015/2016/HQ/W/19 na M/s FEERUM SA, kwa ajili ya usanifu, ugavi, ujenzi, ufungaji, upimaji na uagizaji (Commissioning) wa majengo ya silos, maghala na ukarabati wa majengo yaliyopo vituo vya Ruvuma, Njombe, Songwe, Dodoma, na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba husika, gharama za mradi ilitakiwa kuwa **Dola za Marekani 33,140,791.81**, na mradi ungekamilika tarehe 09 Disemba 2017. Hata hivyo, baadaye muda wa utekelezaji uliongezwa hadi tarehe 31 Disemba 2020. Hadi kipindi hicho, mkandarasi alikuwa tayari amelipwa kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 21.46**, sawa na 65% ya gharama za mkataba, hadi muda wa ukaguzi, mnamo Desemba 2021.

Mheshimiwa Spika, uhakiki uliofanywa na CAG kwenye maeneo ya ujenzi mnamo Desemba 2021, ulibaini kuwa mradi ulikuwa bado haujakamilika, ingawa muda wa kandarasi wa tarehe 31 Desemba 2020 ulimalizika mwaka mmoja uliopita. Aidha, hali ya utekelezaji wa mradi kwa maendeleo ya kazi wakati huo yalikuwa 28% ya ujenzi, 44% ya maghala na 85% kwa silos.

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa CAG umebainisha kuwa mkandarasi amekwisha ondoka eneo la ujenzi tangu tarehe

2 NOVEMBA, 2022

30 Septemba 2020, na alikuwa ametoa notisi ya kusitisha mkataba mnamo tarehe 01 Desemba 2020. Sababu za kusitisha mkataba alizotaja ni pamoja na kucheleweshwa kwa malipo pamoja na kutotolewa kwa Tangazo la Serikali⁴ la Msamaha wa Kodi la Ongezeko la Thamani (VAT). Mkandarasi alidai sababu hizo zinakiuka kanuni na masharti ya mkataba kulingana na kifungu cha 67 cha masharti ya jumla ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano ya muda uliotegemewa hakuleti taswira nzuri ya matumizi mazuri ya fedha za umma. Aidha, matumizi hayo hayaakithi manufaa yaliyokusudiwa ya mradi kwa wananchi.

2.5.3 Malipo yaliyofanywa na TANESCO Kiasi cha za Dola za Marekani Milioni 153.43 Kutokana na Kuvunjwa kwa Mkataba

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 07 Julai 2001, Kampuni ya Symbion Power LLC iliingia mkataba na TANESCO wa kukodisha mitambo ya uzalishaji umeme iliyopo eneo la Ubungo Dar es Salaam. Mkataba huo ulikuwa wa kipindi cha miaka 2 kwa gharama ya **Dola za Marekani 0.0499** kwa kWh kwa kutumia gesi. Muda wa mkataba ulimalizika tarehe 19 Septemba 2013. Kwa kutumia makubaliano yaliyojulikana kama "Power Off-Take Agreement" ya tarehe 28 Juni 2013, Kampuni ya Symbion LLC ilikubali kuendelea kuiuzia umeme TANESCO kwa miaka 2 zaidi

⁴ Government Notice.

2 NOVEMBA, 2022

kutoka tarehe 19 Septemba 2013 hadi tarehe 18 Septemba 2015.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG inabainisha kuwa baada ya hapo TANESCO na Kampuni ya Symbion walianza majadiliano ya kuwa na mkataba wa muda mrefu wa mauziano ya umeme, “Power Purchase Agreement” (PPA). Makubaliano ya awali yalisainiwa tarehe 15 Septemba 2015 ambapo Kampuni ya Symbion ingeziuia TANESCO megawati 112 kwa gharama ya **Dola za Marekani 0.01775** kwa KWh (50% x 0.285 plus 0.0035).

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG inabainisha kuwa ilipofika tarehe 24 Mei, 2016 kulijitokeza kutoelewana kati ya TANESCO na Kampuni ya Symbion hali iliyopelekea TANESCO kuitaka Kampuni ya Symbion kuondoa mitambo yake kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya uamuzi huo kulijitokeza mashauri 2 ya madai dhidi ya TANESCO. Madai hayo toka kwa Kampuni ya Symbion na Wanahisa wa Symbion yalifunguliwa Chemba ya Kimataifa ya Biashara (ICC)⁵ na Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogogoro ya Uwekezaji (ICSID)⁶. Jumla ya madai ambayo TANESCO ilikuwa inadaiwa katika mashauri yote 2 ni **Dola za Marekani 1,566,254,652.41**.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG inaendelea kufafanua kuwa ilipofika mwezi Julai, 2018 pande zote 2 zilianza

⁵ Rejea ICC Case Na. 22661/T0.

⁶ Rejea ICSID case Na. arb/19/USD.

2 NOVEMBA, 2022

majadiliano ya kutatua mgogoro huu nje ya Mahakama. Mnamo tarehe 21 Mei, 2021, pande hizo 2 zilifikia makubaliano (Deed of Settlement) ambapo makubaliano yalihusu malipo ya **Dola za Marekani 153,434,206.83** bila kujumuisha kodi na gharama nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malipo haya yaliyofanyika kupitia makubaliano ya pande mbili, CAG amebainisha hoja kuu mbili kama msingi wa sababu zilizoifikisha TANESCO katika hatua hiyo na ambazo bado zinahusina na suala hilo. Hoja hizo ni kama ifuatavyo: -

a) Usimamizi wenye dosari wa mkataba husika na kutofanyika kwa upembuzi wa kina kabla ya kuvunja mkataba kati ya TANESCO na Symbion. CAG ana maoni kuwa uchunguzi wa kina haukufanyika kabla ya kuvunjwa mkataba husika bila ya kuangalia athari za kifedha ambazo TANESCO ingepata siku za baadaye; na

b) Mapungufu katika makubaliano yaliyofikiwa kati ya TANESCO na Symbion. Katika suala hili CAG anafafanua kwamba, makubaliano hayo hayajaweka wazi iwapo malipo yanayofanywa na Serikali kwa niaba ya TANESCO kwenda Symbion yatatambuliwa (Treated) kama mkopo, ruzuku au mtaji. Hali hii inaweza kuleta taswira isiyo sawa katika vitabu vya hesabu za TANESCO kama matakwa ya Kanuni za Kimataifa za Ukaguzi yanavyoelekeza. Kifungu 15 cha IAS⁷ 1 kinanukuliwa kama ifuatavyo: -

⁷ International Audit Standard.

2 NOVEMBA, 2022

“...Presentation of financial statements) provides that, financial statements shall present fairly the financial position, financial performance and cash flows of an entity. Fair presentation requires the faithful representation of the effects of transactions, other events and conditions in accordance with the definitions and recognition criteria for assets, liabilities, income and expenses set out in the Framework..”

Mwisho wa Kunukuu.

Mheshimiwa Spika,ni kwa msingi huo, makubaliano hayo yanatakiwa kufafanua kwa kina hoja za ukaguzi zilizojitokeza ili kutoa taswira sahihi kijasibu katika hesabu za TANESCO.

2.5.4 Kuchelewa Kukamilika kwa Ujenzi wa Gati la Kuegeshea Meli Katika Bandari ya Mtwara, Mradi wa Sh. 137,385,612,736.75

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Serikali imepata hasara kutokana na usimamizi usioridhisha wa mikataba hasa ile ya ujenzi ni katika bandari ya Mtwara. Katika eneo hili, TPA ilikuwa ikitekeleza mradi wa ujenzi wa gati moja zaidi la kuegeshea meli kwa mkataba wenye thamani ya **Sh. 137,385,612,736.75**.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, uhakiki uliofanywa na CAG ulibaini kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa gati hilo kwa mujibu wa mkataba licha ya kutolewa ongezeko la muda mara kwa mara. Athari za ongezeko la muda wa utekelezaji wa mkataba ni ongezeko la gharama za ujenzi hivyo

2 NOVEMBA, 2022

kuisababishia Serikali hasara. Aidha, kusudi na lengo la ujenzi wa gati hilo litachelewa kufikiwa hivyo kukosa thamani halisi ya fedha za umma.

2.6 Hali ya Ukwasi Katika Baadhi ya Taasisi za Kimkakati za Serikali (TPDC, TANESCO na STAMICO)

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, Kamati ilipitia taarifa za fedha za mashirika ya kimkakati 3. Mashirika hayo muhimu kwa uchumi wa nchi yetu ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Mheshimiwa Spika, lengo la uchambuzi wa taarifa husika za fedha pamoja na kuangalia matumizi ya fedha za umma hasa kwenye eneo la mikopo inayochukuliwa na mashirika hayo, lakini pia Kamati ilitaka kujiridhisha na hali ya ukwasi (Liquidity) na uwezo wao wa kutimiza majukumu waliyopewa kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijielekeza kwanza kwa kuangalia uwiano wa mtaji na madeni (Debt to equity ratio) kwa mashirika husika. Kwa ujumla uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mashirika hayo 3 yana changamoto ya mtaji. Kwa msingi huo, mashirika hayo yanategemea zaidi mikopo ili kuendesha shughuli zao za kila siku. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, TANESCO, TPDC na STAMICO katika mwaka 2020/2021 zilikuwa na uwiano usio mzuri wa madeni ukilinganisha na mtaji wa ujumla.

Mheshimiwa Spika, uwiano huo ambao sio mzuri kifedha, miongoni mwa mambo mengine, ulitokana na mikopo ya ziada na ongezeko la gharama ya kukopa kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya mikopo iliyochukuliwa hapo awali na hivyo kutozwa riba. Mchanganuo wa uwiano wa madeni na mtaji kwa mashirika hayo matatu umechambuliwa katika Jedwali Na. 2.2 hapa chini.

Jedwali Na. 2.2 Hali ya mtaji na madeni kwa TANESCO, TPDC na STAMICO

Na.	Shirika	Kiasi (TZS) (Millioni)		Gearing Ratio (Debt to Equity Ratio %)
		Madeni Yote	Jumla ya mtaji	
1.	TANESCO	13,497,177	3,790,924	356
2.	STAMICO	94,856	24,613	385
3.	TPDC	3,517,423	257,137	1,368

Chanzo: Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za TANESCO, STAMICO na TPDC kwa mwaka 2020/2021

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.2 hapo, juu uwiano wa madeni na mtaji kwa mashirika yote ni zaidi ya 100%. Hii ina maana kwamba, mali nyingi za mashirika husika zinagharimiwa na mikopo.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha pili ambacho kilitumika kupima hali ya ukwasi katika mashirika tajwa hapo juu kilikuwa ni uwiano wa mali na madeni ya muda mfupi. Kwa kutumia uwiano huo (The current ratio) ambao unapataikana kwa kugawanya mali za muda mfupi kwa madeni ya muda mfupi (Total current assets/Total current

2 NOVEMBA, 2022

liabilities), ilibainika kuwa mashirika hayo yote yana uwiano chini ya 1.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya jambo hili ni kwamba, katika kipindi cha muda mfupi mashirika husika hayana uwezo wa kugharamia mahitaji yao ya kifedha pindi yatakapojitokeza. Uchambuzi wa uwiano huo umefafanuliwa katika Jedwali Na. 2.3 hapa chini.

Jedwali Na. 2.3: Uwiano wa mali na madeni ya muda mfupi kwa TANESCO na STAMICO

Na.	Taasisi	Mali za Muda Mfupi TZS (Millioni)	Madeni ya Muda Mfupi (TZS (Millioni)	Mtaji (TZS) (Millioni)	Uwiano wa Mtaji (1:1)
1	TANESCO	1,918,525	3,250,450	- 1,331,925	0.59:1
2	STAMICO	33,932	59,531	-25,599	0.57:1

Chanzo: Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za TANESCO na STAMICO kwa mwaka 2020/2021

Mheshimiwa Spika, hali ya mtaji kwa mashirika haya sio ya kuridhisha kama inavyoonekana katika Jedwali Na.2.3 hapo juu. Ili kutekeleza majukumu ya kila siku, mashirika hayo hulazimika kutumia mikopo kugharamia shughuli zao. Kamati iliamua kuileta hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kuzingatia kuwa mashirika haya ni muhimu. Hivyo kwa kutokuwa na mtaji yanatumia fedha nyingi za umma kugharamia riba za mikopo katika taasisi za fedha ili kutimiza majukumu yao. Riba hizo ni fedha za umma ambazo zinatakiwa kutumika kuleta tija katika maeneo mengine.

2 NOVEMBA, 2022

2.7 Matokeo ya Uchambuzi wa Kaguzi Maalumu

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza kupitia na kuchambua jumla ya taarifa 4 za Kaguzi Maalumu zilizofanyika kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021. Matokeo ya uchambuzi kwa kila taarifa ni kama ifuatavyo: -

2.7.1 Ukaguzi Maalumu wa Mradi wa REA Awamu ya Pili Mkoani Mara Ambapo REA Ilipata Hasara ya Sh. Milioni 329.62

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 22 Septemba 2020 Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alipokea maombi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupitia barua yenye Kumb. Na. PCCB/8/3/VOL.LXXV1/10/OP 06 iliyoomba kufanyika kwa Ukaguzi wa Kiuchunguzi katika Miradi ya Usimikaji wa Miundombinu ya Umeme katika Vijiji visivyo na umeme Mkoani Mara ikiwa ni utekelezaji wa Miradi ya REA awamu ya II na ya III.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulilenga kubaini iwapo Serikali ilipata hasara wakati wa utekelezaji wa Mradi wa REA Awamu ya II na ya III kwa vifaa ambavyo vilinunuliwa na kulipiwa wakati wa utekelezaji wa Mradi wa REA Awamu ya II na havikutumika. Vifaa hivyo vilitakiwa kukabidhiwa Serikalini (TANESCO Mkoa wa Mara) lakini havikukabidhiwa na mkandarasi kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa, REA ilifanya malipo ya **Sh. 106,771,469.28** (ikijumuisha KOT) kwa mkandarasi kwa kuzingatia hati za kuwasilisha vifaa

2 NOVEMBA, 2022

(Delivery Notes) zilizokuwa na udanganyifu. Hii ilitokana na ukweli kwamba mzalishaji wa vifaa husika alikana kutoa hati hizo kwa Kampuni ya DERM Electrics (T) Limited. Aidha, malipo ya kiasi cha **Sh. 91,115,356.72** (ikijumuisha KOT) hayakuthibitika uhalali wake kufuatia mkandarasi Kampuni ya DERM Electrics (T) Limited kutumia hati zake za uwasilishaji vifaa badala ya mzalishaji na kutokuwepo kwa hati halisi zinazothibitisha kupokelewa kwa vifaa husika katika eneo la Mradi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa Kampuni ya DERM Electrics (T) Limited ilinunua na kutovitumia vifaa vyenye thamani ya **Sh. 329,620,735.80** (ikijumuisha KOT) wakati wa utekelezaji wa Mradi wa REA Awamu ya II. Aidha, vifaa hivyo havikukabidhiwa kwa Msimamizi wa mradi, TANESCO Mkoa wa Mara, hivyo kuisababishia REA hasara.

Mheshimiwa Spika, dosari nyingine iliyobainika katika ukaguzi huu wa kiuchunguzi ni kwamba, Kilomita 10 za Njia ya Msongo wa Kati (33Kv Medium Voltage Distribution Line) haikutengenezwa wakati wa utekelezaji wa mradi wa REA Awamu ya II. Pia, wateja wapya 4,168 na 545 (New customer connection) wa Njia 1 na Njia 3 mtawalia, waliokusudiwa na mradi huu hawakuweza kunufaika. Hivyo malengo ya mradi hayakufikiwa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli REA ambapo alitoa majibu kwa baadhi ya hoja za ukaguzi huo maalumu. Hata hivyo, hoja inayohusu kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kampuni na wahusika kwenye kuisababishia Serikali hasara hazijachukuliwa hadi sasa. [1]
[SEP]

2 NOVEMBA, 2022

2.7.2 Ukaguzi Maalumu wa Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji Kuhusu Viza Stika Bandia

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa, mnamo tarehe 02 Agosti 2019, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) alibaini uwepo wa viza stika bandia zilizokamatwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA). Katika upelelezi uliofanywa na Ofisi ya DCI ilibainika kuwa viza stika bandia hizo zilikuwa zikiuzwa kwa raia wa kigeni walioingia nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na watumishi wa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) alimuomba CAG kufanya ukaguzi maalumu kuhusiana na uuzaji na ukusanyaji wa fedha za mauzo za viza stika kwa raia wa kigeni walioingia nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) katika kipindi cha miezi sita (6), kuanzia tarehe 1 Januari 2019 hadi 30 Juni 2019.

Mheshimiwa Spika, lengo la Ukaguzi huu Maalumu lilikuwa ni kubaini wahusika na hasara ambayo Serikali imepata katika uuzaji wa viza stika bandia kwa raia wa kigeni walioingia nchini kupitia KIA na kupendekeza hatua stahiki za kuchukuliwa na Afisa Masuuli wa Idara ya Uhamiaji (Fungu 93).

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu wa kiuchunguzi ulibaini kuwa, katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Januari 2019 hadi 30 Juni 2019, Watanzania 41 na wageni 107,119 waliwasili nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Kati ya wageni 107,119 waliowasili nchini,

2 NOVEMBA, 2022

wageni 11,341 walipata viza kwa njia ya mtandao, wageni 7,044 walipata viza kutoka kwenye Ofisi za Balozi zilizopo nchi mbalimbali na wageni 13,678 hawakuwa na viza kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo misamaha, pasi, mikataba. Aidha, wageni 41,286 walilipa viza walipowasili KIA. Wageni 212 waliwasili KIA lakini walinunua viza stika wakiwa katika viwanja vya Ndege vya Julius Nyerere (JNIA) na Abeid Amani Karume (AAKIA).

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa wageni 33,558 waliwasili nchini kupitia KIA. Hata hivyo, taarifa za wageni hao ambazo ni pamoja na fomu za kuingia nchini (entry form), stakabadhi za mapokezi ya fedha (ERV), na taarifa za uwekaji fedha benki (deposit slip) hazikupatikana kwa ajili ya uhakiki. Kwa sababu hiyo, ukaguzi haukuweza kuthibitisha kiasi cha mapato ambacho Serikali ilipaswa kupata kutoka kwa wageni hao.

Mheshimiwa Spika, katika hoja ya 2, matokeo ya ukaguzi huo maalumu yaliendelea kubainisha mapungufu makubwa kwenye Mfumo wa Maombi ya Viza (VAS) uliokuwa unatumika kurekodi taarifa za wageni waliolipia viza wakati wa kuwasili, pamoja na wale wenye viza zisizolipiwa (gratis VIZA). Taarifa katika mfumo wa VAS zilirekodiwa na kukamilishwa baada ya mgeni husika kulipia ada za viza na kupokea stakabadhi ya mapokezi ya fedha (ERV).

Mheshimiwa Spika, pamoja na Idara ya Uhamiaji (Fungu 93) kuwa na Mfumo wa VAS, pia ilikuwa na mfumo wa "PISCES" ambao ulikuwa unafuatilia masuala yote ya kiusalama. Mfumo huu ulihifadhi taarifa zote za Watanzania na wageni

2 NOVEMBA, 2022

wenye marufuku ya kuingia nchini na ilikuwa ni lazima kwa abiria wote wapitie kwenye Mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia dosari za kimfumo, ukaguzi ulibaini kuwa watumishi 32 wa Idara ya Uhamiaji KIA walifuta na kuziondoa kwenye kanzidata taarifa 21,208 za wageni walioingia nchini na ambao walilipa kiasi cha **Sh. 2,427,255,600**. Hata hivyo, Kiasi hicho cha fedha hakikuwasilishwa benki na hivyo kusababisha Serikali kupoteza mapato ya takribani **Sh. 2,427,255,600**.

Mheshimiwa Spika, CAG ameifahamisha Kamati kuwa Idara ya Uhamiaji (Fungu 93) imeacha kutumia mfumo wa VAS kuanzia tarehe 23 Agosti 2019 na badala yake imeanza kutumia mfumo mpya wa utoaji wa viza kwa njia ya kielektroniki (e-viza).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hadi tunapotoa taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu, CAG alikuwa hajafanya mapitio na ukaguzi wa mfumo huo mpya ili kubaini uthabiti wake na iwapo mapungufu ya mfumo wa zamani ambayo yalisababisha upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali yamepatiwa ufumbuzi. Vilevile wahusika waliotajwa na ukaguzi huu maalumu baadhi walifikishwa kwenye vyombo vya sheria na kisha kuachiwa huru na wengine hawajachukuliwa hatua za kisheria hadi sasa.

2.7.3 Ukaguzi Maalumu wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo

Mheshimiwa Spika, Kifungu Na. 29 (1) cha Sheria ya Ukaguzi

2 NOVEMBA, 2022

wa Umma ya Mwaka 2008, kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kufanya ukaguzi wa aina yoyote pale anapoona inafaa. Pia, katika kifungu cha 29(2), Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kuombwa na Mtu yeyote, Taasisi, Shirika la Umma, Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Bodi yoyote ya Umma kufanya Ukaguzi Maalumu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu umetokana na kubainika kuwepo na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani katika mapato na ubadhirifu katika ukusanyaji wa mapato wakati wa ukaguzi wa kawaida hivyo kupelekea Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuamua kufanya ukaguzi huu maalumu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu maalumu ulianza tarehe 12 Oktoba, 2020 baada ya taratibu za kuandaa na kuidhinisha hadidu za rejea na kuandaa mpango mkakati wa ukaguzi kukamilika. Ukaguzi huu maalumu ulifanyika ili kukidhi lengo lililoainishwa katika Hadidu za Rejea. Katika kufanya ukaguzi huu maalumu, timu iliongozwa na Hadidu za Rejea zifuatazo: -

a) Kuhakiki Mfumo wa udhibiti wa ndani (Internal controls) wa kukusanya mapato ikijumuisha mifumo ya kielektroniki (GePG) iwapo ni madhubuti na ulifanya kazi kikamilifu kwa kipindi cha mwaka 2019/20; na

b) Kuhakiki mapato yote yaliyotakiwa kukusanywa na yaliyokusanywa kwa kipindi cha mwaka 2019/20 na kubaini iwapo kulikuwapo na ubadhirifu wowote wa mapato. [1]
[SEP]

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia hadidu za rejea nilizozitaja hapo juu, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi huu maalumu kama ifuatavyo:-

a) Stakabadhi za makusanyo ya maduhuli kutolewa nje ya mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (Government electronic Payment Gateway)

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 69(1) na (2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inaelekeza kuwa (1) Hakuna mabadiliko yatakayofanywa kwa stakabadhi yoyote, leseni, au hati nyingine inayofanana na hizo, na ikiwa kosa limefanywa katika kukamilisha nyaraka hiyo au ikiwa hati hiyo imeharibiwa, hati ya halisi na nakala zitawekwa wazi kuwa zimefutwa na afisa aliyepewa mamlaka ya kutoa hati; (2) Pale kosa linapofanywa katika hati iliyotajwa katika kifungu kidogo cha sheria (1) nakala halisi, hazitaharibiwa, lakini lazima zihifadhiwe na kutolewa kwa ukaguzi wakati inapohitajika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu hiyo inasoma, nanukuu;

“No alterations shall be made to any receipt, license, or other similar document and if an error is made in completing the document or if the document is otherwise spoiled, the original and the counterfoil or copies shall be clearly marked as cancelled and initialed by the officer empowered to issue the document. (2) where an error is made in the document referred to in sub regulation (1) the original, counterfoil or copies shall not be destroyed, but they must be retained intact and produced for inspection when

2 NOVEMBA, 2022

required.”

Mheshimiwa Spika, Timu ya Ukaguzi iliweza kujiridhisha kuwa stakabadhi tajwa zilitolewa nje ya mfumo baada ya kufanya mambo 2. Kwanza kuingia kwenye Mfumo wa Malipo (GePG) na pili kuangalia namba za kumbukumbu kama zipo kwenye mfumo, namba za kumbukumbu zote za malipo ya **Sh. 76,106,600** hazikuweza kuonekana.

b) Watumishi 7 wasiokuwa na sifa kusajiliwa na kupewa haki ya kutumia mfumo ^L_{SEP}

Mheshimiwa Spika, muongozo wa kiwango cha Kimataifa cha Usalama wa Mifumo, ISO/IEC 27002 inayohitaji mgawanyo wa majukumu kuzingatiwa wakati wa utoaji wa haki (Access Rights) kwa watumiaji wa mfumo. Ukaguzi Maalumu ulibaini kuwa jumla ya watumishi ishirini (20) walisajiliwa katika mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini. Kati ya watumishi hao kumi na moja (11) ni wahasibu, wawili ni maafisa TEHAMA na saba (7) ni watumishi wenye kada tofauti na Wahasibu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulibaini kuwa watumishi hao ambao sio wa kada ya Uhasibu wamesajiliwa na kupewa haki ya kutumia mfumo kwa hadhi ya “SP service manager” ambayo inamruhusu kufanya majukumu yoyote ndani ya mfumo ingawa ilitakiwa wapewe haki za kuingia kwenye mfumo kulingana na taarifa wanazostahili kuona na majukumu yao katika mfumo. Hali hiyo ni kinyume na aya 6.1.2. ya muongozo wa kiwango cha Kimataifa cha Usalama wa Mifumo, ISO/IEC 27002.

2 NOVEMBA, 2022

c) Kutokuwepo kwa mgawanyo wa majukumu ndani ya mfumo wa kukusanya maduhuli (GePG) kwa kada ya wahasibu

Mheshimiwa Spika, muongozo wa kiwango cha Kimataifa cha Usalama wa Mifumo, ISO/IEC 27002 unafafanua mgawanyo wa majukumu kwa kuzingatia wakati wa utoaji wa haki (Access rights) kwa watumiaji wa kwenye mfumo.

[L]
[SEP]

Mheshimiwa Spika, ukaguzi Maalumu ulibaini kuwa Wahasibu wa chuo wote 11 walipewa hadhi sawa katika mfumo (SP Customer Manager na SP Service Manager) ambapo wanakuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yote katika mfumo kama vile kuandaa ankara na kutoa “control number”, kuangalia ankara ambazo zimetolewa na Wahasibu wengine, kuangalia ankara ambazo zimelipwa na ambazo hazijalipwa, kutoa stakabadhi na kuona ripoti zote za kwenye mfumo kinyume na muongozo.

d) Usajili wa wanafunzi kufanyika kabla ya uthibitisho wa malipo ya ada shilingi 17,742,000 [L]
[SEP]

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 5 (1) ya Kanuni za Usajili na Mitihani ya Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo ya Mwaka 2008 inasema “wanafunzi watasajiliwa tu baada ya kulipa kiasi cha ada ambacho kitaamuliwa na Bodi” sehemu hiyo inasoma nanukuu:-

“Students shall only be registered upon payment of prescribed fees the amount which shall be determined by the Board”.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa masomo 2019/20 ulioanza tarehe 20/7/2019 hadi 27/7/2019, Ukaguzi ulibaini kuwa wanachuo hamsini (50) walisajiliwa kabla ya kufanya malipo ya ada kwa kuwa malipo yao yalifanyika baada ya kipindi cha usajili kukamilishwa.

e) Ubadhirifu uliotokana na matumizi ya stakabadhi zisizo halisi za kukiri mapokezi ya ada zenye thamani ya Sh. 76,106,600

Mheshimiwa Spika, ukaguzi maalumu ulipitia kwa kina stakabadhi 296 zenye thamani ya **Sh. 76,106,600** zilizoshukiwa kuwa na mgogoro na taarifa za makusanyo ya Ada na malipo mbalimbali katika daftari la fedha taslimu (Cash book) kutoka katika Mfumo wa kieletroniki wa malipo Serikalini (GePG) na kuthibitisha kuwa hazikutolewa kwenye mfumo kwa kuwa hazikuweza kuonekana kwenye kumbukumbu ya orodha ya malipo yaliyofanywa kwenye mfumo wa kielektroniki wa malipo Serikalini (GePG).

Mheshimiwa Spika, stakabadhi hizo zilizoghushiwa zilionyesha majina ya wahasibu waliotoa stakabadhi ambao ni Sailes Maine Marashi, James William Kankila na Gideon Charles Mhagama na saini zao. Uhakiki wa saini za watuhumiwa ulifanyika katika Maabara ya kiuchunguzi ya kisayansi ya Jeshi la Polisi (Forensic Investigation Bureau) na kubaini kuwa saini zote za watuhumiwa zililingana (match) na maandishi yao yaliyochukuliwa sehemu mbalimbali, hivyo kuthibitisha upokeaji wa ada kwa fedha taslimu kutoka kwa wanachuo, kinyume na waraka wa Hazina Na.3 wenye Kumbukumbu Na.CAB.481/558/01 ukiwataka Afisa

2 NOVEMBA, 2022

Masuuli wa Wizara zote na taasisi za Serikali kuanza kutumia mfumo wa kukusanya maduhuli wa Serikali (GePG).

f) Wanafunzi kufanya mitihani bila ya kulipa ada Sh. 928,268,528

Mheshimiwa Spika, ukaguzi maalumu ulibaini kuwa jumla ya ada kiasi cha **Sh. 928,268,528** hakikulipwa na wanachuo waliofanya mitihani kwa mwaka wa masomo 2019/2020. Kati ya kiasi hicho **Sh. 638,453,928** kilitokana na wanachuo 1,716 waliofanya mitihani kwa kulipa kiwango pungufu na **Sh.289, 814,600** kilitokana na wanafunzi 285 kutokulipa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli - TAMISEMI pamoja na Bodi ya Chuo cha Hombolo ili kupata majibu ya Serikali kuhusu hatua zilizochukuliwa kutokana na matokeo ya ukaguzi huo maalumu. Serikali iliifahamisha Kamati kuwa imechukua hatua za kinidhamu kwa watuhumiwa ikiwa ni pamoja na kushushwa vyeo. Aidha, Chuo kimeimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuongeza ufanisi na usimamizi wa fedha za umma. Hata hivyo, hatua za kisheria kwa wahusika bado hazijakamilika ipasavyo.

2.7.4 Ukaguzi Maalumu wa Mradi wa Orio (Orio Tanzania Project Escrow Account)

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi uliofanyika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020 ilibainika kuwa Wizara ya

2 NOVEMBA, 2022

Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu 52) ilifanya malipo ya **Euro 1,650,832.17** (Sawa na **Sh. 4,251,751,270.48**) kutoka Akaunti 1950237541600 iliyofunguliwa mwaka wa fedha 2014/15 kwa ajili ya mradi wa ugavi wa vifaa tiba vya Kiuchunguzi kutoka Uholanzi (ORIO PROJECT). Pamoja na mambo mengine, Akaunti hii ilikuwa haikaguliwi tangu mwaka wa fedha 2014/15 na vifaa tiba vilivyolipiwa mwaka wa fedha 2019/20 vilikuwa bado havijapokelewa.

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka aliyonayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali chini ya kifungu 78 ya Ukaguzi wa Umma, 2009, CAG aliamua kufanya ukaguzi Maalum utakaoweza kupata Taarifa kamili juu ya miamala yote iliyofanyika katika akaunti tajwa hapo juu na kufuatilia kwa kina kuhusu mradi mzima na hali ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mujibu wa taarifa ya ukaguzi maalumu ilibainika kuwa tarehe 27 Novemba, 2012 Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha (Kwa Sasa Wizara ya Fedha na Mipango) iliingia Mkataba Na. ORIO09/TZ/05I na Serikali ya Uholanzi kupitia Wizara ya Biashara ya Nje na Ushirikiano wa Maendeleo ya Ufalme wa Uholanzi kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Ugavi wa vifaa tiba vya kiuchunguzi ujulikanao kama Orio.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulikuwa na thamani ya **Euro 23,000,000** kulingana na makubaliano ya awali na baadaye thamani ya mradi iliongezeka hadi **Euro 23,819,509**. Mradi huu ulikuwa unachangiwa na pande zote mbili kwa 50% kila

2 NOVEMBA, 2022

mmoja. ^[1]Mradi ulikuwa na lengo la kuboresha miundombinu ya Hospitali nchini Tanzania hasa katika huduma za uchunguzi wa mionzi na picha, huduma za akina mama na kuboresha huduma za kitabibu katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mradi huu, baada ya makubaliano ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uholanzi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliingia Mkataba Na. ME/007/2012-13/HQ/G-W-S/01 na Kampuni ya “Philips Medical System Netherland B.V” ya Uholanzi kwa ajili ya Ugavi wa Vifaa tiba vya kiuchunguzi. Mkataba huu wa miaka 6 ulikuwa na thamani ya **Euro 22,422,471.00** na ulisainiwa tarehe 16 Septemba, 2014. Utekelezaji wa huu Mkataba ulitegemea kuisha Julai, 2016 kwa awamu ya kwanza ya usambazaji wa vifaa na Julai 2021 awamu ya pili ya utumiaji wa vifaa na matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa taarifa hiyo ya ukaguzi maalumu na kubaini hoja zifuatazo: -

- a) Serikali ilichelewa kuweka mchango wake wa fedha kwenye akaunti ya Orio kiasi cha **Euro 2, 900,000** kwa mujibu wa matakwa ya mkataba. Jambo hili lilisababisha kuchelewa utekelezaji wa mradi kwa takribani kipindi cha miezi 19;
- b) Dosari katika manunuzi ikiwa ni pamoja na baadhi ya manunuzi kufanyika bila ya kujumuishwa katika mpango wa mwaka wa manunuzi kinyume na Kifungu 75(1) cha Kanuni

2 NOVEMBA, 2022

za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013;

- c) Kutofanyika kwa mafunzo ya kitaalamu (Biomedical Engineers Training) kwa mujibu wa mkataba. Kwa mujibu wa nyongeza "H" ya mkataba wa Orio, sehemu ya gharama za mkataba ilijumuisha mafunzo ambayo ukaguzi maalumu ulibaini hayakuwa yamefanyika;
- d) Malipo yasiyokuwa na tija (Nugatory expenditure) ya kiasi cha **Sh. 665,138,998** kinyume na Kifungu 21 (2) cha Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001. Malipo haya yalitokana na ucheleweshaji wa Serikali kulipa fedha za kugomboa mizigo toka bandarini;
- e) Kutumia muda mrefu kutoka kupokea mizigo hadi kuifunga na kuanza kufanya kazi. Changamoto hii ilibainika hususan kwenye mitambo ya CT Scan na MRI. Mathalani kwa hospitali ya Bugando, mashine ya MRI ilipokelewa tarehe 15 Januari, 2021 hata hivyo hadi uhakiki unafanyika tarehe 24 Juni, 2021 mashine hiyo ilikuwa bado haijakabidhiwa rasmi kwa hospitali; na
- f) Dosari katika shughuli za ujenzi wa vyumba vya kuhifadhi vifaa tiba kwa baadhi ya hospitali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea na kuchambua Taarifa ya Ukaguzi huu Maalumu wa Akaunti ya ORIO, Kamati ilipata fursa ya kufanya mahojiano ya kina na Afisa Masuuli Fungu 52 – Wizara ya Afya. Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati jitihada ambazo zimechukuliwa ili kurekebisha dosari zilizoibuliwa na CAG. Hatua hizo ni pamoja na kufanya mapitio ya mkataba husika ili kuondoa

2 NOVEMBA, 2022

masharti hasi yaliyomo katika mkataba huo. Katika sehemu ya 3 ya taarifa hii, Kamati imetoa pendekezo la namna Wizara inavyoweza kuboresha usimamizi wa mikataba mikubwa ya afya.

2.8 Dosari za Msingi Zilizobainishwa na CAG

Mheshimiwa Spika, CAG alibainisha dosari za msingi katika matumizi ya fedha za umma katika maeneo mengine kama ifuatavyo: -

2.8.1 Kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 (R.E.2020) na Miongozo ya Usimamizi wa Fedha za Umma

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 kama ilivyorejewa mwaka 2020, ndio Sheria ya msingi kabisa inayotoa mwongozo wa namna bora ya usimamizi, matumizi na udhibiti wa makusanyo na matumizi ya Fedha za Umma. Aidha, Sheria hii ni mahsus katika kuliwezesha Bunge kudhibiti na kusimamia fedha za umma, rasilimali na masuala yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Spika, mapitio na uchambuzi wa kina wa Kamati pamoja na mahojiano na Maafisa Masuuli mbalimbali, umebaini uwepo wa matukio ya ukiukwaji wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura 348. Kamati inawasilisha katika taarifa hii masuala yaliyobainika katika eneo hili na kwa mafungu husika kama ifuatavyo: -

2 NOVEMBA, 2022

(a) Kutohibitishwa Uwepo wa Mapato ya Kiasi cha Sh. 3,567,797,000 na Matumizi ya kiasi cha Sh. 3,562,364,709 Katika Shirika la Masoko Kariakoo

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 10/07/2021 jengo la Shirika la Soko la Kariakoo liliungua kwa moto uliosababisha kuteketea kwa nyaraka na taarifa muhimu za shirika, bidhaa za wafanyabiashara na mali nyinginezo. Kutokana na hali hiyo Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alishindwa kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa wa ukaguzi wa taarifa za kifedha za Shirika la Soko ya Kariakoo (KMC) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021.

Mheshimiwa Spika, maeneo mahsusi ambayo yalisababisha CAG kushinda kutoa maoni katika Shirika la Masoko Kariakoo ni kama ifuatavyo: -

- i. CAG hakuweza kuthibitisha mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ya kiasi cha **Sh. 3,567,797,000** yaliorekodiwa katika taarifa za fedha za Shirika la Masoko ya Kariakoo kwa sababu hakupewa uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za mapato husika, kama vile ankara za wateja au bili, risiti, mikataba ya watoa huduma kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato na mikataba ya wapangaji. Aidha, CAG hakuweza kujiridhisha kwa njia mbadala kuhusu mapato ya **Sh.3, 567,797,000** yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2020/2021, kama yalivyoainishwa katika taarifa ya mapato na matumizi ya Shirika;
- ii. CAG hakuweza kuthibitisha matumizi ya **Sh. 3,562,364,709** kwa sababu hakupewa vocha za malipo na nyaraka za uthibitisho zinazohusiana na malipo tajwa. Aidha, CAG

2 NOVEMBA, 2022

hakuweza kujiridhisha na kuthibitisha kwa njia mbadala kuhusu matumizi ya **Sh. 3,562,364,709** yaliyofanyika katika kipindi cha mwaka 2020/21 kama yalivyoainishwa katika taarifa ya mapato na matumizi ya Shirika;

- iii. [SEP] CAG hakuweza kuthibitisha madeni ambayo shirika linadai ya jumla ya **Sh. 2,451,703,331** (Trade and other receivables) yaliyoripotiwa katika taarifa ya mizania (Statements of financial position) ya tarehe 30 Juni 2021;
- iv. [SEP] CAG hakuweza kuthibitisha madeni ya kibiashara na mengine ambayo shirika linadaiwa (trade payables and other payables) ya jumla ya **Sh.1, 223,152,000** kwa sababu CAG hakupewa nyaraka sahihi za madeni hayo ikiwa ni pamoja na mikataba ya watoa huduma, vocha za malipo, ankara, hati za manunuzi, risiti, na nyaraka nyinginezo zinazohusiana na madeni hayo; na
- v. CAG hakuweza kuthibitisha mali, mitambo na vifaa vya **Sh. 55,466,235,364** vya Shirika kwa sababu hakuweza kupatiwa daftari la mali zisizohamishika (fixed assets register), Pamoja na nyaraka nyingine zinazohusiana na mali hizo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati katika eneo hili ni kwamba, taasisi zote za Serikali zinatakiwa kuwa na njia mbadala ya kutunza taarifa muhimu za fedha ili kunapotokea majanga kama ya moto au mafuriko, basi iwepo njia mbadala ya kupata taarifa hizo. Hili ni takwa la kisheria la Sheria ya Fedha za Umma Sura 348.

Mheshimiwa Spika, hivyo janga la moto lilolotokea Kariakoo linaweza kutumika kuficha matumizi mabaya ya fedha za

2 NOVEMBA, 2022

umma kwa CAG kutopewa nyaraka muhimu za fedha ili kukamilisha ukaguzi. Kamati imetoa pendekezo mahsusi katika suala hili kwenye sehemu ya 3 ya taarifa hii.

(b) Malipo ya Fidia Zaidi ya Kiwango Kilichopo Kwenye Taarifa ya Tathmini Kiasi cha Sh. 1,070,637,576 na Malipo ya Usumbufu Sh. 434,129,600 Kulikofanywa na DART

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ulibainisha uwepo wa hoja ya ukaguzi inayohusu malipo ya **Sh. 1,070,637,576** kama fidia. Fidia hii ililipwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usajili wa Ardhi ya Mwaka 1999 (R.E 2019) na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya Mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, hoja hii inatokana na maelezo ya DART kuwa jedwali la malipo ya **Sh. 1,070,637,576** linahusisha malipo yaliyofanyika kwa wahusika 17 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, DART walifafanua kuwa malipo hayo ni mwendelezo wa malipo yasiokuwa yamefanyika kati ya mwaka 2010 na 2013.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, CAG aliifahamisha Kamati kuwa hadi ukaguzi huu unakamilika hakuwa amepewa nyaraka kuthibitisha uhalali wa malipo hayo kwa wahusika 17. Hii ni pamoja na kutokuwepo muhtasari uliosainiwa kupitisha malipo ya uthamini wa ardhi kwa wahusika. Aidha, malipo hayo ya fidia yalikusisha pia malipo ya fedha za usumbufu kiasi cha **Sh. 434,129,600**. Hata hivyo, CAG katika taarifa yake alifafanua kuwa hapakuwa na uthibitisho

2 NOVEMBA, 2022

kuonyesha kuwa Serikali ndiyo ilitoa idhini ya kulipa riba ya usumbufu kwa walalamikaji.

(c) **Kutoandaliwa Hesabu na Kutofanyika kwa Ukaguzi wa Hesabu za Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Polisi (Police Force Rewards Fund) Katika Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeanzisha Mfuko wa Tuzo (Rewards Fund) ambao umeanzishwa chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi (The Police Force and Auxiliary Services Act; Cap 322) ili kuchukua nafasi ya Mfuko uliokuwa ukiitwa Mfuko wa Tozo na Zawadi (Police Rewards and Fines Fund). Kwa mujibu wa Kifungu cha 66 (4) cha Sheria hiyo Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Polisi (Police Rewards Fund) ulianzishwa mahususi kwa ajili ya ustawi wa askari.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Fungu 28 – Jeshi la Polisi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021, CAG alibaini uwepo wa kiasi cha **Sh. 35,382,216,828** ambayo ni fedha iliyowekwa kwenye akaunti Benki Kuu kutokana na mfuko wa tuzo na tozo. Hata hivyo pamoja na uwepo wa fedha hizo katika mfuko wa zawadi, CAG alibaini hapakuwa na Kanuni za kusimamia uendeshaji wa mfuko huo na hesabu za mfuko hazikuwasilishwa kwa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 30(3) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 kinamtaka kila Afisa yeyote wa Serikali aliyekabidhiwa nafasi ya kuendesha mfuko maalumu, kuandaa na kuwasilisha kwa CAG hesabu za mfuko kwaajili ya ukaguzi kila inapotakiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Nukuu ya sehemu ya Kifungu husika ni kama ifuatavyo: -

“ ...Any public officer administering a fund established or deemed to have been established under section 17, and any public officer administering any agency, trust or other fund or account not provided for in this section, shall prepare, sign and transmit to the Controller and Auditor – General Financial Statements of that agency, trust or other fund or account in accordance with International Accounting Standards (IAS)..”

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, hatua ya Afisa Masuuli wa Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi kutoandaa taarifa ya hesabu za mfuko huo kwa kipindi chote ili zikaguliwe ni kinyume na masharti ya Sheria ya Fedha za Umma Sura 348. Aidha kutokuwepo kwa Kanuni za uendeshaji wa mfuko kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma na matumizi mabaya ya fedha za umma.

2.9 Umiliki na Uendeshaji wa Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO)

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 07 Septemba, 2022, Kamati ilikutana kupitia na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Kampuni ya Uendelezaji wa Kiwanda cha Ndege cha Kilimanjaro (KADCO) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika Kikao hicho Kamati ilibaini uwepo wa hoja ya ukaguzi inayohusu uendeshaji wa KADCO. Hoja hiyo kimsingi inahusu misingi ya kisheria ya uendeshaji wa KADCO hasa ikizingatiwa kuwa KADCO ni Shirika la Umma lakini kuna mkataba wa miaka 25 wa uendeshaji (Concession agreement) wa Kampuni ya Uendelezaji Wa Kiwanja Cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro (KADCO). Mkataba huu ni baina ya Serikali na KADCO uliosainiwa tarehe 17 Julai 1998 ambao kwa masharti yake ulitakiwa uwe umepitiwa na kuhuishwa mwaka 2013 na unatakiwa kukamilika tarehe 16 Julai 2023.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ilibua changamoto kwa Kamati ambapo Kamati iliitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Bodi ya KADCO, Msajili wa Hazina (TR) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kuwasilisha maelezo ya kina kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 09 Oktoba, 2022, wahasika niliowataja hapo juu walifikia mbele ya Kamati kwa ajili ya kuwasilisha maelezo ya ziada kuhusiana na hoja ya uendeshaji wa kisheria na mkataba wa KADCO. Katibu Mkuu Sekta ya Ujenzi na Msajili wa Hazina waliieleza Kamati kwamba hoja ya mkataba wa uendeshaji inafanyiwa kazi na kikosi kazi kilichoundwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Hata hivyo, ilibainika kuwa jambo hili halijapatiwa ufumbuzi kwa wakati kwani mkataba huo wa uendeshaji utamalizika muda wake tarehe 16 Julai 2023.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Kamati iliamua kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya CAG kuhusu KADCO na kubaini kuwa Kampuni ya Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege ya Kilimanjaro (Kilimanjaro Airports Development Company Limited - KADCO) ilisajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 mnamo tarehe 11 Machi, 1998 kama kampuni binafsi ikiwa inamilikiwa na Kampuni mbili ambazo ni Mott MacDonald International Limited aliyekuwa na hisa 99%; na Inter Consult Limited aliyekuwa na hisa 1%.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuundwa KADCO lilikuwa kuwezesha uwekezaji katika kiwanja cha KIA. Kwa misingi hiyo, Serikali na KADCO waliingia mkataba wa wanahisa (Shareholders agreement). Mkataba huu ulisainiwa tarehe 17 Julai, 1998 ili kurekebisha umiliki wa Kampuni ya KADCO kwa kuongeza wanahisa wengine na hivyo kuifanya Serikali kumiliki 24% ya hisa za KADCO na 76% kumilikiwa na wanahisa wengine kwa mgawanyo ufuatao: -

- a) Mott MacDonald International 41.4%;
- b) South Africa Infrastructure Fund- SAIF 30%; na
- c) Inter Consult (T) Limited 4.6%.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 10 Novemba, 1998 Serikali iliingia Mkataba wa uendeshaji (Concession agreement) na KADCO. Mkataba huo uliipa KADCO haki ya kipekee ya kuendeleza Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kwa kipindi cha miaka 25. Ilipofika mwaka 2006, Serikali ilifanya tathmini ya utendaji wa kampuni na kubaini changamoto zifuatazo: -

2 NOVEMBA, 2022

- a) Wanahisa wenza kushindwa kuwekeza katika uendelezaji wa miundombinu ya KIA na hivyo kusababisha utendaji usioridhisha;
- b) Serikali kutonufaika kutokana na kutokuwepo kwa kipengele cha kuitaka KADCO kulipa ada ya uendeshaji wa KIA (Concession fee);
- c) Kutokuwepo kwa kipengele kinachoweka masharti ya ukomo wa mkataba na badala yake mkataba umeweka kipengele ambacho kinaweka masharti ya kuhuisha mkataba kila baada ya miaka 15; na
- d) Kuwepo kwa kipengele kinachoipa KADCO haki ya pekee ya kuzuia uwepo wa kiwanja kingine cha ndege cha kimataifa ndani ya usawa wa mzunguko (radius) wa kilomita 240 kila upande kutoka KIA.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizodainishwa hapo juu, mwaka 2008 Serikali ilipendekeza kwa wanahisa wenza kufanya marekebisho ya mkataba. Mapendekezo ya marekebisho hayo yalikataliwa na wanahisa wenza. Hadi kufikia mwaka 2009 hakukuwa na maafikiano na hivyo Serikali iliamua kununua hisa zote za wanahisa wenza na hivyo kufanya Serikali kuwa mwanahisa pekee wa KADCO kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, baada ya kununua hisa, Serikali iliendelea kurekebisha taarifa za KADCO zilizoko BRELA kuhusu hali ya umiliki wa hisa kwa 100% chini ya Msajili wa Hazina. Kufuatia kukamilika kwa utaratibu huo mwaka 2014

2 NOVEMBA, 2022

KADCO ilipewa namba ya usajili (TR 169) kama Kampuni ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na maelezo hayo Kamati kwa kupitia taarifa ya CAG ilibaini uwepo wa hoja ambazo zinatakiwa kutolewa majibu kama ifuatavyo: -

- a) Maelezo kuhusu uhalali na sababu ya kuendelea kuwepo mkataba wa uendeshaji (Concession agreement) kati ya Kampuni ya Uendeshaji Kiwanja cha ndege Kilimanjaro (KADCO) na Serikali unaotarajiwa kufikia ukomo tarehe 16 Julai, 2023;
- b) Maelezo kuhusu mchango ambao wabia wa mwanzo wa KADCO walichangia ulikuwa kiasi gani kwa mujibu wa mkataba na kwa kiasi gani walitimiza masharti ya mkataba huo. Ikumbukwe kuwa Serikali ilitumia fedha za umma takribani (**Dola za Marekani milioni 5.3**) fedha ambazo zilitokana na mkopo uliochukuliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kutoka benki ya CRDB⁸ kununua hisa zote za KADCO; na
- c) Maelezo kuhusu sababu ya msingi ya KADCO kutoendeshwa katika kipindi cha mpito na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) au kuwa kampuni tanzu ya TAA kama uamuzi wa awali wa Serikali ulivyoelekeza na kwa mujibu wa majukumu ya kisheria ya TAA⁹.

⁸ Marejesho ya mkopo husika yalikamilika mwezi Novemba 2014.

⁹ Rejea GN. Na. 504 ya mwaka 1999 kuhusu majukumu ya TAA.

2.10 Utendaji wa Kifedha wa Benki za Serikali (TCB na TIB)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Benki ya Tanzania ya Biashara (TCB) na Benki ya Maendeleo ya TIB. Katika uchambuzi wa hesabu za benki hizo za Serikali, hoja kuu mbili (2) zilibainika kama ifuatavyo: -

a) Ongezeko la Mikopo Chechefu (Non Performing Loans, NPL)

Kwa mujibu wa mwongozo Na. FA.130/170/01/5 uliotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) tarehe 22 Januari 2021, Benki hazitakiwi kuzidisha kiasi cha mikopo chechefu kwa zaidi ya 5%. Hata hivyo ukaguzi wa hesabu za TCB na TIB umebainisha ongezeko la aina hiyo ya mikopo kwa kipindi cha miaka miwili (2) mtawalia. Mchanganuo wa aina hiyo ya mikopo umefafanuliwa katika Jedwali Na. 2.4 hapa chini.

Jedwali Na. 2.4: Mchanganuo wa Mikopo Chechefu Katika Benki za TIB, TADB na TCB

Maelezo	TIB Development Bank		TCB BANK	
	2019	2020	2019	2020
NPL (TZS'Millioni)	260,850	327,296	24,689	93,289
Total Exposure (TZS'Millioni)	628,804	634,105	420,590	617,810
NPL Ratio	41.48%	51.62%	5.87%	15.10%

Chanzo. Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za TIB na TCB kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa ongezeko la mikopo chechefu kwa TIB limechangiwa zaidi na Benki kuwa na changamoto ya mtaji kulikotokana na anguko la kiuchumi kwa sekta zilizokopa toka kwenye Benki hiyo. Kwa upande wa TCB ongezeko la NPL limesababishwa na hatua ya kuunganishwa kwa shughuli za iliyokuwa Benki ya Posta na Benki ya TIB Biashara. Hatua hiyo ilisababisha mikopo chechefu kuongezeka kwa 9.23% ukilinganisha na ile iliyoripotiwa mwaka 2019.

b) Hali ya Utoshelevu wa Mtaji katika Benki za Serikali (Capital Adequacy Ratio)

Kanuni 19(2) ya Kanuni za Benki na Taasisi za Kifedha (Development Finance) Kanuni za Mwaka, 2011, zinaitaka taasisi ya kifedha ya maendeleo kwa muda wote kuwa na mtaji wa msingi (Core capital) na mtaji wa jumla (Total capital) kwa wastani wa 13% and 15% mtawalia.

Uchambuzi wa taarifa za hesabu za TCB na TIB Development Bank, ulibaini kuwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2020 TIB Development Bank na TCB, mtaji ulikuwa 6.9% na 10.94% mtawalia kwa mtaji wa msingi na mtaji wa jumla hivyo kuwa chini ya kiwango kinachokubalika cha 13% and 15% mtawalia. Kwa upande wa TIB, hali ya mtaji kuwa mbaya ilitokanana kupata hasara mfululizo ambapo hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2020 Benki ilikuwa na hasara jumuiifu ya **Sh. Bilioni 134.95** ambayo ilikula mtaji wa Benki.

Kwa upande wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) hali mbaya ya mtaji imesababishwa na kuunganishwa kwa Benki hiyo na Benki ya TIB Biashara, kwani hapo kabla uwiano wa mtaji ulikuwa 16.80% (2019) na 10.94% 2020.

2 NOVEMBA, 2022

Hoja hizo mbili hapo juu ni za muhimu sana, kwa kuwa utoshelevu wa mtaji ni Kigezo muhimu cha Benki kuwa na leseni ya kufanya biashara. Hivyo kihatarishi kinachozikabili Benki hizi ni kikubwa na hivyo kinaweza kusababisha Benki husika kuwekwa chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa mujibu wa Sheria.

2.11 Uchambuzi wa Taarifa za Kaguzi za Ufanisi

Mheshimiwa Spika, katika kipindi tunachokitolea taarifa, Kamati ilifanikiwa kupitia na kuchambua jumla ya taarifa 4 za ukaguzi wa ufanisi. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, hii ni hatua kubwa na ya mfano kwa Bunge kuanza kujadili taarifa za ukaguzi wa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu na kwa tamaduni za Mabunge mengi ndani ya Jumuiya ya Madola, Kamati za Bunge zimekuwa zikipitia na kujadili taarifa za ukaguzi za hesabu (Financial audit) bila kutoa muda wa kutosha wa kupitia na kuchambua taarifa za ukaguzi wa ufanisi (Performance audit reports).

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, matumizi mabaya ya fedha za umma sio lazima yatokane na ubadhirifu katika masuala kama manunuzi au malipo yanayokiuka sheria. Matumizi mabaya ya fedha za umma yanahusisha pia hali ya taasisi za umma kutofikia malengo ya uanzishwaji wake kwa mujibu wa Sheria.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, msingi wa hoja hii unajengwa kwenye uzoefu kuwa, taasisi hizi zinatumia rasilimali za umma kila katika uendeshaji wake ikiwa ni pamoja na malipo ya mishahara, maji, umeme na usafiri. Hivyo iwapo malengo husika ya taasisi hayatafikiwa kwa mujibu wa dhima na dhamira za kuanzishwa kwake, basi hayo pia ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali katika sehemu hii ya taarifa, naomba kutoa uchambuzi wa Kamati kwa taarifa 4 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyiwa kazi ambazo zinabainisha hali ya matumizi yenye dosari katika fedha za umma kama ifuatavyo: -

2.11.1 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Upangaji na Ugawaji wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la ukaguzi ilikuwa ni kubaini iwapo mfumo wa utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu chini ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini unafanya kazi ipasavyo na kama mikopo inatolewa kwa usahihi na kwa haki kwa wanafunzi wenye uhitaji.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulilenga kutathmini ufanisi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kusimamia maombi ya mikopo, utendaji kazi wa mfumo wa upangaji wa mikopo, ufanisi katika kusimamia rufaa za mikopo, ufanisi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika kugawa mikopo kwa waombaji waliofanikiwa

2 NOVEMBA, 2022

pamoja na utendaji kazi wa mfumo mzima wa usimamizi wa sekta ya mikopo ya elimu ya juu pamoja na namna inavyotatua madhaifu yanayobainika katika upangaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu wa ufanisi ulihusisha kipindi cha miaka 5 ambapo kwa ujumla kumeonekana uwepo wa maboresho makubwa katika taratibu za utoaji wa mikopo na ongezeko la idadi ya wanufaika wa mikopo husika. Hali kadhalika, marejesho na uendeshaji kidijitali wa mfumo ya utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kwa mfano kumwekuwa na ongezeko la wanufaika wa mikopo kutoka 116,706 (2016/2017) hadi 149,389 (2020/2021).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, ukaguzi wa ufanisi ulibaini masuala mahsusi ya muhimu ambayo ni kama ifuatavyo: -

- a) Mapitio ya Taasisi 17 yalibaini kuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imekuwa ikipeleka kwa wakati awamu ya kwanza ya fedha. Fedha zimekuwa zikitolewa kwa wastani wa wiki moja kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa masomo;
- b) Upangaji wa mikopo usiotosheleza kwa wanafunzi wapya ambapo Bodi haikuweza kutoa mikopo kwa 100% kwa waombaji waliostahili;
- c) Utoaji wa mikopo inayofikia **Sh. 1,768,247,000** kwa wanafunzi wasiostahili. Mikopo hiyo ilitolewa kati ya mwaka 2016 hadi 2018 kwa wanafunzi ambao hawakuwa kwenye vyuo vya

2 NOVEMBA, 2022

elimu ya juu lakini walipewa mikopo kwa maelekezo ya Serikali;

- d) Muunganiko hafifu wa mfumo wa maombi ya mkopo kwa njia ya mtandao hivyo kushindwa kufungamanisha masharti ya Kifungu cha 4.6 cha Muongozo wa Upangaji na Ugawaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;
- e) Waombaji kupangiwa ada chini ya kiwango na zaidi ya kiwango cha ada stahiki. Kwa mwaka 2018/2019 wanafunzi 6182 walipangiwa mikopo zaidi ya kiwango kwa kiasi cha **Sh.5,668,843,406** na wanafunzi 2,852 walipangiwa mikopo chini ya kiwango kwa upungufu wa **Sh.1,147,016,452**;
- f) Upangaji wa mikopo inayofikia **Sh. 2,255,336,448** kwa waombaji wasiokuwa na uhitaji;
- g) Kutowapangia mikopo wanafunzi wanaostahili kupata mikopo;
- h) Usimamizi hafifu wa bakaa na fedha za wanafunzi wanaohama vyuo; na
- i) Uhamasishaji duni wa vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya mpango wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mahojiano na Afisa Masuuli Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB pamoja na uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati ilibaini masuala muhimu ya ziada ambayo pia yanatakiwa kufanyiwa kazi ili kuongeza wigo wa udhibiti wa

2 NOVEMBA, 2022

matumizi ya fedha za umma katika HESLB. Masuala hayo ni kama ifuatavyo: -

- a) Ilibainika kwamba, utaratibu unaotumika kwa sasa katika utambuzi wa wahitaji wa mikopo unatumia vigezo kadirio (Proxy indicators) ambavyo haviakisi uhalisia wa hali ya familia wanazotoka waombaji;
- b) Mahitaji ya mikopo yamekuwa yakiongezeka na yanatarajiwa kuongezeka zaidi katika miaka michache ijayo kufuatia uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika miundombinu ya elimu msingi na sekondari pamoja na Sera ya elimu bila ada;
- c) Ilibainika pia kuwa mfumo wa sasa wa utambuzi, upangaji na utoaji wa mikopo ya elimu ya juu unaongozwa zaidi na uhitaji (Neediness) ili kuweka usawa (Equity) bila ya kuzingatia aina ya Shahada za wanufaika na kama zinashahabiana na mahitaji ya soko la ajira na uzalishaji;
- d) Kamati imethibitisha kuwa majukumu ya HESLB na ukwasi unaosimamiwa nao unaongezeka kila mwaka; na
- e) Uamuzi wa Serikali wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa stahada uliathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya bodi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa masuala yaliyofafanuliwa katika aya zilizotangulia hapo juu, Kamati imetoa mapendekezo ya kuboresha usimamizi na udhibiti wa fedha za umma katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu katika sehemu ya 3 ya taarifa hii.

2.11.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Matengenezo ya Barabara Unaofanywa na TANROADS

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara ni mojawapo ya sekta ya ujenzi inayosaidia ukuaji wa uchumi wa nchi. Aidha, ni miongoni mwa shughuli ambazo serikali inatumia kiasi kikubwa cha mapato yake. Kwa hali hiyo, Taifa linatakiwa kuwa na imani na uhakika kuhusu ubora na matumizi sahihi ya fedha zinazotumika katika kutekeleza shughuli za matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa rejea ya Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Mfuko wa Barabara ya Mwaka 2021 ilibainisha uwepo wa ongezeko la kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kwa kuzingatia urefu wa mtandao wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hiyo inabainisha kuwa fedha zilizokusanywa kutoka katika Tozo za Ushuru wa Barabara na Mafuta na kuidhinishwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizopo chini ya TANROADS na TARURA, ziliongezeka kutoka **Sh. Bilioni 839.1** kwa mwaka wa fedha 2019/20, hadi **Sh. Bilioni 916.8** mwaka 2020/21. Hivyo kuna ongezeko la **Sh. Bilioni 77.6** ambayo ni sawa na 8% ya makusanyo ya mwaka uliopita yatokanayo na ushuru wa barabara. Katika fedha hizi za tozo, 70% zilipelekwa TANROADS, na 30% zilipelekwa TARURA.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika mwaka wa fedha

2 NOVEMBA, 2022

2019/20, TANROADS ilipokea kiasi cha **Sh. Bilioni 299**, wakati katika mwaka 2020/21 **Sh. Bilioni 369** zilipelekwa katika Mikoa yote kwa ajili ya kazi zilizopangwa za matengenezo ya barabara. Hivyo basi ni muhimu kuhakikisha kuwa mfumo wa matengenezo ya barabara nchini unakuwa na ufanisi ili kupata thamani ya fedha iliyotengwa na iliyotumika katika shughuli za matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la ukaguzi huu wa ufanisi lilikuwa ni kutathmini kama Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) imesimamia ipasavyo matengenezo ya barabara ili ziweze kudumu kwa muda mrefu na katika kipindi kilichotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari ukaguzi huu wa ufanisi ulibaini masuala yafuatayo: -

- a) Uwepo wa barabara zenye ubovu nchini. Ukaguzi ulibaini kuwa barabara nyingi hasa zenye kiwango cha changarawe zina hali mbaya. Aidha ukaguzi ulibaini takribani 13% ya barabara zilikuwa mbovu;
- b) Kutokuwepo na ufanisi katika kuandaa mipango ya matengenezo ya barabara. Ukaguzi ulibaini kuwa TANROADS hawakuwa na mfumo wa usimamizi wa rasilimali za barabara (RAMS)¹⁰ hivyo kuathiri mipango ya matengenezo;
- c) Ukaguzi ulibaini kuwa, mapato ya fedha za barabara yalikuwa hayatoshelezi kugharamia matengenezo ya barabara nchini. Hii inathibitishwa na kupungua kwa uwezo

¹⁰ Roads Assets Management System.

2 NOVEMBA, 2022

wa kifedha katika kugharamia shughuli za matengenezo ya barabara. Timu ya Ukaguzi pia ilibaini kuwa, kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 mpaka 2019/20, fedha zilizotolewa kutoka Bodi ya Fedha za Barabara kwenda TANROADS zilikuwa kati ya 73% na 95% ya kiasi kilichoidhinishwa kwa mwaka;

d) Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa kukamilika kwa kazi za matengenezo ya Barabara ambapo mikataba 643 kati ya 1970 ya matengenezo sawa na 33% ya miradi ya matengenezo ya barabara haikukamilika kwa wakati; na

e) TANROADS haikuwa na uwezo wa kutosha wa kusimamia, kukagua, kufuatilia na kutathmini shughuli za matengenezo ya barabara. Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa TANROADS ilikuwa na upungufu wa 59% ya watumishi katika mwaka wa fedha 2020/21.

2.11.3 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Taratibu za Ukusanyaji wa Maduhuli Katika Sekta ya Madini

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi ya nchi. Mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka 5.2% mwaka 2019 hadi kufikia 6.7% mwaka 2020. Mchango huo unatarajia kuongezeka zaidi hadi kufikia 10% ifikapo mwaka 2025. Ili kufikia malengo haya, ni muhimu kuwepo na usimamizi madhubuti wa mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini nchini.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ukaguzi huu ulifanya tathmini iwapo Tume ya Madini imeweka hatua madhubuti ili kudhibiti usimamizi wa ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na shughuli za uchimbaji madini nchini ili kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia maendeleo endelevu ya matumizi ya rasilimali za madini. Ukaguzi huu ulihusisha miaka ya fedha 2018/2019 hadi 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi ni kama ifuatavyo: -

- a) Kutofanyika kwa kaguzi kutosha za madini. Ukaguzi ulibaini kuwa kiwango cha kaguzi zilizofanyika ni kidogo ukilinganisha na mipango iliyowekwa. Kwa ujumla, ilibainika kuwa, kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21 wastani wa 74% ya idadi ya kampuni za madini na wafanyabiashara wa madini hawakufanyiwa ukaguzi wa kifedha na uhakiki wa kodi na Tume ya Madini. Taarifa hizo za kaguzi ndizo hutumika kuhakiki kodi na tozo nyingine za Serikali;
- b) Ukaguzi ulibaini kuwa uchaguzi wa Kampuni za Madini kwa ajili ya kufanya uhakiki wa mapato ya kila mwaka ulitokana na uainishaji wa maeneo hatarishi kwa kampuni husika hasa kupitia gharama za utafutaji, gharama za mali kama mitambo, gharama za uendeshaji pamoja na mirabaha. Hata hivyo, Tume ya Madini ilifanya ukaguzi usiojitosheleza ili kufutulia uhalisia wa gharama hizo ambazo zinahitajika wakati wa kukokotoa malipo ya kodi;

2 NOVEMBA, 2022

- c) Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo unaotumika sasa wa Huduma za Leseni za Madini Kimtandao “FlexiCadastre¹¹” katika utoaji wa leseni za madini kwa mara ya mwisho ulihuishwa mnamo mwaka 2014, hivyo mfumo huo umepungua ufanisi wa utendaji kazi wake ukilinganisha na idadi kubwa ya maombi ya leseni za madini zinazopaswa kushughulikiwa na mfumo huo;
- d) Ukaguzi ulibaini kupitia uhakiki wa fomu za marejesho ya miamala kuwa, bei na thamani ya madini zilizowasilishwa katika fomu za marejesho hazikuwa za uhakika kutokana na sababu kwamba wafanyabiashara wengi hawakuwa tayari kutangaza kiwango halisi cha marejesho baada ya mauzo ili kupunguza kiasi cha mrabaha wanachotakiwa kulipa kwa mujibu wa sheria; na
- e) Uwepo wa mashine chache za X-Ray Fluorescence (XRF) ambazo hutumika kutambua kiwango halisi cha madini ya metali. Ni muhimu kufahamu kwamba, ukokotoaji wa mrabaha unaolipwa hutegemea tathmini ya kiwango na kiasi cha madini yanayozalishwa. Hivyo, ukaguzi usioridhisha wa kiwango na kiasi cha madini unaweza kusababisha kutokuwa na uhalisia wa mrabaha unaolipwa hivyo kupunguza ukusanyaji wa maduhuli kutoka sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi ni ya muhimu sana katika suala zima la usimamizi wa mapato ya Serikali. Kamati imeafikiana na mapendekezo na ushauri uliotolewa na CAG. Aidha, Kamati ilipokutana na Bodi na Menejimenti ya Tume ya

¹¹ Tovuti ya Huduma za Leseni kwa Njia ya Mtandao inayomilikiwa na Serikali ya Tanzania.

2 NOVEMBA, 2022

Madini ilipokea na kujadili mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi huu wa ufanisi. Hivyo Kamati inarejea mapendekezo husika katika sehemu ya 3 ya taarifa hii ili yawe sehemu ya maazimio ya Bunge lako Tukufu.

2.11.4 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Shughuli za Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya 4 ya ukaguzi wa ufanisi iliyopitiwa na kuchambuliwa na Kamati ilihusu shughuli za usajili wa biashara na utoaji wa leseni. Madhumuni ya ukaguzi huu wa ufanisi ilikuwa ni kutathmini kama Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni (BRELA) ilikua na ufanisi wakati wa kutoa huduma zake za msingi za usajili wa biashara na utoaji wa leseni (usajili wa makampuni, usajili wa jina la biashara, leseni za viwanda na biashara) na kama Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na BRELA inafanya ufuatiliaji kwenye utekelezaji wa shughuli za usajili na utoaji wa leseni.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari ukaguzi huu wa ufanisi ulikuwa na matokeo yafuatayo: -

- a) Ukaguzi huu ulibaini kuwa shughuli za usajili wa biashara na utoaji wa leseni hazikufanyika kwa mujibu wa kifungu namba 4 (2) b cha Sheria ya Uanzishaji wa Wakala (Sura 245 toleo la mwaka 2002);
- b) Ongezeko la gharama za mradi wa Mapitio ya bajeti ya mradi wa utoaji leseni kwa njia ya mtandao (ORS). Mapitio

2 NOVEMBA, 2022

ya bajeti ya mradi yalibainisha kuwa jumla ya **Sh. milioni 329** zilitumiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni kama gharama ya ziada kusaidia ufanisi wa uendeshaji wa mfumo wa usajili;

c) Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni mtandaoni uliunganishwa na mifumo ya nje miwili 2 kati ya 17 iliyotarajiwa kuunganishwa na taasisi nyingine za Serikali;na

d) Mapitio ya Ripoti ya Bodi ya Ushauri ya Wizara, 2019/20, yalibainisha kuwa maombi ya leseni ya biashara yalitakiwa kukamilika ndani ya siku 4 za kazi. Pamoja na matakwa hayo, ukaguzi ulibaini ucheleweshaji wa kutoa leseni kuanzia siku 5 hadi 800, jambo ambalo ni kinyume na viwango vilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Menejimenti ya BRELA ambapo waliwasilisha mpango kazi wa kushughulikia hoja za ukaguzi huu wa ufanisi. Kama ilivyo kwa kaguzi zilizotangulia za ufanisi, Kamati imetoa mapendekezo ya kuzingatiwa kutokana na ukaguzi huu.

2.12 Mapitio na Tathmini ya Hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mapitio na uchambuzi wa taarifa za fedha za mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko hiyo ni NSSF na PSSF. Masuala yaliyobainika katika hesabu za mifuko hususan katika matumizi ya fedha za umma ni kama ifuatavyo: -

2.12.1 Upungufu wa Ukwasi kwa Mfuko wa PSSSF Kulipa Mafao (Insufficient liquidity)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika hesabu za PSSSF kwa kipindi cha miaka 3 mfululizo (Ukiondoa mafao ya kabla ya mwaka 1999) umebaini kuwa kwa kipindi chote hicho mfuko umekuwa ukilipa mafao kwa kiasi kikubwa cha fedha ukilinganisha na kiasi cha michango iliyokusanywa. Hali hii inadhihirika kwa kuwa mafao yaliyolipwa yalizidi kwa kiasi cha **Sh. Bilioni 767**, **Sh. Bilioni 232** na **Sh. Bilioni 307** kwa miaka ya fedha 2020/21, 2019/20 na 2018/19 mtawalia. Uchambuzi wa malipo ya mafao yaliyofanyika kwa kiwango cha juu ukilinganisha na kiwango cha michango umefafanuliwa katika jedwali Na. 2.5 hapa chini: -

Jedwali Na. 2.5: Gharama za Malipo ya Pensheni Ukilinganisha na Michango.

Mh Ch anz o: Taa	Maelezo	2018/19	2019/20	2020/21
		Kiasi TZS (Billioni)	Kiasi TZS (Billioni)	Kiasi TZS (Billioni)
	Michango	1,679	1,322	1,420
	Mafao yaliolipwa	1,986	1,554	2,187
	Kiasi cha mafao kilichoziidi michango	(307)	(232)	(767)

rifa ya hesabu zilizokaguliwa za PSSSF kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kama rejea ya Jedwali Na. 2.5 hapo juu na kwa rejea ya taarifa ya ukaguzi, Kamati ilibaini pamoja na sababu nyinginezo, kushuka kwa uwezo wa mfuko kulipa mafao kunatokana na mzigo wa malipo ya pensheni kwa

2 NOVEMBA, 2022

wastaafu wa kabla ya mwaka 1999 ambao hawakuwa wanachangia kwenye mfuko. Hata hivyo, changamoto ya ongezeko la gharama za malipo ya pensheni ukilinganisha na makusanyo ya michango inaendelea kula hifadhi ya mtaji wa PSSF hali inayohatarisha uwezo wa mfuko huo kutekeleza majukumu yake kwa siku zijazo.

2.12.2 Mikopo ya Muda Mrefu Iliyotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Kiasi cha Sh. Trilioni 1.5

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa za hesabu za NSSF ulibaini uwepo wa madeni ya muda mrefu yaliyotolewa kwa taasisi mbalimbali za Serikali kwa kipindi cha kati ya mwa 1 – 5 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021. Jumla ya deni hilo ilikuwa kiasi cha Sh. Trilioni 1.17 ikijumuisha deni la msingi **(Sh. Bilioni 490.16)** na riba ya **(Sh. Bilioni 684.42)**. Deni hili linahusu taasisi 10 za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa PSSF, deni la muda mrefu hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 lilifikia **Sh. Bilioni 323.98**. Deni hili linahusu taasisi za Serikali na taasisi nyinginezo. Hata hivyo, deni hilo limepungua kidogo kutoka **Sh. Bilioni 856.63** (2019/20). Hii ilifuatia hatua ya Serikali kulipa deni lake kwa kiasi cha **Sh. Bilioni 324.86** katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa Serikali kulipa madeni ya mifuko ya Hifadhi ya jamii kina athiri uwezo wa mifuko kutekeleza majukumu yake ya msingi.

2 NOVEMBA, 2022

2.12.3 Mifuko ya NSSF na PSSSF Kushindwa Kuuza Nyumba na Viwanja

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Kamati ilijielekeza kulipitia kwa kina na eneo la viwanja na nyumba zinazomilikiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii. Katika eneo hili, ilibainika kuwa PSSSF na NSSF wameshindwa kuuza baadhi ya nyumba na viwanja vya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, NSSF ilikuwa na viwanja na nyumba vyenye thamani ya **Sh. Bilioni 137.46** (2019/2020:**Sh. Bilioni 232.25**), thamani ikiwa imeshuka kwa 41% ukilinganisha na mwaka uliotangulia. Aidha, katika mwaka huu tunapotoa taarifa, NSSF ilipata hasara ya kiasi cha **Sh. Bilioni 1.80** kutokana na mauzo ya viwanja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa PSSSF, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, PSSSF iliuzua mali kwa maana ya viwanja na nyumba vyenye thamani ya **Sh. Bilioni 5.80** ikiwa imeshuka thamani kwa 51% ukilinganisha na kiasi cha **Sh. Bilioni 11.84** zilizouzwa kwa mwaka 2019/20. Mali hizi zote ziliuzwa bila ya mfuko kupata faida. Hii kwa kiasi kikubwa imechangiwa na kutokuwa na mikakati madhubuti ya masoko na mauzo.

2.12.4 Kutofikiwa kwa Malengo ya Uwekezaji Katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini pia changamoto nyingine katika mifuko ya hifadhi ya jamii. Changamoto hii inahusu marejesho ya mapato

2 NOVEMBA, 2022

yanayotokana na shughuli za uwekezaji (Net return on investment)¹².

Mheshimiwa Spika, mapitio na uchambuzi wa taarifa za NSSF pamoja na shughuli za uwekezaji ulibaini uwepo wa kiwango kidogo cha faida inayotokana na uwekezaji kwenye majengo na faida hiyo imeendelea kushuka kwa miaka mitano iliyopita kutoka 1.2% mwaka 2017 hadi 0.4% mwaka 2021. Katika hatua hiyo, Kamati ilibaini kwamba, ongezeko la kasi ya uwekezaji katika majengo hauendani kabisa na mapato yanayotokana na uwekezaji huo. Mchanganuo wa namna uwekezaji unavyorejesha mapato katika NSSF umefafanuliwa katika Jedwali Na. 2.6 hapa chini.

Jedwali Na. 2.6: Mchanganuo wa Marejesho ya Faida Kutona na Uwekezaji.

Maelezo	2021	2020	2019	2018	2017
Thamani ya mapato kutokana na uwekezaji TZS "Millioni"	2,151	2,841	2,062	4,588	5,556
Thamani ya uwekezaji TZS "Millioni"	604,665	519,373	418,189	461,645	464,639
Rate of return %	0.4	0.5	0.5	1.0	1.2

Chanzo: Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za NSSF kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kutofikiwa kwa malengo ya uwekezaji kulibainika pia katika mfuko wa PSSF. PSSF waliwekeza jumla ya **Sh. Bilioni 10.19** katika mradi wa ujenzi wa stendi ya

¹² Return on investment reflects percentage of net income (income minus expenses) from investments made. The ratio is a performance measure used to evaluate the efficiency or profitability of an investment.

2 NOVEMBA, 2022

kisasa Msamvu Mkoani Morogoro. Hata hivyo, ilipofika tarehe 01 Machi, 2020, Serikali iliamisha umiliki wa mradi wa stendi Msamvu kwenda kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa bado PSSF haijafidiwa na Serikali gharama ilizotumia kuendeleza mradi huo. Ni muhimu ikafahamika kuwa fedha hizo ni sehemu ya michango ya wanachama na hivyo kutorejeshwa PSSF kunapunguza uwezo wa mfuko kutimiza majukumu yake ipasavyo na malengo ya uwekezaji kutofikiwa.

2.13 Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika taarifa za ukaguzi za mafungu mbalimbali ulibaini ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na kama ilivyorekebisha Mwaka 2016 pamoja na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorekebisha Mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo yalikiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma ni kama ifautavyo: -

- a) Ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi kwa zaidi ya miaka 4 kulikofanywa na TANESCO – Iringa, hali iliyosababisha ongezeko la gharama za mradi kwa **Sh. Bilioni 2.9**. Hoja hii ilijitokeza katika mradi wa urekebishaji wa mashine za

2 NOVEMBA, 2022

kuzalisha umeme (Turbines) katika Eneo la G3 kihansi HPP¹³. Ucheleweshaji huu ulikuwa ni kinyume na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013¹⁴;

b) Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi ilifanya manunuzi ya magari yenye thamani ya **Sh. 2,696,299,773.28** bila ya ushindani wa bei kinyume na Kifungu 160 cha Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 kama zilivyorejewa Mwaka 2016. Aidha, katika manunuzi hayo malipo zaidi ya kiwango kilichodhinishwa na bodi ya zabuni ya kiasi cha **Sh. 386,088,900.99** yalifanyika. Mwisho, CAG amebainisha kuwa malipo ya magari husika yalifanyika kabla ya magari kupokelewa;

2.14 Mapungufu Katika Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

Mheshimiwa Spika, mifumo ya udhibiti wa ndani ni nyenzo na nguzo muhimu katika kuhakikisha kunakuwepo na udhibiti na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kunapotokea changamoto zozote au dosari katika mifumo ya udhibiti wa ndani, kunasababisha mianya ya upotevu wa mapato au matumizi mabaya ya fedha za umma. Kamati imepitia taarifa ya CAG na kubainisha baadhi ya taasisi ambazo zinakabiliwa na mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani. Taasisi hizo na mapungufu yaliobainika ni kama ifuatavyo: -

¹³ Hydro Power Plant.

¹⁴ Rejea Kanuni 19(13) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (2013) zinazotoa mwongozo kuhusu muda wa tathmini za zabuni.

2.14.1 Changamoto za Mifumo Katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, TPA ilipata hati yenye mashaka (Qualified opinion). Sababu za msingi za kutolewa kwa hati hiyo, nyingi zinatokana na mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani. Mapungufu hayo ni kama ifuatavyo: -

- i. TPA inatumia mfumo wa COBOL kama chanzo muhimu cha kutunza taarifa za miamala ya shughuli za Bandari kabla ya kurekodiwa kwenye leja. Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa mfumo huo haujaunganishwa na mifumo mingine ya malipo iliyopo bandarini. Aidha, mfumo huo haupo wazi kwa watumiaji wote wakuu ikiwa ni pamoja hoja kuwa kila bandari inatumia mfumo wake tofauti. Kwa msingi huo, CAG hakuweza kujiridhisha na usahihi wa taarifa za fedha zilizopo kwenye vitabu vya TPA;
- ii. Kutokana na mapungufu ya mifumo ya udhibiti wa ndani madeni ya kiasi cha **Sh. Bilioni 107.72** ambayo yalikuwa yamebainishwa katika taarifa za fedha yalikuwa na dosari. Ilibainika kuwa kati ya **Sh. Bilioni 61.6** ambazo wakaguzi walihakiki ni kiasi cha **Sh. Bilioni 33.4** kilikubaliwa na kuacha salio la **Sh. Bilioni 21. 1**. Kwa msingi huo CAG hakuwa na uhakika wa usahihi wa madeni ambayo TPA inadai;
- iii. Matumizi ya mfumo wa (Terminal Operating Systems) wenye moduli 3 tofauti ambazo ni Harbor View Plus, Cargo Management na billing modules. ^[L]_{SEP} Mifumo hii haisomani hivyo kuwepo na tofauti za kiasi cha mapato na madeni yanayotolewa taarifa; na

- iv. Usahihi wa mapato ya kiasi cha **Sh. Bilioni 186** yaliyokusanywa na TRA kwa niaba ya TPA kama gharama za “wharfage”. Usahihi wa mapato haya haukupatikana kwa sababu ya kutofanyika usuluhishi kati ya taarifa za TRA, TPA na Hazina.

Mheshimiwa Spika, Mapungufu yote yaliyobainishwa hapo juu yanahusiana moja kwa moja na mapato ya Serikali. Hivyo, ni dhahiri kuwa kutoimarishwa kwa mifumo ya udhibiti wa ndani kutasababisha upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali katika TPA.

**2.14.2 Mapungufu Katika Mfumo wa ICT Fungu - 46
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wenye Thamani
ya Sh. Milioni 429,470,000**

Mheshimiwa Spika, katika mapungufu ya mifumo ya udhibiti wa ndani, Kamati ilibaini masuala yafuatayo katika Fungu 46 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hususan katika masuala ya mifumo ya ICT;

- a) Wizara ilitumia kiasi cha **Sh. Milioni 429,470,000** kununua na kusimika mfumo wa ICT. Hata hivyo, ukaguzi ukabaini kuwa hapakuwa na mpango wa namna bora mradi huo utakavyotekelezwa na kukamilishwa;
- b) Katika mfumo huo wenye moduli 8, hadi ukaguzi unakamilika ni moduli 1 pekee ndiyo ilikuwa inafanya kazi kwa ukamilifu;

2 NOVEMBA, 2022

- c) Mfumo husika ulikuwa haujasajiliwa katika kanzi data “portal” ya Serikali (GISP) kinyume na Kifungu 24(2) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019; na
- d) Hapakuwa na muongozo wa utumiaji wa mfumo ili kuhakikisha ufanisi katika matumizi ya mfumo husika.

2.14.3 Mauzo ya Matrekta Yenye Thamani ya Kiasi cha Sh.981,400,000 Yaliofanywa na SUMA – JKT Bila ya Kuwa na Mikataba

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Shirika la SUMA JKT, Kamati ilibaini kuwa katika mradi wa mauzo ya vifaa vya kilimo, SUMA JKT waliuza kwa mkopo vifaa vyenye thamani ya **Sh. 981,400,000** bila ya kuwa na mikataba na wakopaji (Contract agreement).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapungufu hayo, CAG alibaini kutokuwepo kwa sera ya kusimamia ukusanyaji wa madeni (Project credit policy). Kutokana na dosari hizo 2, urejeshaji wa mikopo inayotokana na mauzo ya matrekta na vipuli vyake umekuwa sio wa kuridhisha. Hivyo ni dhahiri fedha za umma zilizotumika katika mradi wa matrekta hazikutumika ipasavyo.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa hesabu za serikali kuu, mashirika ya umma na kaguzi za ufanisi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

3.2 Maoni

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati yanazingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni ya ujumla yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni ya jumla kuwa bado kuna changamoto kwa TRA kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kama ambavyo Bunge linakuwa limeidhinisha. Kutokana na suala hilo, Kamati inasisitiza umuhimu wa Serikali na TRA kwa pamoja kutekeleza mapendekezo na ushauri katika hoja za ukaguzi zinazokuwa zimeibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na maazimio yanayotolewa na Bunge katika kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ili kuipa Serikali uwezo wa kutekeleza mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ina maoni kwamba baadhi ya taasisi za umma zimekuwa zkikiuka sheria katika, ununuzi, usimamizi na utekelezaji wa mikataba. Masuala haya yanaiingiza Serikali katika hasara na upotevu wa fedha za umma. Pamoja na hilo bado kuna baadhi ya

2 NOVEMBA, 2022

watumishi wa umma hawazingatii ipasavyo sheria na taratibu zinazosimamia matumizi ya fedha za umma katika taasisi zao. Kamati ina maoni kwamba, michakato ya kisheria inachukuwa muda mrefu kukamilika kwa wahusika wakati rasilimali za umma zinakuwa zimetumika vibaya. Hili ni eneo ambalo Serikali inatakiwa kulifanyia kazi ili kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

3.3 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika, matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika. Mapendekezo ya Kamati yanasomwa sambamba katika Randama ya 1 iliyoambatishwa na taarifa hii.

3.3.1 Kuhusu Nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kiasi cha Sh. 2,811,461,204,503

KWA KUWA, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imebainisha nakisi ya kiasi cha **Sh. 2,811,461,204,503** cha mapato ambayo hayakukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na mapungufu mbalimbali;

NA KWA KUWA, kutokusanywa kwa mapato hayo kunasababisha upotevu wa mapato ya Serikali na pia

2 NOVEMBA, 2022

kunapunguza uwezo wa Serikali kuwa na rasilimali za kutosha kutimiza majukumu yake;

KWA HIYO BASI, ili kuongeza ufanisi wa makusanyo ya kodi kupitia TRA, Bunge linaazimia kwamba: -

- a) TRA ikamilishe maboresho ya mfumo wa "ITAX" ili kuhakikisha mapungufu yaliyobainishwa na ukaguzi yanafanyiwa kazi na kutunza kumbukumbu sahihi;
- b) TRA iboreshe Kitengo chake cha kiufundi (Technical unit) ili kushughulikia mapingamizi ya kodi kwa wakati unaokubalika kisheria na weledi;
- c) TRA iboreshe hali ya utendaji katika mapitio na makadirio ya kodi ili kuondoa dosari za ukadiriaji wa kodi juu au chini ya kiwango;
- d) TRA iongeze jitihada na kasi ya ukusanyaji wa madeni ya kodi ili kupunguza limbikizo la madeni ya kodi;
- e) TRA iboreshe usimamizi wa mizigo ambayo inapitia hapa nchini kwenda nje ya nchi kwa kuhakikisha ushuru wa forodha unalipwa kwa mujibu wa sheria. Endapo kunabainika ukiukwaji wa sheria, hatua stahiki za kikodi zichukuliwe kwa wakati; na
- f) TRA isimamie ipasavyo ukusanyaji wa ushuru katika bidhaa za mafuta yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi kupitia hapa nchini. Hili lifanyike sambamba na usimamizi madhubuti wa maghala (Warehouses) ili kuepusha upotevu wa mapato ya Serikali.

2 NOVEMBA, 2022

3.3.2Kuhusu Dosari Katika Usimamizi wa Mikataba na Athari Zake katika Matumizi ya Fedha za Umma

KWA KUWA, Kamati imebainisha mapungufu katika uiangiaji na usimamizi wa mikataba kwa taasisi mbalimbali za Serikali;

NA KWA KUWA, mapungufu hayo yamesababisha hasara kwa Serikali na hivyo kupelekea upotevu wa fedha za Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a)Wakala Barabara Tanzania (TANROADS)

- i. TANROADS ihakikishe inaingia mikataba pale tu inapokuwa na uhakika wa fedha za kugharamia mikataba hiyo; na
- ii. Utaratibu wa malipo ya serikali ufanyike kwa ufanisi ili kupunguza ucheleweshaji wa malipo usiokuwa na sababu za msingi ambao unachangia kuvunjwa masharti ya mikataba.

b)Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

- i. TANESCO iboreshe eneo la usimamizi wa mikataba kwa kuhakikisha inapata ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutovunja mikataba bila kufanya upembuzi yakinifu wa matokeo ya hatua kama hiyo;
- ii. Kwa suala mahsusi la malipo yanayofanywa na Serikali kwenda Symbion, Serikali itoe muongozo wa namna TANESCO itakavyotambua malipo hayo katika vitabu vyake

2 NOVEMBA, 2022

vya hesabu kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa ya uandaaji wa hesabu (IFRS); na

- iii. Serikali iimarisha usimamizi katika suala zima la ununuzi na utekelezaji wa mikataba mikubwa kwa kuhakikisha upembuzi yakinifu unafanyika kabla ya ununuzi na wakati wa usimamizi wa mikataba husika. Aidha, inashauriwa Serikali iangalie na kufanya tathmini ya kina kabla ya kutoa dhamana kwa taasisi za umma pale zinapoingia mikataba kwani uzoefu umebainisha kuwa eneo hili linasababisha hasara kubwa kwa Serikali panapotokea kuvunjwa kwa masharti ya kwenye mikataba husika.

c) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA)

TPA ikamilishe majadiliano na mkandarasi wa ujenzi wa gati la kuegeshea meli Mtwara kwa kuchukua na kutekeleza hatua stahiki kwa mujibu wa masharti ya mkataba na kwa manufaa mapana ya Taifa.

3.3.3 Kuhusu Hali ya Ukwasi Katika Baadhi ya Taasisi za Kimkakati za Serikali (TPDC, TANESCO na STAMICO)

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha changamoto za mtaji katika mashirika ya umma ya kimkakati kama TPDC, TANESCO na STAMICO;

NA KWA KUWA, ukosefu wa mtaji wa kutosha unapunguza uwezo wa mashirika hayo kutimiza majukumu yake ipasavyo. Aidha, mashirika husika yanatumia fedha nyingi

2 NOVEMBA, 2022

za umma kulipia mikopo na riba katika uendeshaji wa majukumu yake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

- a) Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR) iangalie namna bora ya kusaidia mashirika hayo kwa kuongeza mtaji wa ziada kwenye uwekezaji mpya (Inject additional capital) ili kuzalisha mapato ya kutosha na kulipa madeni yao;
- b) Mashirika husika yafanye mapitio ya muundo wa mitaji yao (Capital structures) ili kusimamia ipasavyo malipo ya mikopo na kuepuka ongezeko la riba linalotokana na ucheleweshaji wa malipo ya mikopo husika;
- c) Mashirika husika yafuatilie kwa karibu mtiririko wa fedha (Cash flow) kwa kuongeza uzalishaji wa mapato kwa vyanzo vilivyopo; na
- d) Kufanyike majadiliano na wakopeshaji ili kupata masharti nafuu ambayo yataendana na hali halisi ya mtiririko wa fedha ili kuepuka riba na tozo za mikopo iliyoiva.

3.3.4 Kuhusu Kaguzi Maalumu

KWA KUWA, Taarifa za Mdhimiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umebainisha mambo muhimu katika kaguzi maalumu 4 zilizopitiwa na kuchambuliwa na Kamati;

NA KWA KUWA, kaguzi hizo zimebainisha potevu wa fedha za umma takribani **Sh. Milioni 329** na kutofikiwa kwa malengo ya mradi wa REA awamu ya Pili Mkoa wa Mara;

2 NOVEMBA, 2022

upotevu wa mapato ya Serikali yanayotokana na malipo ya visa stika za kughushi; upotevu wa fedha za umma katika chuo cha Hombolo; na kutofikiwa kikamilifu kwa malengo ya mradi wa Orio;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

- a) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa mkandarasi kampuni ya DERM Electrics (T) Limited kutokana na hasara iliyojitokeza. Aidha, hatua stahiki za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa watumishi wa REA waliohusika kusimamia mradi huo kwa kutotimiza majukumu yao ipasavyo;
- b) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi 32 wa Idara ya Uhamiaji waliotajwa kuhusika katika suala hili kwa kuzingatia uhusika wa kila 1 na matokeo ya ukaguzi maalumu;
- c) Serikali ikamilishe hatua za kisheria kwa watumishi 2 waliobainika kujihusisha na ubadhirifu wa fedha za ada za wanafunzi katika chuo cha Hombolo; na
- d) Serikali ifanye mapitio ya kina katika masharti ya mkataba wa Orio ili kuondoa changamoto zilizomo katika masharti ya mkataba huo. Aidha, mkataba huo utoe somo la namna bora ya kubuni na kutekeleza miradi mikubwa ya afya kwa siku zijazo.

3.3.5 Kuhusu Kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma Sura, 348

2 NOVEMBA, 2022

KWA KUWA, kupitia Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati imebaini ukiukwaji wa Sheria ya Fedha za Umma Sura 348;

NA KWA KUWA, ukiukwaji wa Sheria husika unapelekea upotevu wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia yafuatayo: -

a) Shirika la Masoko Kariakoo

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, afanye ukaguzi wa kiuchunguzi (Forensic audit) wa Shirika la Masoko Kariakoo ili kubaini iwapo kuna ubadhirifu wa fedha za umma uliofanyika na kufichwa baada ya soko hilo kuungua moto.

b) Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aombwe kufanya ukaguzi maalumu (Special audit) wa malipo ya fidia kiasi cha **Sh. 1,070,637,576** na malipo ya fedha za usumbufu kiasi cha **Sh. 434,129,600** yaliyofanyika DART ili kubaini iwapo yalifanyika kwa mujibu wa Sheria; na

c) Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi – Fungu 28

- i. Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iandae Kanuni zitakazosimamia uendeshaji wa Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na kubainisha vyanzo vya mapato, mamlaka ya usimamizi, muundo wa mfuko, watumishi wa mfuko na utunzaji wa kumbukumbu za fedha na mali zake; na

2 NOVEMBA, 2022

- ii. CAG akague matumizi yote ya mfuko huo tangu ulipoanzishwa na na kisha kutoa taarifa yake kwa Bunge.

3.3.6 Kuhusu Umiliki na Uendeshaji wa Kampuni ya Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO)

KWA KUWA, mkataba wa uendeshaji kati ya Serikali na Kampuni binafsi ndani ya KADCO (Concession agreement) ulikosa misingi ya kisheria tangu mwaka 2010 wakati ambapo Serikali ilinunua hisa 100% za KADCO baada ya malipo ya fedha za umma **Dola za Marekani Milioni 5.3**;

NA KWA KUWA, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amehoji kuhusu kukamilika kwa mkataba huo wa uendeshaji ambapo hadi sasa Serikali haijandaa mpango mkakati wa kibiashara wa uendeshaji wa KADCO;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

- a) Serikali ifanye tathmini ili kuhamishia shughuli za uendeshaji wa KADCO kwenda kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kama ambavyo inafanyika kwa viwanja vingine vya ndege hapa nchini kwa kuzingatia majukumu ya kisheria ya TAA na uamuzi wa Serikali uliotolewa hapo awali; na
- b) Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaombwa kufanya ukaguzi wa kina (Comprehensive audit) wa mapato na matumizi ya KADCO kuanzia mwaka 2010 baada ya kuanza kumilikiwa kwa 100% na Serikali.

2 NOVEMBA, 2022

3.3.7 Kuhusu Utendaji wa Kifedha wa Benki za Serikali (TCB na TIB)

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha kutokuwepo kwa mtaji wa kutosha kwa benki za Serikali za TIB na TCB;

NA KWA KUWA, kutokuwepo kwa mtaji unaotosheleza kunasababisha benki husika kushindwa kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Aidha, ongezeko la mikopo chechefu lina athari katika fedha za umma zilizowekezwa kwenye benki hizo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

- a) TCB na TIB ziandae na kutekeleza mikakati yenye tija ya kuzuia ongezeko la mikopo chechefu na kufikia lengo la kuwa chini ya 5% kama inayoelekezwa na miongozo ya BOT;
- b) Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza mtaji wa ziada (Additional capital) kwa benki ambazo tathmini itabainisha kuwa zina umuhimu wa kuendelea kuwepo ili zitekeleze majukumu yake kwa mujibu wa sheria hasa takwa la kuwa na mtaji unaotakiwa kisheria (Favorable adequacy ratios); na
- c) Kufanyike upembuzi wa kina ili kuangalia uwezekano wa kuongeza mitaji ya benki hizo kupitia soko la hisa na mitaji ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kutoa fedha za uwekezaji.

3.3.8 Kuhusu Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi

2 NOVEMBA, 2022

KWA KUWA, Taarifa 4 za ukaguzi wa ufanisi zimebainisha masuala kadhaa katika taasisi za Serikali;

NA KWA KUWA, hoja za ukaguzi wa ufanisi zinahusu matumizi ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

a) Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi Wa Elimu ya Juu

- i. Serikali ifanye maboresho ya kisera na kisheria kwa kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mfuko wa Mikopo ya Wanafunzi (Students' Loans Fund) ambao utakuwa na vyanzo endelevu vya mapato ili kukidhi ongezeko la waombaji wa mikopo linalotokana na sera ya Serikali ya elimu ya sekondari bila ada;
- ii. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iisimamie Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB kufanya mapitio makubwa ya kitaasisi (Institutional review) yatakayoshauri aina ya maboresho ya kimuundo, kiutendaji na ughamiraji utakaokuwa muafaka na unaozingatia hali halisi (Socio – economic status) za familia na waombaji wa mikopo na uwezo wa kurejesha mikopo wanapohitimu; na
- iii. Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina ifanye tathmini kuhusu mfumo wa usimamizi ili kujiridhisha na namna bora ya usimamizi wa kimkakati wa Bodi ya Mikopo wa kisera unavyoweza kutekelezwa.

b) Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)

2 NOVEMBA, 2022

TANROADS kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha na Mipango itekeleze kikamilifu hoja zote za ukaguzi wa ufanisi ili kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha za umma.

c) Tume ya Madini

- i. Tume ya Madini ikamilishe utekelezaji wa mapendekezo 7 ya CAG ambayo yapo katika hatua za awali za utekelezaji na ukomo wa utekelezaji wake umeainishwa kuwa kati ya mwaka 2022 hadi 2024;na
- ii. Tume ya Madini iongeze juhudi na itoe kipaumbele kwa ajili ya kutekeleza shughuli zitakazolenga kuongeza ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini.

d) Wizara ya Viwanda na Biashara na BRELA

Wizara ya Viwanda na Biashara na BRELA watekeleze hoja zote za ukaguzi wa ufanisi ili kuongeza mapato ya Serikali.

3.3.9 Kuhusu Mapitio na Tathmini ya Hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

KWA KUWA, uchambuzi wa Taarifa ya CAG umebainisha kupungua kwa uwezo wa mfuko wa PSSSF kulipa mafao yake. Aidha kumekuwa na changamoto za kutofikiwa mapato ya uwekezaji ikiwa ni pamoja uwepo wa deni ambalo mifuko inadai kwa Serikali kiasi cha **Sh. Trilioni 1.5**;

NA KWA KUWA, changamoto zilizobainishwa hapo juu, pamoja na mambo mengine zinapunguza ukwasi wa

2 NOVEMBA, 2022

mfuko wa PSSSF hivyo kupungua uwezo wa mfuko kulipa mafao kwa wakati. Aidha, uwepo wa mikopo ya muda mrefu ambayo haijalipwa inapunguza uwezo wa mifuko kutimiza majukumu yake kwa ufanisi na kutofikiwa malengo ya uwekezaji kunaleta hasara kwa mifuko.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

a) PSSSF iandae mpango mkakati wa kuongeza makusanyo ya michango ili kuongeza ukwasi wa mfuko (Solvency). Aidha, PSSSF iendelee kujadiliana na Serikali namna bora ya kumaliza changamoto ya malipo ya pensheni kwa wastaafu wa kabla ya mwaka 1999 ambao walikuwa hawachangii kwenye mfuko;

b) Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na taasisi za serikali zinazodaiwa na mifuko ziandae mpango wa malipo ya mikopo husika (Loan payment schedule). Aidha, Bunge linashauri kwamba mifuko ya hifadhi ya jamii kuwa na mikakati madhubuti ya udhibiti kabla ya utoaji wa mikopo mipya na pia kuhakikisha mikopo iliyotolewa inakusanywa; na

c) Mifuko iboreshe mikakati ya masoko katika kuuza nyumba na viwanja ili kupata faida. Aidha, kwa majengo yasiokuwa na wapangaji, ni muhimu mifuko ikapitia upya gharama za kodi ya pango ili kuvutia wapangaji wapya na hivyo kuongeza mapato yatokanayo na uwekezaji.

2 NOVEMBA, 2022

3.3.10 Kuhusu Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake

KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa baadhi ya taasisi za umma zimekiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake;

NA KWA KUWA, ukiukwaji wa Sheria husika umesababisha matumizi mabaya ya fedha za umaa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -
Mamlaka ya Udhubiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ifanye ukaguzi wa kiuchunguzi katika manunuzi yenye dosari yaliyobainishwa na Kamati na kisha kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi.

3.3.11 Kuhusu Mapungufu Katika Mifumo ya Udhubiti wa Ndani

KWA KUWA, Taarifa za CAG katika mafungu mbalimbali zimebainisha mapungufu katika mifumo ya udhubiti wa ndani;

NA KWA KUWA, pamoja na mambo mengine mapungufu hayo yanaongeza gharama kwa Serikali na kuchangia katika matumizi mabaya ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI,

2 NOVEMBA, 2022

- a) TPA ikamilishe maboresho ya mifumo ya uendeshaji wa shughuli za bandari ili kusimamia na kudhibiti mapato ya Serikali;
- b) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iitumie na kuishirikisha Taasisi ya Serikali Mtandao (E – Government) kutekeleza mifumo ya ICT na kuepuka kuongeza gharama kwa Serikali; na
- c) SUMA – JKT ihakikishe inarekebisha dosari katika mikataba ya mauzo ya matrekta. Aidha, mikataba yote ya kibiashara inayoiingiwa na SUMA – JKT isiwe na masharti hasi ambayo yanasababisha hasara kwa Serikali.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini na kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwatambua Wajumbe

2 NOVEMBA, 2022

hao kama ifuatavyo: -

- 1) Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb– **Mwenyekiti**
- 2) Mhe. Japheti Ngailonga Hasunga, Mb – **M/ Mwenyekiti**
- 3) Mhe. Dr. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb
- 4) Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele, Mb
- 5) Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
- 6) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
- 7) Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
- 8) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
- 9) Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
- 10) Mhe. Deus Clement Sangu, Mb
- 11) Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb
- 12) Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
- 13) Mhe. Aysharose Ndogoli Matembe, Mb
- 14) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
- 15) Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
- 16) Mhe. Jakcline Kainja Andrea, Mb
- 17) Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
- 18) Mhe. Zubeida Khamis Shaibu, Mb
- 19) Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb
- 20) Mhe. Bakar Mohamed Bakar, Mb
- 21) Mhe. Geoffrey Idelphonc Mwambe, Mb
- 22) Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nanelwa Mwihambi, *ndc* kwa ushauri wake kwa Kamati. Natoa shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati kupitia kwa Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athuman Hussein, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto *ndc*, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Sostenes Maseke na Ndugu Amina Salum Namtema.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, mwisho japo sio kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere. Aidha naishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen), Msajili wa Hazina (TR), Kamishina wa Bajeti (CB) na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM) na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu shughuli za Kamati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
HESABU ZA SERIKALI (PAC)**

02 Novemba, 2022

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hii ni hoja yetu, naona wengine mmekaa, sasa sijui hamuungi mkono. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana Makamu Mwenyekiti. Hoja imeungwa mkono. Hoja za Kamati ni hoja za Bunge, siyo hoja za Serikali, na wao sasa hivi watakuwa wachangiaji kwenye hoja hii. Ahsante sana.

2 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hizi kamati zetu Wabunge wengi watataka kupata nafasi ya kuchangia, tutumie kanuni yetu tupate kamati moja iwasilishe, nyingine itamalizia jioni na tutaanza uchangiaji jioni. Kwa hiyo, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (*Local Authorities Accounts Committee*, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti anakuja kusoma kwa niaba ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, karibu usome maoni ya Kamati.

MHE. STANSLAUS S. MABULA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC): Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuwasilisha Bungeni kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC Mheshimiwa Halima James Mdee Ripoti ya CAG kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Agosti, 2021 Serikali iliwasilisha Bungeni taarifa mbalimbali za hesabu zilizokaguliwa na Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021. Miongoni mwa taarifa hizo ilikuwa ni taarifa ya CAG kuhusu mapato na matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini. Kwa niaba ya Bunge, taarifa hiyo hujadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea zaidi naomba kumpongeza Mheshimiwa Angela J. Kairuki, Mbunge kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri katika Ofisi ya Rais, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Tunamwahidi ushirikiano madhubuti katika kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa iliyowasilishwa Mezani kwako imegawanyika katika sehemu kuu tatu; sehemu ya kwanza inaeleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2022, mbinu zilizotumika katika utekelezaji wa shughuli hizo, wadau walioshirikishwa na nyaraka zilizotumika. Sehemu ya Pili inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya CAG ya 2020/2021 na mahojiano ya Maafisa Masuhuli, vikao na ziara; na sehemu ya tatu ni maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze zaidi katika sehemu ya pili ili niliarifu Bunge mambo yaliyobainika katika mapato na matumizi ya fedha za Umma nchini kisha nilishawishi Bunge lako Tukufu kuafiki maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Mwaka ya CAG na mahojiano ya Kamati na Maafisa Masuhuli katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 CAG alikagua Halmashauri zote 185 nchini zilizokuwepo wakati huo. Kati ya hizo, Halmashauri 178 sawa na 96.2% zilipata Hati zilizoridhisha za Ukaguzi, Halmashauri sita sawa na 3.2% zilizopata Hati zenye Mashaka nazo ni Halmashauri ya Kisarawe, Longido, Mlele, Musoma, Sengerema na Halmashauri iliyokuwa ya Jiji la Dar es

2 NOVEMBA, 2022

Salaam. Halmashauri moja sawa na 0.6 % iliyopata Hati Mbaya ni Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, kwa kifungu cha 10 cha sheria, ukaguzi wa Umma mwaka 2008 kinatamka bayana kwamba ukaguzi unaotekelezwa na CAG ni kwa niaba ya Bunge. Naomba kuliarifu Bunge ya kwamba LAAC imejiridhisha kuwa ukaguzi wa Hesabu wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 ulizingatia misingi ya Katiba, sheria za nchi na viwango vya Kimataifa na Kitaifa vya ukaguzi wa hesabu za Serikali katika kufikia hoja za ukaguzi zilizojadiliwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, pili, ni maeneo yenye changamoto katika mapato na matumizi. Yafuatayo ni maeneo yaliyobainika kutokana na uchambuzi wa taarifa ya mwaka wa fedha ya CAG na majibu ya Maafisa Masuhuli katika kuhusisha hesabu za mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 katika mapato na matumizi ya fedha za Umma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kila taasisi ya Serikali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini, kuna akaunti mahsuszi za benki zinazojulikana kama Akaunti za Amana. Akaunti hizi ni kwa ajili ya kuhifadhi fedha za kazi maalum ambazo ziko nje ya bajeti ya mwaka ya taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba katika Halmashauri mbalimbali nchini akaunti hizi hutumika kama vichaka vya ubadhirifu na kama maficho ya fedha ambazo baadaye hutumika kinyume na makusudi yaliyotarajiwa. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha ulioishia 2021

2 NOVEMBA, 2022

Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ilificha zaidi ya Shilingi milioni 94 ambazo badaye zilikuja kutumika nje ya matumizi yaliyokusudiwa. Huu ni mfano mmoja ambao ni vyema ukatumika kuionesha Serikali ya kwamba Kamati inajua kwamba kuna tatizo la aina hii na linapaswa kuchukuliwa hatua na kudhibitiwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pili, ruzuku ya miradi ya maendeleo hutolewa tofauti na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Katika kila mwaka wa fedha, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hutunga Sheria ya Fedha na Sheria ya Matumizi. Sheria hizi humsaidia CAG kufuatilia maeneo ya Serikali katika kila mwaka husika kwenye kukusanya na kutumia fedha za Umma kabla ya kuliarifu Bunge.

Mheshimiwa Spika, eneo la manunuzi na mikataba linapaswa kutazamwa kwa umakini mkubwa sana kwa sababu ndiko yanakoelekezwa matumizi makubwa ya fedha za Umma na kuna vitendo kadha wa kadha vya kibadhirifu ambavyo visipodhibitiwa Taifa litaendelea kupata hasara. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha ulioishia 2020/2021 yako mambo ambayo Kamati imeyabaini.

(a) Palifanyika ununuzi wa bidhaa mbalimbali zenye thamani ya jumla ya Shilingi bilioni 7.93 bila kuidhinishwa na bodi za zabuni za Halmashauri husika. *(Makofi)*

(b) Palifanyika ununuzi wenye thamani ya Shilingi bilioni 3.84 nje ya mpango wa mwaka wa Halmashauri zaidi ya 24 nchini.

2 NOVEMBA, 2022

(c) Palifanyika ununuzi wenye thamani ya jumla ya Shilingi bilioni 5.37 bila kuitisha nukuu za bei za ushindani katika Halmashauri mbalimbali nchini.

(d) Palifanyika ununuzi wenye thamani ya Shilingi bilioni 1.24 bila kutumia hati ya kuagiza vifaa (*LPO*) katika Halmashauri mbalimbali nchini. Udhaifu huu una madhara mengi katika uhai wa Halmashauri hasa kiuchumi.

(e) Palifanyika malipo ya ununuzi wa bidhaa na huduma yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.02 bila ya wazabuni kukaguliwa na Kamati za ukaguzi na mapokezi.

(f) Palifanyika ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.61 kwa wazabuni ambao hawakuwa na mkataba wa makubaliano na Wakala wa Ununuzi Serikalini (*GPSA*).

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine zilizobainishwa hapo juu katika eneo la manunuzi zilikuwa kwenye miradi ya maendeleo iliyokuwa ikitekelezwa kwa utaratibu wa *force account*. Maoni ya Kamati ni kwamba kuna mazingira ambayo utaratibu huu ulitumika kama kichaka cha matumizi mabaya ya fedha za Umma na mwanya wa uvunjifu wa sheria za nchi. Hivyo ni vyema Serikali ikajifunza namna ya utekelezaji na utaratibu huu kwa nidhamu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaomba Bunge lako lipokee mifano iliyotolewa hapo juu na kuitumia kama onyo kwa watendaji wa Serikali wajue kwamba Bunge hili lina macho, limeona ujanjaujanja unaotumika kufuja fedha za

2 NOVEMBA, 2022

Umma. Linawataka sasa watendaji wenye dhamana ya kukusanya na kutumia fedha za Umma wajirekebishe au wajiandae kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria za nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaomba Bunge lako lipokee mifano iliyotolewa hapo juu kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika uwekezaji wa mitaji ya Umma katika baadhi ya Halmashauri nchini. Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zinayo fursa ya kuwekeza mitaji yao kwa lengo la kutoa huduma na kujipatia manufaa ya kifedha. Hata hivyo, utaalumu unaotumika katika kuwekeza mitaji hii unatia shaka sana kwani:-

(a) Halmashauri nyingi hufanya uwekezaji wa mitaji yao kwa kuiga kinachofanyika kwenye Halmashauri nyingine bila ya kufanya upembuzi yakinifu wa mazingira yao ya kibiashara. Kwa mfano, kila Halmashauri inataka kuwekeza kwenye stendi kubwa ya mabasi au masoko makubwa ya kisasa bila kujali idadi ya watu, usanifu wa miundombinu kulingana na maeneo yao, ukubwa wa miamala ya biashara, mkao wa eneo la kimkakati kibiashara katika masuala ya biashara na mapato yatakayopatikana.

(b) Manunuzi katika utekelezaji wa miradi isiyo ya kiuchumi: Baadhi tu ya mifano ya uwekezaji usio na tija ni ule uliotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa ya Kinondoni na Temeke katika Benki ya wananchi ya Dar es Salaam (DCB)

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam zimewekeza hisa zipatazo 24,036,348 zenye thamani ya Shilingi bilioni 5.77 katika benki ya DCB. Changamoto ni kwamba Utendaji wa DCB hauridhishi kabisa, kwa muda mrefu sasa imekuwa ikipata hasara. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 hisa zake zilishuka thamani kwa Shilingi bilioni 1.20 na hakuna dalili za kuimarika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifuatilie kwa karibu mustakabali wa uwekezaji wa mitaji ya Umma katika benki hii. Mfano mwingine ni Uwekezaji katika Bodi ya Mikopo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Mamlaka 85 za Serikali za Mitaa ziliwekeza Shilingi bilioni 4.88 katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, tangu kuanzishwa kwake mpaka sasa hazijawahi kupata gawio au faida inayotokana na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu ni muhimu sana kitaifa kwa ajili ya kuyakwamua kiuchumi makundi maalum akina mama, vijana na watu wenye ulemavu mijini na vijijini. Kutokana na umuhimu wa mfuko huu ambao upo kwa mujibu wa sheria, kiasi cha 10% ya mapato ya ndani yasiyolindwa hutengwa kila mwaka na kila Halmashauri kwa ajili ya vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu kwa uwiano wa 4:4:2.

Mheshimiwa Spika, mfuko huu una fedha nyingi na za uhakika kutokana na ukweli kwamba ni lazima kila Halmashauri itenge fedha hizo kama takwa la kisheria. Kwa mfano, katika Hotuba ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Fedha iliripoti

2 NOVEMBA, 2022

Bungeni mwenendo wa mapato ya ndani ya Halmashauri zote nchini kwa mwaka 2020/2021 kuwa ilikuwa ni Shilingi bilioni 757 ambayo asilimia 10 yake ni Shilingi billioni 75.7. Huu ni mtaji mkubwa sana endapo utasimamiwa na kutumika vyema.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa za mfuko ni kwamba usimamizi na uendeshaji wa mfuko una udhaifu mkubwa kiasi kwamba tija iliyokusudiwa kitaifa inaweza isifikiwe katika ajira, uchumi wa nchi sambamba na ukubwa.

(a) Halmashauri mbalimbali nchini hazina akaunti mahususi ya benki kwa ajili ya fedha zinazotengwa na marejesho yanayokusanywa. Kutokana na udhaifu huo, kwanza hakuna taarifa mahususi ya hesabu za mfuko na pili ni vigumu kudhibiti uhalali wa vikundi vinavyokopeshwa na mwenendo wao wa marejesho.

(b) Baadhi ya Halmashauri hutoa mikopo bila kujiridhisha na uhalisia wa mikopo ya biashara au uhai wa vikundi vinavyokopeshwa.

(c) Baadhi ya Halmashauri hazina kabisa mipango mikakati ya kudai marejesho ya mikopo inayotolewa. Kwa msingi huu, ni vigumu sana kubaini tija na uendelevu wa mfuko huu kutokana na changamoto hii. Katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Halmashauri zaidi ya 155 hazijafanikiwa kurejesha kiasi cha fedha Shilingi bilioni 47.1 zilizotolewa kwa vikundi hivyo.

2 NOVEMBA, 2022

(d) Halmashauri nyingine hutoa mikopo kwa makundi yaliyo katika maeneo ya mjini tu na kunyima fursa makundi mengine yaliyo vijijini.

Mheshimiwa Spika, namba sita ni stahiki za watumishi kutolipwa ipasavyo. Rasilimali watu ndiyo msingi wa utendaji na mafanikio ya taasisi yoyote ile zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kuna uwekezaji ambao sharti ufanyike ili rasilimali hii iweze kuleta tija sasa au baadaye. Bahati mbaya kwamba katika baadhi ya halmashauri hali haikuwa hivyo. Kwa mfano:-

(a) Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, watumishi 33,405 katika halmashauri mbalimbali nchini hawakulipwa malimbikizo yao ya mishahara yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 63.83 yanayotokana na kupandishwa vyeo katika utumishi wa umma au kuteuliwa kushika nyadhifa za juu, malimbikizo hayo ni ya zaidi ya mwaka mmoja.

(b) Katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino watumishi 144 na wengine 16 wa Kada ya Ualimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba hawakulipwa jumla ya Shilingi Millioni 128.03 ambazo ni gharama za kusafirisha mizigo yao baada ya kufikia umri wa kustaafu na kuhitimisha utumishi wao kwa umma.

(c) Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga haikupeleka kiasi cha Sh.66,491,474 katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, wakati Wilaya ya Ngara haikupeleka kiasi cha Sh.49,229,555. Tabia hii huwaletea tabu sana watumishi wa

2 NOVEMBA, 2022

umma wanapokoma utumishi wao. Ikumbukwe pia kwamba suala hili lilipata kuibua majadiliano makali sana Bungeni tarehe 23 Septemba, 2022 kutokana na swali la Mheshimiwa Anastazia Wambura, alipoiuliza Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana

Mheshimiwa Spika, namba saba ni Hasara ya Kifedha ambayo halmashauri zinaipata kutokana na ushirikiano wake na taasisi zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo halmashauri zimekuwa zikifanyakazi na taasisi zingine za Serikali. Baadhi ya Taasisi hizi ni Wakala wa Manunuzi wa Serikali yaani (*GPISA*), Wakala wa Matengenezo ya Magari Serikalini (*TEMESA*), Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya na Bohari ya Dawa Tanzania (*MSD*). Katika uhusiano huo halmashauri zimekuwa zikipata hasara, kwa mfano:-

(a) Katika mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, *NHIF* haijazirejeshea Halmashauri Jumla ya shilingi bilioni 2.34 kutokana na huduma za tiba zilizotolewa katika katika halmashauri, katika hospitali mbalimbali nchini kwa wanufaika wa Mfuko huo *NHIF* imeshindwa kulipa fedha hizo kwa maelezo ya kwamba fomu za wagonjwa zimejazwa vibaya kiasi cha kutoaminika;

(b) *MSD* haikupeleka dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 katika halmashauri kutokana na sababu mbalimbali zilizo nje na utendaji wa halmashauri zenyewe;

2 NOVEMBA, 2022

(c) Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwenye halmashauri mbalimbali zidi ya (TEMESA) katika matengenezo na ukaguzi wa magari na mitambo; na

(e) (GPSA) imekuwa ikizitaka halmashauri mbalimbali kulipa fedha kabla ya kupata huduma au bidhaa husika ikiwemo uuzaji na uagizaji na ununuzi wa magari. Mara nyingine (GPSA) hurudisha fedha kwa wateja pasipo kukamilisha manunuzi ya magari hayo kwa wakati uliopangwa, hivyo kuzitia hasara halmashauri nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nane, ni utekelezaji wa madawa ya Binadamu kwenye uteketezaji wa madawa ya binadamu kwenye vituo vya Afya; Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka wa Fedha 2021 inaonyesha kuwepo kwa wimbi kubwa la uteketezaji wa madawa ya binadamu yenye thamani kubwa ya fedha. Hali hiyo ya uteketezaji wa madawa hayo imekuwa ikiongezeka katika kila halmashauri kila mwaka hata kama hakuna magonjwa ya mlipuko. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/2019, halmashauri 14 ziliteketeza madawa ya zaidi ya shilingi bilioni 7.3; mwaka 2019/2020, halmashauri 31 ziliteketeza madawa yenye thamani ya shilingi bilioni 1.5; na mwaka 2021, halmashauri 46 ziliteketeza madawa yenye thamani ya shilingi billioni 3.5.

Mheshimiwa Spika, tisa, udhaifu katika kukusanya mapato ya ndani ya halmashauri. Udhaifu uliopo ni kwamba, katika halmashauri mbalimbali ushuru wa huduma hukusanywa bila uthibitisho wa mapato halisi ya kampuni iliyolipa kwa mwaka. Halmashauri zingine hufanya malipo

2 NOVEMBA, 2022

bila kukata kodi ya zuiro, wakati zingine hufanya malipo bila kutumia risiti za (EFD).

Mheshimiwa Spika, kumi, upo upotevu wa Mapato ya Serikali kupitia kwenye mifumo hii ya kieletroniki, hali hii inaweza kuonekana kwa kuangalia marekebisho ya miamala yanayofanywa na maafisa wanaohusika katika mchakato wa ukusanyaji wa mapato hayo isipokuwa pasipokuwa na nyaraka za uthibitisho na uhalali wa marekebisho hayo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2021 halmashauri 27 zilizoonekana kwenye Jedwali Na.5 zilifanya marekebisho ya miamala yenye jumla ya shilingi bilioni 1.6 kwenye mfumo bila ya uthibitisho wa ulazima na uhalali wa marekebisho hayo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende sehemu ya tatu; Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Baada ya maelezo kuhusu matatizo mbalimbali yaliyopo katika mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, naomba kuwasilisha mapendekezo ya Kamati katika Bunge lako hili liyajadili na kuyaafiki kwa ajili ya utekelezaji Serikalini.

Mheshimiwa Spika, moja, kuhusu Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu Wenye ulemavu.

KWA KUWA lengo la Serikali kuwa na Mfumo wa Mikopo wa Vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu ni uwezeshaji kiuchumi na kupunguza makali ya ukosefu wa ajira nchini;

2 NOVEMBA, 2022

NA KWA KUWA Kamati imebaini yakwamba uendeshaji na uendelevu wa Mfuko huo kwa sasa hauko thabiti, kiasi cha kuleta ugumu katika kupata tija iliyokusudiwa;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba katika kila Halmashauri Nchini kuanzishwe:-

- (a) Akaunti Maalum kwa ajili ya fedha zitakazokuwa zinatolewa na kurejeshwa ili kuweka kumbukumbu za vikundi vilivyokopa, kiasi kilichokopwa, shughuli inayofanyika na mwenendo wa marejesho hayo; *(Makofi)*
- (b) Mpango Mahsusi wa utoaji wa elimu kwa wanufaika wa mikopo ili watambue uwepo wa fursa hiyo na wajiandae kunufaika nayo;
- (c) Utaratibu wa kujiridhisha na mipango ya biashara inayoenda kutekelezwa badala ya kutoa mikopo kwa kufuata orodha ya majina ya Wanakikundi; na
- (d) Dhana ya kuutumia Mfuko huu kwa ajili ya kuyakwamua makundi hayo maalum kiuchumi na kuongeza ajira nchini badala ya kutoa mikopo hiyo kiholela.

Mheshimiwa Spika, mbili, ni kuhusu Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa:-

2 NOVEMBA, 2022

KWA KUWA imebanika kwamba kiasi cha ruzuku hiyo katika baadhi ya halmashauri hutolewa kinyume na bajeti iliyoithinishwa kwa mujibu wa sheria;

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato na kudhibiti uvujaji wa njia za mifumo ya kieletroniki ili Taifa lipate fedha za kutosha kugharamia mipango ya maendeleo ya kila mwaka;
- (b) Kuzingatia matakwa ya sheria za matumizi zinapopitishwa na Bunge katika kila mwaka wa Bajeti ili kuendelea kulijengea imani Bunge na wananchi;
- (c) Kuwekwa angalau ukaribio wa kiasi fulani cha ruzuku endapo itabidi baadhi ya halmashauri kuzidishiwa kuliko vile zinavyotokea, kwamba halmashauri zingine hupewa kiasi kidogo mno wakati zingine hupewa zaidi ya asilimia hamsini; na
- (d) Kutorejesha Hazina fedha zinazokuwa zimepelekwa katika halmashauri kwa madai kuwa mwaka husika wa fedha umeisha.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu Uwekevu na Tija katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma:-

KWA KUWA halmashauri zilizo nyingi zimekumbwa na kasumba ya uwekezaji wa masoko na vituo vya mabasi

2 NOVEMBA, 2022

kama vile hakuna maeneo mengine yanayofaa kwa uwekezaji;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha uwekezaji unazingatia fursa za uwekevu na tija katika maeneo mbalimbali ya halmashauri kuliko hali ilivyo sasa ambapo kila halmashauri inataka soko au kituo cha mabasi.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu Manunuzi na Mikataba ya Upatikanaji wa Huduma na Bidhaa Mbalimbali. Bunge linaigiza Serikali kusimamia ipasavyo manunuzi yote ya umma kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na kuridhiwa na Bunge na Maafisa Masuuhuli wote watakaobainika kutosimamia ipasavyo agizo hili wachukuliwe hatua kali za kisheria kwa nia ya kukomesha ubadhirifu na kuliletea taifa manufaa stahiki.

Mheshimiwa Spika, tano, ni kuhusu Upatikanaji wa Stahiki za Watumishi kwa Mujibu wa Sheria:-

KWA KUWA baadhi ya Waajiri hawatekelezi matakwa ya sheria hizo mathalani katika kupeleka michango ya pensheni katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii hivyo kuwaletea Watumishi usumbufu na lawama kwa Serikali wanapostaafu;

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kutoa stahiki za watumishi kwa kuzingatia sheria zilizowekwa na kuchukua hatua kali kwa waajiri wasiozingatia matakwa ya sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, sita, kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri Nchini:-

2 NOVEMBA, 2022

KWA KUWA halmashauri zilizo nyingi zina udhaifu katika eneo hili kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uvujaji wa mapato kwenye mfumo wa kieletroniki, rushwa na kutosimamia ipasavyo sheria, kanuni na taratibu za kifedha;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato katika mifumo ya kieletroniki; na
- (b) Kuhakikisha kuwa Mfumo Mpya wa Ukusanyaji wa Mapato (TAUSI) unaanza kutumika katika Halmashauri zote nchini za Serikali ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023 badala ya hali ilivyo sasa ambapo bado kuna halmashauri zinazoendelea kutumia mfumo wa zamani yaani *local government revenue collection information system* unaoruhusu marekebisho ya miamala kwa namna yenye kutia shaka ya wizi.

Mheshimiwa Spika, saba, kuhusu Matumizi yasiyofaa ya Fedha katika Akaunti za Amana:-

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kuhakikisha fedha zinazo wekwa katika Akaunti za Amana zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kuliko hali ilivyo sasa ambapo akaunti hizo zinaonekana kutumika kama maficho ya fedha ambazo baadaye hutumika kibadhirifu.

Mheshimiwa Spika, nane, kuhusu Upotevu wa Mapato katika Mifumo ya Kieletroniki ya kukusanya mapato:-

2 NOVEMBA, 2022

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kudhibiti mianya ya mapato katika mifumo hiyo na kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watumishi wote watakaobainika kuhusika na upotevu mathalani watumishi walio katika halmashauri ambazo miamala ya mapato hubadilishwa au kufutwa bila uthibitisho wa ulazima wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, tisa, kuhusu Hasara ya kifedha kutokana na Vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri:-

HIVYO BASI Bunge linaishauri Serikali:-

- (a) Kushughulikia mara moja suala la *NHIF* kutorejeshwa gharama za matibabu na vifaa tiba vinavyotolewa na halmashauri kwa wanufaika wa bima ya afya chini ya Mfuko huo katika Mamlaka za Serikali za mitaa;
- (b) Kusimamia ipasavyo *MSD* ili iweze kupeleka dawa na vifaa tiba katika halmashauri kulingana na mahitaji ya halmashauri zenyewe; na
- (c) *GPSA* iwe inatekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zao zilizojiwekea kuzisaidia halmashauri katika utekelezaji wa mipango yao kuliko hali ilivyo sasa ambapo *GPSA* huchangia kuzizorotesha.

Mheshimiwa Spika, kumi, kuhusu Uteketezaji wa Dawa za Binadamu katika Hospitali na Vituo vya Afya:

2 NOVEMBA, 2022

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kutoa maelezo ya kuridhisha, ni kwa nini pamekuwa na kasi kubwa ya kutekeza dawa za binadamu kama vile dawa hizo zinanunuliwa bila mpango mahususi. Aidha, Serikali inapaswa kudhibiti jambo hili kwa baadhi ya dawa zinazoteketezwa siyo za magonjwa ya mlipuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shukurani; Kamati inakushukuru kwa uongozi wako thabiti uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Aidha, tunaipongeza sana Sekretarieti ya Bunge chini ya Katibu wa Bunge Bi Nenelewa Mwihambi. Sekretarieti imetusaidia katika utafiti, uratibu, upatikanaji wa taarifa na ushauri katika masuala mbalimbali ya Kamati. Tunawapongeza Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Bwana Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi katika Sehemu ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wetu wa Kamati Ndugu Dickson M. Bisile akisaidiana na Bi. Jesca Sanga na Ndugu Paul Chima.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi chini ya Ndugu CPA Charles Kichere, Mdhhibiti Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutekeleza wajibu wa wao ipasavyo. Pia tunazipongeza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kila wakati tulipohitaji ufafanuzi wa hoja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa uvumilivu, ushirikiano na uchapaji kazi wa kiwango na naomba majina yao yanukuliwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge

2 NOVEMBA, 2022

kama yalivyo katika Taarifa kuu iliyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika Taarifa hii yamejengwa katika misingi ya Hoja za Ukaguzi wa CAG na yanakusudia kuimarisha nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa ili kuwaletea wananchi maendeleo. Hivyo, ni vyema Serikali ikatambua kwamba Ukaguzi unaotekelezwa na CAG katika mapato na matumizi ya fedha za umma nchini ni kwa niaba ya Bunge na kwamba Hoja za Ukaguzi zinazotolewa na CAG ni hoja za Bunge. Hivyo, katika taarifa hesabu za miaka inayofuata, halmashauri ambayo haitajibu hoja za ukaguzi ipasavyo itahesabiwa na Kamati ya kwamba imekaidi kujibu hoja za Bunge na hatua kali za kinidhamu zitapendekezwa kwa mamlaka zinazohusika hapohapo wakati vikao vya Kamati vikiendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuyaafiki maoni na mapendekezo ya Kamati ya LAAC juu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa Mwaka wa Fedha uliyoishia tarehe 30 Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

2 NOVEMBA, 2022

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU
ZA SERIKALI ZAMITAA KUHUSU HESABU ZA SERIKALI ZA
MITAA ZILIZOKAGULIWA NA MDHIBITI NA MKAGUZI
MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA
2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

Madhumuni ya Taarifa hii ni kulishawishi Bunge liafiki ushauri wa Kamati wa kuitaka Serikali ichukue hatua kuhusiana na maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kama yalivyobainishwa katika Ripoti ya CAG na kuchambuliwa na Kamati. Aidha, Taarifa hii inakusudia kulijulisha Bunge kuhusu hali halisi ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyokusudia kuondoa matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi kilichopita.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu tatu na sehemuya nne inahusu shukurani na kutoa Hoja. Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya utangulizi yanayojumuisha maelezo ya jumla kuhusu Taarifa, Muundo wa Taarifa, misingi ya Kazi na njia au mbinu zilizotumiwa na Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili inabainisha maeneo yenye changamoto katika matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Sehemu hii ni msingi wa Maoni na Mapendekezo katika Sehemu ya Tatu. Mwisho, Taarifa inamalizia kwa shukurani na kutoa Hoja kwa Bunge lako tukufu ili Bunge liamue kuhusu Mapendekezo ya Kamati juu ya tatizo la matumizi mabaya ya fedha za umma.

1.3 Njia zilizotumika

Mheshimiwa Spika, Masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, yanazitaka Taarifa zote za Kamati zinazowasilishwa Bungeni ikiwemo Taarifa hii, zibainishe njia au mbinu iliyotumika kutekeleza majukumu yanayoripotiwa. Kwa ajili ya ukamilifu wa Taarifa hii, Kamati ilifanya yafuatayo: -

(a) Mapitio ya jumla ya Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Lengo lilikuwa ni kubaini maeneo yenye matatizo katika mapato na matumizi ya

2 NOVEMBA, 2022

fedha za umma katika Halmashauri kwa mwaka husika wa fedha.

(b) Mapitio ya Muhtasari wa CAG (Briefing) ambao unaonesha hali halisi iliyopo katika Halmashauri katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hoja za ukaguzi na ushauri wa Kamati hadi kufikia kipindi cha Halmashauri kuitwa mbele ya Kamati.

(c) Mahojiano na Maofisa Masuuli wa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu Hoja za Ukaguzi zilibainishwa katika Ripoti Kuu na Briefing ya CAG.

(d) Mashauriano na Wadau wengine kuhusu Hoja za Ukaguzi zilizojitokeza. Orodha ya Wadau hao ipo kwenye **Kiambatisho A**.

(e) Rejea ya Sheria na miongozo mingine inayohusika ili kujiridhisha na msingi wa matumizi na hoja za ukaguzi. Rejea mahsusi zilizotumika zimeorodheshwa katika **kiambatisho B** cha Taarifa hii.

1.4 Msingi wa kazi ya kusimamia matumizi ya fedha za umma kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zinatambulika kikatiba chini ya Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977). Mamlaka hizi huendesha shughuli zake kwa kutumia fedha za umma ambazo bajeti yake hupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kukaguguliwa na CAG kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi. Kwa msingi huo, ni

2 NOVEMBA, 2022

Wajibu wa Bunge lako kufuatilia nidhamu ya mapato na matumizi katika mamlaka hizo ilikuona ufanisi uliopo katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 08 Aprili, 2021 Serikali iliweka mezani Ripoti mbalimbali za CAG. Miongoni mwa Ripoti hizo ilikuwa ni Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa mujibu wa Kanuni ya 43 (1) & (8) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Ripoti hiyo hujadiliwa na kuwasilishwa Bungeni na LAAC.

1.5 Majumuisho ya Sehemu ya Kwanza

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, katika sehemu ya kwanza, Taarifa inajieleza kuwa inahusu uchambuzi wa Ripoti Kuu ya Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo limebainishwa kuwa ni kulijulisha Bunge maeneo ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Sehemu hii imeonesha msingi wa kazi ya uchambuzi huu na njia zilizotumika kufanikisha kazi hiyo. Sehemu ya Pili itatoa maelezo kuhusu Uchambuzi uliofanyika kwa manufaa ya Bunge ili liweze kuzingatia wakati wa kufanya uamuzi.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA RIPOTI KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

2.1 Malezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kusimamia matumizi ya umma inavyostahili, Kamati ilichambua Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Uchambuzi huu ulilenga kujiridhisha juu ya ufanisi wa mamlaka hizo katika kukusanya na kutumia fedha za umma kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, uwazi na uwajibikaji.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi


Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 CAG alikagua jumla ya Halmashauri zote 185 zilizokuwepo wakati huo. Kati ya hizo, Halmashauri 178 sawa na 96.2% zilipata Hati zinazoridhisha za Ukaguzi, Mamlaka 6 sawa na 3.2 % zilipata Hati zenye Mashaka (Halmashauri za Wilaya za Kisarawe, Longido, Mlele, Musoma, Sengerema na Halmashauri ya lililokuwa Jiji la Dar es Salaam), na Mamlaka 1 sawa na 0.6 % ilipata Hati Mbaya (Halmashauri ya Wilaya ya Bunda).

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa aina za hati za ukaguzi unaashiria kuimarika katika nidhamu ya mapato, matumizi na utaalum katika kuandaa taarifa za fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uimara huu ni kiashiria cha uthabiti wa taasisi za kusimamia uwajibikaji ikiwemo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa, Mabaraza ya Madiwani, Asasi za Kiraia,

2 NOVEMBA, 2022

Vyombo vya Habari na Wananchi kwa ujumla.

Chati Na. 1: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi kwa Mwaka 2020/21



Mheshimiwa Spika, Kwa ajili ya Taarifa hii, Kamati iliweza kuhoji jumla ya Mamlaka 40 za Serikali za Mitaa ambazo ni sawa na 21.6% ya Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa. Vigezo vya msingi vilivyotumika kuziita Mamlaka hizo mbele ya Kamati ni: uzito wa hoja za ukaguzi kifedha na athari zake katika halmashauri, udhaifu wa halmashauri katika kujibu hoja za ukaguzi na kutekeleza mapendekezo ya LAAC na aina ya hati ya ukaguzi ambayo halmashauri imetunukiwa na CAG.

Msingi wa Vigezo hivyo ni Masharti ya Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Vigezo vingine vya ziada ni muda ambao halmashauri imekaa bila kuhojiwa na Kamati pamoja na sauti za umma (public outcry) juu ya mwenendo wa Halmashauri husika. Sababu

2 NOVEMBA, 2022

ya vigezo hivyo inatokana na umuhimu wa jicho la Bunge katika halmashauri zote nchini pamoja na uzingatiaji wa sauti ya wananchi kuhusu rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, Katika Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021, Kamati ilibaini maeneo Kumi (10) yenye changamoto za matumizi mabaya ya fedha za umma. Kwa ujumla wake, maeneo hayo yanahusu mifumo ya udhibiti wa ndani, changamoto za ukusanyaji wa mapato, dosari za usimamizi wa matumizi, rasilimali watu, ununuzi na mikataba katika mamlaka ya serikali za mitaa. Kwa ufafanuzi Zaidi naomba kueleza maeneo hayo kama ifuatavyo;

2.2.1 Matumizi Yasiyofaa ya Akaunti za Amana

Mheshimiwa Spika, katika kila taasisi ya Serikali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa kuna akaunti mahsusi za benki zinazojulikana kama Akaunti za Amana (Deposit Account). Akaunti hizi ni kwa ajili ya kuhifadhi fedha za kazi maalum ambazo ziko nje ya bajeti ya mwaka ya taasisi husika. Ripoti ya CAG ilibainisha matumizi mabaya ya shilingi bilioni 9.74 kutoka katika akaunti za amana kutokana na kutosimamiwa ipasavyo. Matumizi hayo yalibainika katika halmashauri 81. Mfano wa halmashauri hizo ni Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ambayo ilificha zaidi ya shilingi milioni 94 ambazo badaye zilikuja kutumika nje ya matumizi yaliyokusudiwa.

2 NOVEMBA, 2022

2.2.2 Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo kutolewa tofauti na bajeti iliyoi

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 halmashauri 185 zilitengewa bajeti itokanayo na ruzuku ya miradi ya maendeleo ya jumla ya shilingi bilioni 928.05. Upatikanaji na matumizi ya fedha hizo unatokana na masharti ya Sheria ya Matumizi ya Serikali (Appropriation Act) na Sheria ya Fedha za Umma (Finance Act) zinazotungwa na Bunge katika kila mwaka wa fedha. Matumizi ya fedha tofauti na masharti ya sheria hizo kwa vyovyote vile ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Ripoti ya CAG yameonesha kuwa halmashauri 19 ziipokea ruzuku ya maendeleo zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa, halmashauri 163 zilipokea ruzuku ya maendeleo pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa na halmashauri 3 zilipokea kiasi halisi cha bajeti iliyoidhinishwa. Nia ya Serikali inaweza kuwa nzuri lakini ni nje ya utaratibu ulioridhiwa na Bunge katika sheria ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, endapo hali hii haitadhibitiwa kuna uwezekano wa Serikali kuwa na bajeti za aina mbili kwa mwaka. Yaani bajeti inayopitishwa Bungeni kupitia Sheria ya Matumizi ya Serikali na Bajeti isiyopitishwa Bungeni.

Jedwali Na. 1: Ruzuku ya Maendeleo iliyotolewa zaidi ya bajeti

Mwaka wa fedha	Makisio ya mapokezi ya ruzuku (Sh.)	Kiasi halisi kilichopokelewa (Sh.)	Kiasi Kilichopokelewa Zaidi (Sh.)	%	Idadi ya Halmashauri
-----------------------	--	---	--	----------	-----------------------------

2 NOVEMBA, 2022

2020/21	90,184,385,862	137,371,891,387	47,187,505,525	52	19
2019/20	67,272,409,002	87,319,960,255	20,047,551,253	30	29
2018/19	73,433,637,673	96,250,291,206	22,816,653,533	31	26
2017/18	84,214,721,967	106,275,933,616	22,061,211,649	26	23
2016/17	44,446,747,137	62,520,940,402	18,074,193,265	41	14

Chanzo: Ripoti ya CAG kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2020/2021

Jedwali Na. 2: Ruzuku ya maendeleo iliyotolewa pungufu ya bajeti

Mwaka wa fedha	Bajeti Iliyoidhiniswa (Sh.)	Kiasi Kilichotolewa (Sh.)	Kiasi kilichotolewa Pungufu (Sh.)	%	Idadi ya Halmash
2020/21	831,478,155,338	518,946,990,193	312,531,165,145	38	163
2019/20	890,315,258,723	479,897,731,898	410,417,526,825	46	150
2018/19	1,185,489,718,682	628,636,740,919	556,852,977,763	47	167
2017/18	977,228,000,000	497,282,000,000	479,946,000,000	49	165
2016/17	1,034,123,000,000	501,908,000,000	532,215,000,000	51	146

Chanzo: Ripoti ya CAG kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2020/2021

2.2.3 Udhaifu katika Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba

Mheshimiwa Spika, ununuzi na usimamizi wa mikataba ni eneo la matumizi ya kiasi kikubwa cha fedha za umma. Kwa msingi huo, Bunge lilitunga sheria ya kuweka masharti yanayosimamia ununuzi wa umma na mikataba mbalimbali. Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kinamtaka CAG kueleza iwapo matumizi ya fedha za umma katika ununuzi na ugharamiaji wa mikataba yamezingatia sheria, kanuni na taratibu za ununuzi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Bunge lako linaweza kutumia mifano michache ifuatayo iliyobainika katika mwaka wa fedha 2020/2021 kutathmini udhaifu uliopo katika manunuzi na mikataba katika Halmashauri mbalimbali nchini:

(a) Ununuzi wa bidhaa wa thamani ya shilingi bilioni 7.93 uliofanyika bila idhini ya bodi za zabuni kwenye halmashauri 42.

(b) Ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 3.84 ulifanyika bila kuzingatia mpango wa ununuzi katika halmashauri 24

(c) Ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 5.37 katika halmashauri 39 ulifanyika bila kuitisha nukuu za bei za ushindani

(d) Ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 1.24 bila kutumia hati ya kuagiza vifaa (LPO) ulifanyika katika halmashauri 14

(e) Malipo ya ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 2.02 kwa wazabuni wa bidhaa na huduma katika halmashauri 21 yalifanyika bila kuzingatia taarifa za Kamati za Mapokezi na Ukaguzi ukaguzi

(f) Ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 4.61 kwa wazabuni ambao hawakuwa na mkataba wa makubaliano na Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati

2 NOVEMBA, 2022

unaonesha kuwa dosari hizo hazikutokea kwa bahati mbaya na ni ishara ya mkakati maalum unaoratibiwa na baadhi ya watumishi wa umma wasiokuwa na uadilifu kwa lengo la kuwa na upendeleo, udanganyifu na ubadhilifu.

Hali hiyo inasababisha matumizi ya fedha za umma yasiyokuwa na tija ambayo ni tofauti na kusudio la Bunge kuidhinisha bajeti ya matumizi hayo. Athari yake ni kuathirika kwa huduma zinazotolewa na mamaka ya serikali za mitaa kwa wananchi au viwango duni vya niradi ya maendeleo vinavyohusika.

Baadhi ya sababu zinazochangia udhaifu huu ni pamoja Serikali kutokuchukua haraka hatua za kinidhamu dhidi ya Watumishi wanaobainika kuhusika katika ubadhirifu. Lakini pia Halmashauri nyingi kufanya manunuzi kidharura bila kuzingatia mipango ya manunuzi kwa mwaka.

2.2.4 Udhaifu katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na katika Miradi ya Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zinayo fursa ya kuwekeza mitaji yao kwa lengo la kutoa huduma na kujipatia manufaa ya kifedha. Kwa mfano; Halmashauri ya Jiji la Dodoma imewekeza katika miradi mbalimbali kama vile Hoteli ya Kisasa ya Nyota Tano katika Mji wa Serikali wa Mtumba, Soko la Machinga, Maeneo ya Michezo na Burudani Chinangali (Chinangali Park), Stendi Kuu ya Mabasi katika eneo la Nanenane na Maegesho ya Malori katika eneo la Nala.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ukaguzi umebainisha dosari zinazohusu uwekezaji wa mitaji ya umma katika baadhi ya halmashauri nchini. Dosari hizo ni pamoja na uwekezaji unaofanyika bila upembuzi yakinifu wala andiko la biashara. Dosari nyingine ni uwekezaji unaozingatia mikataba ya ujenzi yenye masharti yanayosababisha hasara katika Halmashauri zinazohusika. Hali hiyo inaathiri nia ya kuongeza mapato ya vyanzo vya ndani na kuwa na mtiririko madhubuti wa fedha ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya huduma bora.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Kamati imeonesha kuwa halmashauri nyingi zilifanya uwekezaji bila kuzingatia misingi madhubuti ya uwekezaji huo. Aidha, uamuzi wa uwekezaji katika halmashauri hizo unaweza kutafsiriwa kuwa na kasoro kama ifuatavyo;

(a) Baadhi ya halmashauri hufanya uwekezaji wa mitaji yao kwa kuiga kinachofanyika kwenye halmashauri zingine bila ya kufanya upembuzi yakinifu wa mazingira yao kibiashara (feasibility study) na kuwa na Andiko la kibiashara (Business plan). Kwa mfano; kila Halmashauri inataka kuwekeza kwenye Stendi Kubwa ya Mabasi au Masoko Makubwa ya Kisasa bila kujali idadi ya watu, usanifu wa miundombinu kulingana na maeneo yao, ukubwa wa miamala ya biashara, mkao wa eneo kimkakati katika masuala ya biashara, na mapato yatakayopatikana

(b) Baadhi ya halmashauri zimefanya uwekezaji katika Benki zenye utendaji usioridhisha. Kwa mfano Manispaa

2 NOVEMBA, 2022

za Mkoa wa Dar es Salaam zimewekeza hisa zipatazo 24,036,348 zenye thamani ya shilingi bilioni 5.77 katika benki ya DCB. Utendaji wa Benki hiyo hauridhishi na kwamba kwa muda mrefu sasa DCB imekuwa ikipata hasara. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 hisa zake zilishuka thamani kwa shilingi bilioni 1.20 na hakuna dalili za kuimarika.

Mfano mwingine ni Uwekezaji katika Bodi ya Mikopo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Mamlaka 85 za Serikali za Mitaa ziliwekeza shilingi bilioni 4.88 katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa tangu kuanzishwa kwake mpaka sasa hazijawahi kupata gawio au faida inayotokana na uwekezajihuo.

(c) Mikataba ya ujenzi inakuwa na masharti ama vigezo ambavyo ni hasara kwa Halmashauri zenyewe; Matokeo yake, Uwekezaji katika maeneo hayo umejaa hasara.

Mheshimiwa Spika, ili kunufaika na uwekezaji inamlazimu muwekezaji makini kuzingatia desturi zote za uwekezaji. Haifai kuamua kuwekeza katika vitega uchumi au miradi isiyokuwa na dalili za kupata faida. Aidha, uwekezaji kwa kutumia mikataba yenye sura ya kupata hasara pamoja na uwekezaji kwa kuiga ni mambo yanayosababisha matumizi mabaya ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, dosari za uwekezaji zilizobainishwa, ni miongoni mwa matumizi mabaya ya fedha za umma katika mamlaka za Serikali za mitaa nchini.

2 NOVEMBA, 2022

2.2.5 Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ulianzishwa kwa madhumuni ya kuongeza uwezeshaji kiuchumi kwa vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu mijini na vijijini. Lengo mahsusi la Mfuko ni kuyawezesha Makundi haya yafanye shughuli za kiuchumi zitakazoboresha kiwango chao cha maisha. Kutokana na umuhimu wa Mfuko huu ambao upo kwa mujibu wa sheria, kiasi cha 10% ya mapato ya ndani yasiyolindwa hupaswa kutengwa kila mwaka na kila Halmashauri kwa ajili ya Vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa uwiano wa 4:4:2 mtawalia.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu una fedha nyingi na za uhakika kutokana na ukweli kwamba ni lazima kila Halmashauri itenge fedha hizo kama takwa la kisheria. Kwa mfano; katika Hotuba ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Fedha imeripoti Bungeni mwenendo wa mapato ya ndani ya Halmashauri zote nchini kwa mwaka 2020/ 2021 kuwa ilikuwa ni Shilingi Bilioni 757 ambayo asilimia 10 yake ni Shilingi Billioni 75.7.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanywa na CAG umeonyesha kasoro mbalimbali za uendeshaji wa mfuko huu. Miongoni mwa kasoro hizo ni kama ifuatavyo;

(a) Halmashauri 155 zimeshindwa kukusanya shilingi

2 NOVEMBA, 2022

Bilioni 47.01 zilizotolewa kwa vikundi kutokana na kukosa udhibiti mzuri na usimamizi wa mikopo hiyo;

(b) Halmashauri 11 kushindwa kuhamisha shilingi bilioni 1.24 kutoka akaunti ya amana kwenda akaunti ya mifuko. Hali hiyo inasababisha wasiwasi kama fedha hizo zinaweza kutumika kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanufaika;

(c) Halmashauri 17 zilitoa mikopo ya shilingi bilioni 3.26 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu bila kuzingatia uwiano ulioanishwa; na

(d) Halmashauri 83 hazikuchangia jumla ya shilingi bilioni 6.68 kwenye mfuko kutoka kwenye mapato yake ya ndani.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Kamati imebaini kuwa Uendeshaji wa Mfuko huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Baadhi ya Halmashauri hutoa mikopo bila kujiridhisha na uhalisia wa mipango ya biashara au uhai wa vikundi vinavyokopeshwa;

(b) Halmashauri zingine hutoa mikopo pasipo kutoa elimu ya kutosha ya ujasiriamali kwa wakopaji. Jambo hilo husababisha wakopaji kukopa pasipo kujua kiuhalisia aina ya biashara itakayofanyika, masharti na namna ya urejeshaji mikopo hiyo;

(c) Halmashauri zingine hazina mipango mikakati ya

2 NOVEMBA, 2022

kudai marejesho ya mikopoinayotolewa. Kwa msingi huu, ni vigumu sana kubaini tija na uendelevu wa Mfuko huu;

(d) Halmashauri zingine hutoa Mikopo kwa Makundi yaliyo katika maeneo ya mjini tu hivyo kuyanyima fursa Makundi yaliyo maeneo mengine ndani ya Halmashauri;

(e) Halmashauri zingine hazizingatii uwiano wa mgawanyo vipo vikundi hususani vya Watu wenye ulemavu havinufaiki ipasavyo, ingawa vinastahili. Vilevile, halmashauri zingine hushindwa kuwapa walemavu mikopo hiyo kwa kisingizio eti wapo wachache na kuwa hawajitokezi kuomba Mikopo inayohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ipo changamoto kubwa ya ukusanyaji wa marejesho kwa muda mrefu kama inavyoonekana katika kielelezo kifuatacho.

Jedwali 3: Mwenendo wa mikopo isiyorejeshwa

Mwaka wa fedha	Idadi ya Halmashauri	Kiasi ambacho ijarejeshwa(Sh.)	Asilimia(%)
2020/21	155	47,006,024,260	70
2019/20	130	27,790,189,049	65
2018/19	111	13,794,359,981	59
2017/18	90	10,044,453,656	59
2016/17	84	5,809,326,477	63

2 NOVEMBA, 2022

Chanzo: Ripoti ya CAG kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2020/2021

2.2.6 Baadhi ya Stahiki za Watumishi kutolipwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Rasilimaliwatu ndiyo msingi wa utendaji na mafanikio ya taasisi yoyote ile zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kuna uwekezaji ambao sharti ufanyike ili rasilimali hii iweze kuleta tija sasa au badae. Miongoni mwa uwekezaji huo ni malipo ya mishahara ambayo ni stahiki za rasimali hiyo.

Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG umebaini malimbikizo ya muda mrefu ya mishahara yenye thamani ya shilingi bilioni 63.83 kwa watumishi 33,405 ambayo hayakulipwa. Vilevile kuna madai mengine ya watumishi 71,670 yenye thamani ya shilingi bilioni 96.65 ambayo yalikuwa hayajalipwa yakiwa ni posho za likizo, gharama za uhamisho na posho nyingine. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021:

a) Katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Watumishi 144 na wengine 16 wa Kada ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba hawakulipwa jumla ya shilingi milioni 128.03 ambazo ni gharama ya kusafirisha mizigo yao baada ya kufikia umri wa kustaafu na kuhitimisha utumishi wao wa umma.

b) Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga haikupeleka kiasi cha Tsh 66,491,474 katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wakati Halmashauri ya Wilaya ya Ngara haikupeleka kiasi cha Tsh. 49, 229, 555. Tabia hii

2 NOVEMBA, 2022

huwaletea taabu sana Watumishi wa Umma wanapokoma utumishi wao. Ikumbukwe kwamba suala hili lilipata kuibua majadiliano makali sana Bungeni tarehe 23 Septemba, 2022 kutokana na Swali la Mhe. Anastazia J. Wambura (Mb) alipoiuliza Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana kwamba “Ni lini wastaafu ambao waajiri wao walikuwa hawapeleki michango katika mifukoya hifadhi ya jamii watalipwa haki zao?”

2.2.7 Hasara ya Kifedha kutokana na Vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo ya Wananchi Mamlaka za Serikali za Mitaa hushirikiana na taasisi nyingine za Serikali kama vile Wakala wa Manunuzi wa Serikali (GPSA), Wakala wa Matengenezo ya Magari ya Serikali (TEMESA), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Bohari ya dawa Tanzania (MSD). Ripoti ya CAG imeonesha kuwa mamlaka za Serikali za Mitaa zilipata hasara kutokana na kushirikiana na taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Kamati inaonyesha kwamba taasisi hizo zimekuwa kikwazo kwa matumizi ya fedha za umma kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa kutokana na kupokea fedha zinazolipwa na mamlaka hizo na kutokutoa huduma inavyostahili. Kwa mfano:

a) Upo utaratibu uliowekwa na Serikali kwa Makundi mbalimbali ya Wananchi hususani Wazee kwamba Wahudumiwe kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). Kwa utaratibu huu, Halmashauri hutoa huduma za

2 NOVEMBA, 2022

afya kwa Wanufaika na kudai marejesho NHIF. Kilichobainika ambacho ndiyo hoja ya Kamati ni kwamba NHIF hairejeshi gharama hizo kwa Halmashauri mbalimbali nchini kwa madai kuwa fomu za matibabu zinajazwa vibaya. Mashaka ya Kamati ni pale inapobainika kwamba Wateja wa NHIF wanaojaza formu vibaya ni Vituo vya afya vya Halmashuri tu! Wengine wote wanajaza form vizuri.

Mheshiwa Spika, jumla ya **Shilingi Bilioni 2.34** hazijalipwa katika Mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa nchini kutokana na huduma za tiba zilizotolewa kwa Wanufaika wa Mfuko huo. NHIF imeshindwa kulipa fedha hizo kwa maelezo kwamba fomu za Wagonjwa zilijazwa vibaya kiasi cha kutoaminika. Changamoto hii imeonekana katika mamlaka nyingi za serikali za mitaa na kusababisha hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali haitalitolea suala hili maelezo ya kina, Kamati inalitazama kama ni hali tu ya NHIF kujinufaisha kimapato kwa kukwepa kufanya marejesho ya gharama za Halmashauri.

b) Halmashauri nyingi zimekuwa zikilipa fedha kwenye Bohari ya Dawa Nchini (MSD) pasipo kupelekewa dawa na vifaa tiba kwa wakati. Hali hii imekuwa ni kero kubwa katika baadhi ya halmashauri. Jumla ya dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya **Shilingi Bilioni 1.17** havikupelekwa na MSD katika Halmashauri kutokana na sababu mbalimbali zilizo nje na utendaji wa Halmashauri;

c) TEMESA imekuwa ikitumika kurudisha nyuma utendaji

2 NOVEMBA, 2022

na uzalishaji katika baadhi ya Halmashauri nchini kwa sababu haitoi huduma ipasavyo kwa wateja wake. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwenye Halmashauri mbalimbali kuhusiana na udhaifu wa Chombo hiki katika matengenezo na ukaguzi wa magari na mitambo.

Muheshimiwa Spika; Kutokana na changamoto hii, kuna Halmashauri zimeshindwa kukusanya mapato lengwa kwa sababu ya magari na mitambo yao kuwa mabovu na kushindwa kufanya kazi, hivyo kuchelewesha huduma mbalimbali kuwafikia walengwa.

d) Halmashauri nyingi zimekuwa zikifanya manunuzi mbalimbali kupitia GPSA. Lakini kwa sasa GPSA imekuwa ikishindwa kufanya kazi yake ipasavyo. Hii imetokana na kwamba Halmashauri mbalimbali zimekuwa zikiamurishwa kulipa fedha kabla ya kupata huduma au bidhaa husika, pia kwa upande wa uagizaji na manunuzi magari, wameshindwa kufanya vizuri kwani wamekuwa na tabia ya kurudisha fedha kwa wateja pasipo kukamilisha manunuzi ya magari hayo kwa wakati uliopangwa.

2.2.8 Uteketezaji wa dawa za binadamu katika vituo vya kutolea huduma yaafya

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG ya Mwaka wa Fedha 2020/21 inaonesha kuwepo kwa wimbi kubwa la uteketezaji wa madawa ya binadamu yenye thamani kubwa sana ya fedha. Kwa mfano; katika mwaka wa fedha **2018/19** halmashauri 14 ziliteketeza dawa zenye

2 NOVEMBA, 2022

thamani ya shilingi Bilioni 7.3, mwaka **2019/20**
halmashauri 31 (Bilioni 1.5) na Mwaka **2020/21**
Halmashauri 46 (Bilioni 3.5).

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa ununuzi na usambazaji wa dawa zinazokaribia kuisha muda wake, au kupeleka dawa kwenye maeneo ambayo hayana magonjwa yanayohusika, unaweza kuwa ni mwanya mpya wa upotevu wa fedha za umma nchini. Serikali inapaswa kulitolea suala hili maelezo ya kina ili Bunge lijiridhishe juu ya hali hiyo kwani ikiendelea kwa namna ilivyo taifa litazidi kupata hasara kwa namna yenye kutia mashaka ya ubadhirifu unaopangwa na kuratibiwa ili utokee.

2.2.9 Dosari katika kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri na Serikalikuu.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii, Kamati imebaini maeneo mapya manne ambayo ni mianya ya upotevu wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Maeneo haya ni pamoja na-; Ushuru wa huduma (service levy) kukusanywa bila ya uthibitisho wa mapato halisi ya Kampuni kwa mwaka (turnover), Halmashauri zingine kufanya malipo bila kukata au kutokupeleka Kodi ya Zuiro (withholding tax), Kufanya malipo bila kutumia Risiti za EFD; na kuendelea kuwepo kwa leseni za biashara nje ya Mfumo.

2 NOVEMBA, 2022

Jedwali Na. 1: Kodi ya Zuiyo(withholding tax) Ambayo haikukusanywa.

Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Halmasha uri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Arusha	10,666,954	14.	H/W Mpanda	3,352,986
2.	H/Jiji Arusha	12,426,204	15.	H/M Mpanda	5,532,464
3.	H/W Chato	141,139,943	16.	H/W Mpimbwe	9,780,365
4.	H/Mji Handeni	10,652,329	17.	H/W Mtwara	1,435,604
5.	H/W Kaliua	2,177,940	18.	H/W Nsimbo	11,406,850
6.	H/W Kibiti	2,179,600	19.	H/W Sikonge	7,677,253
7.	H/M Kigamboni	3,274,332	20.	H/M Singida	1,732,680
8.	H/W Kishapu	7,948,005	21.	H/M Tabora	5,179,067
9.	H/W Kyerwa	2,127,883	22.	H/W Tandahimba	11,103,530
10.	H/W Masasi	1,168,895	23.	H/Mji Tunduma	6,574,554
11.	H/W Mbogwe	4,967,716	24.	H/W Ulanga	6,278,200
12.	H/W Monduli	3,320,765			
13.	H/M Moshi	65,955,048		Jumla	338,059,167

Chanzo: Taarifa ya CAG- 2020/21

2.2.10 Upotevu wa Mapato katika Mifumo ya Kielektroniki

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina mifumo ya namna mbalimbali ya kielektroniki kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato na utoaji wa matumizi. Dhamira ya Serikali kuwa na mifumo hii ni kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma, kubana mianya ya upotevu wa mapato hususani kwa njia ya rushwa, wizi na kurahisisha miamala ya mapato na matumizi.

Mheshiwa Spika, ripoti ya CAG imebainisha upotevu wa mapato ya Serikali kupitia kwenye mifumo hii ya

2 NOVEMBA, 2022

kielektroniki. Hali hii inaweza kuonekana kwa kuangalia marekebisho ya miamala yanayofanywa na maafisa wanaohusika na mchakato wa ukusanyaji wa mapato hayo pasipokuwa na nyaraka za uthibitisho wa uhalali wa marekebisho hayo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2020/21 Halmashauri 27 zinazoonekana kwenye Jedwali Na.5 zilifanya marekebisho ya miamala yenye jumla ya Shilingi Bilioni 1.6 kwenye mfumo bila uthibitisho wa ulazima na uhalali wa marekebisho hayo kufanyika.

Jedwali Na. 2: Ankara zilizorekebishwa bila viambatisho

Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)	Na.	Halmashauri	Kiasi (Sh.)
1.	H/W Rufiji	656,820,563	15.	H/W Chamwino	19,673,910
2.	H/W Mbozi	201,359,728	16.	H/M Lindi	17,195,983
3.	H/M Kinondoni	135,994,090	17.	H/W Morogoro	16,316,145
4.	H/W Mkuranga	124,867,127	18.	H/W Bagamoyo	13,663,932
5.	H/W Kilindi	104,869,200	19.	H/W Nsimbo	11,799,744
6.	H/M Iringa	85,640,671	20.	H/W Serengeti	9,875,644
7.	H/W Kibaha	45,589,585	21.	H/Mji Nzega	9,253,626
8.	H/W Kisarawe	31,847,394	22.	H/Jiji Mwanza	8,578,000
9.	H/W Rorya	27,116,121	23.	H/W Bumbuli	7,406,000
10.	H/W Kwimba	25,563,641	24.	H/W Musoma	5,476,000
11.	H/W Korogwe	24,404,486	25.	H/W Nyasa	4,956,250
12.	H/W Mpwapwa	24,148,808	26.	H/W Kaliua	4,301,700
13.	H/W Kiteto	23,285,500	27.	H/W Simanjiro	4,104,100
14.	H/W Mufindi	20,716,628		Jumla	1,664,824,576

Chanzo: Taarifa ya CAG

2 NOVEMBA, 2022

Katika hatua nyingine ya Majadiliano ya Kikao cha tarehe 17 Oktoba, 2022 Katika Ukumbi Namba 37 katika Jengo dogo la Utawala (Utawala Annex) Bungeni jijini Dodoma, mmoja wa Maafisa Masuuli aliarifu Kamati kwamba katika Halmashauri yake alibaini kuwa maafisa mifumo ya TEHAMA hushirikiana na maafisa mapato kusababisha upotevu wa mapato kwenye mifumo. Hii ni ushahidi tosha kwamba ipo mianya ya upotevu wa mapato katika mifumo hiyo unaotekelezwa na maafisa wa Serikali.

Mheshimiwa Spika; Udhaifu mkubwa pia umebainika katika kukusanya mapato kwa kutumia PoS mashine. Halmashauri nyingi zimekuwa zikitumia hiki kama kichaka cha kutumia fedha za makusanyo kinyume cha utaratibu wa matumizi ya fedha husika: -

i) Fedha za ushuru na makusanyo mengine kupitia Pos zinakusanywa na kukaa muda mrefu bila kupeleka benki. Mfano, jumla ya halmashauri 147 hazikupeleka benki kiasi cha shilingi bilioni 17 zilizokusanywa kwa mashine za PoS;

ii) Mashine kukaa muda mrefu bila kufanya kazi, kuzimika hivyo kushindwa kufanya kazi iliyokusudiwa

iii) Wateja kuwa na Vitambulisho vingi vyenye majina yanayofanana

2.3 Majumuisho ya Sehemu ya Pili

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Sehemu ya Pili imeonesha matumizi mabaya ya fedha za umma kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na kutokuzingatiwa kwa sheria, kanuni na taratibu mbalimbali. Aidha, sehemu hii imeonesha dosari za ukusanyaji wa mapato ya Serikali Kinyume na Sheria ya Fedha za Umma, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa na Miongozo mingine kuhusu ukusanyaji wa Mapato. Maeneo makubwa yaliyotajwa yanahusu mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, uwekezaji wa mitaji ya umma katika baadhi ya halmashauri, ununuzi wa huduma na bidhaa na usimaizi wa mikataba. Vilevile, sehemu hii imebainisha changamoto katika ruzuku ya miradi ya maendleo katika mamlaka ya serikali za mitaa, matumizi ya fedha kwenye akaunti za amana na udhaifu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Jambo kubwa la kwenda nalo katika sehemu ya tatu inayohusu maoni na mapendekezo ni kwamba changamoto hizo zinahitaji hatua maalum na muhimu ili kupata ufumbuzi. Bunge kama chombo kinachosimaia matumizi ya fedha za umma kwa niaba ya wananchi linatarajiwa kutoa ushauri madhubuti utakaowezesha kuondoa matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma kwenye mamlaka ya serikali za mitaa.

2 NOVEMBA, 2022

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, kutokana na dosari zilizobainishwa na CAG kwenye eneo la matumizi mabaya ya fedha za umma, Bunge linatarajiwa kutoa ushauri utakaowezesha kuondoa vyanzo vya matumizi mabaya ya fedha za umma. Mtazamo wa Kamati kuhusu maeneo yenye matatizo ya matumizi ya fedha za umma ni kam aifuatavyo;

a) Ili mfuko wa mikopo kwa vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu uwezeshe matokeo ya kiuchumi yaliyokusudiwa, Serikali inapaswa kutatua changamoto zilizopo;

b) Matumizi ya fedha za umma yanapaswa kuendana na dhamira ya bunge ya uidhinishaji wa bajeti. Kwa msingi huo, utoaji wa ruzuku ya miradi ya maendeleo kwa mamlaka ya serikali za Mitaa unatakiwa kuendana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge;

c) Matumizi mabaya ya fedha za umma katika maeneo ya mitaji ya umma ndani ya mamlaka ya serikali za Mitaa yanaweza kuzuiwa kwa kuzitaka halmashauri nchini zizingatie fursa za uwekevu na tija ya miradi;

d) Upotevu wa fedha za umma kutokana na usimamizi mbovu wa mikataba unaweza kudhibitiwa kwa kuwasisitiza maofisa masuuli kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na kuridhiwa na Bunge;

- e) Uongozi bora katika eneo la matumizi ya fedha za umma unaweza kufikiwa pamoja na mambo mengine kwa kuzingatia stahili za watumishi;
- f) Ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri unachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza uwezo wa halmashauri hizo kuwahudumua wananchi na kuleta maendeleo katika maeneo yanayohusika. Lengo la kutumia mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato katika halmashauri nchini linaweza kufikiwa kwa kuchukua hatua kali dhidi ya wahusika wanaoihujumu mifumo hiyo;
- g) Taasisi zinazopokea malipo kutoka mamlaka ya serikali za mitaa zisipohimizwa na kusimamiwa ipasavyo zitaendelea kusababisha madhara katika matumizi ya fedha za umma kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo ni mtazamo wa jumla wa Kamati unaotokana na matokeo ya uchambuzi wa ripoti kuu ya mwaka ya ukaguzi wa mamlaka za serikali za mitaa ya mwaka 2020/21 iliyowasilishwa na CAG. Naomba kulieleza Bunge lako tukufu kwamba mtazamo huo ndio msingi wa mapendekezo ya Kamati nitakayoyasoma.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kutoa hojakuhusu ukaguzi wa hesabu za serikali za mitaa kama ifuatavyo;

2 NOVEMBA, 2022

i) Kuhusu Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

KWAKUWA lengo la Serikali kuwa na Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya Akina Mama, Vijana na Watu wenye Ulemavu ni uwezeshaji kiuchumi na kupunguza makali ya ukosefu wa ajira nchini,

NA KWAKUWA Kamati imebaini kwamba uendeshaji na uendelevu wa Mfuko huo kwa sasa hauko thabiti,

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba katika kila Halmashauri kuanzishwe:

a) Akaunti Maalum kwa ajili ya fedha zitakazokuwa zinatolewa na kurejeshwa ili kuweka kumbukumbu za vikundi vinavyokopa, kiasi kilichokopwa, shughuli inayofanyika na mwenendo wa marejesho.

b) Mpango Mahsusi wa utoaji wa elimu kwa Wanufaika wa mikopo ili Watambue uwepo wa fursa hiyo na wajiandae kunufaika nayo;

c) Utaratibu wa kujiridhisha na mipango ya biashara inayoenda kutekelezwa badala ya kutoa mikopo kwa kufuata orodha tu ya majinaya Wana kikundi;

d) Dhana ya kuutumia Mfuko huu kwa ajili ya kuyakwamua Makundi hayo Maalum kiuchumi na kuongeza ajira nchini badala ya kutoa mikopo hiyo kiholela;

2 NOVEMBA, 2022

e) Tathmini mpya ya Wanufaika wa Mikopo ili kujumuisha Vijana wanaomaliza Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na Vyuho mbalimbali.

ii) Kuhusu Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

KWAKUWA ruzuku ya maendeleo inayotolewa na Serikali kuu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa mwaka husika,

NA KWAKUWA ruzuku hiyo hutolewa kwa misingi ya Sheria ya Matumizi inayopitishwa na Bunge kwa Mwaka husika wa Bajeti, KWAHIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:

a) Kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato na kudhibiti uvujaji kwa njia za mifumo ya kielktroniki ili taifa lipate fedha za kutosha kugharamia mipango ya maendeleo ya kila mwaka;

b) Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Matumizi zinazopitishwa na Bunge katika kila mwaka wa bajeti ili kuendelea kujijengea imani Bungeni nakwa Wananchi;

c) Kuweka angalau ukaribiano wa kiasi fulani cha ruzuku endapo itabidi baadhi ya Halmashauri kuzidishiwa kuliko vile inavyotokea kwamba Halmashauri zingine hupewa kiasi kidogo mno wakati zingine hupewazaidi ya 50%;

2 NOVEMBA, 2022

d) Kutorejesha HAZINA fedha zinazokuwa zimepelekwa katika Halmashauri kwa madai kuwa mwaka husika wa fedha umeisha.

iii) Kuhusu Uwekevu na Tija katika Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

KWAKUWA uwekezaji wa mitaji ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kwa ajili ya huduma na faida ya kifedha itakayoleta huduma bora zaidi,

NAKWAKUWA halmashauri zilizo nyingi zimekumbwa na kasumba ya kuwekeza kwenye masoko na vituo vya mabasi kama vile hakuna maeneo mengine yanayofaa kwa uwekezaji,

KWAHIYOBASI Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha kuwa uwekezaji unazingatia fursa za uwekevu na tija katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri kuliko hali ilivyo sasa ambapo kila Halmashauri inataka soko na kituo cha mabasi tu!

iv) Kuhusu Manunuzi na Mikataba ya Upatikanaji wa Huduma na Bidhaa Mbalimbali

Bunge linaiagiza Serikali kusimamia ipasavyo manunuzi yote ya umma kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na kuridhiwa na Bunge. Na, Maafisa Masuuli wote watakaobainika kutosimamia ipasavyo Agizo hili wachukuliwe hatua kali za kisheria kwa nia ya kukomesha ubadhirifu na kuliletea taifa manufaa stahiki.

2 NOVEMBA, 2022

v) Kuhusu Upatikanaji wa Stahili za Watumishi kwa Mujibu wa Sheria

KWAKUWA stahili za Watumishi zipo kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya Serikali inayopaswa kuzingatiwa na Waajiri na Watumishi pia

NA KWAKUWA baadhi ya Waajiri hawatekelezi matakwa ya Sheria hizo mathalani katika kupeleka michango ya pensheni katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii hivyo kuwaletea Watumishi usumbufu na lawama kwa Serikali wanapostaafu,

KWAHIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kutoa stahiki za Watumishi kwa kuzingatia Sheria zilizowekwa na kuchukua hatua kali kwa Waajiri wasiozingatia matakwa ya Sheria hizo.

vi) Kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri

KWAKUWA mapato ya ndani ya Halmashauri ni muhimu kwa ajili ya kugharamia miradi na huduma mbalimbali za kijamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa,

NAKWAKUWA Halmashauri zilizo nyingi zina udhaifu katika eneo hili kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uvajaji wa mapato kwenye mifumo ya kielektroniki, rushwa na kutosimamia ipasavyo sheria, kanuni na taratibu za fedha

2 NOVEMBA, 2022

KWAHIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:

a) Kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato katika mifumo ya kielektroniki;

b) Kuhakikisha kuwa Mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato (TAUSI) unaanza kutumika katika Halmashauri zote za Serikali ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023 badala ya hali ilivyo sasa ambapo bado kuna Halmashauri zinazoendelea kutumia mfumo wa zamani (Local Government Revenue Collection Information System- LGRCIS) unaoruhusu marekebisho ya miamala kwa namna yenye kutia shaka ya wizi.

vii) Kuhusu Matumizi yasiyofaa ya Fedha katika Akaunti za Amana

KWAKUWA fedha zinazowekwa katika akaunti za amani zinakuwa ni kwa ajili ya matumizi maalum,

NA KWAKUWA imebainika sasa kwamba katika Halmashauri mbalimbali fedha zilizomo katika akaunti hizo zinatumiwa kwa shughuli ambazo hazikutarajiwa,

KWAHIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinazowekwa katika Akaunti za Amana zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kuliko hali ilivyo sasa ambapo Akaunti hizo zinaonekana kutumiwa kama maficho ya fedha ambazo badae hutumiwa kibadhirifu.

2 NOVEMBA, 2022

viii) Kuhusu Upotevu wa Mapato katika Mifumo ya Kieletroniki ya kukusanya mapato

KWAKUWA mifumo mbalimbali ya mapato na matumizi imewekwa kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika Nyanja za mapato na matumizi ya Serikali,

NA KWAKUWA sasa imebainika kuwepo kwa uvujaji wa mpato kupitiakatika mifumo hiyo,

KWAHIYO BASI Bunge linaitaka Serikali kudhibiti mianya ya mapato katika mifumo hiyo na kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa Watumishi wote watakaobainika kuhusika na upotevu mathalani Watumishi walio katika Halmashauri ambazo miamala ya mapato ilibadirishwa au kufutwa bila ya uthibitisho wa ulazima wa kufanya hivyo.

ix) Kuhusu Hasara ya kifedha kutokana na Vitendo vya Taasisi za Serikali dhidi ya Halmashauri

KWAKUWA Kamati imebainisha namna Mamlaka za Serikali za Mitaa zinavyoathiriwa kifedha kutokana na ushirikiano wake na Taasisi zingine za Serikali kama vile NHIF, TEMESA, MSD na GPSA;

NA KWAKUWA athari hizo zinadidimiza kasi ya maendeleo katika Mamlaka hizo,

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali:

a) Kushughulikia mara moja suala la NHIF kutorejeshwa gharama za matibabu na vifaa tiba vinavyotolewa na

2 NOVEMBA, 2022

Halmashauri kwa Wanufaika wa bima ya afya chini ya Mfuko huo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini;

b) Kuisimamia ipasavyo MSD ili iwe inapeleka dawa na vifaa tiba katika halmashauri kulingana na mahitaji ya Halmashauri zenyewe;

c) Kuisimamia GPSA ili iwe inatekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za kazi zao ili kuzisaidia Halmashauri katika utekelezaji wa mipango yao kuliko hali ilivyo sasa ambapo GPSA huchangia kuzizorotesha; na

d) Kuiimarisha TEMESA ili iweze kuzisaidia Halmashauri na Taasisi zingine za Serikali kisha kupunguza malalamiko ya udhaifu wake katika eneo la ukaguzi na utengenezaji wa magari na mitambo katika Halmashauri.

x) Kuhusu Utekelezaji wa Dawa za Binadamu katika Hospitali na Vituo vya Afya.

Bunge linaitaka Serikali kutoa maelezo ya kuridhisha ni kwa nini pamekuwa na kasi kubwa ya utekelezaji wa dawa za binadamu kama vile dawa hizo zinanunuliwa bila mpango mahsus. Aidha, Serikali inapaswa kudhibiti jambo hili kwani baadhi ya dawa zinazoteketezwa siyo za magonjwa ya mlipuko.

4.0 SHUKRANI

Mheshimiwa Spika, Kamati inakushukuru kwa uongozi wako thabiti uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Aidha, tunaipongeza sana Sekretarieti ya

2 NOVEMBA, 2022

Bunge chini ya Katibu wa Bunge Bi. Nanelwa Mwihambi. Sekretarieti imetusaidia katika utafiti, uratibu, upatikanaji wa taarifa na ushauri katika masuala mbalimbali ya Kamati. Tunawapongeza Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Bw. Athuman Hussen, Mkurugenzi Msaidizi katika Sehemu ya Fedha na Uchumi Ndg. Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati ya LAAC Ndg. Dickson M. Bisile akisaidiana na Bi. Jesca T. Sanga na Ndg. Paul Chima.

Tunaishkuru sana Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi chini ya Ndg CPA Charles Kichere Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Tunaipongeza Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bungena Uratibu) na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kila wakati tulipohitaji ufafanuzi wa hoja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wa LAAC kwa uvumilivu, ushirikiano na uchapa kazi, na ninaomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Halima J. Mdee, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Stanslaus S. Mabula, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Agnes E. Hokororo, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Twaha A. Mpembenwe, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Benaya L. Kapinga, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Conchesta L. Rwamlaza, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Elibariki E. Kingu, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Jeremiah A. Mrimi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Jesca J. Msambatavangu, Mb - Mjumbe
10. Mhe. John M. Sallu, Mb - Mjumbe

2 NOVEMBA, 2022

11. Mhe. Joseph Z. Kamonga, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Joseph A. Tadayo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Francis K. Ndulane, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Issa A. Mchungahela, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija H. Aboud, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Maimuna S. Mtanda, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Maimuna A. Pathan, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Masache N. Kasaka, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Ng'wasi D. Kamani, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Rehema J. Migilla, Mb - Mjumbe

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika Taarifa hii yamejengwa katika misingi ya Hoja za Ukaguzi wa CAG. Na, yanakusudia kuimarisha nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa ili kuwaletea wananchi maendeleo. Hivyo, ni vema Serikali ikatambua kwamba Ukaguzi unaotekelezwa na CAG katika mapato na matumizi ya fedha za umma nchini ni kwa niaba ya Bunge. Na, kwamba Hoja za Ukaguzi zinazotolewa na CAG ni Hoja za Bunge.

Hivyo, katika Taarifa za Hesabu za Miaka inayofuata, Halmashauri ambayo haitajibu hoja za Ukaguzi ipasavyo itahesabiwa na Kamati kwamba imekaidi kujibu hoja za Bunge. Hatua kali za kinidhamu zitapendekezwa kwa Mamlaka zinazohusika papo hapo wakati vikao vya Kamati vikiendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuyaafiki Maoni

2 NOVEMBA, 2022

na Mapendekezo ya LAAC juu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

.....

Stanslaus S. Mabula, Mb

MAKAMU MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA

SERIKALI ZA MITAA

03 Novemba, 2022

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti tunakushukuru sana kwa mawasilisho haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa wakati wetu wa kipindi cha kwanza cha kukutana. Tutakutana tena saa kumi na moja ambapo tutaanza na kumsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (*Public Investments Committee*) ili sasa mjadala utaanza kwa ajili ya Kamati zote tatu na Mbunge utaruhusiwa kuchangia zote tatu. Unaweza ukaamua kujiekeza kwenye moja, ukajielekeza kwenye mbili,

2 NOVEMBA, 2022

ukajielekeza kwenye tatu. Kwa sababu kanuni zetu kwa Bunge la Septemba, Bunge la Novemba na Bunge la mwezi wa Kwanza zinatoa dakika kumi na tano kwa Mbunge kuchangia. Kwa hiyo tutaanza na huo utaratibu leo kuchangia dakika kumi na tano kwa yule mwenye hoja zake ili apewe nafasi ya kutoa ushauri vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na naamini tumepata mwanga na kila Mbunge akatazame ile taarifa ya CAG inasema nini kuhusu halmashauri yake itatusaidia sana kwa sababu kuna wakati humu ndani tunazungumza, halafu Mbunge pengine kule kwake mambo kidogo yanakuwa namna fulani. Kwa hivyo yeye ataweza kusema vizuri humu ndani. Haya Waheshimiwa nawatakia kila kheri kwenye kusoma hizo taarifa.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

(Saa 7.37 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya

2 NOVEMBA, 2022

**Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa
Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za
Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa
zilizokaguliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za
Serikali kwa Mwaka wa
Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

na

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa
Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma
kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Mheshimiwa Jerry William Silaa, aje awasilishe maoni ya Kamati.

MHE. JERRY W. SILAA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kufika siku ya leo. Kutokana na ufinyu wa muda naomba taarifa hii yote kama inavyosomeka katika Kitabu cha Kamati iingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya

2 NOVEMBA, 2022

Umma kuhusu Uwekezaji wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na kuliomba Bunge liipokee na kujadili taarifa hii. Lengo ni kulijulisha Bunge lako Tukufu iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma una ufanisi na kwamba umezingatia taratibu, sheria na miongozo mujarabu ya biashara au vinginevyo, kama ilivyofafanuliwa katika Kifungu cha 12 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inagusa mitaji ya umma kwenye vitega uchumi (*Investments*) vya Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na Kampuni ambako Serikali ina hisa chache. Kipindi cha Uwekezaji kinachoripotiwa ni kuanzia Mwezi Julai, 2020 hadi Juni, 2021. Msingi wa yaliyomo kwenye taarifa hii ni taarifa ya utendaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ya Msajili wa Hazina, mwenye jukumu la kusimamia uwekezaji na mali nyingine za Serikali. Uwekezaji huo unafanyika katika Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na kwenye Kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Taarifa. Ili kuliwezesha Bunge hili kufuatilitia mtiririko wa taarifa pamoja na kurahisisha msingi wa uamuzi wa Bunge juu ya hoja hii ya Kamati, naomba kubainisha muundo wa taarifa kwa kutaja sehemu za taarifa na maudhui yake ya jumla. Kimuundo, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Tatu na kumalizia kwa shukurani na kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza inayohusu maelezo ya Utangulizi inahusu msingi wa kazi ya Kamati kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma na wigo wa jukumu

2 NOVEMBA, 2022

hilo. Aidha, sehemu hii inabainisha njia au mbinu zilizotumika kufuatilia ufanisi wa mitaji ya umma. Sehemu ya Pili inafafanua msingi wa ufuatiliaji wa Kibunge wa mitaji ya umma, vigezo vilivyozingatiwa na kueleza matokeo ya ufuatiliaji huo.

Mheshimiwa Spika, msingi na wigo wa kazi wa Kamati na njia zilizotumika. Msingi wa kazi, wigo wa majukumu na njia ya utekelezaji vinasaidia kusadikisha taarifa na kuiwezesha itumike kufanya uamuzi. Ukweli huo umesukuma nia ya kutambulisha msingi, wigo na njia zilizotumika kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ili kubainisha uthabiti wa matokeo ya kazi inayoripotiwa katika taarifa hii, naomba kutaja msingi wa kazi za Kamati ya kufuatilia mitaji ya Umma. Msingi huo unaelezwa katika Kifungu cha 12(2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kifungu hicho kinabainisha kwamba, kazi za Kamati zitatokana na taarifa zinazohusu uwekezaji wa mitaji ya umma katika Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

Mheshimiwa Spika, wigo (*scope*) wa ufuatiliaji wa mitaji ya umma. Kwa kuwa wigo wa kazi unaweka ukomo wa matarajio ya matokeo, naomba kubainisha mipaka ya kazi ya Kamati kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma. Mipaka hiyo imewekwa na Kifungu cha 12(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kifungu hicho kinaifunga kazi ya Kamati kwenye masuala makuu mawili ambayo ni ufanisi na uzingatiaji wa misingi ya kibiashara kwa mitaji ya umma inayowekezwa katika vitega

2 NOVEMBA, 2022

uchumi vya taasisi na mashirika ya umma pamoja na hisa kwenye kampuni za biashara. Kwa msingi huo, Kamati ilijielekeza kwenye kubaini iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma umefanyika kwa ufanisi na kwamba, uwekezaji huo umezingatia taratibu, sheria na miongozo inayofaa.

Mheshimiwa Spika, njia zilizotumika. Kamati imezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge na kubainisha njia au mbinu zilizotumika kutekeleza kazi ambayo matokeo yake yanaripotiwa. Lengo la kubainisha njia zilizotumika katika ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma ni kuliwezesha Bunge kuhakiki kuhakiki uthabiti (*reliability*) na ustahiki (*validity*) wa matokeo ya kazi inayofanyika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitumia njia Nne, kama zinazvyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya taarifa yetu ina uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma. Madhumuni ya kuripoti Bungeni leo hii ni kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi kuhusu matokeo ya ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Ili kufanikisha azma hiyo, sehemu hii inafafanua shughuli za Kamati za kufuatilia mitaji ya umma. Aidha, Taarifa hii inabainisha matokeo ya ufuatiliaji wa mitaji ya umma. Ufafanuzi huo umegawanyika katika sehemu ndogo mbili ambazo ni maelezo kuhusu hali ya mitaji ya umma ilivyo nchini na yaliyobainika kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa hali ya uwekezaji wa mitaji ya umma. Uchambuzi huu unatokana na msingi wa

2 NOVEMBA, 2022

jukumu la Bunge kufuatilia uwekezaji mitaji ya umma. Kazi hiyo ilihitaji uelewa wa dhana ya Mitaji ya Umma na muundo wake. Aidha, mbinu na vigezo vya kuhakiki ufanisi wa mitaji ya umma ni mambo yaliyofanikisha uchambuzi. Kwa kutambua na kuthamini mambo hayo, taarifa hii inatoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa mitaji ya umma ni dhana yenye maana maalum katika suala la ufuatiliaji Kibunge. Uwekezaji huo unajumuisha ununuzi wa hisa kwenye kampuni binafsi kwa lengo la kupata gawio, kulinda thamani, kutoa huduma au kulinda maslahi ya umma kwenye kampuni zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, msingi wa shughuli za kibunge zinazohusu kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma. Serikali inayo wajibu wa kutumia rasilimali za umma kuwezesha ustawi wa watu nchini na maendeleo ya Taifa. Hivyo Serikali inapowekeza kwa kutumia mitaji ya umma, inaendelea kuwa na jukumu la kusimamia uendeshaji wa mitaji hiyo. Bunge nalo linao wajibu wa kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma na kutunga sheria zinazohusu uwekezaji huo na kuidhinisha matumizi ya fedha za umma kwa ajili ya uwekezaji wa mitaji umma.

Mheshimiwa Spika, kwa taswira hiyo Bunge lilitunga Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370. Sheria hiyo, pamoja na Sheria zingine zinampa Msajili wa Hazina jukumu la kuhodhi uwekezaji wa mali zote za umma.

Mheshimiwa Spika, muundo wa uwekezaji wa mitaji ya umma nchini. Muundo wa matumizi na usimamizi wa mitaji

2 NOVEMBA, 2022

ya umma unahusisha Serikali iliyopewa dhamana ya kutumia mitaji ya umma na Bunge (*Legislature*) limepewa jukumu la kutunga sheria kuhusu matumizi ya mitaji hiyo na kusimamia uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, Bunge ambalo Kikatiba, linayo mamlaka ya kipekee (*exclusive cognizance*) ya kujipangia utaratibu wake, linatumia kamati hii kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma na kuripoti Bungeni leo hii. Utaratibu huo ni pamoja na kupokea ripoti hii.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kufuatilia tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma unafanana kimalengo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera katika sekta mbalimbali. Hata hivyo, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake kwa ufanisi, ufuatiliaji huo unaendana na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa msingi huo, naomba kukupongeza kwa dhati kwa uamuzi wako wa kuelekeza taarifa hii pamoja na taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuingia katika Mkutano mmoja. Uamuzi huu, utaliwezesha Bunge kuzingatia baadhi ya mambo yaliyojitokeza kwenye taarifa hii na kuwa msingi wa ushauri wa Bunge wakati litapokaa kama Kamati ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyozingatiwa. Kwa kuzingatia kifungu cha 12(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, vigezo vilivyotumika katika uchambuzi wa taarifa ya uwekezaji ni mambo yanayopima ufanisi wa mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma. Kigezo kingine ni kipimo cha ufanisi wa mitaji kwenye kampuni ambako Serikali ina umiliki wa hisa.

2 NOVEMBA, 2022

Orodha ya mambo hayo imefafanuliwa katika taarifa niliyoweka Mezani leo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uchambuzi. Mbinu kuu zilizotumika kufanikisha uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kuchambua taarifa ya utendaji wa Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Mantiki ya kufanya hivyo inatokana na kuzingatia masharti ya Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370.
- (b) Kuchambua taarifa za uwekezaji za taasisi na mashirika ya umma yanayotumia mitaji ya umma. Mbinu hii iliwezesha Kamati kuoanisha matokeo ya uchambuzi wa taarifa jumuiifu iliyoandaliwa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, mbinu hizo zimewezesha upatikanaji wa matokeo ya uchambuzi yanayoripotiwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa hali ya mitaji ya umma nchini. Uchambuzi uliofanywa ulizingatia thamani ya uwekezaji uliokuwa ukisimamiwa na Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Taarifa ya utendaji ya Msajili wa Hazina ilionesha kuwa kiwango cha uwekezaji wa Serikali ndani na nje ya nchi kilifikia Shilingi Trillioni 67.95. Katika kufuatilia mwenendo wa uwekezaji wa Serikali, Kamati ilitaka kujiridhisha na mwenendo huo kwa kipindi cha miaka Mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 mpaka mwaka wa fedha 2020/2021. Kamati ilibaini kuwa thamani ya uwekezaji wa Serikali ilikuwa ikiongezeka kila

2 NOVEMBA, 2022

mwaka kama inavyoonekana kwenye *graph* Namba 2.1 kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, makusanyo halisi hadi kufikia Juni, 2021 yalikuwa ni Shilingi 637,660,804,553.34. Kiasi hicho ni asilima 69 ya lengo. Kwa sababu hiyo tunaweza kusema kuwa kwa kigezo cha makusanyo yasiyokuwa ya kikodi, ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma umefikia asilimia 69. Uchanganuzi wa aina ya makusanyo unaonekana kwenye *graph* Namba 2.4 ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi zaidi wa aina ya makusanyo ya mapato yaliyopatikana kutokana na mitaji ya umma ulifanyika ili kutoa picha halisi. Kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu naomba kufafanua aina hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa gawio. Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, gawio la kiasi cha shilingi bilioni 308 lilipatikana. Kiasi hicho kilikuwa tofauti na matarajio ya makusanyo ya gawio ambayo yalikuwa ni shilingi bilioni 408.4. Tofauti hiyo ni asilimia 24 ya makadirio ya gawio na kipimo kinachoonesha kuwa ufanisi wa mitaji umefikia asilima 75.61.

Mheshimiwa Spika, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi. Jumla ya shilingi bilioni 395.4 zilikusanywa kutokana na mchango wa mapato ghafi ya mashirika na taasisi za Serikali. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, mapato halisi yalikuwa shilingi bilioni 202.2. Kiasi hicho ni asilimia 51 ya lengo.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, marejesho ya *TTMS*. Msajili wa Hazina alipanga kukusanya shilingi bilioni 15 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2021 ikiwa ni marejesho ya *TTMS*. Lengo hilo ni ongezeko kwa asilimia 22.7 ukilinganisha na mpango wa kukusanya Shilingi Bilioni 11.6 kwa mwaka unaoishia Tarehe 30 Juni, 2020. Kwa takwimu hizo, ufanisi wa mtaji uliotumika katika kuwekeza kwenye mtambo wa *Telecommunication Traffic Management System* ulitarajia kuongezeka kwa asilima 22.7.

Mheshimiwa Spika, makusanyo halisi kutoka mtambo wa *TTMS* kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yalikuwa ni Bilioni 10.3 ikilinganishwa na makusanyo ya Shilingi Bilioni 12.1 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mwenendo huo wa makusanyo unaonesha kuwa, ingawa ufanisi wa mtaji uliotumika katika mtambo wa *TTMS* ulitarajiwa kuongezeka kwa asilimia 22.7, hali halisi ilionyesha kuwa ufanisi ulishuka kwa asilimia 14.9.

Mheshimiwa Spika, rejesho la riba na mikopo. Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipanga kukusanya marejesho ya mikopo kwa kiasi cha Shilingi Bilioni 4.7. Hadi kufikia mwezi Juni, 2021, Msajili wa Hazina alikuwa amekusanya Bilioni 19.32. Kiasi hicho ni ziada ya lengo kwa asilimia 311.1. Ongezeko hilo linatokana na Mamlaka ya Bandari Tanzania kulipa rejesho kwa kiasi ambacho hakikuwekwa kwenye lengo la makusanyo. Hali hii inaonesha kuwa kuna haja ya kuangalia upya vigezo vya uwekaji wa malengo ya makusanyo ya rejesho la mikopo kwa kuwa mikopo hiyo ni kwa maslahi ya ufanisi wa mitaji ya umma.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa utendaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Umma zinazotumia mitaji ya umma. Zaidi ya kuchambua ufanisi wa mitaji, Kamati ilichambua utendaji wa taasisi na Mashirika ya Umma ili kujiridhisha kama uwekezaji katika mashirika hayo na taasisi hizo unaweza kuwa na tija. Matokeo ya uchambuzi huo yalionesha mambo yafuatayo: -

- (1) Mheshimiwa Spika, Taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi. Kamati imebaini kuwa Taasisi nyingi na Mashirika ya Umma huchelewa kupata Bodi. Zipo baadhi ya Taasisi zinazozidi kipindi cha mwaka mmoja bila kuwa na bodi jambo ambalo linaloathiri uamuzi na uendeshaji wa mitaji ya umma kwenye mashirika hayo.
- (2) Mheshimiwa Spika, changamoto ya kupata vibali vya kuajiri. Utaratibu wa Sekretarieti ya Ajira kuchakata ajira zote katika sekta ya umma unaathiri upatikanaji wa wataalam wanaohitajika katika sekta na mashirika yanayotumia mtaji wa umma kujiendesha. Kwa utaratibu huo mahitaji ya kujiendesha kibiashara hayapati uzingatiaji mzuri kutokana na utaratibu wa ajira katika Sekretarieti ya Ajira. Hali hiyo inahitaji kuangaliwa ipasavyo na ikibidi kurekebishwa ili mitaji ya umma itumike kwa ufanisi kwenye mashirika na taasisi.
- (3) Mheshimiwa Spika, uwezo wa SGR kuuzidi uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam. Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha mtaji kwenye ujenzi wa reli ya kiwango cha SGR. Mradi huo utakapokamilika, SGR

2 NOVEMBA, 2022

itakuwa na uwezo wa kubeba mizigo kwa takribani tani 10,000 kwa safari. Sehemu kubwa ya mizigo hiyo inatarajiwa kutoka Bandari ya Dar es Salaam ambayo haina uwezo wa kuingiza na kupakua kiasi hicho cha mzigo. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuongeza ufanisi kwa kuongeza gati katika Bandari ya Dar es salaam na ujenzi wa bandari nyingine.

- (4) Mheshimiwa Spika, kiasi kikubwa cha mikopo chechefu kwa baadhi ya benki zenye mitaji ya umma. Ufuatiliaji wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya taasisi zinakabiliwa changamoto ya kiasi kikubwa cha mikopo chechefu (*non-performing loans*). Mfano wa Taasisi hizo ni Benki ya Rasilimali Tanzania (*Tanzania Investment Bank*) na Benki ya Tanzania (*Commercial Bank*). Kwa matokeo kuna umuhimu wa kutathmini madeni ya mashirika hayo na kuangalia namna ya kuyaondoa kwenye vitabu vya benki bila kuathiri ulipaji wa mikopo inayolipika (*performing loans*).
- (5) Mheshimiwa Spika, upungufu mkubwa wa mtaji kwa ATCL. Kamati imebaini kuwa ATCL inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mtaji. Kwa kampuni sasa inalazimika kukodi ndege kwenye Wakala wa Ndege za Serikali (*TGFA*) hali inayotokana na TGFA kuwa mmiliki wa ndege zote 11 zinazotumiwa na ATCL. Kwa hali hiyo kuna umuhimu wa kuhamisha umiliki wa ndege hizo kwa ATCL.

2 NOVEMBA, 2022

- (6) Mheshimiwa Spika, kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*Tanzania Agricultural Development Bank*). Taarifa inaonesha kwamba, mwaka 2021 Serikali ilijitahidi kuipatia TADB kiasi cha Shilingi Bilioni 208 kama mtaji. Ufuatiliaji wa ufanisi wa mtaji umeonesha kuwa licha ya jitihada hizo, bado kiasi cha mtaji wa kutosha kinahitajika TADB. Kwa ahadi ya awali ya Serikali, Benki hii ilitarajiwa kuwa na mtaji wa Shilingi Bilioni 706. Mtaji huo ungeiwezesha TADB kuongeza wigo kuwafikia wahitaji wengi zaidi. Kwa mantiki hiyo, bado juhudi za Serikali za kuongeza mtaji kwa Benki hii zinahitajika.
- (7) Mheshimiwa Spika, kuathirika kwa kilimo cha pamba kutokana na maelekezo ya Serikali Mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya soko la dunia. Wanunuzi wa pamba kushindwa kulipwa kikamilifu hasara waliyoipata kutokana na uamuzi na maelekezo yaliyotolewa na Serikali mwaka 2019 kwa pamba kununuliwa kwa bei ya juu kuliko bei ya Soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Makubaliano yalikuwa kuwa wanunuzi wanunue pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya Soko kwa makubaliano kuwa hasara yoyote itakayopatikana kwa wanunuzi wa pamba, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Benki ya Tanzania itaifidia. Uamuzi huu ulileta hasara na hadi sasa hasara hiyo ni Shilingi bilioni 21.8 kwa wanunuzi wa pamba.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya serikali ya kuzingatia maslahi ya umma kutokana na uamuzi wake, maelekezo hayo yameathiri sekta ya pamba ikiwepo na utendaji wa Bodi ya Pamba. Hali hiyo ni dosari katika misingi ya biashara na ufanisi wa mtaji unaotumiwa na wanunuzi wa pamba, pia inavuruga mantiki ya Bodi na manufaa yake kwa wakulima wa pamba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na mapendekezo, uchambuzi wa hali ya mitaji ya umma na utendaji wa taasisi na mashirika yanayotumia mitaji ya umma, umejenga msingi wa mtazamo wa Kamati hii kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma. Mtazamo huo ni maoni ambayo ni moyo wa mapendekezo yanayotolewa kwa njia ya hoja. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:

- (a) Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya kikodi kutokana na uwekezaji wa mitaji ya umma unastahili kufanyiwa tathmini;
- (b) Ahadi zinazotolewa na serikali kwa mashirika au taasisi ambako serikali imewekeza mitaji zinapaswa kutekelezwa;
- (c) Utendaji na uendeshaji wa Mashirika ya umma au taasisi ambazo zina mitaji ya serikali unahitaji kuangaliwa vizuri na kupangiliwa inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapendekezo; baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kutoa Hoja kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kama ifuatavyo: -

2 NOVEMBA, 2022

- i. KWA KUWA, ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma unategemea pia uzingatiaji wa misingi ya uendeshaji bora, ambayo inahitaji mashirika na taasisi ziwe na Bodi; na

KWA KUWA, kutokuwa na Bodi kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kuteuliwa kwa wajumbe baada ya Bodii zilizokuwepo kumaliza muda wake ni jambo linaathiri uendeshaji na upatikanaji wa tija ya mitaji katika mashirika na taasisi zinazohusika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

- (a) Serikali ianze mchakato wa upatikanaji wa Wajumbe wa Bodi kwa wakati;
 - (b) Utaratibu uandaliwe ili wajumbe wa Bodi wawe wanaingia kwa vipindi tofauti kwa lengo la kuzuia Bodi kukosa wajumbe pale inapokamilisha muda wake;
 - (c) Mbadala wa “a” na “b”, Marekebisho ya Sheria yafanyike ili Bodi inapomaliza muda wake iendelee kutekeleza majukumu yake mpaka pale bodi mpya itakapopatikana
- ii. Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya kupata vibali vya kuajiri.

KWA KUWA, ajira katika mashirika na taasisi ni mchakato unaowezesha upatikanaji wa wataalamu

2 NOVEMBA, 2022

kwa ajili ya uendeshaji wa mitaji ya umma kwenye mashirika na taasisi hizo, lakini utaratibu wa vibali na mchakato wa ajira kupitia sekretarieti ya ajira umekuwa na changamoto; na

KWA KUWA, Changamoto hiyo inaathiri ufanisi wa mitaji ya umma pamoja na tija ya kuanzishwa kwa mashirika hayo kutokana na kukosa watumishi wanaostahili kwa wakati hata inapokuwa na uwezo wa kuwalipa yenyewe;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke utaratibu wa kuzipatia taasisi zinazojiendesha kibiashara vibali vya kuajiri wenyewe ajira za moja kwa moja.

- iii. Mheshimiwa Spika, uwezo wa SGR kuzidi uwezo wa Bandari;

KWA KUWA, Uwekezaji unaofanywa na Serikali katika Ujenzi wa Reli ya SGR utawezesha Usafirishaji wa mizigo takribani tani 10,000 kwa safari kwa mizigo ambayo kwa sehemu kubwa inatoka Bandari ya Dar es salaam, lakini Bandari hiyo haina uwezo wa kuingiza na kupakua kiasi hicho cha mzigo; na

KWA KUWA, kukosekana kwa mizigo ya kusafirisha kwa kadiri ya uwezo wa reli kutokana na uwezo mdogo wa Bandari ni changamoto inayoweza kuathiri tija ya mitaji inayowekezwa kwenye Bandari na SGR, lakini pia inaweza kutatuliwa kwa kujenga Bandari ya Bagamoyo,

2 NOVEMBA, 2022

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba;

- (a) Serikali inapaswa kuharakisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo; na
- (b) Serikali isimamie Kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kuongeza Gati za kisasa katika Bandari ya Dar es Salaam lengo la yote haya ni kusaidia Bandari.

iv. Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa Shirika la Taifa la Maendeleo – *NDC*;

KWA KUWA, manufaa ya mradi wowote wa uwekezaji yanategemea kuanza kwa mradi lakini mradi wa mchuchuma na liganga unachukua muda mrefu katika hatua za majadiliano yanayoratibiwa na Kamati ya Majadiliano ya Serikali (*GNT*); na

KWA KUWA, Serikali imefanya mabadiliko ikiwemo kuipatia Bodi mpya ya Wakurugenzi pamoja na menejimenti; na

KWA KUWA, kutokukamilika kwa majadiliano ambayo yanaendelea kwa muda mrefu sana tangu kuanza ni jambo linalochelewesha manufaa ya mradi huo, kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa mazungumzo katika Timu ya Majadiliano ya Taifa (*GNT*) yanafikia mwisho au yapelekwe *NDC*, lengo likiwa ni kupata tija iliyokusudiwa katika miradi hii.

2 NOVEMBA, 2022

- v. Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo chechefu (*non-performing loans*)

KWA KUWA, imebainika kuwa baadhi ya taasisi kama vile Benki ya Maendeleo Tanzania (*Tanzania Investment Bank*) na Benki ya Tanzania Commercial Bank zinakabiliwa changamoto ya kuwa na kiasi kikubwa cha mikopo chechefu (*non-performing loans*); na

KWA KUWA, hali hiyo inaathiri mizania ya vitabu vya taasisi, jambo ambalo ni hatari kwa misingi ya kibiashara na uendeshaji wa taasisi zinazotumia mitaji ya umma,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathimini ya madeni hayo na kuangalia namna ya kuyaondoa kwenye vitabu vya Benki, bila kuathiri ulipaji wa mikopo inayolipika (*performing loans*).

- vi. Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa mtaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*);

KWA KUWA, *ATCL* inakabiliwa na changamoto ya mtaji hasi na changamoto ya uendeshaji wa biashara kutokana na utaratibu wa kukodisha ndege kutoka kwa *TGFA*; na

KWA KUWA, kwa kuwa utaratibu huo unaongeza *payables* katika vitabu vya *TGFA*;

2 NOVEMBA, 2022

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iitake Wakala ya Ndege za Serikali Tanzania (TGFA) kuharakisha taratibu za kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kurudisha ndege kwa ATCL.

- vii. Mheshimiwa Spika, kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – TADB;

KWA KUWA, TADB ambayo ni Benki pekee inayohusika moja kwa moja na shughuli za kilimo lakini haijapatiwa mtaji wa kutosha wa kuendana na nia ya serikali ya kuongeza tija kwenye kilimo, kuleta mageuzi ya kilimo na kulisaidia taifa kufikia usalama wa chakula; na

KWA KUWA, pamoja na jitihada za Serikali za kuipatia TADB kiasi cha Shilingi bilioni 208 mwaka 2021, bado kuna ahadi ya Serikali ambayo kama ingetekelezwa benki hii ingekuwa na mtaji wa Shilingi bilioni 760;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali iendelee kuongezea TADB mtaji kwa lengo la kuongezea ufanisi na tija katika Sekta ya Kilimo.

- viii. Mheshimiwa Spika, kuhusu kuathirika kwa kilimo cha pamba kutokana na maelekezo ya Serikali ya mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya soko la dunia;

KWA KUWA, Agizo la Serikali lililoitaka pamba kununuliwa kwa bei ya juu zaidi ya bei ya soko la dunia limeathiri uwezo wa wanunuzi wa pamba kwa kiasi cha

2 NOVEMBA, 2022

Shilingi bilioni 21.8, kiasi ambacho Serikali iliahidi kufidia deni hilo; na

KWA KUWA, deni hilo limeathiri taswira ya Bodi ya Pamba kwa wakulima na kuongeza changamoto katika biashara ya kilimo cha pamba.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mkakati wa kulipa fedha hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo ya kiti chako, ikiwa ni pamoja na ushauri na miongozo kwa kipindi chote cha ufuatiliaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba, kunakuwa na usimamizi bora katika taasisi na mashirika ya umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa taifa.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumshukuru Msajili wa Hazina, Ndugu Benedicto Mgonya kwa ushirikiano wake wa dhati alioutoa kwa Kamati na kushauri namna bora ya kuzifanya taasisi na mashirika ya umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija

2 NOVEMBA, 2022

kwa taifa. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, chini ya uratibu wa Mkurugenzi Idara ya Uwekezaji Bi. Lightness Mauki kwa ushirikiano mkubwa na wa karibu na Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe ila kulingana na changamoto ya muda, naomba nisiwataje lakini majina yao yaingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nanelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa, ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Pia natoa shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu vema shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi wa Idara, Ndugu Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndugu Zainabu Mkamba, Ndugu Mwajuma Ramadhan na Ndugu Charles Wanyancha, pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Modesta Kipiko.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru pia Wanasheria wa Ofisi ya Bunge, Ndugu Elizabeth Malongo na Ndugu Praisegod Lukio pamoja na Kitengo cha Taarifa Rasmi za

2 NOVEMBA, 2022

Bunge kwa utaalumu wao wakati wote wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na taasisi na mashirika ya umma. Maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati yanalenga kuishauri Serikali katika eneo la uwekezaji wa mitaji ya umma ili uwekezaji huo uwe wa ufanisi na ulete tija kwa taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma, na kuijadili ikiwa na Maoni na Mapendekezo ili kuamua na kuiwezesha Serikali kuyafanyia kazi maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI
WA MITAJI YA UMMA KUHUSU UWEKEZAJI WA MITAJI YA
UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI
SEHEMU YA KWANZA**

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Uwekezaji wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, na kuliomba Bunge liipokee na kuijadili Taarifa hii. Lengo ni kulijulisha Bunge lako tukufu, iwapo uwekezaji

2 NOVEMBA, 2022

wa mitaji ya umma una ufanisi na kwamba umezingatia Taratibu, Sheria na Miongozo mujarabu ya Biashara au vinginevyo, kama ilivyofafanuliwa katika Kifungu cha 12 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Kwa madhumuni hayo, Taarifa hii inagusa mitaji ya umma kwenye vitega uchumi (Investments) vya Serikali katika taasisi na mashirika ya umma pamoja na Kampuni ambako Serikali ina hisa chache. Kipindi cha Uwekezaji kinachoripotiwa ni kuanzia Mwezi Julai, 2020 hadi Juni, 2021. Msingi wa yaliyomo kwenye Taarifa hii ni Taarifa ya Utendaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ya Msajili wa Hazina, mwenye jukumu la kusimamia uwekezaji na mali zingine za Serikali. Uwekezaji huo unafanyika katika taasisi na mashirika ya umma pamoja na kwenye Kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Ili kuliwezesha Bunge hili kufuatilitia mtiririko wa Taarifa pamoja na kurahisisha misingi ya uamuzi wa Bunge juu ya hoja hii ya Kamati, naomba kubainisha muundo wa Taarifa kwa kutaja sehemu za taarifa na maudhui yake ya jumla. Kimuundo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Tatu na kumalizia kwa shukurani na kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza inayohusu maelezo ya Utangulizi inahusu msingi wa kazi za Kamati kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma na wigo wa jukumu hilo. Aidha, sehemu hii inabainisha njia au mbinu zilizotumika kufuatilia ufanisi wa mitaji ya umma. Sehemu ya Pili

2 NOVEMBA, 2022

inafafanua misingi ya ufuatiliaji wa kibunge wa mitaji ya umma, vigezo vilivyozingatiwa na kueleza matokeo ya ufuatiliaji huo. Kwenye Sehemu ya Tatu Kamati inabainisha maoni yake ambayo ni mtazamo wa jumla kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma unaotokana na mambo yaliyobainika wakati wa kufuatilia ufanisi wa mitaji ya umma. Sehemu hii pia inatoa mapendekezo kwa mfumo wa hoja ulioelekezwa na Kanuni ya 61 (3) ya Kanuni za Bunge.

1.3 Msingi na wigo wa Kazi za Kamati na Njia zilizotumika

Mheshimiwa Spika, Msingi wa kazi, wigo wa majukumu na njia za utekelezaji vinasaidia kusadikisha (*win credence*) taarifa na kuiwezesha itumike kufanya uamuzi. Ukweli huo umesukuma nia ya kutambulisha msingi, wigo na njia zilizotumika kama ifuatavyo:-

1.3.1 Msingi wa kazi za Kamati kufuatilia Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Ili kubainisha uthabiti wa matokeo ya kazi inayoripotiwa katika taarifa hii, naomba kutaja msingi wa kazi za Kamati ya kufuatilia mitaji ya Umma. Msingi huo unaelezwa katika Kifungu cha 12 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kifungu hicho kinabainisha kwamba kazi za Kamati zitatokana na taarifa zinazohusu uwekezaji wa mitaji ya umma katika mashirika ya Umma na Kampuni ambazo serikali ina hisa.

1.3.2 Wigo (Scope) wa Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wigo wa kazi (**Scope of work**) unaweka ukomo wa matarajio ya matokeo, naomba kubainisha mipaka ya kazi ya Kamati kufuatilia uwekezaji

2 NOVEMBA, 2022

wa mitaji ya umma. Mipaka hiyo imewekwa na Kifungu cha 12 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kifungu hicho kinaifunga kazi ya Kamati kwenye masuala makuu mawili. Masuala hayo yanahusu ufanisi na uzingatiaji wa misingi ya kibiashara kwa mitaji ya umma inayowekezwa katika vitega uchumi vya taasisi na mashirika ya umma pamoja na hisa kwenye Kampuni za biashara. Kwa msingi huo, Kamati ilijielekeza kwenye kubaini iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma umefanyika kwa ufanisi na kwamba uwekezaji huo umezingatia taratibu, sheria na miongozo inayofaa.

1.3.3 Njia zilizotumika

Mheshimiwa Spika, kubainisha njia zilizotumika ni miongoni mwa masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu uwasilishaji wa Taarifa za Kamati Bungeni. Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, imetaka Taarifa hii ibainishe njia au mbinu zilizotumika kutekeleza kazi ambayo matokeo yake yanaripotiwa. Kamati inaamini kuwa, ubainishaji wa njia zilizotumika katika ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma, ni jambo linaloweza Bunge kuhakiki uthabiti (reliability) na ustahiki (validity) wa matokeo ya kazi iliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, Katika kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma Kamati ilitumia njia kuu zifuatazo:

(a) Uchambuzi wa Masharti ya Sheria inayohusika na uwekezaji uliofanyika. Lengo ni kubaini muktadha wa uendeshaji wa mitaji ya umma iliyowekezwa kwenye kila kitega uchumi na kuona kama kuna uzingatiaji wa sheria, taratibu na miongozo mujarabu;

2 NOVEMBA, 2022

(b) Kufanya mahojiano na menejimenti na Bodi za mashirika ya Umma ambayo yanatumia mitaji ya umma. Lengo ni kuthibitisha usahihi wa hali ya mitaji ya umma kabla ya kutoa taarifa Bungeni. Njia hii pia iliongeza undani wa maelezo kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma yanayohusika;

(c) Kupokea na kuchambua Taarifa za Msajili wa Hazina (TR) kuhusu hali ya jumla ya mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma au kwenye Kampuni ambapo serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma. Lengo ni kubaini chumo linalopatikana kutokana na mitaji ya umma (**Returns on investment**). Aidha, njia hii iliwezesha kubaini maslahi ya umma yaliyopo katika matumizi ya mitaji ya umma;

(d) Kushuhudia hali ilivyo kwenye baadhi ya miradi ya uwekezaji inayoendeshwa na taasisi na mashirika ya umma ambayo yanatumia mitaji ya umma. Lengo ni kubaini mandhari ya mitaji ya umma kwenye miradi hiyo na kujiridhisha kuhusu hali halisi uwandani (**In the field**).

1.4 Majumuisho ya Sehemu ya Kwanza

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla sehemu ya kwanza ya Taarifa hii imetambulisha maudhui na mantiki yake, mtiririko wa taarifa na msingi wake na kuahidi mambo yatakayojitokeza kwenye taarifa hii. Kubwa la kwenda nalo katika sehemu ya pili ya taarifa hii, ni madhumuni ya taarifa kulijulisha Bunge kuhusu uwekezaji wa mitaji ya Umma kwenye taasisi na mashirika ya umma na kwenye vitega uchumi ambapo Serikali inamiliki hisa.

2 NOVEMBA, 2022

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoieleza katika sehemu ya kwanza, Madhumuni ya kuripoti Bungeni leo hii, ni kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi kuhusu matokeo ya ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Ili kufanikisha azma hiyo, sehemu hii inafafanua shughuli za Kamati za kufuatilia mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma na kwenye vitega uchumi ambapo kuna hisa za serikali. Aidha, Taarifa hii inalijulisha Bunge kuhusu matokeo ya kazi ya Kamati kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma. Ufafanuzi huo umegawanyika katika sehemu ndogo mbili: Sehemu ndogo ya kwanza inatoa maelezo kuhusu hali ya mitaji ya umma ilivyo nchini na sehemu ndogo ya pili inahusu mambo mbalimbali yaliyobainika kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma.

2.2 Uchambuzi wa Hali ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa hali ya Uwekezaji wa mitaji ya Umma ulihitaji unatokana na msingi wa jukumu la Bunge kufuatilia uwekezaji huo. Ufuatiliaji huo wa kibunge ulihitaji uelewa wa dhana ya Mitaji ya Umma na muundo wake ulivyo. Aidha, mbinu na vigezo vinavyoweza kutumika kuhakiki ufanisi wa mitaji ya umma kwa utaratibu wa kibunge ni mambo yanayofanikisha uchambuzi. Kwa kutambua na kuthamini mambo hayo, Taarifa hii inatoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

2.2.1 Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji wa mitaji ya umma ni dhana yenye maana maalumu katika suala la ufuatiliaji wa Kibunge. Kwa fasili ya kawaida, Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni hatua za serikali kutumia rasilimali za umma kama vile fedha, ardhi, majengo na dhamana nyingine katika taasisi na mashirika ya umma. Uwekezaji huo unajumuisha ununuzi wa hisa kwenye kampuni binafsi kwa lengo la kupata gawio, kulinda thamani, kutoa huduma au kulinda maslahi ya umma kwenye kampuni zinazohusika. Kwa maana hiyo, Rasilimali zote zinazotumiwa na serikali kwenye vitega uchumi mbalimbali ndizo zinazotambulika kuwa mitaji ya umma.

2.2.2 Msingi wa Shughuli za Kibunge zinazohusu Kufuatilia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu kuwa Serikali, kwa maana ya mamlaka ya utendaji (Executive) inao wajibu wa kutumia rasilimali za umma kuwezesha ustawi wa watu nchini na maendeleo ya taifa. Katika kutekeleza wajibu huo, Serikali inapowekeza kwa kutumia mitaji ya Umma, inaendelea kuwa na jukumu la kusimamia uendeshaji wa mitaji hiyo na kuona kama yanapatikana manufaa ya uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, linao wajibu wa kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma. Aidha, jukumu la kutunga sheria zinazoweka masharti ya uwekezaji huo, hutekelezwa na Bunge. Zaidi ya hivyo, Bunge huidhinisha matumizi ya fedha za umma kwa ajili ya uendeshaji wa

shughuli za Serikali. Fedha hizo ni pamoja na fedha zinazotumika kwenye uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimwa Spika, Kwa taswira hiyo ya uendeshaji wa nchi Bunge lilitunga Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 370. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, pamoja na Sheria nyingine kama vile, Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257, Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 Sura ya 439, na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2004, Msajili wa Hazina anawajibika kuhodhi uwekezaji na mali zote za umma. Wajibu huo unagusa pia uwekezaji wa hisa katika taasisi na mashirika ya umma pamoja na Kampuni ambako serikali inamiliki hisa au ina maslahi.

2.2.3 Muundo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma nchini

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inahusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Ufafanuzi wake umejengwa kwenye muktadha wa muundo unaotumika nchini wa matumizi na usimamizi wa mitaji ya umma. Serikali kwa maana ya mamlaka ya Utendaji nchini (Executive) ndiyo iliyopewa dhamana ya kutumia mitaji ya umma kwa maslahi ya nchi. Bunge (legislature) limepewa jukumu la kutunga sheria zinazoweka masharti ya matumizi ya mitaji hiyo pamoja na kusimamia uwekezaji wa mitaji ya umma.

2.2.4 Muundo wa Utekelezaji wa jukumu la Bunge kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma

Mheshimiwa Spika, Bunge ambalo kikatiba, linayo mamlaka ya kipekee (Exclusive cognisance) ya kujipangia utaratibu, limetumia haki iliyotolewa na Ibara ya 89 na ya 96 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu utungaji wa Kanuni za Bunge na uundaji wa Kamati za Bunge, na kuweka utaratibu uliopo wa kufuatilia mitaji ya umma.

2 NOVEMBA, 2022

Utaratibu huo ndio unaoiruhusu Kamati hii kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma na kuripoti Bungeni leo hii.

Mheshimiwa Spika, Utaratibu wa kufuatilia tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma unafanana kimalengo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera katika sekta mbalimbali. Hata hivyo, kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake kwa ufanisi, ufuatiliaji huo unaendana na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa msingi huo, naomba kukupongeza kwa dhati kwa uamuzi wako wa kuelekeza Taarifa hii pamoja na taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuingia katika mkutano mmoja.

Mheshimiwa Spika, Uamuzi wako huu, utaliwezesha Bunge kuzingatia baadhi ya mambo yanayojitokeza kwenye Taarifa hii na kuwa msingi wa ushauri wakati Bunge linapokaa kama Kamati ya Mipango. Naomba kukiri kwamba, uongozi wako unaliinua Bunge kwa viwango vya ufanisi. Bila shaka chini ya uongozi wako, Bunge litaendelea kutoa ushauri bora kwa serikali na kutunga sheria nzuri zinazoisaidia nchi, hususan katika uwekezaji wa mitaji ya umma.

2.2.5 Vigezo vinavyozingatiwa

Mheshimiwa Spika, Kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma ni shughuli ya kibunge iliyowekewa masharti katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kifungu cha 12 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kinaonesha masharti na mipaka kwa kutaja mambo makuu mawili. Miongoni mwa mambo hayo ni ufanisi katika uwekezaji wa mitaji ya umma. Jambo la pili ni uzingatiaji wa taratibu na Sheria pamoja na miongozo ya biashara bora.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, vigezo vilivyotumika wakati wa uchambuzi wa taarifa za uwekezaji ni mambo yanayopima ufanisi wa mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma. Kigezo kingine ni kipimo cha ufanisi wa mitaji kwenye kampuni ambapo serikali ina umiliki wa hisa. Orodha ya mambo hayo kwa ujumla ni kama ifuatavyo:-

(a) Fungu linalopatikana kutokana na faida baada ya uwekezaji wa mitaji ya umma (Gawio);

(b) Makusanyo ya Mchango itokananyo na 15% ya mapato ghafi kutoka Taasisi na mashirika ya umma yanayostahili kuchangia kwa mujibu wa Sheria;

(c) Michango kutokana na makusanyo ya ziada na michango mingine; na

(d) Marejesho ya Mikopo na Riba.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo ni viashiria vinavyosaidia kubaini, iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma unafanyika kwa ufanisi. Aidha, uchanganuzi wa kina wa vigezo hivyo, unasaidia kubaini kiwango cha uzingatiaji wa miongozo na misingi ya biashara. Nalihakikishia Bunge hili kuwa kila mara Kamati ilipochambua Taarifa za uwekezaji, mambo hayo yaliongoza uchambuzi.

2.2.6 Utaratibu uliotumika kufanikisha uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma ni jukumu linalohitaji kufanyika kwa wepesi na ufanisi ili kuwezesha tija iliyokusudiwa. Mbinu kuu

2 NOVEMBA, 2022

zilizotumika kurahisisha jukumu hilo kwa namna iliyofanikisha matokeo ni kama ifuatavyo:

(a) Kuchambua Taarifa ya Utendaji wa Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Mantiki ya kufanya hivyo inatokana na kuzingatia masharti ya Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 370; na

(b) Kuchambua Taarifa za uwekezaji za taasisi na mashirika ya umma yanayotumia mitaji ya umma. Mbinu hii iliwezesha Kamati kuoanisha na matokeo ya uchambuzi wa taarifa jumuiifu iliyoandaliwa na Msajili wa Hazina.


Mheshimiwa Spika, mbinu hizo zimewezesha upatikanaji wa matokeo ya uchambuzi yanayoripotiwa katika taarifa hii. Niliombe Bunge lako tukufu liijadili Taarifa hii na hatimaye kupitisha Mapendekezo ya Kamati kuwa maazimio ya Bunge kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma.

2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Hali ya Mitaji ya Umma nchini

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi uliofanyika ulizingatia thamani ya uwekezaji uliokuwa ukisimamiwa na Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina ilionesha kuwa kiwango cha uwekezaji wa Serikali ndani na nje ya nchi kilifikia shilingi **trillioni 67.95**. Katika kufuatilia mwenendo wa uwekezaji wa Serikali ili kujua hali ya mitaji ya umma, Kamati ilitaka kujiridhisha na mwenendo huo kwa kipindi cha miaka mitano. Yaani kuanzia 2016/2017 hadi 2020/2021 na kubaini kuwa thamani ya uwekezaji wa Serikali ilikuwa ikiongezeka kila mwaka kama inavyoonekana katika grafu Na. 2:1.

2 NOVEMBA, 2022

Grafu Na. 2:1 Taswira ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma



Chanzo: *Ukokotozi wa Kamati kutokana na Takwimu za OMH kwenye Taarifa ya Utendaji kwa mwaka 2020/2021*

Mheshikiwa Spika, Mwenendo wa Uwekezaji kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 unaonesha kuwa thamani ya uwekezaji ilikuwa ikiongezeka lakini kwa kiwango cha ongezeko linalopungua (Increasing at a decreasing rate). Takwimu zilionyesha kuwa thamani ya uwekezaji kwa mwaka 2016/2017 ilikuwa ikipanda hadi kufikia mwaka 2020/2021. Hata hivyo, ongezeko linalopungua ni ishara kuwa kwa siku zijazo thamani hiyo inaweza kushuka. Taswira ya kupungua kwa ongezeko hilo inaonekana katika Grafu Na. 2:2.

2 NOVEMBA, 2022

Grafu Na. 2:2 Mwenendo wa Asilimia ya Ongezeko la Thamani ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma



Chanzo: Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka 2020/2021


Mheshimiwa Spika, baada ya kuangalia uchambuzi wa mwenendo wa jumla, Kamati ilitaka kujiridhisha na ufanisi wa mitaji katika uwekezaji huo. Jambo kuu katika kutathimini uwekezaji wa mitaji ya umma lilikuwa ni uchanganyuzi wa Makusanyo ya Mapato yasiyo ya Kodi.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa Kamati uliwezesha kubaini kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ikiwa ni mapato yasiyo ya kikodi kutoka mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache. Ilibainika kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, jumla ya shilingi **billion 930.30** zilikadiriwa kukusanywa. Mapato hayo yanainishwa katika

2 NOVEMBA, 2022

makundi makuu matano kama inavyoonekana kwenye Grafu Na. 2:3.

Grafu Na. 2:3 Kiasi cha Mapato yasiyo ya Kodi kilichokadiriwa kukusanywa




Chanzo: Taarifa ya Utendaji wa Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, makusanyo halisi ya mapato yasiyo ya kikodi hayakufika kiasi kilichokadiriwa. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Makusanyo ya mapato yasiyo ya kikodi kutoka taasisi na mashirika ya umma pamoja na kampuni ambapo serikali ina umiliki wa hisa chache yalikuwa ni shilingi **637,660,804,553.34**. Kiasi hicho ni **asilima 69** ya lengo. Kwa sababu hiyo tunaweza kusema kuwa kwa kigezo cha makusanyo yasiyo ya kikodi, ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma umefikia **asilimia 69**. Uchanganuzi wa aina za makusanyo unaonekana katika Grafu Na. 2:4.

2 NOVEMBA, 2022

Grafu Na. 2:4 Kiasi cha Mapato yasiyo ya Kodi kilichokusanywa



Chanzo: Taarifa ya Utendaji wa Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi zaidi wa aina za makusanyo ya mapato yaliyopatikana kutokana na mitaji ya umma ulifanyika ili kutoa picha halisi. Kwa manufaa ya Bunge lako tukufu naomba kufafanua aina hizo kama ifuatavyo:-

2.3.1 Ukusanyaji wa Gawio

Mheshimiwa Spika, Gawio ni miongoni mwa manufaa inayopata serikali kutokana na kutumia fedha za umma kwenye uwekezaji. Mapato hayo yanayotokana na faida katika kitegauchumi ni miongoni mwa mambo yanayoweza kubainisha ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma. Takwimu za Msajili wa Hazina zinaonesha kuwa kwa mwaka

2 NOVEMBA, 2022

wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, gawio la kiasi cha shilingi **Bilioni 308.8** lilipatikana. Kiasi hicho kilikuwa tofauti na matarajio ya makusanyo ya gawio ambayo ni shilingi **Bilioni 408.4**. Tofauti hiyo ni **asilimia 24.39** ya makadirio ya gawio na ni kipimo kinachoonesha kuwa ufanisi wa mitaji umefikia **asilima 75.61**.

Mheshimiwa Spika, Vilevile, Kamati ililinganisha ukusanyaji wa gawio kwa kipindi cha 2020/2021 na mwaka 2019/2020. Kwa mwaka 2019/2020, Jumla ya kiasi cha sh. **Bilioni 300.2** kilikusanywa. Kiasi hicho kiliongezeka kwa **asilimia 2.2** hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021. Mfano wa mashirika na taasisi zilizoongeza kiasi cha gawio ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lililoongeza gawio kutoka Shilingi **1,000,000,000/-** hadi shilingi **1,205,000,000/=**.

2.3.2 Michango ya Asilimia 15 ya Mapato Ghafi

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) Sura ya 370 inaelekeza kwamba mashirika yasiyofanya biashara yatoe **asilimia 15** ya mapato ghafi (Gross Revenue) kwa mwaka na kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali (Consolidated Fund). Kwa kuzingatia masharti hayo ya Sheria kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipanga kukusanya shilingi **Bilioni 395.4** kutokana na mapato ghafi (Gross Revenue) ya mashirika na taasisi za Serikali. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, makusanyo halisi ya fedha hizo yalikuwa ni shilingi **Bilioni 202.2**. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 51** ya lengo lililokuwa limewekwa. Kwa maneno mengine kiasi hicho ni pungufu ya lengo kwa **asilimia 49**.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020, Lengo la makusanyo lilikuwa ni sh. **Bilioni 414.90** lakini makusanyo halisi yakawa ni shilingi Bilioni 289.10 ambayo ni **asilimia 70** ya lengo. Takwimu hizo zinaonesha kwamba Msajili wa Hazina alipunguza lengo kutoka shilingi **Bilioni 414.90** mwaka 2019/2020 hadi Shilingi **Bilioni 395.4** kwa mwaka 2020/2021. Kupungua huko kwa lengo ni sawa nakushuka kwa lengo kwa kima cha **asilimia 4.7**.

Mheshimiwa Spika, Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kwamba, matarajio kutoka kwenye ufanisi wa mitaji katika mashirika yanayostahili kuchangia yamepungua kwa **asilima 4.7**. Kwa maneno mengine, ufanisi wa mitaji katika eneo hilo ulitarajiwa kushuka kwa **asilimia 4.7**.

Mheshimiwa Spika, Ulinganifu wa makusanyo ya mchango kwenye Mfuko mkuu wa Hazina kati ya Mwaka 2019/2020 na mwaka 2020/2021 unaonesha kupungua kwa makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 27.8**. Hali hiyo inaonesha kwamba kiwango cha ufanisi kilichotazamiwa kushuka wakati wa kuweka lengo kimekuwa kidogo sana ikilinganishwa na uhalisia wa kupungua kwa ufanisi wa mitaji kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa Taasisi zilizochangia kwa kiwango kilichopungua ikilinganishwa na mchango kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iliyoshuka kutoka mchango wa **Sh. Milioni 300** kwa mwaka 2019/2020 hadi milioni 200 mwaka 2020/2021.

2.3.3 Marejesho ya TTMS

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Hazina amepewa jukumu la kuweka malengo ya kifedha kwa taasisi na mashirika ya Umma yanayotumia mtaji wa serikali. Katika kutekeleza jukumu hilo, Msajili wa Hazina alipanga kukusanya Shilingi **Bilioni 15** kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021. Lengo hilo ni ongezeko kwa **asilimia 22.7** ikilinganishwa na mpango wa kukusanya sh **Bilioni 11.6** kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2020. Kwa takwimu hizo ufanisi wa mtaji uliotumika katika kuwekeza kwenye Mtambo wa kuhakiki mawasiliano kwa njia ya simu (TTMS) ulitarajiwa kuongezeka kwa asilima **22.7**.

Mheshimiwa Spika, Makusanyo halisi ya mapato yasiyo ya kikodi kutoka Mtambo wa TTMS kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yalikuwa ni sh. **Bilioni 10.3** ikilinganishwa na makusanyo ya sh. **Bilioni 12.1** kwa mwaka 2019/2020. Mwenendo huo wa makusanyo unaonesha kuwa, ingawa ufanisi wa mtaji uliotumika katika mtambo wa TTMS ulitarajiwa kuongezeka kwa **asilimia 22.7**, hali halisi ilionyesha kuwa ufanisi ulishuka kwa **asilimia 14.9**.

2.3.4 Rejesho la Riba na Mikopo

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974, inairuhusu Serikali kutoa dhamana kwa taasisi na Mashirika ya Umma ili yaweze kukopa katika taasisi na Mashirika ya Fedha. Aidha Sheria hiyo inairuhusu Serikali kuchukua mikopo katika mashirika na taasisi za Fedha na kuzikopesha taasisi na mashirika ya umma na baadaye mikopo hiyo hurejeshwa.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Hazina amepewa jukumu la kufuatilia ulipaji wa mikopo inayostahili kulipwa. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Msajili wa Hazina alipanga kukusanya marejesho ya mikopo kwa kiasi cha sh. **Bilioni 4.7**. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, Msajili wa Hazina alikuwa amekusanya kiasi cha Sh. **Bilioni 19.32**. Kiasi hicho ni ziada ya lengo kwa **asilimia 311.1**. Ongezeko hilo linatokana na Mamlaka ya Bandari Tanzania kulipa rejesho kwa kiasi ambacho hakikuwekwa kwenye lengo la Makusanyo. Hali hii inaonesha kuwa kuna haja ya kuangalia upya vigezo vya uwekaji wa malengo ya makusanyo ya rejesho la mikopo kwa kuwa mikopo hiyo ni kwa maslahi ya ufanisi wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Msajili wa Hazina alipanga kukusanya jumla ya shilingi **Bilioni 4.7** ikiwa na marejesho ya mikopo. Lengo hilo ni sawa na lengo la makusanyo ya marejesho ya mikopo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Ingawa lengo la kiasi cha kukusanywa kililingana, lakini kwa uhalisia makusanyo halisi yalitofautina kati ya mwaka 2019/2020 na mwaka 2020/2021. Tofauti hiyo ya makusanyo imetokana na Urejeshaji wa Mikopo uliofanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania.

2.3.5 Ziada na Michango Mingine

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 370, inazitaka Taasisi au mashirika ya umma kuwasilisha **asilimia 70** ya kiasi cha ziada kilichobakia baada ya kuondoa gharama za uendeshaji na matumizi yanayoruhusiwa. Kwa kuzingatia masharti ya sheria hiyo, Msajili wa Hazina alipanga kukusanya kiasi cha sh. **Bilioni**

2 NOVEMBA, 2022

106.7 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lakini alikusanya sh. **Bilioni 96.8.**

Mheshimiwa Spika, Kiasi cha lengo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilipungua kwa **asilimia 10.2** ikilinganishwa na lengo la makusanyo la shilingi **Bilioni 118.8** kwa mwaka 2019/2020. Hata hivyo, kiasi cha makusanyo halisi kwa mwaka 2020/2021 kilipungua kwa **asilimia 38.14** ikilinganishwa na makusanyo ya sh. **Bilioni 156.5** cha Makusanyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla, mwenendo wa mapato yasiyokuwa ya kodi kutokana na uwekezaji, unaonesha kupungua kwa makusanyo hayo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Miongoni mwa sababu ni kupungua kwa taasisi zilizotoa gawio na kuathiri kiasi cha gawio ikilinganishwa na gawio lililopatikana kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kwa sababu hiyo, ipo mantiki ya kusisitiza tathmini inayoweza kubainisha uwezo wa Mashirika na Taasisi zote wa kutoa gawio na kuchangia katika Mfuko wa Serikali.

2.4 Matokeo ya Uchambuzi wa Utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma zinazotumia Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, zaidi ya kuchambua ufanisi wa mitaji, Kamati ilichambua utendaji wa taasisi na Mashirika ya Umma ili kujiridhisha kama uwekezaji katika mashirika na taasisi hizo unaweza kuwa na Tija. Matokeo ya uchambuzi huo yalionesha mambo yafuatayo:-

2.4.1 Taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Wakurugenzi ni chombo kikuu cha uamuzi katika Taasisi na Mashirika ya Umma katika

kufanikisha tija ya mitaji ya serikali katika mashirika hayo. Pamoja na hivyo, Kamati imebaini kuwa Taasisi nyingi na mashirika ya umma huchelewa kupata Bodi. Zipo baadhi ya taasisi zinazozidi kipindi cha mwaka mmoja bila kuwa na bodi jambo linaloathiri uamuzi na uendeshaji wa mitaji ya umma kwenye mashirika hayo.

2.4.2 Changamoto ya kupata vibali vya kuajiri

Mheshimiwa Spika, Utaratibu wa Sekretarieti ya ajira kuchakata ajira yote katika sekta ya umma unaathiri upatikanaji wa wataalamu wanaohitajika katika taasisi na mashirika yanayotumia mtaji wa umma kujiendesha. Kwa utaratibu huo mahitaji ya kujiendesha kibiashara hayapati uzingatiaji mzuri kutokana na utaratibu wa Ajira katika sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Spika, Utaratibu wa ajira unaochukuliwa kwa ujumla ikilinganishwa na ajira katika wizara na Idara za Serikali, hauendani kabisa na misingi pamoja na miongozo mujarabu ya kibiashara. Hali hiyo inahitaji kuangaliwa ipasavyo na ikibidi kurekebishwa ili mitaji ya umma itumike kwa ufanisi kwenye mashirika na taasisi zinazohusika.

2.4.3 Uwezo wa SGR kuzidi uwezo wa Bandari ya Dar es

Salaam

Mheshimiwa Spika, Kama inavyofahamika, Serikali imetumia mtaji wa umma kuwekeza kiasi kikubwa cha mtaji katika ujenzi SGR. Mradi huo wa uwekezaji utakapokamilika, SGR itakuwa na uwezo mkubwa wa kubeba mizigo, takribani tani 10,000 kwa safari. Mizigo mingi inatarajiwa kutoka Bandari ya Dar es Salaam ambayo haina uwezo wa kuingiza na kupakua kiasi hicho cha mizigo. Hali hii

inaonesha umuhimu wa kuongeza ufanisi kwa kuongeza gati katika Bandari ya Dar es salaam na ujenzi wa bandari nyingine.

2.4.4 Umuhimu wa Shirika la Taifa la Maendeleo – NDC,

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Maendeleo limepitia hatua mbalimbali za mabadiliko ya kiuendeshaji ikiwemo mabadiliko ya bodi ya kiutendaji na Menejimenti. Huenda hali ya uendeshaji wa Shirika hilo ilitokana na changamoto za Bodi na menejimenti ya Shirika. Hata hivyo, Bado kuna umuhimu wa kuangalia ukomo wa majadiliano yanayoendelea chini ya Shirika hilo kuhusu Mradi wa Mchuchuma na Liganga.

2.4.5 Kiasi kikubwa cha mikopo Chechefu kwa baadhi ya benki zenye mitaji ya umma

Mheshimiwa Spika, Mikopo chechefu inaathiri sana mizania ya taasisi na mashirika ya umma yanayotumia mitaji ya serikali. Ufuatiliaji wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya taasisi zinakabiliwa changamoto ya kuwa na kiasi kikubwa cha mikopo chechefu (non-performing loans – NPLS). Mfano wa Taasisi hizo ni Benki ya Maendeleo Tanzania – TIB na Benki ya Biashara Tanzania – TCB. Matokeo hayo yanaonesha umuhimu wa kutathmini madeni ya mashirika hayo na kuangalia namna ya kuyaondoa kwenye vitabu vya benki bila kuathiri ulipaji wa mikopo inayolipika (performing loans).

2.4.6 Upungufu Mkubwa wa Mtaji kwa ATCL na TGFA

Mheshimiwa Spika, Mtaji ni jambo la msingi kwa uendeshaji wa kitega uchumi au shirika lolote. Changamoto ya mtaji inaweza kuathiri ufanisi wa mtaji kidogo unaoweza

2 NOVEMBA, 2022

kutumika. Aidha, ukosefu wa mtaji unaweza kuathiri uendeshaji wa Taasisi au Shirika linalohusika. Katika kipindi kinachoripotwa, Kamati imebaini kuwa ATCL inakabiliwa na changamoto ya upungufu Mkubwa wa mtaji.

Mheshimiwa Spika, ATCL kwa sasa inalazimika kukodi ndege TGFA ili iweze kutekeleza jukumu lake la usafirishaji wa anga. Ukodishaji huo unatokana na TGFA kuwa mmiliki wa ndege zetu 11 zinazotumiwa na ATCL. Hali hiyo inatokana na nia njema ya Serikali kutumia utaratibu huo wakati inafufua shirika la ndege la ATCL. Hata hivyo, kwa hali ilivyo kwenye mtaji wa ATCL kuna umuhimu mkubwa kuhamishia umiliki wa ndege hizo kwa ATCL ambayo ukiondoa tatizo hili inajiendesha kwa faida.

2.4.7 Kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – TADB,

Mheshimiwa Spika, TADB ndio benki pekee inayohusika moja kwa moja na shughuli za wakulima. Hata hivyo, Benki hiyo haijapatiwa mtaji wa kutosha kufanikisha dhima yake. Hali hiyo haiendani na azma ya serikali ya kuongeza tija kwenye kilimo, kuleta mageuzi ya kilimo na kulisaidia taifa kufikia usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, taarifa zinaonesha kwamba, mwaka 2021 Serikali ilijitahidi kuipatia TADB kiasi cha Sh. Bilioni 208. Ufuatiliaji wa ufanisi wa mtaji umeonesha kuwa licha ya jitihada hizo, bado kiasi cha mtaji wa kutosha kinahitajika kwa TADB. Kwa ahadi ya awali iliyotolewa na Serikali, Benki hii ilitarajiwa kuwa na mtaji wa Sh. **Bilioni 760** ambao angalau ungeiwezesha TADB kuongeza wigo na kuwafikia

2 NOVEMBA, 2022

wahitaji wengi zaidi. Kwa mantiki hiyo, bado juhudi za Serikali za kuongeza mtaji kwa benki hii zinahitajika.

2.4.8 Kuathirika kwa kilimo cha Pamba kutokana na maelekezo ya Serikali ya Mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya Soko la dunia;

Mheshimiwa Spika, Wanunuzi wa pamba kushindwa kulipwa kikamilifu hasara waliyoipata kutokana na uamuzi na maelekezo yaliyotolewa na Serikali mwaka 2019 kwa pamba kununuliwa kwa bei ya juu kuliko bei ya Soko la dunia. Aidha, Makubaliano yalikuwa kuwa wanunuzi wanunue pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya Soko kwa makubaliano kuwa hasara yoyote itakayopatikana kwa wanunuzi wa pamba, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Benki ya Tanzania (BOT) itaifidia, uamuzi huu ulileta hasara na hadi sasa hasara hiyo ni shilingi **Bilioni 21.8** kwa wanunuzi wa pamba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya serikali ya kuzingatia maslahi ya umma kutokana na uamuzi wake, Maelekezo hayo yameathiri sekta ya pamba ikiwepo na utendaji wa Bodi ya Pamba. Hali hiyo ni dosari katika misingi ya biashara na ufanisi wa mtaji unaotumiwa na wanunuzi wa Pamba, pia inavuruga mantiki ya Bodi na manufaa yake kwa wakulima wa Pamba.

2.4.9 Matumizi ya TEHAMA,

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Mifumo ya TEHEMA katika utoaji wa huduma na kumbukumbu za mapato na matumizi katika taasisi na mashirika ya umma yanayotumia mtaji wa umma, yanaongeza ufanisi na kudhibiti fedha za umma. Taarifa mbalimbali zilionesha kuwa zipo taasisi na mashirika

2 NOVEMBA, 2022

ya umma ambazo hazijajielekeza kwenye matumizi ya TEHAMA kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa taasisi na mashirika hayo ni Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (National Health Insurance Fund – NHIF). Mfuko huu una kila nafasi na fursa ya kuboresha mifumo yake ya TEHAMA ili kuondosha mianya ya udanganyifu. Kwa kufanya hivyo, Mtaji wa umma uliowekezwa katika NHIF utakuwa na ufanisi na maslahi ya Serikali yataendelea kupatikana inavyostahili. Maelezo hayo yanaonesha kuwa Taasisi na Mashirika yanayohusika yanahitaji kuhimizwa kutumia mifumo ya TEHAMA ili kuboresha huduma zao na kudhibiti mapato na matumizi katika uendeshaji. Suala hilo linahitaji juhudi na msisitizo wa Serikali pamoja na ufuatiliaji wa karibu.

2.4.10 Mwingiliano wa Majukumu kwa baadhi ya Taasisi za Umma

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika utangulizi wa Taarifa hii, Serikali hutumia fedha za umma kuwekeza katika mashirika na taasisi kwa ajili ya kufanya biashara au kusimamia maslahi ya umma. Azma hiyo inawezeka kutimbia iwapo majukumu na shughuli za mashirika na taasisi zinazohusika yatapangwa na kuratibiwa inavyostahili. Tofauti na hivyo, juhudi za uwekezaji wa mitaji ya umma katika taasisi na mashirika ya uma zinaweza zisiwe na matokeo chanya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa taarifa mbalimbali zilizofanyiwa kazi na Kamati, ilibainika kuwepo kwa muingiliano wa majukumu miongoni mwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma. Katika hali hiyo, majukumu

2 NOVEMBA, 2022

yanayotekelezwa na shirika au taasisi moja yanaonekana yangepaswa kutekelezwa na mamlaka nyingine kwa lengo la kuleta ufanisi na tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa mwingiliano wa majukumu miongoni mwa baadhi ya mashirika au taasisi ni utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege (TAA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Katika uendeshaji, TANROADS inatekeleza jukumu la ujenzi wa Viwanja vya ndege wakati kimsingi lilipaswa kuwa chini ya TAA. Changamoto hiyo inahitaji kufanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi, vinginevyo hali hiyo inaathiri ufanisi wa kiasi cha fedha kinachowekezwa pamoja na kuathiri uthabiti wa maslahi yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine la mwingiliano miongoni mwa Mashirika au taasisi zinazotumia mtaji wa umma ni mali za shirika au taasisi moja kumikiwa na shirika au taasisi nyingine. Maelezo hayo ni halisi kwa mali za MSCL zinazomilikiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA). Kamati inatambua kuwa awali MSCL ilikuwa chini ya TPA lakini kwa sasa inajitegemea. Kwa sababu hiyo, kuna umuhimu wa kufanyika marekebisho ya Sheria zinazohusika ili kila zilizokuwa mali za MSCL zirejeshwe kwa MSCL

2.5 Majumuisho ya Sehemu ya Pili

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Serikali inatumia fedha za umma kwa ajili ya kuwekeza ili kupata faida au kusimamia maslahi maalum. Uwekezaji huo unafanyika katika taasisi na mashirika ya umma au kwenye Kampuni za Biashara ambako Serikali ina umiliki wa hisa chache au inasimamia maslahi yake kwa niaba ya wananchi. Katika kusimamia

2 NOVEMBA, 2022

ufanisi wa mitaji na maslahi yake pale inapowekezana, Serikali husaidiwa na Msajili wa Hazina ambaye huongozwa na Sheria, taratibu na miongozo mujarabu ya biashara.

Mheshimiwa Spika, Bunge ambalo ni Chombo cha wananchi limefuatilia hali ya mitaji ya umma kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya umma. Katika Taarifa hii hali ya mapato kutokana na mitaji hiyo na utendaji wa mashirika yanayotumia mitaji ya umma imeelezwa katika taarifa hii. Kutokana na hayo, Taarifa hii inabainisha maoni na mapendekezo katika sehemu ya tatu.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa hali ya mitaji ya umma na utendaji wa taasisi na mashirika yanayotumia mitaji ya umma, umejenga msingi wa mtazamo wa Kamati hii kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma. Mtazamo huo ni maoni ambayo ni moyo wa mapendekezo yanayotolewa kwa njia ya hoja. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:

(a) Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya kikodi kutokana na uwekezaji wa mitaji ya umma unastahili kufanyiwa tathmini ili kubaini uwezo halisi na misingi ya mwongozo wa ukokotoaji na upangaji wake.

(b) Ahadi zinazotolewa na serikali kwa mashirika au taasisi ambako serikali imewekeza mitaji zinapaswa kutekelezwa kwa mustakabali wa ufanisi wa mitaji inayotumika kwenye taasisi na mashirika ya umma.

2 NOVEMBA, 2022

(c) Utendaji na uendeshaji wa Mashirika ya umma au taasisi ambazo zina mitaji ya serikali unahitaji kuangaliwa vizuri na kupangiliwa inavyotakiwa kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija ya mitaji ya umma inayotumika.

Mheshimiwa Spika, mtazamo huo ndio msingi wa mapendekezo ninayoyatoa kwa njia ya Hoja kama inavyoelekeza kanuni ya 61 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 leo hii. Naamini Bunge litaijadili Hoja hii na hatimaye kupitisha Maazimio kuhusu Uwekezaji wa mitaji ya Umma.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, Baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kutoa Hoja kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kama ifuatavyo:-

3.2.1 Taasisi kutokuwa na Bodi ya Wakurugenzi

KWA KUWA, ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma unategemea pia uzingatiaji wa misingi ya uendeshaji bora, ambayo inahitaji Mashirika na taasisi ziwe na Bodi,

NA KWA KUWA, Kutokuwa na Bodi kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kuteuliwa kwa wajumbe baada ya Bodii zilizokuwepo kumaliza muda wake ni jambo linaathiri uendeshaji na upatikanaji wa tija ya mitaji katika mashirika na taasisi zinazohusika,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

(a) Serikali ianze mchakato ya upatikanaji wa Wajumbe wa Bodi kwa wakati,

2 NOVEMBA, 2022

(b) Utaratibu uandaliwe ili wajumbe wa Bodi wawe wanaingia kwa vipindi tofauti kwa lengo la kuzuia Bodi kukosa wajumbe pale inapokamilisha muda wake.

(c) Mbadala wa (“a” na “b”), Marekebisho ya Sheria yafanyike ili Bodi inapomaliza muda wake iendelee kutekeleza majukumu yake mpaka pale bodi mpya itakapopatikana.

3.2.2 Changamoto ya Kupata Vibali vya Kuajiri

KWA KUWA, Ajira katika mashirika na taasisi ni mchakato unaowezesha upatikanaji wa wataalamu kwa ajili ya uendeshaji wa mitaji ya umma kwenye mashirika na taasisi hizo, lakini utaratibu wa vibali na mchakato wa ajira kupitia sekretarieti ya ajira umekuwa na changamoto,

NA KWA KUWA, Changamoto hiyo inaathiri ufanisi wa mitaji ya umma pamoja na tija ya kuanzishwa kwa mashirika hayo, kutokana na kukosa watumishi wanaostahili kwa wakati hata inapokuwa na uwezo wa kuwalipa yenyewe,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke utaratibu wa kuzipatia taasisi zinazojiendesha kibiashara vibali vya kuajiri wenyewe ajira za moja kwa moja.

3.2.3 Uwezo wa SGR kuzidi uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam

KWA KUWA, Uwekezaji unaofanywa na Serikali katika Ujenzi wa Reli ya SGR utawezesha Usafirishaji wa mizigo takribani tani 10,000 kwa safari kwa mizigo ambayo kwa sehemu kubwa inatoka Bandari ya Dar es salaam, lakini Bandari hiyo haina uwezo wa kuingiza na kupakua kiasi hicho cha mizigo.

2 NOVEMBA, 2022

NA KWA KUWA, Kukosekana kwa mizigo ya kusafirisha kwa kadiri ya uwezo wa reli kutokana na uwezo mdogo wa Bandari ni changamoto inayoweza kuathiri tija ya mitaji inayowekezwa kwenye Bandari na SGR, lakini pia inaweza kutatuliwa kwa kujenga Bandari ya Bagamoyo,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba,

(a) Serikali inapaswa kuharakisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo; na

(b) Serikali isimamie Kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kuongeza Gati za kisasa katika Bandari ya Dar es Salaam lengo la yote haya ni kusaidia.

3.2.4 Umuhimu wa Shirika la Taifa la Maendeleo – NDC

KWA KUWA, Manufaa ya Mradi wowote wa uwekezaji yanategemea kuanza kwa mradi lakini mradi wa mchuchuma na liganga unachukua muda mrefu katika hatua za majadiliano yanayoratibiwa na Kamati ya Majadiliano ya Serikali (GNT),

NA KWA KUWA, Serikali imefanya mabadiliko ikiwemo kuipatia Bodi mpya ya wakurugenzi pamoja na Menejimenti,

NA KWA KUWA, Kutokukamilika kwa majadiliano ambayo yanaendelea kwa muda mrefu sana tangu kuanza ni jambo linalochelewesha manufaa ya mradi huo,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa mazungumzo katika GNT yanafikia mwisho

au yapelekwe NDC lengo likiwa ni kupata tija iliyokusudiwa katika miradi hii.

3.2.5 Mikopo Chechefu (Non-performing loans - NPLS)

KWA KUWA, Ibebainika kuwa baadhi ya taasisi kama vile Benki ya Maendeleo Tanzania – *TIB* na Benki ya Biashara Tanzania – *TCB* zinakabiliwa changamoto ya kuwa na kiasi kikubwa cha mikopo chechefu (non-performing loans – NPLS),

NA KWA KUWA, Hali hiyo inaathiri mizania ya vitabu vya taasisi, jambo ambalo ni hatari kwa misingi ya kibiashara na uendeshaji wa taasisi zinazotumia mitaji ya Umma,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathimini ya madeni hayo na kuangalia namna ya kuyaondoa kwenye vitabu vya Benki, bila kuathiri ulipaji wa mikopo inayolipika (performing loans).

3.2.6 Upungufu wa Mtaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania – ATCL

KWA KUWA, ATCL inakabiliwa na changamoto ya mtaji hasi na changamoto ya uendeshaji wa biashara kutokana na utaratibu wa kukodisha ndege kutoka kwa TGFA,

NA KWA KUWA, kwa kuwa utaratibu huo unaongeza payables katika vitabu vya TGFA,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iitake Wakala ya Ndege za Serikali Tanzania (TGFA) kuharakisha taratibu za kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kurudisha ndege kwa ATCL.

2 NOVEMBA, 2022

Kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – TADB, KWA KUWA, TADB ambayo ni Benki pekee inayohusika moja kwa moja na shughuli za kilimo lakini haijapatiwa mtaji wa kutosha wa kuendana na nia ya serikali ya kuongeza tija kwenye kilimo, kuleta mageuzi ya kilimo na kulisaidia taifa kufikia usalama wa chakula,

NA KWA KUWA, Pamoja na jitihada za Serikali za kuipatia TADB kiasi cha Bilioni 208 mwaka 2021, bado kuna ahadi ya serikali ambayo ingetekelezwa Benki hii ingekuwa na mtaji wa sh. **Bilioni 760,**

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali iendelee kuongezea TADB mtaji kwa lengo la kuongezea ufanisi na tija katika Sekta ya Kilimo.

3.2.8 Kuathirika kwa kilimo cha Pamba kutokana na maelekezo ya Serikali ya Mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya bei ya Soko la dunia;

KWA KUWA, Agizo la Serikali lililoitaka Pamba kununuliwa kwa bei ya juu zaidi ya bei ya soko la dunia limeathiri uwezo wa wanunuzi wa pamba kwa kiasi cha shilingi Bilioni 21.8 kiasi ambacho Serikali iliahidi kufidia deni hilo,

NA KWA KUWA, Deni hilo limeathiri taswira ya Bodi ya Pamba kwa wakulima na kuongeza changamoto katika biashara ya kilimo cha pamba,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mkakati wa kulipa fedha hizo kwa lengo la kuongeza ufanisi wa sekta hiyo.

2 NOVEMBA, 2022

3.3 Mambo ya Jumla kuhusu Maoni na Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla Kamati imezingatia umuhimu wa tathmini ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kikodi kutokana na uwekezaji wa mitaji ya umma. Aidha, suala la ahadi zinazotolewa na serikali kuhusu mitaji ya umma pamoja na umuhimu wa kuimarisha mitaji hiyo, ni mambo ya msingi katika mapendekezo ya maazimio niliyoyatoa. Kubwa katika sehemu hii ni kuliomba Bunge liyajadili na hatimaye kufanya uamuzi.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo ya kiti chako ikiwa ni pamoja na ushauri na miongozo kwa kipindi chote cha ufuatiliaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba, kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Vilevile, napenda kumshukuru Msajili wa Hazina, Ndugu Benedicto Mgonya kwa ushirikiano wake wa dhati alioutoa kwa Kamati na kushauri namna bora ya kuzifanya Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na ufanisi

2 NOVEMBA, 2022

katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija kwa Taifa. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, chini ya uratibu wa Mkurugenzi Idara ya Uwekezaji kwa ushirikiano mkubwa na wa karibu na Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jerry William Silaa, Mb _ Mwenyekiti
2. Mhe. George Natany Malima, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb _ Mjumbe
4. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb _ Mjumbe
5. Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb _ Mjumbe
6. Mhe. Charles M. Kajege, Mb _ Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb _ Mjumbe
8. Mhe. Dorothy George Kilave, Mb _ Mjumbe
9. Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb _ Mjumbe
10. Mhe. Haji Amour Haji, Mb _ Mjumbe
11. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb _ Mjumbe
12. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb _ Mjumbe
13. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb _ Mjumbe
14. Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb _ Mjumbe
15. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb _ Mjumbe
16. Mhe. Sanya Jusa Jaffar, Mb _ Mjumbe
17. Mhe. Silyvestry Francis Koka, Mb _ Mjumbe
18. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb _ Mjumbe

2 NOVEMBA, 2022

- | | | | |
|-----|-------------------------------------|---|--------|
| 19. | Mhe. Vuma Hole Augustine, Mb | _ | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb | _ | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Dr. Pius Stephen Chaya, Mb | _ | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Condester Michael Sichalwe, Mb | _ | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb | _ | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nanelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Pia natoa Shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu vema shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndugu Zainabu Mkamba, Ndugu Mwajuma Ramadhan na Ndugu Charles Wanyancha pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Modesta Kipiko. Tunawashukuru pia Wanasheria wa Ofisi ya Bunge, Ndugu Elizabeth Malongo na Ndugu Praisegod Lukio pamoja na Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge kwa utaalamu wao wakati wote wa vikao vya Kamati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati yanalenga kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo uwe wa ufanisi na ulete tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge

2 NOVEMBA, 2022

ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma, na kuijadili ikiwa na Maoni na Mapendekezo ili kuamua na kuiwezesha Serikali kuyafanyia kazi maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Mhe. Jerry William Silaa, Mb.

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC)**

2 Novemba, 2022

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kama ilivyo ada ninayo majina hapa ya Wabunge ambao tutaanza nao katika uchangiaji, alafu tutaendelea pia na uchangiaji katika sikuchache zijazo. Kwa siku ya leo tutaanza na Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza jioni ya leo. Katika hoja tatu kubwa zilizowasilishwa jioni ya leo. Hoja ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Hoja ya

2 NOVEMBA, 2022

Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na ile Kamati ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika fursa hii niliyopata mimi mjadala wangu utajikita katika taasisi kubwa mbili. Leo nitajadili Fungu Namba 28 – Jeshi la Polisi na Fungu Namba 93 – Jeshi Uhamiaji. Katika ripoti ya CAG na ripoti iliyowasilishwa leo na Kamati ya PAC kuna mambo muhimu ambayo yamezungumzwa; na mimi katika uchambuzi wangu nitaanza na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Polisi, katika ripoti ya CAG na ripoti ya Kamati imeonesha ndani ya Jeshi la Polisi kuna mfuko ambao ulianzishwa na Jeshi la Polisi unaoitwa *Reward and Fine Fund* ambao kwa jina lingine unaitwa Tuzo na Tozo. Mfuko huu ulianzishwa kwa nia njema. Nia ya Serikali au Jeshi la Polisi ilikuwa ni kwa ajili ya ustawi wa Polisi ili kuwawekea mazingira mazuri, ikiwemo ujenzi wa nyumba zao na miradi mbalimbali. Lakini uanzishaji wa mfuko huu ulikuwa na sheria yake, na sheria ile ilitungwa; na kulingana kufuatana na taratibu na mahitaji ya sheria ya fedha na kufuatana na kuanzishwa kwa mfuko huu miaka 10 ilitakiwa kwanza ipate idhini, kwa maana kanuni zitungwe na Waziri mwenye mfuko husika.

Mheshimiwa Spika, lakini cha ajabu mpaka hivi ninavyoongea ni zaidi ya miaka kumi na CAG amebaini kwamba mfuko huo umekuwa ukipokea ela na unafanya matumizi lakini Waziri hajawai kutunga kanuni zinazoelekeza namna fedha zitumike. Tafsiri yake ni kwamba mfuko umekuwa ukijiendesha kienyeji.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nataka kusema, kwamba fedha zimekuwa zikikusanywa na chanzo kikubwa cha fedha kwenye mfuko huu ni huduma ambazo wamekuwa wanazitoa kwenye ulinzi wa taasisi za fedha, migodi na sehemu nyingine. Mfuko huo una fedha nyingi na Jeshi la Polisi linaweza kukusanya bilioni 10 hadi bilioni 15 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, lakini fedha hizi hazina mwongozo wa kanuni uliotungwa na Waziri, hakuna Mhasibu wa kusimamia mfuko huu na haujawahi kukaguliwa tangu uanzishwe na CAG, na, hakuna hesabu zilishawahi kufanywa kwenye mfuko huu. Bahati mbaya huu mfuko kuna ukiukaji mkubwa sana. Kwa mfano mkataba unaingia na taasisi ya fedha, *let us say* wanaingia mkataba wa milioni 80 kwa mwezi; sasa mchezo unaofanyika ni kwamba, wale Askari wanaopangiwa kwenda kufanya majukumu wanalipwa posho kutokana na hizo fedha, na baadaye Jeshi la Polisi likihitaji malipo wanakata kulingana na ile fedha waliolipa kwanza wale Polisi waliotoa huduma.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba kunafanyika matumizi ya fedha mbichi. Yaani ina maana wanafanya *invoice discounting* wanachukua ela yao mapema. Hapa pana-*create* mwanya, fedha zinaweza zikachukuliwa nyingi. Kama Jeshi la Polisi lilitakiwa kukusanya milioni 80 unaweza ukakuta mwisho wa siku *invoice* wanayo peleka ni milioni 20, milioni 80 zimechukuliwa zikiwa mbichi.

Mheshimiwa Spika, mimi sipingi askari wetu wanapofanya kazi ya kulinda malindo haya kupewa *risk allowance*, lakini *risk allowance* lazima iwe na utaratibu

2 NOVEMBA, 2022

wake kwa miongozo ya Sheria ya Fedha. Huwezi ukachukua tu huko benki unakolinda kwamba wanakulipa huko huko. Benki au migodi imeingia mkataba na Jeshi la Polisi, kwa hiyo ilibidi fedha zote ziingie kwanza kwenye mfuko halafu Jeshi la Polisi lifanye *arrangement* ya kuwalipa askari kule kule na si kule wanapofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hilo limeendelea na haijulikani sasa utaratibu upi wanafanya ili kufanya *reconciliation* ya fedha hizo. Hivyo, Kamati iliona na CAG aliona kupitia mazingira haya kunaweza kukawa na upotevu wa fedha nyingi kwa sababu *control* yake ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, CAG alielekezwa kwenda kufanya ukaguzi maalumu kwenye mfuko huu ambao umekaa zaidi ya miaka kumi haujafunga hata hesabu zake. Mpaka sasa hivi kuna kigugumizi na ushirikiano wanaopata ni mdogo. Sasa nashindwa kuelewa ni kwa nini CAG hapewi ushirikiano wa kufanya hii *special audit* ili sasa umma ujue na sisi Wabunge kwa niaba ya wananchi tujue, fedha hizo zilizokusanywa kwenye mfuko huo ni kiasi gani, matumizi yake yalikuwa yapi na kwa nini kanuni ya kuongoza na *guide* namna ya matumizi ya mfuko huo hazijatungwa mpaka leo? Sipati majibu ya mambo haya na mabo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu ni mfuko ambao una fedha nyingi, na umesikia mara nyingi hata Mheshimiwa Waziri akiwa anajibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, wakiomba kituo cha Polisi anawaambia tutaenda kuchukua kwenye tozo na tuzo. Lakini hiyo, tozo na tuzo

2 NOVEMBA, 2022

haina *control* yoyote, ni kama kichaka fulani hivi. Sasa hatuwezi katika nchi hii, na hizo fedha hazipitishwi wala haziidhinishwi na Bunge, zinaishia huko. *IGP* anamwandikia *Pay Master General*; anataka bilioni 10, zinakuja kwa *IGP* zinaenda kwenye matumizi moja kwa moja, hakuna utaratibu wa namna hiyo. Hivyo, kuna ukiukwaji wa Sheria ya Fedha maana hakuna *control* yoyote wala hesabu zinazowekwa.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe nishauri mambo yafuatayo; mfuko huu una fedha nyingi, pamoja na kutumika hadi anapoondoka *CAG* zipo fedha kwenye akaunti yao huko *BOT*, bilioni 35 karibia na milioni 300 na kidogo, na bado wanaendelea kukusanya. Niombe, kama tuna nia njema na tunataka kuweka *transparency* kwenye matumizi ya fedha za umma, niombe mambo yafuatayo: -

- i. Wa-*suspend* matumizi kwenye mfuko huu mpaka kanuni ziundwe na Waziri mwenye dhamana.
- ii. Serikali ijikite kwenda kumpa *CAG* ushirikiano afanye *audit* ili tujue kuna nini na fedha hii imetumikaje kwenye mfuko huu.
- iii. Tuombe wakaandae hesabu, inakuwaje mfuko ambao hauna mhasibu upo tu na *billions of money* zipo tu zinachukuliwa kiholela. Waende pale wakatuandalie hesabu na sisi tuweze kujua ni jambo gani linaendelea kwenye mfuko huu wa tozo na tuzo.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Kuna njia rahisi, tuwasaidie Serikali, tunahangaika tunashida na vituo vya polisi nchi nzima. Tengenezeni *arrangement* kwani kile chanzo kina fedha ambazo ni *stable and sustainable*, nendeni kwenye *financial institution* mkaombe *mortgage* mjenge kwa wakati mmoja Vituo vya Polisi nchi nzima. Halafu, kwa kuwa ile fedha kwa kuwa *source* iliyo *stable* mtaenda kulipa huo mkopo na tutakuwa na Vituo vya Polisi nchi nzima bila upendeleo na kila mtu ataona manufaa ya mfuko huu, kuliko wakati huu ambapo *IGP* akiwa huru ataona sasa hivi nina *interest* na sehemu gani ngoja nikajenge majengo hapa. Akiondoka *IGP* huyo ana-*abandon* majengo yale anakuja *IGP* mwingine anaanzisha uelekeo wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatuna *direction* kwenye mfuko huu. Kama nchi tutafakari kwa pamoja, twende tukafanye jambo la muhimu kwenye mfuko huu, ili uletwe. Na kwa kuanzia mwaka wa fedha ujao tupitishie hapa makadirio ya mapato na matumizi ya mfuko huu ndani ya Bunge hili na hapo ndipo tutakuwa tumefanya kazi. Tumekosea sana tumevunja Sheria ya Fedha, hatujali tunaenda tu.

Mheshimiwa Spika, niombe sana, Serikali ipo hapa, hili jambo mkiendelea ni bomu kubwa sana, kuna ubadhirifu mkubwa upo *hidden* kwenye huu mfuko. Mkiuacha bila Kwenda kuufanyia hatua za haraka bomu litakuja kulipuka, tusije tukalaumiane.

Mheshimiwa Spika, hilo nimemaliza. Nadhani watakuwa wamenielewa juu ya mfuko huu wa tozo na tuzo. Niwaombe kabisa tena mambo mengine ya kuja

2 NOVEMBA, 2022

kutuambia tutakwenda tutaenda kuchukua; m-suspend huo mfuko mpaka mfuata taratibu zote zinazo wahitaji kama Serikali ili kusiwe na mkanganyiko. Hiyo nimemaliza naomba niende kwenye fungu lingine la uhamiaji Fungu Namba 93.

Mheshimiwa Spika, hii ni taasisi nyingine iliyo ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Mambo ya kusikitisha kabisa, nitatoa *literature* moja juu ya kilichotokea pale Uhamiaji. Alisema hapa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, kuna habari ya *stickers* za *visa*. Hizi *stickers* za *visa* ni kichaka ambacho kinagharimu Taifa letu hasara kubwa. Wale Maafisa wa Uhamiaji ulikuwa ni mradi wao wa kujitengenezea mabilioni.

Mheshimiwa Spika, walikuwa na mambo mawili; mwaka 2019 CAG alienda pale kufanya *special audit* tena ilikuwa ya *interval* ndogo ya miezi sita, kuanzia Januari mpaka Juni, 2019, kukagua namna ya utoaji wa *stickers* za *visa* kwa wageni wanaokuja ndani ya nchi. Alikutana na maajabu makubwa sana. Alikuta kwanza kuna *visa* zaidi ya 33,500 zilizotolewa ni *fake*. Yaani wale Maafisa Uhamiaji walienda kujitengenezea hizo *stickers*, wakagawa, wakachukua hela, wakaweka mfukoni zaidi ya Shilingi 3,800,000,000/=, maisha yakaendelea *business as usual*.

Mheshimiwa Spika, walipoendelea kukagua wakakuta zaidi ya *visa* 21,705; zilipokelewa fedha zikaingizwa kwenye *database* ya Uhamiaji, baadaye wale Maafisa wakaenda kufuta zile taarifa zote kwenye *database*, wakachukua zaidi ya Shilingi 2,516,000,000/= wakagawana wafanyakazi 40, maisha yakendelea, *business as usual*. (Makofi)

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kilichokuja kutokea sasa, Maafisa saba wakapelekwa Mahakami wakafunguliwa kesi ya Uhujumi Uchumi kwenye Mahakama Kuu Moshi. Wakakaa pale gerezani miaka miwili, baadae *DPP* akafanya *nolle prosequi* kwamba sina nia ya kuendelelea na kesi hii. Wakarudi kazini, wakaendelea kupiga maisha. Tuki-*audit* mwakani tutakuta wametupiga tena Shilingi bilioni sita, *business as usual*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima kama Taifa tutafakari. Watu 40 wamekula vituo vya afya sita peke yao, na wamerudishwa kazini, wameingia kwenye *payroll* na maisha yanaendelea. Sisi tunakuja kupiga kelele hapa, tutawasadiaje Watanzania masikini tuliowaacha huko Vijijini, waliotutuma ndani ya Bunge hili? Watu wachache wananufaika na fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana watu wa Serikalini, ninyi mliopewa dhamana na Mheshimiwa Rais, katusaidieni katika mambo haya. Kuwaachia watu wanakula fedha, wamerudi wako ofisini na hiyo *audit* ilikuwa ni *trend* a miezi sita, *just imagine* kama unge-*audit* ya miaka mitano, si ungekuta karibia bajeti ya Wizara nzima watu saba wamekula, *business as usual* na maisha yanaendelea! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hili la Uhamiaji nadhani *message* mmeipata vizuri kitu gani nakusudia kusema. Nendeni mkafanye upya, mrudie na ule mfumo, hao watu walienda kufuta vitu kwenye *database*. Ule mfumo mmeuanzishaa upya, nendeni pia mkafanye *reconciliation* baada ya ku-

2 NOVEMBA, 2022

abandon ule mfumo wa zamani: Je, huu mfumo mpya una-*address* yale matatizo? Au *mme-create* mfumo mpya ambao ni *loophole* nyingi kutupiga zaidi na zaidi! Kwa hiyo, nawaomba watu wa Serikali mkawe makini kuangalia hasara tuliyosababishwa, lakini watu hawa waliosababisha wizi wa namna hiyo kuwarudisha ndani ya Uhamiaji ina-*send message* mbaya kwa wale waliopo mle, kwamba, kumbe unaweza ukapiga hela! Mimi napokea mshahara wa Shilingi 800,000/=, mwenzangu kapiga Shilingi bilioni mbili kaenda kupumzika kidogo gerezani mwaka mmoja amerudi, tumeendelea na Shilingi bilioni mbili na hakuna chochote! Naye atakuwa *attempted*, atachukua naye Shilingi bilioni tano, naye ataenda kukaa gerezani mwaka mmoja atarudi *nolle prosequi*, maisha yataendelea. Ndugu zangu, haya ni mambo ya kusikitisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo kubwa ambalo pia niwaombe watu wa Serikali, nimepitia sana ripoti ya CAG katika *area* ya *compliance* kwenye *Public Procurement Act*. Yaani taasisi hii, ile sheria ni kama wameiweka huko kwenye kabati wanajiendeshea mambo. Nimeona Jeshi la Polisi pale, hata *issues* zao za *procurement*, 70% ya *issues* zote walizozifanya ni *non-compliance* na sheria. Wanaenda kulipa fedha wakandarasi bila hata kazi kukamilika, *Auditor* anaenda kukuta fedha zimelipwa na mradi haupo.

Mheshimiwa Spika, kuna Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa walinunua magari, magari yenyewe hayo yalilipiwa zaidi ya Shilingi bilioni mbili na milioni mia saba na kidogo, lakini magari yenyewe hayapo. Kwa maana hayo magari yalilipiwa hata kabla hayajawa *delivered*. Yaani *you pay before delivery of goods*. Katika bajeti hiyo, tena

2 NOVEMBA, 2022

wame-exceed. Bajeti iliyokuwa *approved* na *budget approving authority* ilikuwa ni Shilingi milioni 388. Kwa bahati mbaya, unakuta wamefanya *expenditure* ya Shilingi 2,400,000,000/= bila *budget approving authority*.

Mheshimiwa Spika, sasa *variance* unayoiona hapo kwenye Shilingi 2,300,000,000/= iliyokuwa *approved*, *variance* ni kubwa sana. Sasa tuki-*entertain* mambo haya na tukaona hii ndiyo *culture* ya kuendesha mambo yetu ndani ya Serikali, tuta-*create vacuum* kubwa kwenye Taifa hili. Watu wataacha ku-*comply*, tutakuwa na hizi *documents* kama urembo tu na watu watakuwa hawa-*comply*. Kwa sababu tunaweka wenyewe sheria, badala ya kuzifuata, tunaweka kwenye makabati, tunaanza kutumia sisi wenyewe tunavyofikiria. Haiwezi kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, nimeona pale *TTCL* kwenye manunuzi, yaani ni wezi. Tuombe *PPRA* ikafanye *special audit* kwenye mashirika haya ambayo tumeona. *Compliance* kwenye Sheria ya Manunuzi ni mbaya. *Compliance* siyo ile ambayo, inaishia tu kwamba tume-*comply*, ni *compliance* ambazo zina *impact* kwenye *finance*. Kwa sababu unakuta umesaini mkataba na mtu, hakuna *power of attorney*, kwa maana ule mkataba *is null and void*. Mmempa kazi, kesho na kesho kutwa asipo-*perform* hamwezi kumshitaki. Hakukuwa hat ana mtu aliyepewa *power* ya kisheria ya kusimamia mkataba wa Shirika. Shirika kubwa kama *TTCL* yanafanyika mambo ya ajabu kama haya. Nawaomba ndugu zangu, kuna *issues* nyingi sana kwenye *compliance* ya manunuzi. Nendeni mka-*scrutinize document* ya CAG muone *weight* ilivyo na

2 NOVEMBA, 2022

significant impact itakayotupelekea. Kutakuwa na *issue* za *litigation*, tusipoona hapa tutashtakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna mkataba mmoja nimekuta pale *TTCL* wa Shilingi bilioni tano. Wamesaini ule mkataba na Mkandarasi alitakiwa amalize ndani ya miezi ya mitatu, ilikuwa ni kutengeneza ule mfumo wa short sms, lakini mpaka leo una zaidi ya miaka tisa hajawahi kumaliza. Nikawauliza sasa *position* ya mkataba kama huu ni upi? Yaani yeye alitakiwa awakabidhi kazi ndani ya miezi mitatu, lakini amechukua zaidi ya miaka mitano na mnaendelea na maisha na mnasema *this is good, let us live, business as usual*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, ajiandae.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya Afya. Kipekee sana nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kweli amekuwa akitekeleza na kupeleka fedha nyingi sana kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, namshukuru yey pamoja na wasaidizi wake wote.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita zaidi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kama nilivyotangulia kusema, Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake wamepeleka fedha nyingi kwenda kutekeleza miradi ya hospitali, vituo vya afya, zahanati, kujenga shule na mambo mengi yanafanyika katika maeneo yetu, nasi sote ni mashahidi wa yale ambayo yanatekelezwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nini matarajio kama nchi? Matarajio ni kuona kwamba miradi ile inatekelezwa kikamilifu na inakuwa na thamani ya fedha iliyopelekwa katika hayo maeneo. Kwa bahati mbaya sana katika baadhi ya maeneo, hasa kwenye Halmashauri za pembezoni, ili miradi ile iende ikakamilike vizuri, lazima kuwe na rasilimali watu wa kutosha. Ila kwa bahati mbaya Halimshauri zetu za pembezoni kuna upungudu mkubwa sana wa rasilimali watu kiasi ambacho utekelezaji wa miradi ile unakuwa chini ya kiwango. Ukienda unakosa watu wa manunuzi, unakosa ma-engineer, unakosa wahasibu na mambo kadha wa kadha. Kwa hiyo, matokeo yake miradi mingi inatekelezwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, labda nikupe mfano wa uchache au upungufu wa watumishi katika baadhi ya Halmashauri. Ukienda kwenye ripoti ya CAG, ziko Halimashauri nyingi ambazo zimebainisha upungufu wa watumishi ikiwemo Kasulu DC, kuna uhaba wa watumishi 163 sawa na 52% tu. Ukienda Nanyamba Mji kuna upungufu wa watumishi 932; ukienda Halmashauri ya Kilwa, walimu peke yake, kuna upungufu wa walimu 735; Ukienda Newala DC kuna upungufu wa watumishi 1,087 waliopo ni 1,088 tu; ukienda

2 NOVEMBA, 2022

kwenye maeneo mengi kwenye kata hakuna Maafisa Maendeleo ya Jamii, sehemu ambayo tunapeleka fedha nyingi sana zile za mikopo ya 10% lakini hakuna wasimamizi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika baadhi ya Halmashauri hakuna Wakaguzi wa Ndani, hawapo. Pia Maafisa Manunuzi kwenye Halmashauri zetu nalo ni changamoto, wengi waliopo ni wale walioazimwa na Halmashauri na wanakosa sifa. Sasa matokeo yake ni kwamba miradi mingi, kwa sababu hawa watumishi ambao tunawakosa ndio ambao wangtakiwa kusimamia miradi hiyo kwa ukamilifu, miradi imekosa thamani halisi ya fedha kama vile ambavyo tulikuwa tunatarajia.

Mheshimiwa Spika, rasilimali watu ndiyo uti wa mgongo kwenye utendaji wa hizi Halmashauri. Kwa mfano, umepeleka fedha hiyo asilimia 10 ili iende kwenye hayo makundi ya akina mama, vijana, pamoja na watu wenye ulemavu, lakini hakuna mfuatiliaji kule. Zile fedha zinaenda kuzama, kwa sababu zitapelekwa, lakini nani wa kuwaelimisha? Hayupo. Nani atasimamia? Hayupo. Kwa hiyo unakuta fedha nyingi zinapotea.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye Taarifa ya Mkaguzi na Mdhhibiti wa Hesabu za Serikali, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ni Shilingi bilioni 47.1 hazijarejeshwa. Hizi ni fedha nyingi ambazo zingefanya kazi nyingi sana katika Halmashauri zetu. Ukirudi miaka mitano nyuma, ni zaidi ya Shilingi bilioni 100 zimeshindwa kurejeshwa, zimezama.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, matokeo yake ni kwamba Halmashauri na wale ambao tuliwatarajia waende tukawainue kiuchumi wanakosa kuinuliwa kiuchumi kwa sababu hizo fedha ambazo tulitarajia zirudi zikawasaidie watu wengine hakuna mtu wa kuelimisha na kutoa elimu ya kutosha pamoja na usimamizi wa hayo makusanyo kule kwenye maeneo ya kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye suala la manunuzi, kama ambavyo Mjumbe ambaye ametangulia kusema, fedha nyingi katika Halmashauri zetu zinaenda upabde wa manunuzi, lakini hakuna watu wa manunuzi. Kwa hiyo, unakuta Mkurugenzi anakwenda kumwazima; natolea tu mfano, mwalimu, mtu ambaye hana sifa ya kutosha kwenye eneo hilo, ndiye anaenda kusimamia manunuzi. Ukienda kwenye ripoti ya CAG, kiasi kikubwa cha fedha kimepotea kwa sababu ya kukosa watu wenye sifa wa kusimamia manunuzi ya Umma. Wanafanya manunuzi lakini hayafuati taratibu na kanuni ambazo zimeandaliwa na PPRA.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kukosekana kwa *engineer* katika Halmashauri zetu; tulienda kwenye Halmashauri mojawapo kwenye mkoa huu ambao tupo, tulimkuta mtu ambaye alikuwa anasimamia ujenzi wa bwalo pamoja na bweni, alikuwa ni Mwalimu. Kwanini alikuwa anasimamia Mwalimu? Amewekwa pale kwa sababu ya ukosefu wa *engineer* pale Halmashauri. Kwa hiyo, kawekwa yeye. Tulikuta miradi ile kwa kweli ilikuwa inasikitisha sana.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kwa sababu fedha hizi zinatokana na kodi za wananchi, lakini lengo ni kutoa huduma kwa wananchi pale ambapo miradi itakamilika vizuri. Naiomb Serikali basi, ijitahidi kuajiri watumishi ambao wataenda ku-cover gap lililopo kwa sasa ili miradi iwe na thamani ya fedha ambazo zinapelekwa kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine, nilizungumzia suala la upungufu wa walimu katika baadhi ya maeneo, vile vile, ukosefu wa watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nao ni mkubwa. Naiomba Serikali ifike mahali sasa tuajiri watumishi ambao wana utashi wa kuishi kwenye maeneo husika au wale ambao wanatoka kwenye maeneo yao. Kwa sababu ipo changamoto kubwa, mtumishi anapoenda kwenye eneo ambalo jiografia yake inakinzana na yeye, anakaa kwa muda mfupi, anataka kutoka. Nafahamu kwamba Tanzania ni yetu sote, kila mmoja anatakiwa kuishi popote, lakini ipo hiyo changamoto sana ambayo tunai-experience site. Mtu anaenda kuripoti na anataka arudi, matokeo yake upungufu hauishi kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia tuweke muda maalum kwa mtumishi kuhama, yule ambaye amepata ajira. Muda ambao haupungui miaka mitatu ili angalau tu-retain wale ambao wapo. Otherwise haya maeneo ya pembezoni ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yataendelea kubakia bila kuwa na watumishi na hali inazidi kuwa mbaya kwa sababu lengo ni watumishi wawepo ili huduma zikaweze kutolewa ipasavyo. Watumishi wanapokosekana, huduma pia zinakosekana.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, lingine naomba pia Serikali ibaini upungufu kwa kila Halmashauri za pembezoni, ili wakati wa kutoa ajira, basi kipaumbele kiwe ni yale maeneno ambayo yana upungufu mkubwa. Kwa sababu haiwezekani kila siku baadhi ya maeneo watumishi wanakuwa wachache. Imekuwa kama ni wimbo, kuna maeneo yana watumishi wengi na mengine yana watumishi wachache. Sasa hao ambao ni wachache, utoaji wa huduma inawawia pia vigumu. Kwa hiyo, tufanye Sensa ya makusudi, tubaini hali ilivyo ili linapokuja suala la ajira, basi watumishi wapelekwe au tutoe kipaumbele katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limejitokeza kwenye ripoti ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ni tatizo la fedha kutopelekwa benki zinazokusanywa kwa mfumo wa POS. Hii ni changamoto kubwa na imejitokeza katika maeneo mengi. Kwa mwaka 2020/2021 peke yake ni Shilingi bilioni 17 hazikupelekwa benki. Tafsiri yake rahisi tu ni kwamba hizo fedha zimeingia kwenye mifuko ya watu, lakini zingekuwa zimewekwa benki zingefanya mambo ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunakwamisha kwa sababu kwenye bajeti Kuu ya Taifa inabajetiwa pia na fedha zinazotokana na makusanyo kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, unakuta bajeti kuu ya Taifa haitimii kwa sababu kuna fedha huku nyuma ambazo zimewekwa kwenye mifuko ya watu ambao siyo waaminifu. Naiomba Wizara ambayo inasimamia TAMISEMI kuweka mfumo ambao ni madhubuti utakaodhibiti hili suala za fedha kutopelekwa benki.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, fedha hizi siyo za leo kwa sababu huu ni mwaka wa pili, kw sababu ni za mwaka 2020/2021, Shilingi bilioni 17 hazijaenda benki hadi leo. Wamechukuliwa hatua gani ambao wamehusika? Mpaka sasa baadhi ya maeneo unakuta bado. Kesi nyingi ziko TAKUKURU, wengine wamepelewa Polisi, lakini kile ambacho tulikuwa tunataraji, kwa sababu lengo letu lilikuwa tupate zile fedha zikatoe huduma kwa wananchi. Kwa hiyo, inachelewesha pia utoaji huduma kwa wananchi kwa sababu fedha zimeingia kwenye mifiuko ambayo siyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba TAMISEMI, ule mfumo wa kielektroniki wa *TAUSI* uanze kufanya kazi ili tuweze ku-*monitor* haya mambo mengine amabyo yanaweza pia kurekebishika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali amelibainisha kwenye Hesabu ya 2020/2021, nalo ni suala la vitendea kazi kwa watumishi. Nimeongea hapa kuhusu Maafisa Maendeleo ya Jamii, lakini pia tuna ma-*engineer* wanaosimamia miradi, tuna wahasibu, wakusanya mapato, wanahitaji vitendea kazi ili waweze kufika kwenye maeneo ambako wanaweza kutoa hizo huduma au kukusanya mapato. Halmashauri nyingi hazina vitendea kazi kwa watu hao. Unakuta internal auditor yupo pale, anatakiwa kumkagua Mkurugenzi, Mkurugenzi hampi usafiri; kwa sababu akimpa usafiri, maana yake anaenda kumtafutia yeye changamoto. Kwa hiyo, hapewi usafiri, kiasi kwamba sasa unakuta kazi ya internal auditor inakuwa ngumu sana, namna gani atafika akakague miradi ili aje abainishe

2 NOVEMBA, 2022

yaliyopo huko *site*? Anashindwa kwa sababu hana vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara tuangalie Halmashauri, tuwawezeshe waweze kufika kwenye maeneo. *Engineer* yupo, anatakiwa akakague miradi, na sasa hivi miradi ipo mingi kwenye kata zetu, lakini *engineer* yupo Halmashauri, hana usafiri wa kumfikisha huko *site*. Matokeo yake sasa, kwa sababu yeye hawezi kufika kwa wakati, basi ana-*delegate*, anawaambia walioko *site* kama ni watu wa Afya, kama ni watu wa Elimu au nani, wasimamie hiyo miradi wao, lakini wao tukumbuke kwamba hawana ujuzi wa majukumu ambayo wanapewa. Matokeo yake ni miradi inazidi kuharibika kwa kukosa vitendea kazi vya kuwafikisha maeneo mbalimbali ya kusimamia miradi kule *site*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine niseme kidogo ni suala la wahasibu. Nilitangulia kusema kwamba wahasibu ni wachache, lakini unakuta maeneo mengine wahasibu hawa wamepitwa na wakati, kwa maana ya kwamba mifumo inabadilika kila siku ya ufungaji wa hesabu za mwaka, lakini wahasibu hawa hawana mafunzo ya namna ya kufunga hesabu hizo za mwaka. Matokeo yake inapofika ufungaji wa hesabu za mwaka wanapita, wanahaha kwenye maeneo mbalimbali kutafuta watu wa kuwafungia hesabu zao. Ni suala ambalo linapoteza fedha nyingi za Halmashauri, kwa sababu wangekaa kwenye vituo vyao wakafunga wenyewe hesabu zao ingepunguza hizo gharama za kupita wanazunguka kutafuta watu waweze kuwafungia hesabu zao za mwaka. Kwa hiyo, hili ni tatizo ambalo lazima Wizara zinazosimamia Mamlaka za

2 NOVEMBA, 2022

Serikali za Mitaa walione, waone namna nzuri ambayo watatoa mafunzo kwa wahasibu ili waendane na utaratibu na mfumo mpya unaotumika sasa wa ufungaji za hesabu hizi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, wengine ambao wanafanya wao wenyewe, wanasema poteleambali tunafanya, unakuta hesabu zao ni mbaya, hata CAG anashindwa kuisoma hiyo hesabu ya Halmashauri husika na matokeo yake wanaipa hati ambayo siyo yenyewe, lakini ni kwa sababu tu ya upungufu wa ujuzi kwa wahasibu ambao wapo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Johnson Mpina na Mheshimiwa Aida Joseph Khenan ajiandae.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nizipongeze hizi Kamati tatu za *PAC*, *LAAC* na *PIC* na nimpongeze CAG wote kwa pamoja ametuonesha njia ya kupita na njia ya kusemea.

Mheshimiwa Spika, nakuwa na maneno magumu sana ya kusema lakini hata lugha ya kutumia naikosea, sijui nitafanyaje, yaani najiuliza maswali mengi sana kwamba hivi hizi nyimbo tunaimba tunamwimbia nani? Yaani tunaimba ili iweje?

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nitatoa ripoti baadaye kwa kutumia mfano wa halmashauri yangu, lakini najiuliza wewe unasoma na sisi tunasoma vitabu kwamba, kazi ya Mbunge ni kuishauri Serikali, sasa na wewe ni mtaalamu wa sheria utakuja uniambie tukishauri, tukishauri miaka thelathini tunafanyaje, yaani sisi kazi yetu ni kuishauri Serikali sasa tumeshauri,tumeshauri,tunafanyaje? *(Makofi)*

SPIKA: Wacha nikusaidie, kazi yetu siyo tu kuishauri Serikali; kuna muda wa kuishauri Serikali, kuna muda wa kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Wakati tutakapokuwa tunajadili Mpango yale mapendekezo ya Mpango, tutakuwa tunaishauri Serikali, wakati huu wa kujadili ripoti ya CAG tunaisimamia Serikali. Kwa hiyo kama kuna jambo limeshauriwa, likashauriwa, likashauriwa, wewe umeliona ambalo unaona Bunge lifanyie maamuzi fulani ndio wakati wako huu. kwa sababu Serikali kwenye jambo hili na wao watakuwa wachangiaji kama mwingine, yaani haya yote yeliyosemwa na Kamati, yanayosemwa na Wabunge hapa watakaokuja kuhitimisha hoja ili Bunge lifanye maamuzi ni Kamati zetu, kwa maana ya Wenyeviti. Kwa hiyo saa hizi tunaisimamia Serikali, kwa hiyo endelea na mchango wako, hatushauri tu tunaisimamia pia. Karibu.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, ahsante, umenipa ufafanuzi mzuri. Sasa nitoe mfano wa Halmashauri ya Bunda ambayo ukienda kwenye chati ya kwanza kabisa kwenye jedwali la kwanza la ripoti hii ya LAAC, ni halmashauri moja tu kati ya halmashauri 184 yenye hati chafu ambayo ni hati mbaya. Sasa juzi wakati LAAC

2 NOVEMBA, 2022

inaendelea nilienda kwenye Kamati ya LAAC nikakuta kwenye ile ripoti ya Kamati ya LAAC wameandika Bunda imepata hati isiyoridhisha, nikajiuliza mbona CAG amesema ni hati mbaya? Mkaguzi aliyekuja kutoka Ofisi ya CAG akaniambia kwamba hiyo hati mbaya hatutumii, tunatumia lugha nzuri ya kutoridhisha, lakini ripoti ya CAG nimeisoma na ripoti ya Kamati nimeisoma imeandika Bunda hati mbaya. Sasa najiuliza ukaguzi wa CAG wanaenda kule halmashauri, wanakuta mambo mabaya, wanakuja kwenye Kamati halafu wanaanza kulemba, hiyo nayo hapana. Kwa hiyo tuache, kama mambo ni mabaya ni mambo mabaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka nitoe mfano...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Bunda, acha nikusaidie, siyo hati mbaya ni hati chafu ama inaitwa mbaya? Ama mbaya na chafu ni sawa? Hii inaitwa hati chafu na ndiyo ilivyoitwa huku, ndiyo inavyoitwa huku, kwenye taarifa, ni hati chafu maana mbaya na chafu ni vitu viwili tofauti. Endelea.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, sasa sitaki kwenda kwenye hiyo lugha kwa sababu nimesoma ripoti ya CAG imesema hati mbaya, nimesema ripoti ya LAAC imesema hati mbaya iliyoko hapa sasa hivi, kwa hiyo Kiswahili tuachane nacho tuendeleo na ambayo nataka kusema mimi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, 2000 ni majedwali hapa nasema utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi miaka iliyopita 2012/2013, ripoti kama hii ilienda Bunda kukawa na hoja

2 NOVEMBA, 2022

moja ya kujibiwa, haikujibiwa 2012/2013. Mwaka 2013/2014, hoja moja haikujibiwa; mwaka 2014/2015 hoja mbili hazikujibiwa; mwaka 2015/2016, hoja moja haikujibiwa; mwaka 2016/2017, hoja tatu hazikujibiwa; mwaka 2017/2018, hoja mbili, ikajibiwa moja; mwaka 2019/2020, hoja kumi na tisa, zikajibiwa tisa; jumla kutoka miaka yote hiyo tuna hoja 27 Bunda. Tukitoka hapo wanasema hati ya ukaguzi zilizotolewa miaka mitatu iliyopita, mwaka 2018, hati isiyoridhisha; mwaka 2019, hati yenye mashaka; mwaka 2020/2021, hati isiyoridhisha.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kujenga hoja yangu kutokea hapo, kwamba sasa tukisoma ripoti za 2012/2013, 2013/2014 na 2014/2015, zote zina ushauri wa CAG na Wabunge na matatizo yako palepale. Sasa niseme tuchukue uamuzi mgumu sasa tuseme, kwa ushauri huu sasa, kabla sijaenda Bunda, tuseme hivi katika hoja za LAAC na PAC, Bunge liseme hivi idara yoyote, wizara yoyote, taasisi yoyote ya umma ambayo haikutekeleza maagizo ya CAG na Wabunge mpaka tarehe 30 mwezi wa bajeti zao tusipitishie, si ndio tunasimamia au tunasemaje sasa, kwa sababu sasa tunamwambia nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme maneno mazuri hapa, kwamba CAG anaenda mbele ya Rais, anasema maneno mazito mazito umma unasikiliza, rais anatoa maelekezo tunasema vikao vya PAC na LAAC vitaangalia. Vikao vinakuja vinaangalia, vinaleta ushauri hapa, tunatoa ushauri miaka inapita, tunatoa ushauri miaka inapita, tunatoa ushauri, miaka inapita, ni lini sasa tutafanya maneno ambayo wananchi wanaweza wakasema tumechukua hatua.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, naomba kwenye Bunge hili tuchukue hatua, ndiyo maamuzi yangu, popote ambapo kuna fedha imeliwa, ukisoma fedha zilizoliwa katika idara mbalimbali ni kichefu chefu. Watoto wetu hawana madawati sasa hivi, watu wanalilia shule za msingi kuna maboma, bado tuna matatizo ya maji, tuna matatizo mengi, tunamhurumia nani anayekula fedha za umma? Kwa nini watumishi wa Serikali wa Tanzania hawaogopi hela ya umma? Wenzetu waliotutawala hapa juzi tu, siyo tu kula hela ukisema uongo Bungeni umeondoka, ukileta kabajeti hakana faida umeondoka, hapo uongee nini sasa? Sisi watu wanaokula hela ni walewale, wanaokula hela ni walewale, wanaendelea tu, kuna nini kinaendelea hapa? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende Bunda, Bunda nimekwenda kwenye LAAC, bahati nzuri Mwenyekiti aliyekuwepo ni aliyekuwa anaongea hapa, ukienda kwenye zile fedha za ile 4.4.2 haikwenda 41,461,000,000. Ukienda kwenye 20% za vijiji kurudishwa kwenye maendeleo 11,465,000,000 haikwenda; ukienda fedha za maendeleo 260,000,000 hazikwenda; ukienda fedha mbichi 96,000,000 zimeliwa kabla hazijaingia benki; tumepewa 1,000,000,000 na mama ya kujenga Halmashauri ya Wilaya, 626,62,000 wamepewa wazabuni, hawajaleta vifaa, yaani wamepewa tu nenda mkanunue, nenda mkanunue, bila ukaguzi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, LAAC imeomba kwenda Bunda, naomba uwape ruhusa waende, wasimamie watakuletea madudu. Leo tunapozungumza hapa mama ametoa fedha

2 NOVEMBA, 2022

467,000,000 kwa sekondari mbili, karibu milioni mia sita na kitu, wamekwenda kwenye kiwanda cha dragoni, wamenunua bati moja 69,140 badala ya 52,000 tumeenda Madiwani, tumekwenda mpaka tumepata vielelezo vyote vya kutosha, tukawaambia watumishi rudisheni hela, hawajarudisha wanasema eti TAKUKURU imechukua taarifa inapeleka. Hivi hizi hela za umma zitaliwa mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, leo ukimwambia mwananchi wa kawaida kwamba fedha yake ya hospitali imeliwa shilingi laki moja ni tofauti na kumwambia bandari imekula 30,000,000. Wananchi wanapopelekewa fedha na mama inawauma sana kuliwa kwa sababu miradi yao haitaenda. Sasa hivi vitu tunafanyaje kweli kama tuna Mawaziri, tuna nani, tunafanyaje? Hivi kweli tunamlilia nani kila siku hii Serikali? Mimi si nimwombe mama aniteue hata Waziri wa TAMISEMI jamani hata siku moja? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunafanyaje sasa vitu vinaliwa vinaenda tunaangalia kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu ndio hayo machache tu. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Haya. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ajiandae

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii uliyonipa niweze kuchangia hizi taarifa za Kamati ya PAC, LAAC na PIC ambazo zimeripoti juu ya taarifa ya CAG.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa ajili tu ya kumbukumbu Mheshimiwa Getere alikuwa WEO, naona tumefuatana Ma-WEO hapa na mimi nilikuwa WEO wa Kata ya Ngoboko, kwa hiyo tuko hapa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana na kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote hizi tatu, hoja zao walizoziwasilisha hapa Bungeni zimesheheni mambo mengi zimesheheni uchambuzi mkubwa juu ya taarifa na juu ya matumizi ya fedha za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nikianza na taarifa ya PAC labda kwa sababu nimepitia haraka. Kuna mambo makuu matatu ambayo sijayaona na nilitarajia niyaone kwenye taarifa hii. Deni la Serikali, Kamati ya PAC wanajua kwamba deni la Serikali kwa mujibu wa takwimu zilizowasilishwa kipindi kile zilionyesha kwamba Serikali imekopa zaidi ya kile kilichoruhusiwa na Bunge. Kwa hiyo tulitarajia kwamba kama sehemu hii ya deni la Taifa ingewasilishwa, wangeweza kuwa wameeleza vizuri juu ya mkanganyiko huo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, jambo ambalo nilitarajia kwamba wangeweza kulieleza vizuri kwenye taarifa hii Kamati ya PAC ni suala la malimbikizo ya kodi za makinikia shilingi trilioni 360, ambazo maelezo yanatolewa kwamba fedha hizi zimeshasamehewa zote, lakini maelezo mengine yanatolewa fedha hizi hazijasamehewa. Hili nalo nilitarajia kwenye taarifa ya PAC lingekuwa limeandikwa vizuri, lingelielekeza hili Bunge kujua hatma ya hili eneo.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu nililotegemea lielezwe vizuri ni eneo la uhamishaji wa bei ya mauziano ya bidhaa na huduma baina ya makampuni yenye mahusiano ya kimataifa, *transfer enterprising* ambako katika taarifa ya CAG ya mwaka 2019/2020 na mwaka 2020/2021 ilionesha kwamba katika hili eneo hatukusanyi mapato yanayostahili. Kwa hiyo nilitarajia Kamati hii ingeweza kushughulika na haya maeneo, lakini bahati mbaya sana sikuweza kuyaona kwenye taarifa yao.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nataka kuchangia hapa ni suala la malipo yaliyofanywa na Serikali kwa Kampuni ya *Symbion Power LCC*. Serikali imelipa bilioni 360 kwa hii kampuni kwa maana ya dola milioni 153.43. Mkaguzi anatueleza na Kamati imetueleza kwamba makubaliano haya yalifanyika bila kujumuisha kodi wala gharama zingine. Sasa maswali ya kujiuliza ni kwa nini Serikali illipe bilioni 350 kwa Kampuni ya *Symbion Power* bila kuangalia *Symbion Power* inadaiwa kodi kiasi gani na Serikali, bila kuangalia gharama ambazo *Symbion Power* anahusika kuilipa Serikali na je, kulikuwa na udharura gani haraka tu baada ya makubaliano Mei, 2021 ya kulipa hizi fedha, kwa nini zililipwa haraka palepale na kama zililipwa kwa dharura namna hiyo, nani aliidhinisha fedha hizi? Kwa maana Bunge hili lilikuwa tayari limeshaidhinisha bajeti ya mwaka 2020/2021, sasa ilipofika Mei zimelipwa bilioni 350 na Serikali kwa Kampuni ya *Symbion Power*. Hizi fedha zilitoka wapi? Nani aliziruhusu wakati Bunge hili lilikuwa limeshapitisha bajeti tayari?

Mheshimiwa Spika, katika huo mwaka wa fedha tulikuwa na miradi mingi ya maendeleo iliyokuwa inatakiwa

2 NOVEMBA, 2022

kutekelezwa. Serikali iliwezaje kulipa fedha hizo wakati bajeti ya Serikali ilikuwa imeshapitishwa? Hata hivyo, Mkaguzi hapa anatuambia kwamba hapa kulikuwa na usimamizi mbaya wa mkataba. Hawa waliosimamia mkataba vibaya mpaka nchi yetu wameisababishia kulipa bilioni 350 ni akina nani? Mbona hawajatajwa? Waliosababisha mpaka tukala hasara hii kwa Serikali hii ya wananchi maskini, bilioni 350 imesababishwa na mtu kusimamia mkataba mbaya, aliyesusimamia huu mkataba mbaya ni nani mpaka tukalipa shilingi bilioni 350 na kwa nini huyo mtu hatajwi? Aliusimamamia vipi huo mkataba vibaya?

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ulikuwa unaisha tarehe tarehe 18/09/2015, lakini ulikuja kuuhishwa na makubaliano ya tarehe 15/9/2015, siku tatu kabla ya mkataba kufika mwisho. Mkataba huu ulihuishwa kwa dharura namna hiyo kulikuwa na shida gani kwa sababu Bunge la wakati huo lilikuwa limeshaambiwa kwamba huu mkataba umefika mwisho na hautaendelea.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani shilingi za Watanzania bilioni 350 kulipwa bila kufanyika uhakiki wa kutosha. Najjuliza hizi kodi za Serikali, yaani huyu *Symbion Power* analipwaje kwa sababu cha kwanza kama yeye alikuwa anatudai shilingi bilioni 350, sisi tulikuwa tunamdai kodi, kodi zetu ni shilingi ngapi tunazomdai? Leo anakuja kulipwa shilingi bilioni 350, nchi hii ya maskini, kweli kabisa?

Mheshimiwa Spika, suala la Tatu, ni malimbikizo ya kodi ambazo zilikuwa zinashikiliwa na Mamlaka ya Rufani za Kodi (TRAB na TRAT) yapatayo Trilioni 360. Serikali ilituambia hapa

2 NOVEMBA, 2022

Tarehe 24 Januari, 2020, Serikali ilifuta madai haya, kwa maana Serikali tukawa hatudai tena. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya CAG ya Mwaka 2019/2020 inatambua kuwa Serikali inadai Shilingi Trilioni 360, ilipofikia taarifa ya CAG ya mwaka 2020/2021 CAG anasema: “inaonesha kuwa kesi za makinikia zipatazo 45 zenye thamani ya Shilingi Triloni 5.595 ziliamuliwa na Mamlaka za Rufani za Kodi, *TRAB* na *TRAT*”. Kodi hizo zilipoamuliwa, Serikali ikaagizwa kufafanya majadiliano na makampuni hayo yaliyotakiwa kulipa hizo kodi. Kwa hiyo, inaonekana kwamba katika Mahakama hizi, ziliamua kati ya Trilioni 360 zilion nchi yetu inastahili kulipwa, kwa maana ya Mahakama Trilioni 5.595.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikafanya majadiliano na makampuni hayo yanayotakiwa kulipa ili wakubaliane namna ya kulipa. Kampuni la kwanza ambalo linatajwa kwenye Taarifa ya CAG ni Kampuni la *North Mara Gold Mine*; Kampuni ya Pili ni *Pangea Mineral Limited*; Tatu ni *Bulyanhulu Gold Mine* na Nne ni *ABG Exploration*. Kwa mujibu wa taarifa ya CAG ya Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, nikafuatilia ripoti za viongozi waliokuwepo kama waliweza kulisamehe hili deni. Nikafuatilia taarifa ya vikao vyote ambavyo Mheshimiwa Rais Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliwahi kukaa na *Barrick* juu ya jambo hili. Nikafuatilia taarifa za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kama aliwahi kuzungumza jambo lolote kuhusiana na kusamehewa kwa kodi hizi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, hotuba zote za Viongozi hawa nimezisikiliza, hakuna mahali popote ambako wamesema fedha hizi zimefutwa. Mahakama iliagiza kampuni ya madini pamoja na Serikali yajadiliane namna ya kulipa Trilioni 5.595. Aliyeenda kufuta kodi za Watanzania hizo ni nani? Serikali lazima ituambie ukweli juu wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala hili lipo kwenye taarifa ta CAG ukurasa wa 60 mpaka 63, Mheshimiwa CAG alete taarifa juu ya jambo hili ili Watanzania wajue hitimisho na ukweli wake juu ya fedha zao. Nchi hii maskini haiwezi kuingia kwenye makubaliano ya kwenda kusamehe kodi kubwa zote hizo, halafu tukaendelea kwenda kutoza kodi kwa wananchi, kodi ndogondogo tunaendela kutoza, halafu wafanyabiashara wakubwa kama hao wanasamehewa na nani? Kwa ajili ya nini? Tulishaelezwa kule mwanzo hizi kodi zilipatikanaje! Watu walikuwa wanatengeneza mahesabu ya aina mbili, mahesabu ya kulipia kodi na mengine ya kukwepea kodi na kuonyesha uhalisia kule kwao wanaporipoti, tuliona ukweli huo! Sasa aliyeenda kusamehe alisema nini? Kwamba mlifanya vizuri tu kutupunja, tumewasemehe. Alienda kusamehe akisema nini katika nchi maskini kama hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umesema vizuri sana leo, kwamba sisi tunaisimamia Serikali na Serikali leo itoe kauli juu jambo hili, tulimalize. CAG akachukue *documents* zote, kama kweli Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alisamehe hili deni, kama kweli Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alisamehe hili deni. Tuletewe hapa ili tuweze kufanya maamuzi zaidi kama Bunge. *(Makofi)*

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, suala la Nne ni kuhusu *TRA*, Kamati hapa imetueleza, inasema kwenye eneo la malimbikizo ya kodi yasiyo na kesi. Amesema vizuri hapa Mtendaji wa Kata mwenzangu ameeleza vizuri sana, kwamba hivi tutasemaje sasa, tuna Taasisi yetu inayohusika na ukusanyaji wa mapato ya Serikali, inafika mahali kwa mwaka mmoja kodi ambayo haijakusanywa na hazina kesi Mahakama ni Trilioni 3.87. Katika Taasisi inayokusanya hata Trilioni 20 haifikishi. Trilioni 3.87 hazijakusanywa na hazina Mahakamani, sasa hii Taasisi yetu inachangamoto gani? Wanaeleza kwamba malimbikizo haya yameongezeka kwa asilimia 95 ya madai ya kodi.

Mheshimiwa Spika, hii taasisi yetu ina shida gani, kwa sababu hata tungeongea namna gani, hatuwezi kuyaleta maendeleo ya Watanzania kama hii taasisi haiwezi ikafanya kazi sawasawa. Trilioni 3.87, hizi ni zile kodi ambazo hazina kesi Mahakamani, kuna kodi ambazo zina kesi Mahakamani, ukizijumlisha zote hizo karibia asilimia 30 ya mapato hatuyakusanyi! Sasa kama hatuyakusanyi, tuta-*survive* namna gani? Maendeleo tuliyoyaahidi na kwenye Ilani ya Uchaguzi na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, tutaujenga na tutalipa na nini? Madeni tunayokopa leo tutayalipa na nini? Kama hatuwezi kukusanya kodi, tukaweza kulipa madeni, tukaweza kujenga, tukaweza kuhudumia Serikali.

Mheshimiwa Spika, ifike mahali sasa tuwe tunaambiwa ukweli, eneo hili la Taasisi yetu ya *TRA* kama inalo tatizo ambalo lenyewe lipo juu ya uwezo wake kwa nini tusiambiwe kama Bunge tuamue? Kuna mambo mengine

2 NOVEMBA, 2022

tu wanalalamika, mara watumishi wachache, hivi kweli kabisa anayepanga watumishi unaweza ukaamua Taasisi inayolipa watu mishahara yote na yenyewe ikawa na upungufu wa watumishi kabisa kabisa ukawa na nia njema na Watanzania hawa?

Mheshimiwa Spika, *TRA* ikose fedha ambaye analipa mishahara ya watu wote, *TRA* anapeleka fedha za maendeleo kote, ambaye anatulipia Deni la Taifa, huyo naye awe na upungufu wa watumishi? Kama kuna matatizo yaliyojificha kwa *TRA*, kama ni udhaifu wa *TRA* uwekwe wazi, kama kuna udhaifu wa *TRA* ambao upo juu ya uwezo wao, Bunge hili linahitaji kufanya maamuzi, tufanye maamuzi leo, tuiwezeshe Taasisi hii na tuchukue hatua kwa wale ambao wanaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumza malimbikizo ya kodi yasiyokuwa na kesi yamefikia trilioni 7.54 jumla...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Mpina, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Simbachawene.

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba Mheshimiwa Mbunge anayechangia Mheshimiwa Mpina, ameshalizingumza hili jambo hili Bungeni mara kadhaa. Pengine Mheshimiwa Mpina ili aweze kutenda haki na kwa

2 NOVEMBA, 2022

sababu yeye ni Mwanataaluma wa eneo hili ni vizuri akaelezea vizuri kinachotokea katika masuala ya rufaa za kodi. Kunapokuwa na mgogoro, kodi ikawa inabishaniwa kati ya Mlipa Kodi na TRA kile kiasi ambacho hakibishaniwi mfanyabiashara anayetakiwa kulipa huwa kinalipwa na Serikali inachukuwa kiasi chake. Kinachobaki ambacho kina-*dispute* kinaingia kwenye mgogoro, kwa hiyo ni kwa sababu ni maisha ya shughuli mbalimbali zinazoendelea na wafanyabiashara, kuna uwekezaji, kuna mambo mbalimbali, huendelea kwa sababu ni suala la mgogoro na ni suala la haki.

Mheshimiwa Spika, katika kundi la hao wanaodaiwa wengine waloshafunga makampuni, wameshindwa kufanya biashara, hapa mnasema tuvutie wawekezaji, hapa mnasema tuhakikishe kwamba wawekezaji wanapata mazingira mazuri, ni katika mazingira hayo ambayo yamepelekea hata baadhi ya wawekezaji kuondoka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali makini kama hii ambayo tunatafuta pesa kila siku, hatuwezi tukaacha kudai kodi, hatuwezi tukaacha kudai mapato ambayo Serikali inataka kuyapata, lakini sasa tunapokutana na mgogoro ambao kile kiasi kinachobishaniwa kinabaki katika mgogoro lakini kile cha msingi kinakuwa kimelipwa. Kwa hiyo, hakuna hakuna fedha iliyoachwa makusudi ila kuna kesi. Kesi ni suala la haki jamani, hauwezi kusema leo hii kwa sababu ni Serikali mmeacha. Isionekane hivyo, kwa hiyo ielezwe vizuri. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mpina unaipokea taarifa hiyo?

2 NOVEMBA, 2022

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, taarifa yake siipokei na sababu ya kutokuipokea ingekuwa haya maelezo yake yanakubalika angeyapeleka kwa CAG, CAG angetuandikia hapa Kamati inasema malimbikizo haya yanatokana na kutokushughulikiwa ipasavyo kwa madeni ya kodi mathalani mwaka 2020/2021. Hawa Mawaziri wetu wasome taarifa, wasiwe wanapoteza muda wetu hapa tunapochangia hapa Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kusisitiza malimbikizo ya Trilioni 7.54 na hizi hazina kesi Mahakamani, TRA walitakiwa kukusanya, nikaeleza kwamba kwa mwaka mmoja wamefeli kukusanya malimbikizo ya Trilioni 3.87, mwaka mmoja wa 2020/2021. Kama tutaenda namna hiyo, utakusanya kodi ya nani, kama tutaenda hivyo, tutaijenga nchi yetu kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba mambo makubwa kama haya yakiletwa hapa Bungeni, yakielezwa kwa ufasaha, Bunge lako litaelewa na litajua hata lichukue hatua gani.

Mheshimiwa Spika, kama muda unaniruhusu nimalizie suala la mwisho. Suala la mwisho ni suala la utoaji mikopo asilimia 10 ya akina mama, vijana na Wenye Ulemavu. Wenzangu hapa wamechangia na bahati nzuri Kamati ya LAAC imelizungumza suala hili, ninachotaka kushauri ni kwamba sasa hivi tunavyoenda hili eneo ni kubwa, Taasisi inayosimimia ambayo siku hizi inaitwa *Division* ya Maendeleo ya Jamii, haina uwezo wa kulisimamia jambo hili. Idara Zetu za Maendeleo ya Jamii hazina watu

2 NOVEMBA, 2022

competent wa mambo ya fedha, hazina watu *competent* wa kusimamia mikopo, unaenda kumchukua Afisa wa Maendeleo ya Jamii asambaze mkopo wa Bilioni Mbili, asambaze mkopo wa Bilioni Kumi, asisimamie, azikusanye, azilitele, akaunde vikundi na akopeshe tena.

Mheshimiwa Spika, jambo hili tulianzisha vizuri lakini kadri tunavyoenda zipo halmashauri mapato yao kwa mwaka ya *own source* yanafikia hata Bilioni Ishirini. Kwa maana hiyo, ukichukua asilimia kumi yake kwa mwaka wanapata bilioni Mbili, ukichukua kwa miaka Saba tu, wanafikia kile kimo cha kuanzisha benki cha Bilioni 15. Sasa kama ndivyo ilivyo, kwa nini tusianzishe utaratibu wa hizi fedha zikakusanywa, tukaingia na benki ambazo zinapatikana maeneo ya karibu, NMB na CRDB, tukaweka masharti ambayo hayaathiri malengo na maksudi yaliyowekwa na Serikali. Mikopo hii ikaanza kupitia kwenye Benki, lakini mchakato wake wa awali utakanywa na hii Idara yetu ya Maendeleo ya Jamii na fedha hizo zikaanza kutolewa kwenye Benki, ambako kuna *competent personnel* waliosomea mambo ya utoaji wa mikopo, kule kuna watu wanaoweza kuifuatilia mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunashuhudia changamoto nyingi, sehemu zingine upendeleo mkubwa, wanapewa kundi la watu hela yote ya Halmashauri inachukuliwa na watu wawili watatu inaisha, sehemu nyingine fedha hawakusanyi, unakuta asilimia 20 tu ya marejesho leo miaka mitatu, miaka mingapi. Kwa hiyo, kwa changamoto hizi za upendeleo na uwezo wa kusimamia kodi zenyewe na idara zetu na upungufu wa watumishi tulionao, hili eneo hatuna uwezo wa kulisimamia vizuri.

2 NOVEMBA, 2022

Ningesauri tuende kwenye *MOU* na benki zinazoweza kuhudumia suala hili, najua linaweza kufanyika vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, zipo taasisi kama *PASS* ziliweza ku-*guarantee* watu wetu kwenye kilimo, wanafunzi vijana na kadhalika zina-*guarantee*, sasa Serikali na yenyewe...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia. Kabla ya yote nipongeze taarifa zote za Kamati Tatu na niwapongeze Wajumbe kwa namna ambavyo walijitoa kuchakaka na kujadili kwa kina taarifa hizi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na umuhimu wetu kama Muhimili wa Bunge, kuna sehemu pekee ambayo sisi tumepewa hiyo neema ya kuisimamia Serikali. Kama kuna eneo Taifa letu linapata hasara na kupoteza fedha ni eneo la mikataba, nami nitajikita eneo hilo la mikataba.

Mheshimiwa Spika, wakati tunajadili hapa taarifa iliyopita ya Kamati yetu ya *PAC*, ilijadili kuhusu mkataba

2 NOVEMBA, 2022

ambao ulikuwa unahusiana na *NFRA* wa ujenzi wa vihenge, mpaka leo nazungumza hakuna kitu kimefanyika, kwa namna nyingine alizungumza Mheshimiwa Getere hapa kwamba tunamwambia nani? Unaweza usimuelewe, lakini kama tunazungumza tunaleta taarifa kama Kamati ya Bunge ili Bunge lipitisha na Bunge likapitisha tunakuja kutoa taarifa kwa mara nyingine jambo lile halijatekelezwa, inatia uchungu wakati mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yule Mkandarasi hatujui anafikiri nini mpaka leo, lakini wakati Wabunge wanajadili yale matrekta mabovu, ndiyo huyo huyo msumbufu Mkandarasi ambae hakuna maamuzi yoyote yamefanyika mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nazungumzia suala la mikataba nilikuwa najiuliza machache sana, kwa nini tunaingia mikataba mibovu? Je, nchi yetu inashida ya Wanasheria? Je, ni kweli nchi yetu imeshindwa kuwashirikisha kikamilifu wanasheria wetu washauri vizuri tunapoingia mikataba? Ni kweli Wanasheria wanapitia hiyo mikataba kabla hatujaingia kwenye hiyo mikataba? Na ni kweli wanatoa ushauri wa kina? Je, huo ushauri ni kweli Wizara inazingatia?

Mheshimiwa Spika, ukianza kutazama hasara hizo ambazo tunazipata kama Taifa kupita mikataba, utapata maswali mengi ambayo hayana majibu. Aidha, Wanasheria wetu wanatumika kuhujumu nchi yetu, kwamba wanajua kwamba mikataba huu tumwambia yule mtu apite uchochoro ambao anaweza kutokea. Ninatoa mfano tu wa vitu vichache kwa sababu ni vitu vingi ambavyo tunapata hasara kama Taifa. Ukitazama Shirika letu la

2 NOVEMBA, 2022

Umeme TANESCO, Symbion namna walivyoingia huo mkataba na hasara ambayo tumeipata kama Taifa ya malipo ya Dola za Kimarekani Milioni 153.43.

Mheshimiwa Spika, ni huzuni na inaumiza sana, yaani wameshaingia mkataba, umeanza kutekelezeka, wanafika katikati wanagundua kuna makosa, wanaamua sasa ngoja tujiondoe kwenye huo mkataba. Hawajui madhara yanayoweza kutokea baada ya wao kujiondoa, ndiyo hapo ninaposema, Je, ni kweli Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inashirikishwa kwenye mikataba hii? Hasara hii ya Dola za Kimarekani, Milioni 153 ingesaidia Watanzania wangapi huku kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri watu wawe wanaangalia ikitokea mkataba kama huu umeingiza hasara kwenye Serikali yetu, ni watu gani wameshiriki, wakiwa wanachukuliwa maamuzi mapema inawezekana tukaokoa fedha zingine kwenye mikataba mingine inayokuja na wengine wakajifunza, kwamba kwa kupelekea hasara kwenye Taifa, yeye mwenyewe anaweza akatolewa pale kama mfano, lakini unaona mambo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya tumewahi kushauri Bunge lililopita, kwamba ni vizuri Bunge lishirikishwe kwenye mikataba hii, kwa sababu hasara inayotokea kwenye Taifa ni wananchi wetu wanaoenda kuumia. Ni vizuri kama Bunge litashiriki yawezekana tukashauri mambo kadhaa kabla ya kupata hasara kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ambazo zinaingiza hasara pia kupitia mikataba ni TANROADS. Kwa hali ya

2 NOVEMBA, 2022

kawaida, siamini kwamba TANROADS wanaweza kukosa Wanasheria makini wa kushauri kuingia kwenye mikataba. Mara nyingi tunapata hasara kwenye TANROADS sehemu gani? Ni pale ambapo, TANROADS inashindwa kuwalipa Wakandarasi kwa wakati. Wanasheria kama wameshirikishwa ni lazima washauri. Ukitazama kila Bunge hili jambo litazungumzwa. Sasa kama linazungumzwa kila Bunge halafu tunakuja tena tunazungumza, ndiyo maana tunarudi kulekule kwa Mheshimiwa Getere, tunasema nini na tunamshauri nani? Lakini kwa sababu ni wajibu wetu tutaendelea kushauri.

Mheshimiwa Spika, TANROADS pekee yake, wameingiza hasara ya Bilioni 68.73 kwa kuchelewa kuwalipa Wakandarasi. Hizi fedha ambazo Mheshimiwa Rais anazunguka kutafuta, kwamba watoto wasihangaike kwa ajili ya madarasa, lakini kuna nyingine hasara za ajabu na za kizembe tu zinafanyika kwenye Taifa letu. Kuna haja ya kuangalia vizuri mikataba yote kuna shida gani, nani anakubaliana na hili jambo, nani yuko nyuma ya haya mambo yanayofanyika. Mimi siamini kama Wanasheria wanashirikishwa kikamilimu na kama wanashirikishwa wao wenyewe wanahusika kutuhujumu kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la vihenge nimkwishalizungumzia. Yule mkanadarasi hatujui mpaka leo anawaza nini na fedha alishalipwa zaidi ya Dola za Marekani milioni 33, yuko huko na hatujui nini kitaendelea mpaka leo; kwa sababu yeye alikuwa ametishia kupeleka mahakamani lakini sisi kama taifa tupo tu na kuna vihenge havijamalizika mpaka leo. Kwa hiyo kuna haja sasa ya kufanya maamuzi kwenye jambo hili.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri kwenye jambo hili. Ninashauri Serikali ichukue hatua za makusudi kwa watendaji wote waliosababisha hasara hizo kwa makosa ya uzembe au kwa makosa ya kuruhusu kuingia mikataba kama hiyo ambayo inaleta hasara kwa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanapokuwa wanasikia kuna mkataba umesainiwa, wanaambiwa tu hivyo; lakini baadaye ukija kukuta mambo yaliyopo; lile kundi ambalo linakuwepo pale wakati mkataba unasainiwa; sisi tunaamini kabla ya kusaini kuna watu wameshaka, jopo la wataalamu mbalimbali likapitia ule mkataba, unamaslahi kwa taifa? Je, ni hasara gani ambayo tunaenda kuipata kama taifa? Je, hakuna eneo lingine ambalo tunaweza tukapata fedha mpaka kuingia kwenye mkataba mbovu?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba hatua zichukuliwe, pia zichukuliwe kwa wakandarasi wote ambao wanafanya makusudi na uzembe wakiamini kuna uchochoro wa kutokea; kwamba kuna sehemu watatokea tu. Ndiyo maana nasema na wanasheria wanakuwa wanahusika kwa wakati mwingine. Kwa sababu kama mkataba wameupitia na wanajua lazima washauri vizuri, wakiwashauri vizuri tutajua kwamba shida ipo kwa wataalamu wetu na hatua zichukuliwe kwa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nimezungumzia kwenye suala la mikataba, narudia tena kusema. Kuna haja ya uchunguzi wa kina tunapokuwa tunaingia kwenye hii

2 NOVEMBA, 2022

mikataba kama wanasheria wetu au Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashirikishwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naomba nihame hapo kidogo, niende kwenye kamati ya LAAC. Katika miradi ambayo inaendelea hivi sasa kwenye halmashauri zetu, ikiwemo ujenzi wa madarasa; ni jambo jema sana ambalo analifanya Mheshimiwa Rais. Ukitazama jambo hilo jema, tuna ma-engineer wachache sana; wamezungumzia changamoto ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, leo walimu wameingizwa kusimamia ujenzi wa hiyo miradi kwenye halmashauri zetu. Mwalimu anajua taaluma yake ni kufundisha, unampeleka akasimamie jengo ambalo, tena ni la *pressure*. Ukitazama zile fefdha za COVID, wote mnajua presha iliyokuwepo kwenye ujenzi wa yale madarasa. Umemuweka mwalimu, tena kwa bahati mbaya zile kamati zote nne walimu wapo. Kwa hiyo walimu zile siku 90 zote badala ya kufikiri kuwafundisha wanafunzi wetu wanafikiri kuhusu miradi ya ujenzi. Kwa bahati mbaya zaidi, yeye kwa sababu si taaluma yake, ukitazama yale madarasa ya COVID, nafikiri Waheshimiwa Wabunge wote wameshapita kwenye maeneo yao wameona. Mimi sijajua kama ni lile jina, au ni nini.

Mheshimiwa Spika, kabla hayajakamilika, yana ufa. Unaanza kuwaza ni jina hili lenyewe COVID ndilo limeendana na hii kasi inayokwenda ya madarasa kuharibika au kuna nini?

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kunakuwa na masharti mengi, ni vizuri tujue, tuko hapa leo kuna madarasa ambayo yalijengwa na wazazi wetu yapo imara; lakini madarasa ya sasahivi yanajengwa, yaani ni kama watu hawawi na mtazamo kwamba hivi tunajenga hili darasa tukitazamia miaka mingapi mbele? Wanatazama kumaliza, ukifika pale utaona rangi inapendeza, ndani ya miezi mitatu ufa umetokea pale, yaani mambo hayaeleweki.

Mheshimiwa Spika, na kama ni wajibu wetu sisi kama Bunge, kuisimamia Serikali, kuna haja ya kuona kwamba mikopo tunayokopa, tunalenga nini? Tunataka kua-achieve nini? Tunataka ku-achieve kwa muda gani ambao tunafikiri kwamba angalau lile lengo ambalo tumelenga litaonekana kwa muda fulani.

Mheshimiwa Spika, leo tunamaliza ndani ya mwaka mmoja hali ni mbaya; kuanzia kwenye sakafu, ukuta na unaanza kujiuliza ni kwanini? Ni kwa sababu ya *pressure* tuliyokuwa nayo ya kujenga madarasa au shida ni kwa sababu wataalamu wetu hawakutosha. Tulitumia walimu wenye taaluma nyingine kuwapeleka kwenye taaluma ambayo si ya kwao labda ndiyo maana hayo mambo yametokea.

Mheshimiwa Spika, hapo nataka nizungumze kidogo kwenye suala la hawa watu ambao wanaitwa maafisa manunuzi kwenye halmashauri zetu. Yaani kama unavyoona changamoto hizi zingine, ukienda kwenye halmashauri, yaani kila mradi ukienda lazima utakuta kuna madudu tu kwa hawa watu wanaitwa maafisa manunuzi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, kuna haja ya kufuatilia kwa kina, je, wale maafisa manunuzi waliopo kule ni kweli wana taaluma hiyo? Kwa sababu fedha hizi zote ambazo tunapeleka, mabilioni na mabilioni, wasimamizi ndio hawa wanaoenda kuhusika na manunuzi. Ni kweli wanayo elimu ya kuweza kusimamia hizo fedha? Kama sivyo kuna haja sasa ya kuendelea kupitia upya, kwenda kuwatazama, halmashauri kwa halmashauri ili kama shida ni maafisa manunuzi kwamba hawapo wenye sifa, Serikali ifanye kazi ya ziada ya kuwaajiri hao kwanza kwa kuwa wao ndiyo wanaokwenda kuhusika na manunuzi ya kila kitu.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema hapa, kwamba ni vizuri yale mabaraza na kamati za fedha wanapokutana na Wabunge wahusike. Muda mwingi tupo hapa Bungeni. Ulipokuwa unazungumza asubuhi, kwamba na ninyi Wabunge muone huko mnakotokea, kiukweli hali ni mbaya, na ukifika huwezi kuwaambia mlikopita hapa hamkufanya vizuri watakushangaa. Kwa hiyo kwa sababu wewe undingia *automatically* kwenye kamati hiyo inabidi uliache tu lipite, liende, eeh!

Mheshimiwa Spika, na kwa mazingira ya kawaida huwezi kusimama mle ukaanza kukosoa, wanasema wewe ni mjumbe wa Kamati ya Fedha na Mipango, lakini hukuwepo wakati hilo jambo linafanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba na hilo jambo mliangalie tena, kwa sababu tukipunguza hayo mambo wenyewe

2 NOVEMBA, 2022

kule hapa tuatapunguza mambo mengine ambayo hayana sababu. Wabunge tutakwenda huko sisi wenyewe kwenda kusaidia haya badala ya kuja kuleta hoja nyingine ambazo hazina sababu ya kuwepo hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Simon S. Lusengekile, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, ajiandae.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa hii nafasi. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Sisi watu wa Manyoni tunamshukuru sana kwa fedha ambazo ameleta nyingi sana za miradi.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitachangia maeneo makubwa mawili. Eneo la kwanza nitachangia kuhusu Mfuko wetu wa Bima ya Afya ya Taifa, na nitajikita zaidi kwenye suala la matumizi ya TEHAMA. Eneo la pili nitachangia kuhusu mfumo wa ujenzi wa viwanja vya ndege ambao kwa sasahivi kuna mkanganyiko kati ya TANROADS na Wakala wa Usimamizi wa Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA).

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la bima ya afya. Sasahivi tunaenda kwenye mchakato ambapo tunataka kuja na bima ya afya kwa wote. Naomba nikiri

2 NOVEMBA, 2022

kwamba nimepitia taarifa ya CAG na tumefanya uchambuzi kwenye kamati yetu ta PIC. Sidhani kama Shirika la Bima ya Afya ya Taifa ambalo hili shirika tunalo sasahivi lina uwezo wa kuistahimili kubeba watu takribani milioni 61.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Shirika la Bima ya Afya linahudumia wanufaika takribani milioni 4.6. Kati ya hawa milioni 4.6 milioni 1.2 ni wale wanaochangia. Tunategemea kama tutakuja na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, hili shirika litahudumia watu zaidi ya 60,000,000.

Mheshimiwa Spika, nikwambie tu kwamba shirika letu linamatatizo makubwa sana na nitaomba niyaseme.

Mheshimiwa Spika, nimepitia taarifa ya CAG, lakini tulipitia taarifa ya TR. Vile vile tulifanya uchambuzi kwenye kamati yetu. Shirika hili lina matatizo makubwa matatu. Kwanza, tulitegemea hili shirika liweze kujikita zaidi kwenye matumizi ya TEHAMA. Shirika linatumia kwa kiwango kidogo sana TEHAMA, hususan maeneo ya vijijini. Lingine, kuna udanganyifu mkubwa sana kwenye utoaji wa ile huduma, hususani kwenye matumizi ya kadi. Nitatolea mfano baadae. Jambo la tatu, tulitegemea shirika lingejikita zaidi katika kukusanya madeni, hata hivyo Shirika halijaweza kukusanya madeni. Kuna madeni mengi sana ya zaidi shilingi bilioni 10 yapo nje, na tunategemea hili shirika lijikite kweye uwekezaji; litaweza kuwekeza vipi kama halina *capacity* ya kukusanya madeni?

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, hoja yangu ni kwamba, tunategemea mbali ya kwamba hili shirika lengo lake ni kusajili wanachama na kutoa huduma, lakini linahitaji

2 NOVEMBA, 2022

kujikita katika kuwekeza. Uchambuzi wetu tulioufanya kwenye Kamati ya PIC, tuliona kwamba kama itaenda na *trend* hii nadhani uwezo wake wa kuwekeza utakuwa mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, nilifanya uchambuzi wa taarifa ya CAG. Katika taarifa ya CAG, nitatoa mfano. Kuna wafanyakazi 2,495 wa sekta binafsi ambao wanatoka katika kampuni 87, hawa walisajiliwa kama wafanyakazi wa umma. Hili ni tatizo kubwa sana la mfumo wa TEHAMA. Jambo lingine, taarifa ya CAG inasema kuna wanachama 165 ambao kimsingi sheria inasema wale wategemezi wasizidi watano, lakini wanachama zaidi ya 165 walikuwa na wategemezi ambao wamezidi kiwango kile ambacho sheria imesema. Hili ni tatizo kubwa la mfuko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba kuna wategemezi 73 waliosajiliwa kama wachangiaji. Hili pia ni tatizo kubwa sana la mfumo wetu wa TEHAMA. Mbali na hiyo, taarifa ya CAG, inasema kwamba kuna wanufaika 731, ambao ni wanaume walipata huduma ya upasuaji wa kujifungua, na haya malipo yalilipwa. Naomba nirudie, taarifa ya CAG, inasema, kuna wanufaika 731, wanaume walipata huduma ya kujifungua na haya madai yakapelekwa NHIF yakalipwa. Hili ni tatizo kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, kuna wanachama 444, walipata huduma ya *full blood picture* zaidi ya mara moja kwa siku. Narudia tena, kuna wanachama 444, walipata huduma ya picha kamili ya

2 NOVEMBA, 2022

damu, yaani *full blood picture* zaidi ya mara moja kwa siku ndani ya siku 30. Hili ni tatizo kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kulingana na kanuni za *NHIF*, ni kwamba mwanachama akipewa miwani mara moja kwa mwaka, hatakiwi kupewa miwani tena. Madai yaliyopelekwa na wanachama, kuna wanachama walipata miwani zaidi ya mara moja ndani ya mwaka mmoja. Hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine kubwa. Nimepitia taarifa ya CAG. Katika taarifa ya CAG, kwanza kuna madai ambayo yalikataliwa kabisa na shirika la bima. Kwa mfano, madai kutoka Muhimbili na madai kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete zaidi ya Shilingi bilioni 3.87 yalikataliwa. Sababu ya kukataliwa ni kwamba kuna kughushi na taarifa zisizo rasmi. Ndiyo maana nimesema kama tunataka hili shirika ndiyo libebe bima ya afya kwa wote, kama tu hii asilimia nane, kwa sababu sasahivi linachukua asilimia nane ya watu wote, je, tukimpa asilimia 100, zaidi ya watu milioni sitini, hili shirika linaweza likastahimili? Kwa hiyo tuna matatizo makubwa sana

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hiyo ni kwamba, katika mwaka wa 2019 na 2020, shirika lenyewe lilikataa zaidi ya madai ambayo yanatakribani shilingi bilioni tatu, madai ambayo wenyewe waliyakataa, kwamba haya ni madai ambayo ni batili. Kwa hiyo hii inaonesha kabisa kwamba tuna matatizo makubwa sana kwenye shirika letu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, shirika limeshindwa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 11. Tunategemea shirika

2 NOVEMBA, 2022

liende likawekeze lakini linadai taasisi za umma zaidi ya shilingi bilioni nane na linadai taasisi za sekta binafsi zaidi ya shilingi bilioni mbili, zipo nje hawajalipa na tunategemea hili shirika lijiendeshe. Haya ni matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninashauri; kwanza hili shirika tunategemea tulipe mzigo mkubwa baadaye wa kusimamia bima ya afya kwa wote, lakini tumeona halina uwezo wa kukusanya madeni na wakati huo huo mfumo wa TEHAMA bado unasumbua sana. Nashauri kwamba tulifanyie *restructuring* hili shirika ili tunapokuja na hoja kwamba linahitaji kubeba bima ya afaya kwa wote liwe na uwezo wa kubeba bima ya afaya kwa wote.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba tumeona kuna matatizo makubwa sana ya TEHAMA hususan maeneo ya vijijini ambako hakuna mitandao, na kuna muda ambapo kama hakuna mtandao ndani ya masaa 24, wanatakiwa wawe wamesha-*submit* zile *claims* zao na wakishindwa ku-*submit*, *system* ina-*reject*. Kwa maana hiyo mimi nashauri; kwamba tunahitaji vile vile kuangalia ule mfumo wa TEHAMA, upitiwe upya na hivyo uweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nitachangia leo ni kuhusu mfumo wa ujenzi wa Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 Serikali iliamua kuhamisha majukumu ya ujenzi wa viwanja vya ndege kutoka TAA (Wakala wa Kusimamia Viwanja vya Ndege) kwenda TANROADS.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na nia njema, lakini nadhani umefika muda muafaka sasa, tumejitathmini. Sisi tumechambua ndani ya Kamati yetu, tukaona kwamba bado ni muda muafaka ambapo majukumu ya kujenga viwanja vya ndege yarudi TAA.

Mheshimiwa Spika, kwanini tunasema hivyo? Ukiangalia *international standards zina-guide* kwamba, wataalamu wengi wa kujenga viwanja vya ndege, wa kutoa *guidance* wapo TAA. Tunatambua kwamba kweli tuna wataalamu wetu wapo TANROADS, lakini wale wengi wameboba kwenye ujenzi wa madaraja, barabara na mambo mengine. Kwa hiyo hii imekuwa hoja; na kuna muda ambapo wakati vile viwanja vinatengenezwa vinakuwa havina zile *international standards*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi...

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chaya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ulenge.

T A A R I F A

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba; si tu hilo la kupora miradi kutoka TAA kuipeleka TANROADS, lakini pia chanzo kikuu cha mapato kwa TAA ni *passenger service charge*, ambayo dola 40 kwa kila anayepanda ndege za kimataifa, na shilingi 10,000 kwa kila anayepanda

2 NOVEMBA, 2022

ndege za ndani. Fedha hizi zote zinakimbizwa *TRA* wakati *TCAA*, kampuni ambayo inafanya kazi zinazolandana na *TAA*, wanakusanya na kufanya miradi yao ipasavyo. Kuna nini kutokuiamini *TAA* kufanya kazi zake ipasavyo? Hiyo ndiyo taarifa niliyotaka kumpa.

SPIKA: Hilo swali anapaswa kulijibu Serikali au anapaswa kulijibu mwenyekiti wa Kamati. Maana unayempa taarifa ni yeye, atamuuliza nani swali sasa maana yeye ni mjumbe wa Kamati?

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, nimeongezea tu mchango wake *in terms* ya taarifa kwamba siyo hilo, kuna hili lingine pia linaibana *TAA*.

SPIKA: kwa maana nyingine ni kwa ajili yako na wengine. Yaani hizi hoja ni hoja zetu sisi kama Bunge. Kwa hiyo ukiuliza swali ni kwamba mwenyekiti. Kama swali alilokuwa anauliza Mheshimiwa Mpina maana yake mwenyekiti wa kamati atakapokuja kuhitimisha ataanza kujibu yale maswali. Kwa hiyo wewe umeeleweka na Mheshimiwa nadhani pia ameshakuelewa hoja yako.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa muongozo wako.

SPIKA: Karibu sana.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa huo muongozo...

2 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Mheshimiwa Chaya, subiri kidogo. Mheshimiwa Chaya unaipokea taarifa hiyo?

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Spika, naipokea na ninashukuru kwa ufafanuzi wako.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba nia ya Serikali ya kuhamisha ujenzi wa viwanja vya ndege kutoka TAA kupeleka TANROADS kipindi kile haikuwa nia mbaya. Hata hivyo ndhani muda muafaka umefika sasa kwamba turudishe yale majukumu kutoka TANROADS tuyarudishe TAA, na nimetoa sababu za msingi. Kwanza watu wa TAA ndiyo wana-*guide* zile *international standards* za ujenzi wa viwanja vya ndege, wana wataalamu ambao wapo TAA, wanye ubobezi kwenye masuala ya ndege na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba TANROADS tuna wabobezi wengi sana kwenye kujenga barabara na madaraja. Kwa hiyo tumeliona hili na tumelijadili katika Kamati yetu. Tunaishauri Serikali, muda muafaka umefika sasa kurudisha yale majukumu ambayo tuliyapeleka TANROADS yarudi TAA ili basi TAA iwe na majukumu kamili ya kuhakikisha, kwamba wanajenga vile viwanja vya ndege, wanasimamia viwanja vya ndege na vile vile wana-*provide* ile *maintenance* kwa ajili ya viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na ninaunga mkono hoja. (*Makofi!*)

2 NOVEMBA, 2022

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangala ajiandae.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia taarifa za Kamati zetu tatu, *PAC*, *LAAC* pamoja na *PIC*. Kwanza nianze kwa kuzipongeza sana Kamati hizi tatu kwa kazi kubwa ambazo wamefanya kuhakikisha kwamba wanapata ripoti iliyo salama na wametuletea hapa leo.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya ya kutafuta fedha, ingawa yapo mambo ambayo yameelezwa kwenye taarifa za Kamati ambayo si mazuri kwa nchi juu ya ubadhirifu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika ripoti hii nitajikita maeneo matatu. Jambo la kwanza ni eneo la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Pia nitachangia uendeshwaji wa Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro (*KIA*) na la tatu kama muda utakuwa bado unaruhusu nitazungumza kidogo Wakala wa Mabasi Yaendayo kwa Haraka (*DART*).

Mheshimiwa Spika, CAG amefanya ukaguzi wa ufanisi katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kuna mambo yamebainika ambayo yanahitaji kupelekewa miongozo ya namna ya uendeshaji wa mifumo ya upatikanaji wa wanafunzi ili waweze kunufaika na mikopo inayotolewa.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, jana tumezungumza sana hapa juu ya hoja ambayo ililetwa na Mheshimiwa Ezra juu ya wanafunzi ambao hawajapata mikopo. Katika ukaguzi huu wa ufanisi uliolenga kuangalia ufanisi wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wetu. Vilevile ukaguzi huu ulilenga kuangalia ufanisi wa namna zinavyoshughulikiwa rufaa pale ambapo wanafunzi wanapokuwa wamekata rufaa juu ya upatikanaji wa mikopo yao.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo machache ambayo yamebainika. Kwenye taarifa ile alifanya ukaguzi wa miaka mitano, lakini kuna mwaka 2018/2019 mwaka ule ulikuwa na shida kubwa. Ilibainika kwamba wanafunzi 6,182 walipewa mikopo zaidi ya kiwango walichotakiwa kupewa chenye thamani ya 5,670,000,000, kiwango hiki kama wangepewa wanafunzi wengine ambao hawakupata mikopo tungepata wanafunzi wengine 2,835. Tungegawa katika halmashauri zetu 184, kila halmashauri wanafunzi 15 wangufaika na fedha hizi ambazo walipewa wanafunzi zaidi ya kile walichokuwa wanahitaji.

Mheshimiwa Spika, nikisema hivi naamanisha nini hapa? Namaanisha kwamba mwanafunzi amekubaliwa kupewa kiasi fulani cha mkopo, lakini katika *reality* wakati anapokuja kupewa mkopo ule anapewa zaidi ya kile kiwango alichokubaliwa, inapelekea wanafunzi wengine kukosa mikopo na huu ulikuwa ni mwaka mmoja wa 2018/2019. Ukiangalia katika miaka yote mitano aliyofanya ukaguzi wa ufanisi CAG 13,000,000,000 zilizidishwa kwa wanafunzi ambao walikuwa wanapewa zaidi ya mikopo husika.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, wanafunzi 2,852 walipewa mikopo chini ya kile kiwango walichokuwa wamekubaliwa pale awali. Hii inaamanisha nini? Maana yake mwanafunzi amekubaliwa atapewa asilimia kadhaa, lakini mwisho wa siku anakuja kupewa chini ya kile kiwango ambacho alitakiwa kupewa. Tunamfanya mwanafunzi asimalize masomo yake au tunamfanya mwanafunzi kuhangaika na masomo yake. Nini kilifanyika hapa? Zaidi ya 1,147,000,000 wanafunzi hawakupewa stahiki waliokuwa wanatakiwa kupewa.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi 756 walipewa mikopo bila kuwa na sifa za kupewa mikopo, yaani hawana sifa ya kupewa mikopo lakini wakapewa, thamani yake 2,255,000,000. Hapa napo tungepata wanafunzi wengi ambao wangeweza kunufaika na mikopo hii hata pale Mbeya Jiji nao wangepata kupitia fedha ambazo kuna wanafunzi walipewa ambao walikuwa hawahitajiki kupewa mikopo.

Mheshimiwa Spika, nini sasa hapa tafsiri yake? Tafsiri yake katika Bodi yetu ya Mikopo bado kuna shida ya mfumo unaotumika katika utoaji wa mikopo ya elimu ya juu. Kama mwanafunzi alitakiwa kupewa 1,000,000 anapewa 1,200,000 tafsiri yake ufanisi wa ule mfumo siyo salama. Hapa umefanyika ukaguzi wa ufanisi. Sasa ukifanyika ukaguzi wa hesabu itakuwa tatizo zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashauri sasa kama inawezekana tufanye ukaguzi wa kina juu ya mfumo unaotumika wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Ukisoma

2 NOVEMBA, 2022

ripoti ya CAG inakupa *indication* kwamba mfumo siyo salama kwa kutoa mikopo kwa Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika ukaguzi huu uangalie hizi 5,670,000,000 za 2018/2019 walipopewa wale wanafunzi zaidi hao wanafunzi walikuwepo kule *site* au kuna watu walikuwa wanawapa halafu baadaye wanakwenda kuzichukua? Hizo ndio *indication* za hii. Je, hao wanafunzi waliopewa mkopo wakati hawana sifa hao waliowapa bado wako ofisini? Kwa hiyo ukifanyika ukaguzi wa kina utayabaini haya mambo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niende eneo la pili, eneo la uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro unaoendeshwa na Kampuni ya KADCO, hapa bado kuna shida. Kampuni ya KADCO iliingia mkataba na Serikali mwaka 1998 ili kuendesha Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro kwa miaka 25. Wakasainishana mkataba, ule mkataba Serikali ikawa na hisa asilimia 24 na kampuni ikawa na hisa asilimia 76. Katika kuendesha ule uwanja inaonekana ufanisi haukuwa mzuri. Serikali 2009 kupitia Baraza la Mawaziri wakakubaliana kununua hisa zote za KADCO kwa asilimia 100. Mwaka 2010 Serikali ilinunua hisa zote za KADCO kwa asilimia 100. TAA ililipa fedha milioni 5.3 fedha za Kimarekani sawa na milioni karibu 12.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 baada ya Serikali kununua zile hisa nini kiliendelea? Uendeshwaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro umeendelea kuendesha kama *private entity*. Wameendelea kuwa na mkataba wa *concession agreement*. Sasa unajiuliza maswali ya kutosha. Swali la kwanza, kama Serikali imenunua hisa zote asilimia

2 NOVEMBA, 2022

10,0 maana yake Serikali 100% ndio mmiliki wa kiwanja. Kwa tafsiri ya kawaida uendeshwaji wa kiwanja ulitakiwa kuwa chini ya Serikali kupitia TAA. Sasa hii *concession agreement* iliyopo wanaoendelea kutumia mpaka leo mpaka kesho na jana ni kati ya mkataba wa Serikali na watumishi wa KADCO walioko Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro au ni kati ya KADCO kama *private entity* na Serikali? Kama ni hili la pili nini maana ya kununua hisa kwa asilimia 100. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama Baraza la Mawaziri lilishauri kiwanja kile kiendeshwe na TAA kwa nini hakikuendeshwa mpaka leo? Kwanza cha ajabu zaidi hata fedha wanazokusanya KADCO mpaka leo tunaweza kusema wanazitumia fedha mbichi, kwa nini? Kwa sababu hazipiti Mfuko Mkuu wa Serikali, yaani wao wanakusanya kesho wanapanga matumizi, wanatumia. Wana kipengele kidogo tu wanalipa *dividend* Serikalini kwa TR hapo tu. Mwaka 2021 wame-*declare* kulipa 350,000,000.

Mheshimiwa Spika, sasa nashauri kwamba, kwa kuwa Serikali ilinunua hisa zote asilimia 100, sasa kiwanja hiki shughuli zote za uendeshaji zirudi TAA. Kwa nini nasema hivyo? tulipohoji kwa Afisa Masuhuli kwa nini wameamua kuendeleza hizi alitujibu jibu *simple* sana anasema kiwanja hiki kipo kimikakati ya kibiashara. Sasa mimi tu wa la saba wa Busega kule inaniingia kweli kichwani kwamba Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam hakiko kibiashara eti cha Kilimanjaro kiwe kibiashara zaidi? Kama ingekuwa ni kibiashara basi Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam ndicho kiko kibiashara zaidi kuliko Kiwanja cha Kilimanjaro. Kwa hiyo, nashauri tufanye hivyo. (Makofi)

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, la pili tufanye *special audit* ili kuangalia mapato yote yaliyopatikana katika miaka 10 hii yote ambapo KADCO walikuwa wanaendesha kiwanja kile kama Serikali, ili tubaini kama fedha hizi zilitumiwa vizuri na sheria za fedha zilifuatwa. Tukifanya yale yote yatatusaidia kujua ni kwa kiwango gani tumepata hasara kule Kilimanjaro. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nataka nichangie ni Wakala wa Mabasi Yaendayo kwa Haraka (DART). Tumeona Taarifa ya Kamati imesema hawa DART walilipa 1,700,000,000 kama fidia kwa wananchi kuachia maeneo, lakini CAG anasema fedha hizi zilikuwa nyongeza ya malipo nje ya *valuation report* iliyokuwepo, yaani *Valuation* inasema lipa 5,000,000,000 wao wakalipa zaidi 1,700,000,000. Sio hivyo tu, wakalipa na posho za usumbufu 435,000,000. CAG alipoomba kibali, walipata wapi kibali cha kuongeza kulipa fidia hawana. Hivi kweli wanapata wapi ujasiri wa kulipa 1,500,000,000 nje ya *valuation report*? Wanajibu kirahisi tu waliambiwa na Serikali. CAG anauliza leteni hicho kibali mlichopewa na Serikali, hawana. Hivi tumefika kuendesha taasisi yetu kwa *style* hiyo?

Mheshimiwa Spika, hapa kuna madudu ya kutosha juu ya malipo ya 1,500,000,000. Vilevile hapa tufanye *special audit* kuwabaini wale wote waliolipwa 1,500,000,000 kama ilikuwa ni halali. Pia wachukuliwe hatua watumishi ambao wameisababishia hasara Serikali kwa kulipa watu bila kufuata *valuation report*.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ni fedha za Watanzania na kibaya zaidi miongozo inasema *valuation* ikifanyika leo

2 NOVEMBA, 2022

baada ya miezi sita, mnaongeza *interest* kwa wale mliowakadiria. Baada ya miaka miwili, miongozo inasema kurudia *valuation*. Sasa wale muda umepita miaka 10, hawajafanya tena *valuation*, wanaibuka tu kulipa zaidi 1,570,000,000. Hili haliwezekani tufanye *special audit DART* ili tupate taarifa rasmi, fedha hizi wahusika waliolipwa na tuone tija kwa wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo moja la kumalizia. Ukienda pale Soko la Kariakoo, nafikiri liliungua mwezi Julai mwaka jana, pale napo kuna shida. Tunawaza kwamba, baada ya kufunga mwaka wa fedha 2021 kwa maana Juni, baada ya siku 10 tu soko likaungua, *documents* zote zikaungua, hamna cha risiti ya mapato, hamna cha risiti ya matumizi. CAG amewapa *unqualified report*, lakini ni kwa nini? Hapana siyo *unqualified report* amewapa *disclaimer report* ameshindwa kutoa maoni kwa sababu hamna *document* yoyote inayomfanya ku-*verify* mapato ya 3, 500,000,000 na matumizi ya 3, 500,000,000.

Mheshimiwa Spika, sasa hii kwa akili tu ya kawaida inanitafakarisha na kunifanya nione inawezekana Soko la Kariakoo liliungua baada ya *documents* hizi kutoonekana ofisini. Ni akili tu ya kawaida inanituma hivyo. Kwa nini baada tu ya kufunga mwaka wa fedha Juni, siku 10 tu, halafu mwisho wa siku CAG ameenda pale hamna *document* yoyote ameshindwa ku-*verify* matumizi ya 3, 500,000,000. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa leo nimekuja na *special audit* tu mwanzo mwisho. Hapa napo ifanyike *special audit* ya 3,500,000,000 tujue tatizo kubwa lilikuwa ni nini. Sasa sijui

2 NOVEMBA, 2022

watapata wapi *document*, lakini najua kwa sababu itakuwa ni *special* na kwa sababu *special* unaweza ukawahoji watu, CAG atajua namna ya kufanya, lakini mwisho wa siku tupate mbichi na nzuri kwa hapa kwenye Soko la Kariakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja za Kamati. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangala na ikiwa muda wetu utaruhusu tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kukushukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia taarifa ambazo zipo mbele yetu. Kwanza niwapongeze sana Wenyeviti wote wa Kamati hizo tatu ambazo tunazijadili leo, lakini niipongeze sana Serikali kwa juhudi kubwa ambayo inafanywa ya kuwekeza kwenye taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tuna jumla ya takribani mashirika na taasisi 237 na kati ya hizo 10 zimewekeza nje ya nchi yetu ya Tanzania. Kwa mwaka 2020/2021, Serikali imekwishawekeza mtaji wa thamani ya shilingi trilioni 67 na *point*. Kwa kweli ni juhudi kubwa sana na Serikali inafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwekezaji huo ambao ni zaidi ya asilimia 63.8 toka ilipoanza kuwekeza mwaka 2016/2017, ilikuwa kama trilioni 49 na kidogo, lakini mpaka

2 NOVEMBA, 2022

2020/2021 tumefikia trilioni 67, kwa kweli ni uwekezaji mkubwa ambao Serikali inaufanya.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma kwa kweli tumeshuhudia kwa macho kuona ni jinsi gani Serikali yetu ya Tanzania chini ya Mama Samia Suluhu Hassan inawekeza.

Mheshimiwa Spika, mbali na kuwekeza bado kuna changamoto. Changamoto kubwa ambazo tumeziona ni pamoja na kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa wakati kwa baadhi ya Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma. Kusipokuwepo na hizi Bodi za Wakurugenzi, usimamizi wa fedha ambayo Serikali imewekeza unakuwa na mashaka. Kuna taasisi zaidi ya miaka miwili haina Bodi ya Wakurugenzi.

Kwa mujibu wa Sheria kama Bodi ya Wakurugenzi haipo. Katibu Mkuu wa Wizara husika anawajibika kusimamia ile Taasisi, naye ana muda wake wa kusimamia ile taasisi si zaidi ya miezi kumi na mbili, lakini unakuta Katibu Mkuu bado anasimamia hiyo taasisi zaidi ya miaka miwili, ufanisi unakua mdogo, ufanisi unakuwa na mashaka.

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka mwezi Machi, 2022 wakati Mheshimiwa Rais anapokea ripoti ya CAG alitamka akasema yeye masuala mazima ya uteuzi ya hizi bodi yakifika mezani kwake hachukui muda kuyasaini na kazi zikaendelea. Hivyo basi, tuwaombe Wizara na Taasisi ambazo zinasuasua au kuna *delay* fulani ya kuteua hizi Bodi za Wakurugenzi, basi ziweze kufanya hivyo ili taasisi na fedha hiyo ambayo ni ya Watanzania imewekezwa iweze

2 NOVEMBA, 2022

kuwa na tija. Kuna taasisi zingine ambazo zinachelewa sana kupata vibali vya ajira, unakuta ina watumishi wachache, unakuta kuna watumishi wa muda, lakini unaweza ukakuta tena kuna watumishi ambao wanakaimu zaidi ya miaka sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anapokaimu kwenye *position* moja zaidi ya miaka sita, mitano hata ile *confidence* ya kufanya kazi anakuwa hana. Anakuwa hana maamuzi kamili ya kuweza kufikia maamuzi ili taasisi iweze kusonga mbele. Nashauri mamlaka husika waweze kufuatilia kujua kwamba ni taasisi ngapi ambazo zina matatizo au changamoto hizo. Tunamshukuru sana na kumpongeza sana *TR*, amekuwa akifanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba anasimamia haya Mashirika ya Umma yanafanya kazi zake kwa ufanisi, lakini kuna mambo mengine ambayo kama Serikali, kama Wizara, kama Taasisi husika ni lazima waweze kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kuchangia kujikita kwenye Shirika moja la Umma ambalo kwangu naona kama ni uti wa mgongo, Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*Tanzania Agricultural Development Bank*). Benki hii inamalengo yake matatu, naomba niyarejee; la kwanza ni kusaidia utoshelezi wa usalama endelevu wa chakula Tanzania. Lengo la pili ni kuchagiza mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo cha biashara. Lengo la tatu, ni kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi. Ni ukweli usiopingika, kilimo ndio ndio uti wa mgongo kwa Taifa letu.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ambayo tumeipitisha mwaka huu Wizara ya Kilimo imetengewa zaidi ya bilioni 900 na kidogo. Ukiangalia Benki hii inawajibika moja kwa moja kwa wakulima wa Nchi yetu ya Tanzania. Ukiangalia tena mtaji ambao wanao hii Benki ya Maendeleo ya Wakulima Tanzania, bado haukidhi. Kwanza Benki yenyewe iko *Stationed* Dar-es -Salam, mikoani kule ambako kuna wakulima, mikoa ya pembezoni hakuna tawi lolote. Sasa nashauri kwamba, Serikali kwa sababu ilishaji-*commit* kuwapa mtaji hii benki na iliahidi kuwapa bilioni 700 na ikasema itakuwa inatoa bilioni 100 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi tunapoongea Benki hii imekwishapewa bilioni 208 ina jumla ya mtaji bilioni 268, bado ni kidogo sana kwa majukumu ambayo benki hii inayo ya kuhakikisha kwamba kilimo cha umwagiliaji Tanzania kinakua, kuhakikisha kwamba wakulima wa kule Shinyanga, Songwe na Tanzania nzima wananufaika na hii mikopo ya benki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiiwezesha Benki ya Kilimo, tukawa-*link* na Wizara ya Kilimo ambapo Wizara ya Kilimo ina fedha ambazo zinakwenda moja kwa moja kwenye kilimo cha umwagiliaji, wana fedha ambazo zinakwenda kukopesha na kuwapa wakulima pembejeo, kuna fedha ya ufuatiliaji na usimamizi, lakini kuna fedha ya kuweza kuwapa miundombinu kama matrekta wakulima wadogo wadogo. Benki hii ikiwa *linked* pamoja na Wizara ya Kilimo ikasimamia zile fedha ambazo tunategemea wakulima wa Tanzania wakopeshwe waweze kutengeneza kilimo cha umwagiliaji, waweze kukopa matrekta, tunaweza tukawakomboa wakulima wa Tanzania.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nishauri kama inawezekana, kama ni sera, sheria au kanuni ziangaliwe tuone ni kwa jinsi gani benki hii itakuwa inafanya kazi kwa karibu sana na Wiizara ya Kilimo ili kuweza kurahisisha kuwakopesha Watanzania pembejeo, matrekta na kuwawezesha kwa namna yeyote ile ili uchumi wetu uweze kukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna Benki ambazo zinatoa mikopo kwa wakulima wa Tanzania, lakini Benki yetu ya (*TADB*) haijawafikia Wakulima wengi. Ukiangalia katika taarifa unaona kabisa kwamba kuna vikwazo ambavyo Serikali inaweza kukaa chini na kuvirekebisha, mfano, wakati benki inahitaji kukopa, labda imepata uhitaji mkubwa wa watu ambao wanahitaji kukopa ili waweze kufanya shughuli za kilimo, lakini kutokana na masharti ambayo yanakuwepo ni lazima Serikali ikope kwa niaba ya ile benki.

Mheshimiwa Spika, kukishindanishwa benki mbili kati ya hii Benki ya Maendeleo ya Kilimo na benki nyingine labda ya binafsi, zote zinakwenda nje ya nchi kwenda kukopa, ukiangalia masharti ya hii Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo ya Tanzania na masharti ya benki zingine, unakuta kwenye hii Benki ya kwetu ya Kilimo kuna vikwazo. Ni lazima mchakato ufanyike na unachukua zaidi ya miaka miwili, mitatu, lakini Benki nyingine au Taasisi nyingine ambayo haina milolongo ya vikwazo, haina milolongo ya *procedures* wao wanakwenda *direct* kama ni Ufaransa, kama ni *Canada* wanachukua mkopo, wanakuwa fedha na kuanza kukopesha.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, ushindani wa Benki ya Kilimo na ushindani wa benki zingine, kwa kweli benki yetu inaonekana bado haina tija kukidhi soko, kukidhi ushindani ambao benki zingine unazifanya. Ningeshauri tuangalie taratibu zetu kama Serikali, kama nchi kuweza kuinusuru benki yetu hii, kuweza kuiongezea mtaji ili basi hii benki kwanza iwe na matawi mengi Tanzania, iwe na matawi mikoani isikae Dar-es -Salaam peke yake na iwe na matawi sehemu ambazo kweli wanalima. Kwa sababu Dar-es-Salaam wakulima ni wachache, sana sana wengi ni wakulima labda wa Msimbazi pale kulima mbogamboga, lakini wakulima ambao wanaitaji huu mkopo wako mikoani na vijijini.

Mheshimiwa Spika, nashauri kabisa kwamba ni vizuri tukaangalia Serikali ikatoa mtaji ambao iliahidi kila mwaka ingewapa bilioni 100, basi iwape hizo fedha na ikiwezekana iwaongezee zaidi ili Benki yetu sasa iwe na ushindani na iwe na tija na iweze ku-*complete* na benki zingine na Watanzania wote waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na mengi ya kusema kwa leo, isipokuwa nashauri tu kwamba hizo bilioni 700 ambazo Serikali iliahidi na ilisema kwamba itatoa kwa *instalment* kila mwaka, basi ifanye juu chini ili Benki yetu ya Maendeleo ya Wakulima iweze kupewa mtaji na wakulima waweze kunufaika na kile ambacho Serikali imewekeza kwenye taasisi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ningependa sana kuwapongeza TANROADS kwenye sekta ya uwekezaji wa SGR, niipongeze sana Serikali ya Mama Samia Suluhu

2 NOVEMBA, 2022

Hassan, Kamati yako ya PAC ilipata fursa ya kuweza kutembelea na kukagua kuangalia uwekezeaji ambao umefanywa wa SGR.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli unaingia kwenye ile treni unasema hivi kweli tupo Tanzania? Hivi kweli Tanzania tumefikia hatua hii? Ni maendeleo makubwa ambayo yamefanyika. Unafika karibu na Kilosa kule unaingia kwenye handaki, kwenye shimo, yaani daraja lipo chini mpaka unasema waoo! Kwa kweli Tanzania tumepiga hatua, nawapongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, kazi hazijasimama, hazijalala, wanachapa kazi. Kwa hiyo niwapongeze sana Serikali kwa kutoa fedha kwa kuwekeza fedha na sisi Watanzania, Wabunge kama Wawakilishi wa Watanzania tunasema kwamba fedha zetu ambazo Serikali imeweza kweli zinafanya kazi, zinaonekana kwa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kingwangalla.

MHE. DKT. HAMISI A. KINGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote tatu pamoja na Wajumbe wao kwa kazi kubwa waliyofanya ya kutuletea taarifa zilizosheheni uchambuzi wa kina juu ya mambo mbalimbali yanayohusu mustakabili mwema wa Taifa letu.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, nitaanzia pale alipoishia Mheshimiwa Saimon Msonge kuhusiana na KADCO kuweka taarifa sawa tu. *In fact* KADCO ilipokuwa inaingia Mwaka 1998 Mwezi Julai wakati wanasaini mkataba ilikuwa imeshasajiliwa kama kampuni yenye malengo ya kwenda kuendesha Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro miezi mitatu kabla lakini kwenye mkataba wake na Serikali Taasisi hii ya KADCO ilikuwa inapewa mkataba wa miaka ishirini na tano, *Concession's Agreement* (mkataba wa uendeshaji), lakini mkataba huo utaweza kuhuishwa kila baada ya miaka 15, lakini hauna kiwango cha *fee au charge* yeyote ile ambayo KADCO itaenda kulipa Serikali. Kampuni hiyo baada ya kusajiliwa miezi kadhaa baadaye ikaiuzia Serikali ya Tanzania asilimia 24 ya hisa. Kwa hiyo Serikali akawa sehemu ya hiyo kampuni ya KADCO.

Mheshimiwa Spika, pamoja na masharti hayo ya ajabu ya mkataba huo, mkataba ambao kimsingi haukuweka vifungu vya ukomo, kampuni hiyo ya KADCO pamoja na Serikali kushindwa kuivunja kwa sababu hakukuwa na ukomo baada ya maamuzi ya Baraza la Mawaziri mwaka 2009, Serikali ika-*resort* kununua zile hisa za wanahisa wengine ambao walikuwa Kampuni ya South Africa ilikuwa inaitwa *SAIF* ilikuwa kampuni ya Uingereza ilikuwa inaitwa *Mott MacDonald International*, lakini pia kulikuwa na kampuni ya Tanzania ya *Inter-Consult* ambayo ilikuwa na hisa asilimia 4.6 tu wakati wale *Mott MacDonald* walikuwa na zaidi ya asilimia 41, nawale *SAIF* walikuwa wana asimilia 30. Serikali ikakopa pesa takribani bilioni 12.5 (5.3 USD) ikanunua zile hisa za wale wanahisa.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Baraza la Mawaziri yalikuwa yanaelekeza kwamba zile hisa zikinunuliwa hasahasa uendeshaji ya Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro utapelekwa chini ya mikono ya TAA.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kusikitisha ni kwamba mpaka leo kile kiwanja kinaendeshwa na Kampuni ya KADCO. Sasa ukijiuliza kama maamuzi ya Baraza la Mawaziri yalikuwa kwamba baada ya zile hisa kununuliwa na Serikali ikakopa Benki ya CRDB 5.3 milion USD na TAA wale wakalipa kufikia mwaka 2014 wakawa wamemaliza lile deni, kwa nini bado kuna KADCO mpaka leo? Hupati majibu. Hata hivyo, KADCO wale wanaendesha ile kampuni ambayo asilimia mia inamilikiwa na Serikali kupitia TR msajili wa Hazina na mkataba wao uliuhishwa tena mwaka 2008 kwa sababu katika ule mkataba wa awali mkataba una uhai wa miaka 25, lakini ikifika miaka 15 unahuishwa tena, kwa hivyo uliuhishwa tena mwaka 2008 kabla hata ya ile miaka 15.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye hili unaona wazi kwamba jinsi ilivyoanzishwa hii KADCO na jinsi ilivyokuja kumpa Serikali asilimia 24 na jinsi baadaye Serikali ilivyokuja kununua zile hisa pale mwanzoni na jinsi ambavyo hii KADCO mpaka leo bado inaendelea kuendesha na kusimamia shughuli za uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro, kuna harufu kubwa ya upigaji kwamba KADCO ni dili tupu. KADCO inanuka rushwa, inanuka mipango na hatuelewi wale waanzilishi walikuwa akina nani? Kwa nini walianzisha kampuni hii na akina nani halisi walio nyuma ya hii KADCO ambao mpaka leo

2 NOVEMBA, 2022

wanaendelea kuipa mafao na mafanikio ambayo haipo kihalali?

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wake walijajiwa na *private company*, lakini mpaka leo bado wapo wanakusanya mapato pale, hatujui yanaenda wapi, CAG hajui yanaenda wapi. Kama wana mkataba wa *Concession Agreement* tulimhoji Katibu Mkuu alipokuja mbele ya Kamati yetu, akasema KADCO inaendelea kuendesha ule uwanja kwa sababu kuna *Concession Agreement* ambayo ilisainiwa mwaka 1998. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukamwambia sasa hiyo *Concession Agreement* inabaki kwa masharti yapi? Kwa sababu mkataba wa ukodishwaji maana yake kuna kiwanja cha pesa ambacho unalipa. Kwa hivyo sasa wale KADCO hawalipi chochote Serikalini, lakini wanakusanya na kile wanachokikusanya wanakipeleka wapi na wanakusanya kwa Mkataba upi au kwa makubaliano yapi? Unakosa majibu. Walishindwa kujibu, tukawapa muda watuletee na mpaka leo hawajawahi tena kuleta majibu ya ziada. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Kingwangalla nalinda muda wako. Hebu nisaidie, hii KADCO inaitwa KADCO kule BRELLA ni nani mmiliki halali wa hii Kampuni kwa sasa? Ni nani mmiliki? Bado ni wale waliokuwepo ambao walishalipwa ile asilimia 100 iliyolipa Serikali ama kuna mahali hapo imebadilika imekuwa ya Serikali? Yaani kwamba nikienda BRELLA leo nitawakuta wale wamiliki au naikuta Serikali?

2 NOVEMBA, 2022

MHE. DKT HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi KADCO inamilikiwa na Serikali ya kwa asilimia mia moja chini ya Msajili wa Hazina toka huo mwaka 2010.

SPIKA: Sasa, samahani nakuuliza wewe kwa sababu unaonekana unazijua sana hizo taarifa na mimi nataka nizijue. Kama Serikali ilishanunua hii Kampuni maana yake ni ya Serikali.

MHE. DKT HAMISI A. KIGWANGALLA: Ndio.

SPIKA: Ni mahali gani inatokea tena kurejea kwa wale watu ambao walikuwepo tangu mwanzo?

MHE. DKT HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Nataka kuelewa tu siyo kwamba wewe ndiyo Serikali, maana hii sasa ni ya kwetu sisi, hii ni taarifa ya Kamati, kwa hiyo nataka nifahamu vizuri.

MHE. DKT HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, nakuelewa vizuri na *actually* huo mkanganyiko unaoupata wewe na ndiyo mkanganyiko alioupata CAG na ndiyo mkanganyiko tulioupata sisi na ndiyo maana tunaona kwamba hakuna haja ya kuendelea...

SPIKA: Labda swali langu la mwisho. Kama Serikali imeshalipa asilimia mia moja huo mkataba unatambuliwaje mpaka kuna maswali ya kuhuishwa wanahuisha kitu gani ambacho hakipo? Kwa sababu Serikali si ilishanunua asilimia moja? Sasa, ni mkataba gani tena unaoendelea

2 NOVEMBA, 2022

mpaka unahitaji kuhuishwa tena na ukasema haujaisha, haujaisha vipi, wakati...

MHE. DKT HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, Mkataba ulisainiwa Mwaka 1998, ilipofika mwaka 2008 kukawa na hoja kwamba KADCO wameshindwa kufanya uendelezaji kadri ulivyokuwa mkataba wa awali wa mwaka 1998 na hivyo Mkataba ule uvunjwe. Sasa katika kikao cha Baraza la Mawaziri ikaonekana kwamba waende waka-*negotiate* ili kuvunjwa ule mkataba. Wale KADCO ambao ni wabia wa Serikali kwa kipindi kile cha awali wakakataa kuvunja ule mkataba, walipokataa kuvunja ule mkataba ndipo Serikali sasa ikaamua kununua zile hisa za wale wanahisa wengine ambazo nimesema alikuwepo *Mott MacDonald International* alikuwa na asilimia 41, alikuwepo *SAIF* alikuwa na asilimia 30, alikuwepo *Inter-Consult Limited* alikuwa na asilimia 4.6 na Serikali alikuwa na asilimia 24. Kwa hivyo Serikali akawalipa wale ili waondoke.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mkataba ule Serikali kuamua kununua zile hisa mwaka 2009, mwaka mmoja nyuma 2008, mkataba ule wa awali wa *concession agreement* ile ikahuishwa upya mwaka mmoja kabla, kwa hivyo inapaswa kuisha mwaka 2023. Leo hii wanasema wanaendelea kuitumia KADCO kuendesha Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro kwa kutumia *concession agreement*. Sasa *concession agreement* na nani? Kama KADCO ni mali ya Serikali kwa asilimia 100, Serikali inampa kampuni nyingine tena ambayo ni ya kwake haki ya kutekeleza majukumu ambayo yangepaswa kutekelezwa na TAA.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo kwenye maamuzi ya Baraza la Mawaziri, maamuzi yalisema hivi *categorically* kabisa, *very explicitly* kwa lugha ya kisheria kwamba, *share* za KADCO za wale wabia binafsi zinunuliwe na Serikali na sikishanunuliwa na Serikali Uwanja wa Ndege wa KIA urudishwe chini ya TAA ili auendeshe kama ambavyo anaendesha viwanja vingine vyote vya ndege, ikiwemo kiwanja kikubwa zaidi hapa nchini cha Dar-es-Salaam, lakini hilo halijawahi kufanyika toka 2010 mpaka leo. Sababu wanayosema ni kwamba, kinachofanya wasiiondoe KADCO ni *concession agreement* ambayo ilisainiwa wakati Serikali akiwa kwenye ubi ana wadau wa sekta binafsi hao niliowataja. Kwa hivyo, ndiyo mkanganyiko tunaousema.

Mheshimiwa Spika, unachokiona kwa kuwa, kule kwenye KADCO wanakusanya mafao na yale mafao sasa hayaji kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina yanaenda kwenye ile kampuni ya KADCO, ndiyo tunasema kuna harufu ya kwamba, pengine hii KADCO inawanufaisha baadhi ya watu ambao wako nyuma yake, ndiyo maana hawataki kuiondoa. Nafikiri nimejieleza vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye hoja yangu ya pili. Napenda kuzungumzia suala la mradi mkubwa wa kimkakati wa reli ya kisasa (SGR). Kulitokea hoja hapa nafikiri ilikuwa Bunge la Bajeti ambapo ilionekana kuna utata kwenye namna tenda ya awamu ya tano ya mradi wa SGR ilivyotolewa kwa njia ya *single source* kwa kampuni inayotokea nchi ya marafiki zetu *Republic of China*. Ikaonekana kwamba, majibu yaliyotolewa hapa ni kwamba *single source* kwenye *phase five* ya SGR imefanya

2 NOVEMBA, 2022

tumepata Mkandarasi kwa gharama nafuu sana na hii ni reli iliyokuwa inatoka Tabora kwenda Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia ile hoja, nakumbuka, walisema huyo aliyepewa ni yule ambaye ametekeleza awamu ya tatu ambayo inatoka Mwanza mpaka Isaka, kule kwenye ile *lane* hajafanya kazi yoyote mpaka sasa, huu takribani ni mwaka wa pili hajafanya chochote. Kwa hivyo inakuwaje ameongezewa kipande cha Tabora kwenda Kigoma, hiyo ndiyo hoja iliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi hoja yangu ni kwamba, mwezi Agosti mwaka huu TRC wametangaza awamu ya sita ambayo inatoka Uvinza kwenda Gitega, nchi jirani ya Burundi kupitia Msongati. Wametangaza *open tendering process competitive bidding* ushindani unaruhusiwa, kwa maana hiyo wamerudi kwenye kile ambacho walikikataa. Sasa kama *single sourcing* ambayo wameitumia kwenye kipande cha kutoka Tabora kwenda Kigoma imetupa ahueni kwa nini kwenye awamu hii ya sita wamerudi tena kwenye ushindani wakati mwanzoni walisema ushindani haulipi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilipenda kuhoji suala hilo na pengine kuomba Bunge lako Tukufu liridhie kufanya uchunguzi maalum wa namna zabuni zote za mradi huu mkubwa wa kimkakati zilivyotolewa ili tuwe na majibu yaliyo *clear* bila kutubabaisha-babaisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuzungumzia eneo la pili kwenye mradi huu wa SGR. Pale Dar-es-Salaam reli ya

2 NOVEMBA, 2022

SGR inapaswa kuingia bandarini na ifahamike kwamba, kwenye biashara ya uchukuzi kwa njia ya reli kinacholipa zaidi ni mizigo ni *cargo*, hata sio abiria. Kwa hivyo, *cargo* kwa kiasi kikubwa inapaswa kuchukuliwa bandarini moja kwa moja ili kwanza kuongeza *efficiency* ya bandari, lakini pili kule kuna mapato makubwa zaidi ukilinganisha na mapato ya abiria.

Mheshimiwa Spika, sasa miradi hii ya SGR inavyotolewa inatolewa kwa njia ya *design and build*. Kwamba, anayebuni ule mradi anafanya usanifu wa ule mradi ndiye ambaye atajenga mradi husika. Ilikuwa je Serikali ikaingia mkataba wa kujenga reli ambayo ilianza pale juu, pale *station*, kuja mpaka Morogoro na ikafuata awamu ya pili kuja mpaka Makutupora bila kuweka *link* ya kuingia bandarini (*port link*)?

Mheshimiwa Spika, kwamba, walikuwa wanawaza nini? Mkandarasi ame-*design* reli halafu hajaifikisha bandarini, halafu sasa hivi wanaanza mchakato wa kutangaza kipande cha kutoka pale *station* kuingia bandarini na kinawasumbua kidogo kwenye *design*. Kwa hivyo, nilipenda kulizungumzia hilo kwa sababu linaleta utata namna ambavyo reli itakuja ku-*land* kule bandarini kwa sababu, bandarini ni chini na hapa *station* ni juu. Sasa inasumbua magari yapatika wapi? Nafasi kule ndani inasumbua itakuwaje? Sasa ilikuwaje waka-*design* mradi wa kuendeleza bandari na huku juu waka-*design* mradi wa SGR bila kuweka *link* ya moja kwa moja ya hivi vitu viwili, pia bila kuweka *link* ni namna gani watu wataingia na kutoka bandarini kwa miguu, kwa magari na kwa treni kwa njia nyingine zozote zile ambazo zinapaswa kutumika?

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, *design* ya miradi mikubwa kama hii inapaswa kufuata njia ambayo inaitwa *multi-modal designing*. Kwamba, unapo-*design logistics* za sehemu lazima ufanye *consideration* ya aina zote za usafiri na uchukuzi zitakazopita katika eneo hilo. Iwe kama kuna urahisi wa kufika kwa ndege, kufika kwa *helicopter*, kufika kwa baiskeli, kufika kwa miguu, kufika kwa *trams*, kufika kwa gari, magari ya abiria, magari binafsi, ni lazima uweke *consideration* ya mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa bandari yetu na hii SGR vilipodizainiwa (*design*) mradi wa kutanua bandari ulivyodizainiwa (*design*) na mradi wa SGR walivyo-*design* hawakufanya hiyo *multi modal kind of designing*. Kosa hili pia unaliona kwenye mradi wa *BRT*. *BRT* imekuwa *designed* kwa gharama kubwa sana ukilinganisha na *BRT* nyingine ambazo zimejengwa katika nchi mbalimbali duniani, sisi ya kwetu inaendana na nchi moja tu ya Colombia.

Mheshimiwa Spika, walipo-*design* wanamwaga zege ya takribani nchi 10/12. Ni zege nzito sana kiasi kwamba, wangeweza kwa hapa juu kuweka *provision* ya *tram*, yaani treni nyepesi ya kupita mijini. Hapo inapaswa kuzingatiwa kwamba, Jiji la Dar-es-Salaam kwa sensa ya juzi limekutwa na watu karibu 5.6 million. Kwa siku watu wanao-*move*, wanao-*commute* katika jiji la Dar-es-Salaam wapo kati ya Laki Nne mpaka Laki Tano.

Mheshimiwa Spika, sasa usafiri huu wa *BRT* ndani ya muda mfupi tu utapoteza mantiki yake, hautaweza kuwasafirisha watu kutoka eneo moja kwenda jingine kwa

2 NOVEMBA, 2022

ufanisi ambao ulitarajiwa wakati wa *designing* kwa sababu, kwanza *designing* ilifanyika zaidi ya miaka 20 iliyopita wakati huo Jiji la Dar-es-Salaam lilikuwa lina wakazi waliokuwa wanakadiriwa *4.3 million*, leo hii imeshafika hapo, kama tunaenda hivi kwa *trend* hii, miaka 30 ijayo *population* ya Dar-es-Salaam ita-double pengine tutakuwa na wakazi zaidi ya Milioni 12. Hapo maana yake ni nini, kama hukufanya *multi modal designing*, ukaweka *provision* ya barabara za juu, ukaweka *provision* ya *trams* kwenye hiyo *BRT* hapohapo, maana yake huo mradi ni *white elephant*. Na tumekopa, kwenye hii awamu ya kwanza, Dola 150,000 za Kimarekani na ambazo tunazilipa Watanzania kupitia kodi zetu. Kwa hivyo, tunatarajia wataalamu wetu wanapo-*design* hii miradi wasitutie hasara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili napenda kuchangia kuhusu uendeshaji sasa wa hiyo *lane* ambayo sisi tumekopa, kama nchi. Juzi hapa nimeona kwenye vyombo vya habari kwamba, *BRT* ile *lane* inakodishwa kwa kampuni ya nje. Bahati mbaya sana *BRT is not rocket science*. Siyo sayansi ya kurusha roketi kwenda mwezini ama kwenda kwenye sayari nyingine, ni kitu rahisi sana, *lane* iko pale unaweka basi juu yake, Dereva analiendesha, linasimama kwenye vituo vyote, watu wanapanda na kushuka. Kwenye sehemu ya tiketi unaweka tu mfumo, ukishaweka ule mfumo *immediately* unanza ku-charge. Leo hii analetwa mwekezaji wan je kuja kuendesha *BRT*, mwisho wa siku akipata faida anaondoka na pesa zake zote kupeleka nje ya nchi. Nini maana ya *local content* tunayoizungumza kila siku? (Makofi)

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, tunao waendeshaji wakubwa wa mabasi hapa Tanzania na mabasi yanaenda sehemu mbalimbali. Mtu anaendesha mabasi 50 hadi 100 yanatoka Dar-es-Salaam yanakwenda Bara kwenye Mikoa mbalimbali na wanaweza hizo *operations*. Kuna u-*special* gani kwenye kuendesha mabasi katika Jiji la Dar es Salaam? Hiyo ni nukta ya kwanza. Nukta ya pili, Dar es Salaam kulikuwa kuna usafiri *dedicated* wa UDA mpaka mwaka 1983 ambapo Serikali iliamua kuwaruhusu waendeshaji binafsi kwa sababu UDA ilionekana kushindwa kubeba mzigo wa uchukuzi katika Jiji la Dar es Salaam. Baada ya waendeshaji binafsi kuingia, mwanzo wa daladala kuingia, leo hii Dar-es-Salaam tuna mabasi takribani 7,000 yanayochukua watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine na yanamilikiwa na takribani watu 5,000 mbalimbali.

SPIKA: Dakika moja, malizia, kengele ya pili ilishagonga.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, pamoja na ajira ambazo zinatolewa kwa wanaoagiza yale mabasi kuyaleta hapa nchini, wanaofanya ukarabati wa mabasi kwa maana ya gereji na mafundi gereji, lakini pia Mama Lishe wanaouza chakula kwa hao makondakta, matanboy, pamoja na mafundi wanaofanya kazi kwenye hizo gereji, sheli mbalimbali ambazo zinapata watu wenye daladala wanaweka mafuta, zote hizi kwa ujio wa *BRT* maana yake hizi ajira zote zinakufa. Na hizi ajira zikifa ni takribani ajira 20,000 mpaka 30,000 hizi ajira zikifa tulitarajia basi walao yale mafao ya uwekezaji tulioufanya kwenye *BRT* basi yabaki hapa nchini na yasichukuliwe na mtu ambaye anatoka nje ya nchi.

2 NOVEMBA, 2022

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haikuweka utaratibu wa kumlazimisha *operator* atakayetoka nje atakapokuja hapa nchini basi lazima awe na *partnership* ya lazima na kampuni ambayo leo hii inaendesha *BRT*? kwa nini hayakuwekwa hayo masharti? (*Makofi*)

SPIKA: Haya, ahsante sana.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge. Nami nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wetu, Makamu Wenyeviti, pia wajumbe wa Kamati hizi ambazo zimeweza kupitia taarifa mbalimbali ambazo zinatupa fursa sisi kama Bunge ya kuweza kuzijadili na baadaye tutoe maazimio kwa maana ya tufanye maamuzi juu ya hoja mbalimbali ambazo zinaendelea kujitokeza.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo mambo machache kwa sababu, tutaendelea na kujadili taarifa hii kwa siku tatu zijazo, kwa maana ya kesho siku ya Alhamisi, siku ya Ijumaa na Jumamosi. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, hoja zinazozungumzwa hapa na Wabunge ni hoja mtambuka zinaenda kwenye Wizara mbalimbali ambazo baadhi ya hoja hizo kabla Bunge halijafanya maamuzi tutataka kupata, wakati wa michango yenu Serikali, ili muwe mmechangia kwa sababu, tutakapofanya maamuzi tutakuwa hatuna tena kurudi nyuma itabidi mkayatekeleze hayo tutakayokuwa tumeamua. Kwa hiyo, ni muhimu sana

2 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Mawaziri kuwepo wakati Kamati hizi zinajadili hoja hizi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika kusema hivyo ni muhimu wawepo na wazipate hoja za Wabunge kwa sababu, haya mambo ya mnajadili jambo moja miaka inaenda inarudi, taarifa ni ileile, aahhaa, hayo hayakubaliki. Na kwa sababu, hayakubaliki tutataka hoja ikishajadiliwa Wabunge wametoa mawazo yao, hasa kwenye hoja zinazosimamiwa na Kamati hizi kwa sababu, hizi ni hoja za ukaguzi kwa hiyo, lazima tufike mahali tuzimalize. Yale ya ushauri, hatuko kwenye ngazi ya ushauri sasa hivi, sasa hivi ni Bunge linaisimamia Serikali, kwa hiyo ni muhimu sana Serikali ikawepo Bungeni kusikiliza Bunge linachosema. *(Makofi)*

Wakati wa ushauri hilo ni jambo tofauti kwa sababu ushauri unaweza ukakubaliwa ama ukakataliwa, lakini kama tulishashauri halafu Serikali haikuchukua, halafu ukaguzi ukafanyika, ndiyo tuko hapa sasa kusema Serikali tulishauri haukusikia, sasa tumeamua hivi. Kwa hiyo, ni muhimu sana Mawaziri na Naibu Mawaziri kuwepo Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni kwamba, hizi hoja ni za kamati kwa hivyo, ni hoja zetu. Kwanza ni kukumbuka kuunga mkono hoja ya Kamati kwa sababu, hakuna anayepinga hoja ya Kamati kwa sababu ni hoja yetu. Unaweza ukasahau kuunga mkono hoja ya Serikali, lakini hoja ya Kamati ni muhimu sana kwa sababu ni hoja ya Bunge. Hilo moja, lakini la pili, wakati tukichangia ni muhimu kujielekeza kwenye yale mambo ambayo katika Bunge hili

2 NOVEMBA, 2022

tutafanyia maamuzi. Ukijielekeza kwenye kutoa ushauri wa kuishauri Serikali ifanye hivi, unaishauri Serikali ifanye hivi, sasa hivi kwenye ngazi hii ya hizi taarifa za hizi kamati tuko kwenye kuisimamia Serikali, maana yake Bunge litaiagiza Serikali nini cha kufanya. Maana yake ni nini? (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, unaposimama kuchangia jitahidi sana kwanza uwe umeelewa hoja iliyo mbele yetu, Kamati imeleta hoja gani ambazo inataka kuliongoza Bunge ili baadae tufanye maazimio, tufanye maamuzi, tuiagize Serikali kufanya nini. Ukileta jambo jipya nje ya pale, labda ulete jambo ambalo na lenyewe sasa ndiyo nataka kufafanua, ukileta jambo jipya ambalo halina uhusiano na hesabu za Serikali ambazo zimeshakaguliwa kwa mwaka 2020/2021 yaani hilo jambo lako litakuwa ni jipya na maana yake litakaguliwa huko badae kama lina tatizo. Kama ni kushauri ni ngazi nyingine, ngazi hii tusiishauri Serikali kwa sababu, ipo sawa itachukua, lakini kimsingi siyo saa ya kuishauri ni saa ya kuisimamia Serikali.

Sasa, yale uliyoyapitia kwenye Kamati unaweza kutazama ni kawaida, ni kama Serikali ambavyo huwa tunaishauri halafu inakuja kusema imechukua ushauri upi na upi haijachukua, itafanya hivi, kwingine inafafanua. Vivyo hivyo Wabunge wanavyochangia, hasa wale ambao siyo Wajumbe wa Kamati zenu Wenyeviti, ni muhimu sana kusikiliza hoja zao na wengine wanazungumzia hoja ambazo ziko kwenye vitabu vya CAG, lakini taarifa za Kamati hazijazisema. Kwa hivyo, ni muhimu sana Wenyeviti kufuatilia michango hiyo ili huko baadaye wakati wa kuhitimisha hoja zenu mtayatazama yale maazimio yenu, mtatazama yepi yaongezeke kupitia michango ya

2 NOVEMBA, 2022

Waheshimiwa Wabunge ili na yenyewe yawe sehemu ya maagizo ya Bunge kwa Serikali. Kwa hiyo, lazima hilo nalo lieleweke. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge anaweza kuwa amesoma taarifa ya CAG na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati husika pengine hilo hawakuliona lina umuhimu, lakini baada ya kuja humu ndani na michango ilivyotokea imeonesha kwamba, jambo hilo ni la umuhimu. Aidha, mtafafanua kwa nini hamlichukui kwamba, tuiagize Serikali na hapa nitatoa mfano, Ripoti ya PAC ambayo pengine ndiyo ingetarajiwa kuwa na taarifa zile za mapungufu ya NHIF ya kuhusu kulipa zaidi wanaume 700 waliojifungua na kukataa kulipa pesa hospitali ya Muhimbili ama JKCI, yaani hoja kama zile hazipo kwenye Taarifa ya PAC, lakini Mjumbe akizileta na ziko kwenye Taarifa ya CAG lazima Mwenyekiti uwe hapa umesikiliza vizuri, umeandika, ukafuatilia kama ambavyo Serikali hufuatilia.

Sisi tukiiambia Serikali inafuatilia halafu inaleta hapa ufafanuzi halafu kuna mengine wanakubali mengine wanakataa, ndivyo Mwenyekiti utakachofanya, mengine utatoa ufafanuzi, mengine utabadilisha taarifa yako uweke maazimio ya ziada. Sasa Wabunge ili tuwasaidie Wenyeviti, tusiende tunazunguka kwenye ile taarifa tunaogelea, wao wametuongoza, sisi tunatafuta kile ambacho wametuongoza tunakubaliananacho ndiyo maana tunaunga mkono hoja, kama kuna cha ziada lazima useme ni wapi kinaongezwa?

Waheshimiwa Wabunge, maana wakati mwingine maazimio yako tayari humu, lakini ungependa yatumie

2 NOVEMBA, 2022

lugha fulani hivi ambayo Serikali itaona kweli inaelekezwa. Kwa hiyo, unaruhusiwa kwa ngazi hiyo kusema kwamba, namna azimio hili lilivyoandikwa Serikali tutarudi tena mwakani tutalikuta, tuandike hivi, halafu Wenyeviti watatueleza kama wanakubaliana na hayo ama hapana, ndivyo utaratibu ulivyo.

Kwa hivyo, ni muhimu na wewe unapochangia sema, msaidie Mwenyekiti ni ukurasa wa ngapi wa taarifa ya Kamati yake, ukurasa wa ngapi wa taarifa ya CAG, ili na yeye apate urahisi wa kuweza kufuatilia hoja yako ili aitolee ufafanuzi baadaye au arekebishe ama aongeze maazimio kwenye taarifa yake, ili Bunge tusiwe tena tunaenda mbele tunarudi nyuma, Taarifa hii ya CAG tukishamaliza hapa kujadili tutaitumia huko badaye kama rejea, siyo tena kama hoja. Maana hoja za CAG za kuishia 2021 Juni, tunapaswa kuzimaliza hivi sasa, zile ambazo haziishi kwa sababu za kisheria, pengine hizo, lakini nyingine zote Wabunge hatutatakiwa kurejea huko. Tutarejea huko kwa rejea kwamba, tulisema. Kwa hivyo, ni muhimu sana kujielekeza huko Waheshimiwa Wabunge. Na sote tushiriki kwenye hili zoezi, maana huwa tunaelezana kila siku shughuli yetu ni kutunga sheria, kuismamia Serikali, kushauri Serikali. Sasa hivi ni kuisimamia Serikali na tuisimamie Serikali.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, kuna tangazo la mwisho kutoka kwa Katibu:-

Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba, siku ya kesho, Alhamisi, tarehe 03 Novemba, kutakuwa na semina ya masuala ya Bima ya Afya kwa wote mara baada ya kusitisha Kikao cha Bunge, Saa Saba Mchana

2 NOVEMBA, 2022

katika Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa kuhudhuria wote semina hiyo muhimu kwa sababu, kama nilivyotangaza ratiba jana, tutakuwa tukijadili Muswada huu wiki ijayo kwa hiyo, ni muhimu kuhudhuria semina hii, ili kama kuna mambo mengine hayaeleweki vizuri basi tukaelewe huko. Halafu saa ya kuja kutunga sheria wote tuwe na uelewa mmoja. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Kamili, asubuhi.

(Saa 2.01 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 3 Novemba, 2022, Saa Tatu Asubuhi)